

BUNE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Tano-Tarehe 12 Novemba, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatuhu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge,) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Tukae.

Katibu!

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

MWENYEKITI: Waziri wa Elimu, Sanyansi na Teknolojia.
Namuona Naibu Waziri Mheshimiwa Ole Nasha.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Chuo Kikuu cha Dodoma kwa Mwaka 2016/2017 (*The Annual Report and Accounts of the University of Dodoma for the year 2016/2017*).

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu!

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Swali letu la kwanza kwa siku ya leo linaulizwa na Mheshimiwa Hassan Elias Masala Mbunge wa Nachingwea na linaulizwa kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 55

Hali ya Elimu Mkoani Lindi

MHE. HASSAN E. MASALA aliuliza:-

Lindi ni kati ya Mikoa iliyio nyuma kielimu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia mkoa huo illi uweze kupiga hatua kielimu?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, namuona Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha hali ya elimu Mkoani Lindi, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo ifuatayo:-

(i) Kuongoza fursa ya elimu kwa watoto waliokosa kutokana na umbali wa kwenda na kurudi shulen kwa kujenga shule shikizi 12 kuititia proramu ya *EQUIP-T*. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015/2016 hadi mwaka 2017/2018 programu hiyo imetumia jumla ya shillingi 726,720,000 kujenga shule shikizi 12 kwenye Wilaya zote sita za Mkoa wa Lindi.

(ii) Kuwapatia mafunzo walimu wote wa darasa la kwanza hadi la nne stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji.

(iii) Kugawa vitabu 415463 vya darasa la kwanza hadi la Nne ili kuboesha taaluma.

(iv) Kuajiri na kuwapangia kazi walimu 180 katika Mkoa wa Lindi kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 na mwaka 2017/2018.

(v) Kupeleka jumla ya shilingi 3,077,000,039 kwenye Halmashauri za Mkoa wa Lindi kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 2017/2018 ambazo zimetumika kujenga madaasa 89, matundu ya vyoo 210, mabweni 12, bwalo moja la chakula na kukarabati shule 14. Vilevile katika kipindi hicho, Serikali imepeleka shillingi 1,951,680,959.88 katika Halmashauri za Mkoa wa Lindi kwa ajili ya usimamizi wa shughuli za elimu 10%, upangaji wa ikama ya walimu 20%, ujenzi wa madarasa mapya 40% na ukamilishaji wa maabara na vyumba vya madarasa 30%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kushirikisha wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo katika kutatua changamoto za elimu katika Mkoa wa Lindi ikiwemo kudhibiti utoro wa wanafunzi na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Masala.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini pamoja na hayo naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wilaya sita zilizoko ndani ya Mkoa wa Lindi Nachingwea ni moja ya wilaya ambayo kijigrafia ni kubwa sana, lakini pia ndiyo wilaya inayoongoza kwa kuwa na shule nydingi za msingi karibu 105. Naomba kufahamu vigezo vilivyotumika kugawa hii fedha

kwa ajili ya shule shikizi. Mahitaji ya Wilaya ya Nachingwea ilikuwa shule 10; lakini wametoa shule mbili sawa na Halmashauri zingine. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anieleze upendeleo ambao ana weza kutoa kwa Wilaya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili naomba kujuu moja ya uwekezaji mkubwa uliofanya na Serikali yetu ni ukarabati wa Chuo cha Elimu Nachingwea, chuo hiki kimeshahapeka wanafunzi wa diploma lakini mpaka hapa ninapozungumza Wizara imetoa maelekezo ya kuondoa wanachuo wote na kuwapeleka Chuo cha Dakawa, Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sababu zipi ambazo zimepelekea wanachuo hawa kuondolewa katika Wilaya ya Nachingwea wakati hawa wanachuo walikuwa wanasaldla kuboresha elimu katika maeneo yale? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Asante majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Hassan Masala nilipata fursa ya kutembelea jimboni kwake na Wilaya kwake ni mionganoni mwa majimbo makubwa, na nimeenda nikajionea, tukatembea naye hata tukafika hata Kilima Londo kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anauliza je, ni vigezo vipi ambavyo vimetumika katika kugawa ukilinganisha Wilaya yake ni kubwa.

Naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, katika kupeleka kipaumbele tunazingatia jiografia halisi na kwa ujumla kwa Mkoa wa Lindi ulikuwa na tatizo kubwa. Na ndio maana swali lake la msingi anaongelea mkoa mzima. Kwa hiyo katika kupambana na tatizo la ufaulu duni

na elimu duni kwa mkoa. Kwa hiyo, tumelitizama kwa picha ya Mkoa mzima na baada ya hapo tutaenda *case to case* na kulinganisha jilografia ya wilaya yake ni kubwa hakika tutazingatia katika kutatua changamoto zilizo kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili anauliza Chuo cha Ualimu ambacho kilikuwa tayari kilishaanza kudaili wanafunzi kwa maana wanachuo lakini sasa hivi kilichotokea ni kwamba wamehamishwa na kipelekwa Dakawa. Ni vizuri majibu yakatolewa na mheshimiwa akaridhika naomba tukishamaliza Kipindi cha Maswali na Majibu ni vizuri tukawasiliana na Mheshimiwa Mbunge tukajuwa haswa tatizo ni nini. Kwa sababu ni azma ya Serikali kuhakikisha maeneo ya kujifunzia yanakuwa salama na tujuwe sababu ambayo imesababishwa mpaka wanachuo hao wakahamishwa kipelekwa Dakawa.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Nape na Mheshimiwa Kemi.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulinze swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za Mkoa wa Lindi kuboresha elimu yetu tulipitisha mwaka jana katika kilo moja ya korosho tukate shilingi 30 kwa ajili ya kuboresha elimu na kwa Halmashauri ya kwangu tulipata zaidi ya milioni 400 na jitihada hizi zilikuwa zinakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa wote tunajuwa hali iliyotokea kwenye korosho, nini mpango wa Serikali kuendeleza utaratibu mzuri amba tulikuwa tumeshauanzisha kwa sababu kwa hali iliyotokea kwenye korosho hatuwezi kuipata hii fedha, sasa huu utaratibu utasimama na tulishaanza kwenda vizuri?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu ya swali hilo kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niendele kumpongeza Mheshimiwa Nape, nimepita jimboni kwake kwa ujumla wake hamasa iliyo kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi inapokuja suala la kuchangia kwenye elimu siyo ya kutilia shaka hata kidogo. Na uamuzi huo wa busara ambao wananchi walikubaliana kuhakikisha kwamba kuna kiasi cha fedha ambacho kinakatwa kwa ajili ya kwenda kufanya mapinduzi makubwa ya elimu hakika sisi Serikali tutazingatia kwa sababu azma ni njema tutahakikisha. Ni vizuri Mheshimiwa Nape tusubiri najua kabisa natamani korosho zinunuliwe, Iakini ambacho tulichokubaliana kwa ajili ya kupeleka kwenye suala la maendeleo na elimu linatekelezwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kemilembe.

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada kubwa zilizofanywa na Serikali lakini kuna upungufu mkubwa sana wa walimu wa Sayansi nchini. Kwenye ripoti ya CAG ya mwaka 2017/2018 imeonesha Mkoa wa Mwanza, Jimbo la Buchosa kuna baadhi ya shule hakuna kabisa walimu wa sayansi na tunategemea wanafunzi wetu wa kidato cha pili wafanye mitihani yao fomu two na wafafulu.

Je, Serikali inamkakati gani wa kuongeza walimu wa sayansi ili iweze kupatikana katika shule zote nchini?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Walimu wa sayansi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba kuna upungufu mkubwa wa walimu wa masomo ya sayansi na chimbuko hili kwa ujumla ni tatizo ambalo limekuwa likiikabili dunia,

watoto wetu/vijana wamekuwa hawapendi kujifunza masomo ya sayansi. Mbunge atakuwa ni shahidi kwamba hivi karibuni tulikuwa tumetoa nafasi za ajira kwa ajili ya walimu wa sayansi tukijua kwamba kuna upungufu mkumbwa sana wa walimu hao na popote pale fursa inapopatikana tutahakikisha kwamba tunaongeza walimu wa sayansi kwa maana ya hisabati, fizikia na mengine ya namna hiyo ili watoto wetu wajifunze sayansi kwa sababu dunia ya leo bila kuwa na walimu wa sayansi hakika hatuwezi kushindana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ni mhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunakabiliana na changamoto hii kadri bajeti inavyoruhusu tutuhakikisha walimu wengi wanaajiriwa ili wakawafundishe watoto wetu.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea Waheshimiwa swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo na linaulizwa kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 56

Utaratibu wa Kutumia Vitambulisho Kukata Tiketi za Boti

MHE. MATTAR ALI SALUM aliuliza:-

Wananchi wa Tanzania Zanzibar wanaposafiri kwa kutumia boti hulazimika kuwa na vitambulisho ndio wauziwe tiketi. Hali hiyo huwa ni usumbufu mkubwa kwa wananchi.

Je, kwa nini Serikali isiondoke hitaji la kitambulisho kwa Mtanzania wakati wa kukata tiketi?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo. Namuona Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa watu wanaotaka kusafiri katika vyombo vya usafiri majini kuwa na vitambulisho wakati wa kukata tiketi na wakati wa kupanda chomboni ni utaratibu muhimu ambao unapaswa kuendelea kusimamiwa kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kulinda usalama wa abiria, mali, meli na uchafuzi wa mazingira. Aidha, ni wajibu wa nchi kama mwanachama wa Shirika la Bahari Duniani (*IMO*) kuzingatia viwango vya usalama wa abiria na ulinzi wa meli na bandai kwa mujibu wa Mikataba wa Kimataifa kuhusu Usalama wa Meli na Bandari (*International Ship and Port Facility Security (ISPS) Code*) ambao Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umeridhia na unasisitiza watu wote wanaoingia maeneo ya bandari yanayohusisha abiria wa ndani na wa kimataifa wajulikane kwa kuititia vitambulisho vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhakikisha uzingatiaji wa sheria na kanuni za nchi ambazo zimetafsii mahitaji ya Mikataba ya Kimataifa ilioridhiwa na nchi mwanachama. Kanuni mahsusizi litengenezwa chini ya Sheria ya Usafiri Majini. Kanuni hizi zinaelekeza kila mmiliki wa meli kutekeleza na kusimamia matakwa ya kuhakikisha taarifa za msingi zinazohusu watu waliomo ndani ya chombo zinachukuliwa na kuachwa bandarini kabla ya meli kuondoka. Aidha, taarifa hizo sahihi hupatikana kuititia vitambulisho vya abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwa kumbukumbu na takwimu sahihi za abiria wanaosafiri kwa vyombo vya majini ili kusaisia pindi itokeapo dharura. Taarifa hizo pia huhitajika

na taasisi zingine kulingana na mahitaji kama vile vyombo vya ulinzi na usalama, makampuni ya bima, Mamlaka ya Udhibiti Ulinzi na Usalama Majini, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari na taasisi nyinezo.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mattar.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa swali zuri ambalo amelijib, Mheshimiwa Waziri naomba kuhuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu wengi awana ni watanzani laini hawana vitambulisho ambavyo vinahitajika kusafiria na wanakosa fursa hii muhimu ya kusafiri. Je, Serikali inawaambia vipi wenye vyombo hivi vya usafiri ili hawa watu waweze kupata nafasi fursa hii kuitumia ili waweze kutumia katika kusafiri? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba wapo watu wengi ambao hawana vitambulisho, lakini ni wazi pia Serikali imechukuwa hatua ya kuweza kufanya usajili wa wananchi wake Bara na Visiwan. Nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya zoezi la usajili wa wananchi kukamilika huu usumbufu ambao unatokea hautatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitumie nafasi hii kuelekeza wamiliki wa vyombo kutokuwasumbua wananchi, kwa sababu ninatambua kwamba hatua kadhaa ambazo zinaweza zikafanyika pale ambapo mwananchi anakuwa hana kitambulisho ili uweze kumtambua na kutokumpa usumbufu wakati akisafiri. Kwa hiyo, nielekeze maeneo yote na sisi kama Serikali tutaendelea kufuatilia kuhakikisha wakati

Serikali inafanya juhudzi za kusajili wananchi wake basi hapawi na usumbufu pindi wananchi wanasafiri kutoka aidha Visiwani kuja Bara au kutoka Bara kwenda Visiwani.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kule Mafia huko Mheshimiwa Dau.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Meli (*TASAC*) imeweka utaratibu wa vyombo vya usafiri vinavyosafiri kati ya Nyamisati na Kilindoni, Mafia kupakia abiria 50 tu bila kujali ukubwa na uzito na uwezo wa chombo, jambo ambalo limepelekea kadha kubwa sana watu wengi kukosa nafasi na kulazimika kulala Nyamisati mpaka siku nne. Je, ni lini Serikali itavipanga vyombo hili kulingana na uwezo wake wa kubeba abiria badala ya kuweka *flat rate* kwa watu wote bila kujali uwezo wa chombo?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni mpongeze Mheshimiwa Mbunge anafuatilia sana hii hali ya usafiri wa kutoka Nyamisati kwenda Mafia, nafikiri pia Mheshimiwa Mbunge upo na swali lako tutajibu siku za hivi karibuni tutatoa maelezo ya kutosha. Lakini niseme tu kwamba kama kuna usumbufu ambao labda kufanya wananchi wachache wengine wabaki kwenye maeneo la Nyamisati itabidi tuliangalie kwa macho mawili ili kuondoa usumbufu. Wakati ule utaratibu wakuwa na nakujenga chombo cha kuwasafirisha wananchi wa kutoka Nyamisati kwenda Kilindoni Mafia na kutoka Mafia kurudi huku Nyamisati wakati harakati za ujenzi wa chombo unaendelea wakati unachukuwa muda kidogo huu usumbufu tuweze kuuondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalizungumza nipate kwa ufasaha namna ilivyo tuweze kuchukua hatua ili huu usumbufu tuweze kuondoa wakati tunajenga chombo kingine.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tupo nyuma ya muda, tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu linaendelea kuulizwa kwa Wizara hiyo hiyo ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 57

Ujenzi wa Barabara ya Mpanda – Kahama

MHE: JOHN P. KADUTU aliuza:-

Kumekuwepo na ahadi ya ujenzi wa barabara kutoka Mpanda kwenda Kahama kupitia Kaliua, Uyowa, Ulyankulu na Ushetu, inavyoonekana mpango huu utachukua muda mrefu sana.

(a) Je, Serikali ipo tayari kuitengeneza kwa kiwango cha molamu hasa kipande cha kutoka Kaliua, Uyowa hadi eneo la Makazi Barabaa ya 13?

(b) Je, Serikali ina mpango gani kuimarisha barabara ya kutoka Tabora kwenda Ulyankulu, Kahama hasa ikizingatiwa kwamba barabara hizi ni muhimu kwa uchumi wa nchi kutokana na uzalishaji wa tumbaku na mazao ya chakula katika eneo hilo?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) inaendelea na kazi ya upembizi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mpanda - Ugalla – Kaliua – Ulyankulu – Kashihii - Ushetu – Kahama yenye urefu wa kilometra 428 ikihusisha na usanifu wa Daraja la Ugalla ambapo kiasi cha shilingi milioni 912.979 kimetengwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019 kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa, Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya matengenezo ya aina mbalimbali ya barabara hizi ili ziweze kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ikitenga kiasi cha shilingi bilioni 1,390.083 na katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali ikitenga shilingi bilioni 1.238 kwa ajili ya matengenezo ya aina mbalimbali ya barabara ya Kaliua, Uyowa hadi Makazi kwa kiwango cha changarawe. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shilingi bilioni 1,361.97 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Kashishi-Ulyankulu-Kaliua hadi Lumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha za matengenezo ya aina mbalimbali kila mwaka kwa barabara ya Tabora-Ulyankulu ili iweze kupitika majira yote ya mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ikitenga kiasi cha shilingi milioni 232.840 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe na katika mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 2,263.889 kwa ajili matengenezo ya aina mbalimbali pamoja na ujenzi wa kilometra 2.5 wa sehemu ya barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Kadutu.

MHE. JOHN P. KADUTU: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Je, lini kazi hii ya upembuzi na usanifu itakamilika kwa barabara hiyo ambayo sehemu kubwa upande wa pili wa Mpanda kabla ya Ugalla ni misitu mikubwa?

(ii) Kwa kuwa mvua zimeanza kunyesha Jimboni Ulyankulu na kwa kuwa barabara si nzuri, pamoja na Serikali kutenga pesa hizo, lini matengenezo hayo yataanza? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi kama nilivyojibu katika majibu yangu ya swali la msingi kwamba kazi hii inaendelea na nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia barabara hii muhimu kwa sababu eneo hili la Ulyankulu linazalisha mazao mbalimbali, lakini pia masoko yao wanaweza kuyapata kwenye Mkoa wa Shinyanga, Mkoa ya Geita na hii barabara imekuwa muhimu sana katika eneo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi ya upembuzi yakinifu inaendelea kukamilika na hatua za manunuzi nikuombe uvute subira kwamba tunaweka msukumo mkubwa ili usanifu tuweze kupata gharama halisi za ujenzi wa barabara ili Serikali iweze kupata fedha za kuweza kujenga barabara hii.

Kwa hiyo, nikuombe uvute subira saa nyingine/hata baadaye tunaweza kuzungumza ili tuone wataalam wamefikia hatua nzuri na lini watakamilisha hili wakati mwingine wanaweza wakawa na na majibu mazuri kwa wananchi wa Ulyankulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu (b) ni kwamba kweli kipindi cha mvua kinakaribia na barbara hali sio nzuri kwanza niseme barabara hii aliyouliza katika eneo la Ugalla kazi ya kukamilisha michoro ya ujenzi wa daraja imeshakamilika tunatafuta fedha ili tuweze kujenga lengo barabara hii iweze kupitika. Lakini pia tumejiandaa zipo hatua mbalimbali za manunuzi kuhakikisha tunaiboresha barabara hii zipo hatua za mwisho fedha zipo, Bunge lako lilitengeta fedha tutahakikisha kwamba tunasimamia maeneo korofi kuhakikisha kwamba yanapitika wakati hatua za kuiboresha barabara hii katika kiwango cha lami kinaendelea.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Amar.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi illi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alipofanya ziara mkaao wetu wa Iringa alizindua barabara ya *Greet North Road* inayotoka Cape Town kwenda Cairo na kuahidi kujenga kwa lami mchepuo ili kuchepusha magari makubwa sana yanayopita pita katikati ya mji ambayo yanahatarisha sana wananchi wa Mkoa wa Iringa. Je, lini ahadi hiyo itatimia?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi Na Mawasiliano Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu muda mrefu amefuatilia sana fidia za wananchi ambapo barabara hii ya mchepuo itapita, mara nyingi amezungumza juu barabara hii. Lakini niseme namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa sababu katika eneo hili bararaba inapopita tumelipa fidia za wananchi wote ambao walikuwa wanahitaji, ili kuwa jambo muhimu sana ili ujenzi wa barabara uweze kuanza kujengwa na hata muda

tuliota wa ziada kwa wananchi kujitokeza kama kuna shida yoyote ya malipo yao hajajitokeza mwananchi ambaye amekuwa na malalamiko kuonyesha kwamba Serikali imewatenda haki wananchi imewalipa fidia eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge zile hatua za ujenzi sasa zinaendelea, kama unavyojuu hatua za ununu zi zinaendelea, wakati wowote ujenzi wa barabara hii muhimu ya mchepuo ambayo itaondoa usumbufu mkubwa wa magari yaliyokuwa yanapita katika mji wa Iringa tutakuwa tumeuondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tupo hatua nzuri niwahakikishie wananchi Iringa na Mheshimiwa Mbunge kwamba harakati zinaenda vizuri na ni mshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wakati wa ziara yake kama ulivyojema Mbunge alitoa maelekezo ili fedha ipatikane kwa ajili ya ujenzi wa mchepuo huu. Kwa hiyo, usiwe na wasawasi wakati wowote tutaingia kazini kuhakikisha mchepuo huu unakamilisha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hussein.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa makao Makuu ya Wilaya Nyang'hwale ipo Karumwa na Karumwa ni barabara moja tu na kuna msongamo mkubwa wa magari ambayo yanapita pale zaidi ya magari 200 kwa kutwa lakini vumbi linatimka sana.

Je, Serikali ipo tayari kutujengea kilometra mbili za lami ili kuweza kupunguza hatari ya maambukizi kama vile *TB* kutokana vumbi?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nailbu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatalia sana hii barabara hasa hasa hii barabara ambayo inaweza kuunga mpaka Kashishi. Juzi na nimejibu hapa Mheshimiwa Mwenyekiti kile kipande kingine cha kuwaunga wananchi wa Nyang'hwale na makao makuu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme juhudhi za Mheshimiwa Mbunge amekuwa akizifanya muda mrefu ametuwezesha kujenga Kama kilometra 4.2 kupunguza hii aina ya kadha ambayo anaizungumza juu ya vumbi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge unafahamu tumeanza kujenga maeneo yamekuwa na usumbufu tumepata kilometra 4.2 kwa hiyo nikuhakikishie tutalizama vizuri tukipata fedha hizi kilometra 2 ambazo amezungumza Mheshimiwa Mbunge wala usiwe na wasiwasi tutaondoa hili vumbi lakini kutoa usumbufu ambao wananchi wanaupata katikati ya mji hasa hasa eneo hili ambalo umelitaja la Karumwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge muda wetu sio rafiki, tunaendelea na swali linalofuata kwa Wizara hiyo hiyo ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba.

Na. 58

Ujenzi wa Barabara ya Mtwara - Newala – Masasi

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA aliuza:-

Barabara ya Mtwara - Newala - Masasi imetengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kilometra 50 kwa kiwango cha lami kutoka Mtwara hadi Mnivata.

Je, ni lini ujenzi huo utaanza?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) ilmekamilisha kazi ya upembizi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujezi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mtwara - Masasi-Newala yenye urefu wa kwa kilometra 210 ikiwemo na Daraja la Mwiti tangu mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali impanga kuijenga barabara hili kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza ni sehemu ya barabara ya Mtwara - Mnivata (kilometra 50) ambapo ujenzi wake ulianza tarehe 17 Aprili, 2017 na unategemewa kukamilika tarehe 17 Januari, 2019 kwa gharama ya shilingi 89,591,000,000.08. Aidha, Serikali imeendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ujenzi wa barabara hiyo ambapo katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga kiasi cha shilingi 10,000,000,000.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya barabara iliyobaki ya kuanza Mnivata - Newala hadi Masasi yenye urefu wa kilometra 160 itajengwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Mhemimiwa Chikota.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti Asante kwa kunipa nafasi pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Ni kweli ujenzi umeshaanza lakini ni ahadi ya ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi na viongozi wakuu wa Serikali kwamba kutakuwa na wakandarasi zaidi ya mmoja.

Kwa hiyo, napenda kupata kauli ya Serikali je, ni lini ujenzi awamu ya pili kutoka Mnivata kwenda Tandahimba – Newala hadi Masasi ujenzi huu utaanza?

Swali la pili ni kuwa Mkandarasi anayejenga kutoka Mtwara hadi Mnivata *speed* yake ya kusuasua na sababu kubwa ni kwamba hajalipwa, je, nini ningependa kupata kauli ya Serikali nini kimefanyika kwa mkandarasi huyo ameshalipwa malipo yake?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Elias Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza uniruhusu nimpongeze Mheshimiwa Chikota kwa namna anavyoshirikiana na sisi kwa sababu nilivyotembelea kuona ujenzi wa barabara hii kutwa nzima nilifanya naye kazi na mambo mengi alitoa ushauri tunaendelea kuyazingatia kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikupongeze sana na endelea na moyo huo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuijenga barabara hii mpaka Masasi unaendelea na kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge barabara hii utekelezaji wake uko kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi, lakini pia ahadi ya Mheshimiwa Rais na sisi tunatambua kwamba ile kiu iliyopo kwa wananchi kuweza kuwasaidia kwa sababu hii barabara ndefu sana imekuwa na usumbufu mkubwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Chikota usiwe na wasiwasi sisi tunaendelea kutafuata fedha pale tutakapokuwa tumepata fedha tutaweza kwenda kufanya awamu nyingine ya pili ili tuweza kuendelea kupunguza urefu wa hii barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme ziko hatua mbalimbali zinachukuliwa ili yale maeneo yaliyokuwa korofituhakikisha kwamba tumeyaboresha. Yapo maeneo yana mpangilio ya milima ambayo kuna miteremko mikali na kona kali Mheshimiwa Mbunge utakubaliana na mimi tuliona na

tumepata fedha kwa ajili ya kuboresha maeneo hayo. Wakati tunaendelea kuongeza awamu nyingine kwenye ujenzi wa barabara hii lakini maeneo yote korofii ikiwepo sehemu ambazo ni hatari za madaja tuanendelea kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine amezungumza juu ya *speedya* mkandarasi ambaye najenga barabara ya Mtwara Mnivata. Sisi kama Wizara tumeendelea kufanya ufuutiliaji mzuri ili kuhakisha kwamba matatizo ya mkandarasi yanaondoka kwa sababu sio suala la fedha peke yake kulikuwa na uzembe fulani unatokea pale, kwamba wakati mkandarasi kila akiwasilisha *certificate* alikuwa analipwa lakini ilikuwa haiendani na kasi ya malipo anayolipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona asilimia kwa mujibuwa ujenzi kwenye malipo ilikuwa kubwa kuliko kazi yenye, kwa hiyo tunaendelea kulisimamia hilli na hivi karibu Mheshimiwa Waziri alipita eneo lile ili kuhakisha kwamba tunaweka msukumo wa kipekee barabara hii iweze kukamilika hizi kilometra 50 na sisi tutahakikisha kwamba katika kipindi ambacho mkataba unasema hapatakuwa na sababu ambazo sio za msingi za kucheleshwa ujenzi wa barabara hiyo.

Kwa hiyo, niendelee tu kutoa maelekezo na kumuonya mkandarasi asitafute sababu. Sisi tunaendelea kumlipa kadri *certificate* zinavyokuja, barabara hii wananchi wanaisubiri aongeze kasi na kila wakati tutaendelea kuangalia eneo hili kuhakisha kwamba kazi inaendana na ulipwaji wake fedha.

MWENYEKITI: Ahsante, napenda majibu ya nyongeza yawe mafupi na maswali yawe mafupi, ili wengine wape nafasi ya kuuliza na mimi sitaongea sana. Mheshimiwa Chegeni halafu Mheshimiwa Tunza Malapo.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kazi ambazo Wizara hii ya Ujenzi inafanya, Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga barabara

kwa kiwango cha lami barabara ya Nyashimo - Ngasamo - Dutwa ambapo vilevile ndipo jimboni kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua utekelezaji wa barabara hii unategeme kuanza lini?

MWENYEKITI: Ahsante jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na uchukuzi na Mawasiliano. Tena unihakikishie maana na mimi ni huko huko.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chegeni amekuwa akiifuatilia sana barabara hii ya Nyashimo kwenda Dutwa na nafahamu na hivi karibuni una swali ambalo umeuliza juu barabara hii na barabara zingine. Nikuhakikishie ni dhamira yetu kama Serikali kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais, lakini ni dhamira yetu kutekeleza pia maelekezo ya llani ya Chama cha Mapinduzi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ni lini hasa tarehe ziwezi kuitaja, Mheshimiwa Mbunge nikuombe saa nytingine hata baadae tuanaweza tukateta nitafute taarifa za kina ili na wewe utakapokuwa ukiwapa maelezo wananchi wa jimboni kwako ili angalau tuwe na *data* za uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe kuwa tutateta ili tuweze kuona hasa hasa kwenye mpango mkakati wetu tumeiweka namna gani, lakini kikubwa ahadi za Mheshimiwa Rais tunaendelea kuzitekeleza kama nilivyosema hivi karibuni kwamba zipo ahadi ni nydingi, zipo nydingi ambazo ambazo tumeshazitengeleza kwa asilimia mia moja, ziko zingine zipo na hatua kadhaa za utekelezaji na zipo zingine zipo kwenye hatua za awali. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tuonane ili niweze angalau kuzungumza tuone kwa usahihi hali ya barabara ya Nyashimo kwenda Dutwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tunza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuruku hicho kipande zha kutoka Mtwara mpaka

Mnivata cha kilometra 50 ukisoma huku kwenyu mpango ni asilimia 30 ndio imejengwa na Mheshimiwa Waziri anasema itakamilika mwaka 2019. Nataka kujua kama imeanza kujengwa 2017 mpaka leo ni 30% mpaka Januari 2019 ni muujiza gani wanataka kuutumia ili hiyo barabara iwe imejengwa?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika utekelezaji wa bajeti ambayo tumeendelea kuizungumza imeonyesha kwamba bararaba hii iko 30%. Lakini ni kweli katika jibu langu kwa mujibu wa mkataba barabara hii iwe imekalimika hapo mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taratibu za namna tunavyoweza ku-*manage* mkataba ndio maana kama nilivyojibu katika jibu langu la nyongeza kwa Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali lake la msingi, nimesema kwamba Mheshimiwa Waziri alitembelea eneo hili hivi karibu kwa lengo la kuangalia sasa hiyo miujiza yaani kwa maana zipo taratibu ambazo tunazitazama kama ilivyo katika sheria.

Kwa hiyo, kama italazimika saa nyingine kumuomba Mkandarasi aweke *sub contract* pale ili kuahikisha barabara hii inakwenda kwa kasi iweze kwenda. Lakini kifupi ni kwamba kwa mujibu wa sheria na taratibu tunaendelea kuhakikisha lile jambo ambalo lilichelewesa kama litakuwa liko *aligned* na sheria linakubalika tutakuja na marekebisho kama ilivyo katika taratibu zilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutamjulisha Mheshimiwa Mbunge pale kama marekebisho tutayafanya kwa mujibu wa taratibu kwamba ni dhahiri hii barabara itakamilishwa kama kimsingi sisi kama Serikali hatutaruhusu sababu ambazo sio za msingi za kucheleshwa ujenzi wa barabara.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yahaya Massare.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniapa nafasi hii na mimi niulize swali la nyongeza. Matatizo yaliyopo huko barabara ya Mtwara - Newala - Masasi yanafanana na kabisa na barabara ya Mkiwa - Itigi hadi Noranga kilometra 56.9 ambazo Serikali imeahidi kuzijenga kwa kiwango cha lami. Je, ni lini sasa mradi huu utaanza?

MWENYEKITI: Ahsante. Ni lini mradi huo kutoka Mkiwa utaanza.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu ujenzi harakati za ujenzi wa barabara hii, kutoka Mkiwa - Itigi - Noranga zimekwishaanza, Mheshimiwa Mbunge anafahamu tumezungumza mara nyingi kwamba tuko kwenye hatua ya manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba watakapokamilisha hatua za kutengeneza mikataba kipande hiki cha barabara kitaanza. Lakini niseme tumeshaanza kuunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Mbeya na Mheshimiwa Mbunge anajua kwamba tumekuwa na mpango wa baadhi ya maeneo tumeshaanza kujenga. Kwa hiyo, kuna ule upande wa Mbeya kuja Itigi tunaendelea kujenga, lakini na upande wa kutoka Itigi kwenda Mbeya tunaendelea kujenga. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba uvute subira lakini muda wowote mkataba utasainiwa kazi ya ujenzi wa kipande hiki cha barabara Mkiwa -Itigi - Noranga utaanza.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Martha Mlata atafuatiwa na Mheshimiwa Nsanzugwanko.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti asante, nilikuwa napenda tu kumuuliza Naibu Waziri kwamba wananchi wanaotumia barabara ya Sipuka kutoka Singida - Ndago hadi Kizaga wamesubiri sana hiyo ahadi kwamba

mnatafuta mkandarasi kwa ajili ya kwenda kuanza kuweka lami.

Sasa naomba uwape jibu maana hawana taarifa nini kinaendelea, hiyo barabara inaanza kujengwa lini kwa kiwango cha lami? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ni lini tu mtapata fedha muanze kujenga.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mlata nikupongeze sana kwa sababu barabara hii muhimu sana umekuwa ukifatilia maana yake ulikuwa kila wakati anazungumza juu ya ujenzi wa Daraja la Sibiti. Niseme tu kwamba tunatafuta fedha, tukipata fedha ujenzi wa kipande hiki utaanza ili kutuunganisha na eneo hili la Daraja la Sibiti. Lakini kitu kizuri ambacho niwafahamishe wananchi na Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba baada ya Rais kutuwekea jiwe la msingi katika ujenzi wa Daraja la Sibiti ambao ni sehemu ya muunganiko wa barabara ya Mheshimiwa Mbunge unauliza, kwamba sasa tuna kilometra 25 ambazo zitaongezwa pale ili sehemu korofii yote tuwe na kipande cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizi ndio taarifa mpya Mheshimiwa Mbunge uzichukue ili wananchi wajue kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha sasa wananchi wa Singida tunawaunganisha na Mikoa ya Simiyu, Shinyanga na Mwanza kuititia katika daraja la Sibiti ikiwa barabara hii muhimu ya kutoka Sepuka- Ndago- Kizaga...

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani barabara anayouliza ni hii ambayo inapita kuja kwenye Jimbo la Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, tunaendelea na usanifu wa barabaa hii, aniwie radhi, nilikuwa nafikiri barabara amekuwa akiipigia kelele muda mrefu, tunaendelea na usanifu tutafanya usanifu wa barabara hii, Bunge hili limepitisha shilingi milioni 200 kwa ajili usanifu wa kipande hiki cha

barabara. Kwa hiyo, barabara hii baada ya usanifu tu Mheshimiwa Mbunge tutajenga barabara hii, ili tuweze kutoka eneo hili la Kizaga na mimi barabara hii niliitembelea kuiona usumbufu wananchi walipata wakati wa mvua.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Nsanzugwanko.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nilikuwa naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri barabara ya Uvinza - Maragarasi Darajani ina fedha za *Kuwait Fund* na huu ni mwezi wa tano tangu fedha hizo zinakaa hazina, ni kwa nini barabara hiyo hajaanza kujengwa?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS JOHN KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha za Kuwait zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ili sasa tuweze kuiunganisha vizuri Mkoa wa Kigoma na Mkao wa Tabora, na ni kweli fedha zipo, lakini tulichelewa kwa sababu ya zile *logistic* za upande wa *handling* ya VAT baada ya mabadiliko ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sasa baada ya maelekezo na taratibu kukamilika wakati wowote kwamba ujenzi utaanza, lakini na unafahamu hata kile kipande ambacho hatukuwa na fedha, utaratibu wake wa kutangaza kazi kwa maana ile barabara sasa kutoka Tabora mpaka Kigoma tunaikamilisha ili iungane na kile kipande kinachokutoa wewe kutoka Kidahwe kwenda Kasulu, tunakwenda mpaka Nyakanazi.

Kwa hiyo, barabara yote hiyo iko na *commitment*, jambo zuri niliseme ili wananchi wa Kigoma wafahamu sasa hii barabara muda mrefu umekuwa na kiu sasa dawa yake imepatikana.

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani na linaulizwa kwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Na. 59

Vigezo Vinavyotumika Kuajiri Vijana wa Jeshini

MHE. HAMAD SALIM MAALIM aliuliza:-

Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) ni Jeshi linalojumuisha sehemu mbili za Muungano.

Je, ni vigezo gani vinavyotumika kuajiri vijana wa Jeshi la Ulinzi la Tanzania?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vinavyotumika kuajiri vijana katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ni kwa mujibu wa Kanuni ya 5.01 ya Kanuni za Majeshi ya Ulinzi, Juzuu ya Kwanza (Utawala) kifungu cha kwanza kinachoelezea kuhusu sifa za kuandikishwa na sifa hizo ni hizi zifuatazo:-

- (i) Awe raia wa Tanzania;
- (ii) Asiwe mwanachama wa chama chochote cha siasa;
- (iii) Awe na tabia nzuri;

- (iv) Awe na umri usiopungua miaka 18; na
- (v) Kutimiza masharti mengine yote ambayo Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi anaweza kuyatoa.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Hamad Salim Maalim.

MHE. HAMAD SALIM MAALIM: Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, Mheshimiwa Waziri amesema hapa kwamba vigezo vinavyotumika ni vitano hivi, katika vigezo hivi hakuna kigezo kwamba kijana lazima awe amepitia JKT au kule kwetu Zanzibar awe amepitia JKU, je, kigezo hiki hakimo katika kuwateua vijana kuingia katika Jeshi?

Swali la pili, katika vigezo alivyovitaja alisema kwamba asiwe mwanachama wa chama chochote cha siasa, lakini kule kwetu Zanzibar au Pemba hususan Pemba vijana wetu wapokwenda kufanya usaili wa Jeshi hudaiwa kadi za chama, je, wanaofanya hivi ni kosa? Ahsante. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi na Kujenga Taifa.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyeekiti, kuhusu kigezo cha kwamba kijana awe amepita JKT au JKU hicho ni kigezo kipyta, ile Kanuni niliyoisoma ni Kanuni ambazo zimebekwa miaka mingi iliyoita. Lakini hivi karibuni tumeamua kwa makusudi kwamba vijana wote ambao watakuwa wanaajiriwa katika majeshi yetu wawe wamepitia JKT au JKU.

Kwa hiyo, hicho kigezo kipyta kipo na ndivyo tunavyofanya na sio Jeshi peke yake ni vyombo vyote vyaa Ulinzi na Usalama wanalahizimka sasa kuajiri vijana walipopita JKT au JKU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili kwamba kigezo kinasema asiwe mwanachama na huko Pemba watu huwa wanadaiwa kadi, hili sina uthibitisho nalo, na kama Mheshimiwa anao ushahidi ateletee lakini sisi katika vigezo vyetu hili la Uanachama inavyotakiwa hasa asiwe mwanachama wa chama chochote.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Na. 60

Ujenzi wa Soko la Kimataifa Katavi

MHE. SALOME W. MAKAMBA (K.n.y. MHE. RHODA E. KUNCHELA) aliuliza:-

Je, ni lini mradi wa ujenzi wa Soko la Kimataifa utaanza katika Mkoa wa Katavi?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara namuona Mheshimiwa Anthony Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za awali za ujenzi wa soko la Kimkakati linalotegemewa kujengwa katika Mkoa wa Katavi umekwishaanza kwa kutambua eneo na Wananchi wanaoishi katika eneo husika ambao wameridhia kupisha ujenzi wa soko hilo. Hatua inayofuata ni Serikali kulipa fidia kwa wananchi baada ya kufanya tathmini ya eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi milioni 44 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa andiko la mradi kwa ajili ya kuomba fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo linalotegemewa kujengwa soko linazungumziwa lipo katika Halmashuri ya Wilaya Mpanda, Tarafa ya Karema, Kata ya Karema, Kijiji cha Itetemya katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Katavi wafanyabiashara hasa wa Soko la Busogwe, Soko Kuu na Soko la Mpanda Hoteli wanasumbuliwa sana kutozwa kodi na kulazimishwa kusaini mikataba. Serikali ina Mpango gani kwenda kuhakikisha wafanyabiashara hawa amba ni walipa kodi wanakuwa katika mazingira mazuri ya kufanya biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili changamoto iliyoko Mpanda iko pia katika halmashauri ya Mji wa Kahama ambapo wafanyabiashara wamehamishiwa katika Soko la Dodoma. Lakini Soko lile lina miundombinu hafifu hakuna barabara, hakuna umeme, wanashindwa kufanya kazi zao na wanapoteza pesa nyingi na kodi kwa Taifa. Serikali ina mpango gani kuboresha mazingira ya Soko la Dodoma ili wafanyabiashara waweze kufanya kazi na kuingiza pato Taifa? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa kifupi kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali

kuhakikisha inaweka mazingira wezeshi na rafiki kwa wafanyabiashara kufanya biashara zao pasipo vikwazo vyovyyote. Kwa mazungumzo aliyosema Mheshimiwa Mbunge, kama Serikali tutayafanya kazi na kuyafatilia. Lakini pia nitoe rai katika Mabaraza ya Biashara na Mkoo na Wilaya husika waweze kufatilia na kutatua changamoto hiyo ambayo iko ndani mkoa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la soko la Dodoma, ni kweli Halimashauri imetenga eneo ambalo limewaweka wafanyabiashara wadogo wadogo katika eneo ambalo linaitwa Dodoma na hivi sasa kwa mujibu wa maelekezo ya Mkuu wa Mkoo nguvu zote zinaelekezwa katika eneo hilo ili kuliwekea miundombinu rafiki na pia kuwafanya wananchi wote wa eneo hilo waende kununua bidhaa katika Soko la Dodoma ili kulijengea uwezo na kuongeza idadi kubwa ya wateja.

Kwa hiyo, mpango wa Serikali hivi sasa ni kuhakikisha kwamba eneo hili linabobereshwa kupeleka miundombinu rafiki pamoja na nishati ya umeme, lakini vilevile kuweka utaratibu kwamba wanunuzi wote wa bidhaa mbalimbali waende katika eneo la Dodoma kwa ajili ya kupata mahitaji yao, ndio mpango wa kukuza soko hilo la Dodoma katika Kahama.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gashaza.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swalii la nyongeza. Katika Jimbo langu la Ngara upo mradi wa ujenzi wa Soko Mkakati eneo la Nzanza, Kata ya Kabanga ambalo Soko hili lilitakiwa kukamilika mwaka 2014, lakini mpaka sasa hivi limetelekezwa linazidi kuchakaa gharama za ujenzi zinazidi kuongezeka. Je, ni lini Serikali itawenza kukamilisha soko hili muhimu ambalo ni muhimu kwa wakulima na wafanyabiashara wa Jimbo la Ngara?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkoo, Mheshimiwa Anthony Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali kuona masoko yote na miundombinu yote inakamilika ili shughuli za wafanyabiashara wanaotumia masoko yale ianze mara moja. Nimuhidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kulifatilia ili kazi hii ikamilike mapema na wananchi wa Ngara wanufaike na ujenzi wa soko hilo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona naomba niulize swali moja, na kushukuru Serikali kujenga Soko la Kimataifa Hanang pale Endagau na vilevile kwa Mheshimiwa Jenista kutembelea soko lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua kwamba kama Serikali itaona umuhimu wa kujenga miundombinu yote hasa mizani ya kupima mazao kusudi soko lile lifanye vizuri kwa sababu limezungukwa na maeneo mengi ambayo yanalima nafaka kwa wingi na kwa tija iliyo kubwa? Ahsante.

MWENYEKITI: Haya ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri ya Mkuu, Mheshimiwa Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Soko hilo limetekelezwa chini ya mradi wa *MIVARF* chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge soko hilo lina maana kubwa kwa wakazi wa Hanang na kama Serikali itaendelea kuboresha mazingira ili hayo mahitaji ya Mheshimiwa Mbunge ya kuongeza miundombinu ya ziada yaweze kukamilika na Wananchi wafuarahie uwepo wa soko hilo. Kwa hiyo, nimuhidi tu kwamba kama Serikali tunaona umuhimu wa kufanya hivyo na kazi hiyo iko njiani itatekelezeka.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawasihi tena tuko kazini, unaposhauriana mshauriane kwa sauti ya chini na humu ndani tunataka tusikilize majibu yanayotolewa na Serikali. Nilitaka kumuuliza Mbunge mmoja yaliyosemwa na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi atuambie kwa kifupi majibu yalikuwa ni nini, maana naona walikuwa *busy* na mambo mengine, tunaendelea.

Swali linalofuata ni kwa Wizara hiyo hiyo, linaulizwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia Mbunge wa Mtwara Vijijini, samahani sana Mheshimiwa.

Na. 61

Mkakati wa Kuendeleza Viwanda

MHE. HAWA A. GHASIA aliuliza:-

Je, kuna makakati gani wa kuendeleza viwanda katika Mji wa Mtwara na Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara?

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri kwa niaba.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya Serikali kwa sasa ni kuhakikisha kuwa malighafi zinazopatikana kila mkoa zinaongezwa thamani kabla ya kuuzwa yakiwemo mazao ya kilimo. Hivyo Wizara yangu imekuwa ikihamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda katika maeneo ambayo malighafi za kutosha zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mkoa wa Mtwara, Mkakati wa Serikali ni kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika fursa zilizopo Mtwara zikiwepo uongezaji wa thamani gesi asilia, korosho, ufuta na mengine. Kuhusu uongezaji thamani gesi asilia inayopatikana Mtwara, Serikali imehamasisha uwekezaji katika Kiwanda cha Mbolea kitakachojengwa eneo la Msanga Mkoo, Mtwara Mikindani kinachosubiriwa sasa ni kufikiwa makubaliano ya bei ya gesi asilia kati ya Serikali na Wawekezaji wa mbolea. Aidha, Serikali inaendelea kufatilia viwanda vyote vilivyobinafsishwa vilivyopo Mkoani Mtwara ili kuhakikisha vinafanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia mamlaka ya EPZ inahamasisha uwekezaji katika maeneo maalum ya Uwekezaji, juhudzi za pamoja za kuboresha mazingira katika eneo la *Mtwara Free Port* kwa kujenga miundombinu ikiwemo ya barabara na umeme unatosheleza ili kuvutia wawekezaji zinaendelea. Naamini Mheshimiwa Mbunge atashirikiana na wizara na halmashauri yake katika kutafuta wawekezaji hao kupitia makongamano ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kuwapongeza Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa juhudzi wanazozifanya kwenye kuhamasisha uwekezaji wa viwanda katika mikoa yao.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kwanza kufanya masahihisho, Msanga Mkoo haipo Mtwara Mikindani, Msanga Mkoo iko Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara na Mbunge wake ni Hawa Abdulrahman Ghasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili ni mara kama ya tatu najibowi ndani ya Bunge na kuhusu suala la Kiwanda cha Mbolea tangu mwaka 2012 majadiliano na mwekezaji yanaendelea na kiwanda hicho Halmashauri za Mtwara

pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara kipindi hicho walishirikiana kumtafuta mwekezaji huyu. Sasaje, majadiliano hayo ambayo yamechukua zaidi ya miaka minne yanategemea kukamilika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na swali la pili, kitendo cha kuchukua muda mrefu kukamilisha majadiliano ambayo Halmashauri za Mkoa wa Mtwara zillijiweka pamoja na kutafuta mwekezaji na kuingia naye ubia hayajakamiliika, hamuoni kama mna tukatisha tamaa ya kuweza kutafuta wawekezaji wengine?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali, Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ya msingi katika swali la Mheshimiwa Hawa Ghasia. Nimpongeze Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa kweli katika ufuatiliaji wake tangu mwaka 2012 katika suala hili la Kiwanda cha *Petrochemical*/na Mbolea kule Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na maswali yake mawili ya nyongeza ningependa kumpa ufanuzi mfupi sana Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa heshima ya wananchi wa Mtwara pia.

Kwanza pamoja na kumpongeza, ni lini taratibu za majadiliano zitakwisha? Kwanza ningependa kumpa taarifa Mheshimiwa Hawa Ghasia kwamba maendeleo yanakwenda vizuri sana, kilichochelewesha ni kwamba tangu mwaka 2013 kampuni nyeza ambayo ni *Ferostal* ambao wanafanya biashara inayofanana walikuwa kimsingi wameingia makubaliano na Serikali kupitia *TPDC* kwa bei ambayo ilikuwa dola 3.83 lakini baadae waliona kwa upande wa kibiashara haiwalipi.

Kwa hiyo, wakaomba wapunguziwe kwa kuwekewa ruzuku ya Serikali na ndiyo mambo ambayo sasa bado tunaendelea kujadiliana nao wawekezaji wa *Ferostal*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wawekezaji wa Helium ambao wapo Mtwara kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, wao wanatazamia sasa tukishakamilisha majadiliano pamoja na *Ferostal* nao sasa watatumia hiyo kama mfano wa kuendelea na majadiliano yao kati yao na Serikali. Kwa hiyo, tunakwenda vizuri Mheshimiwa Hawa Ghasia, mara baada ya kukamilisha uwekezaji huu utaendelea katika Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala lake la pili kwamba imechukua muda mrefu na inaweza ikakatisha tamaa wananchi wa Mtwara. Kwanza, nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze, mazingira ya uwekezaji katika Mji wa Mtwara na Lindi kwa sasa hivi ni mazuri sana hasa baada ya kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa kutoka Dar es Salaam mpaka Lindi na Mtwara tangu mwezi Mei.

Kwa hiyo, wawekezaji wengi wanaendelea kuja na hivi viwanda viwili kwa sababu tunaendelea na majadiliano, ni matarajio yetu yatafikiwa muafaka na wananchi wa Mtwara wataendelea kuwekeza zaidi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa *Engineer Chiza*.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa Serikali imeweka mbegu za mafuta na hususan mchikichi katika mazao ya kipaumbele katika Taifa letu na kwa kuwa katika Mkoa wa Kigoma sasa hata misa inayotumika katika viwanda vyta kutengeneza sabuni nyingine inatoka nchi jirani ya Burundi.

Je, sasa Serikali imejipangaje kuanzisha viwanda vyta kuchakata zao hilo la chikichi katika Mkoa wa Kigoma hususan katika Wilaya za Kakonko, Kibondo, Kasulu na Kigoma yenye?

(*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, ahsante Mheshimiwa Dkt. Kalemani Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Chiza katika kuuliza swali la kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya viwanda vyta mchikichi Kigoma na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu Halmashauri za Kigoma, Kasulu na nyingine katika Mkoa wa Kigoma zimeshatenga maeneo kwa ajili ya viwanda mahususi hasa katika zao la michikichi. Tulipokwenda kuzindua miradi ya umeme waliainisha maeneo na tayari tumeshaanza kufanya survey maeneo ya viwanda ili sasa viwanda vyta mchikichi katika maeneo ya Kigoma waweze kuwekeza kwa urahisi zaidi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zainab Mndolwa.

MHE. ZAINAB A. MNDOLWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenyewe viwanda wanaotengeneza vinywaji baridi (*soft drinks*) mfano Cocacola, Sayona na Azam hutumia sukari maarufu *industrial sugar* na sukari hiyo huagizwa nchi za nje.

Je, ni lini Serikali itaaniszha kiwanda ambacho kitazalisha sukari hiyo hapa hapa nchini kuliko kuagiza nchi za nje? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Mavunde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali moja ya mikakati ambayo tunaendelea kuifanya kazi hivi sasa ni

uhamasishaji mkubwa na kuvijengea uwezo viwanda nya ndani kwa ajili ya uzalishaji wa sukari. Ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba viwanda vyetu nya ndani vingi vinakuwa na *capacity* kubwa ya uzalishaji wa sukari na hasa sukari ya viwandani ili kuondokana na tatizo kubwa ambalo limekuwa likiikumba nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa miradi mikubwa inatekelezwa ambayo kwa kuanzia, Serikali kuitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeamua kuwekeza katika mashamba makubwa mawili katika eneo la Mkoa wa Morogoro kwa lengo la kuwa na kiwanda kikubwa cha uzalishaji wa sukari ili kuondokana na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge aamini tu kwamba Serikali inafahamu changamoto hiyo na tunaendelea kuwa na mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba tunaondokana na changamoto hiyo.

MWENYEKITI: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda swali linalofuata linaliuza kwa niaba na Mheshimiwa Prosper Joseph Mbene, Mbunge wa Morogoro Kusini linaliuza kwa niaba yake na Mheshimiwa Janet Mbene.

Na. 62

Kuongeza Uzalishaji wa Mafuta ya Kula Nchini

MHE. JANET Z. MBENE (K.n.y. MHE. PROSPER J. MBENA) aliuliza:-

Mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni takribani tani 400,000 kwa mwaka. Uzalishaji wa ndani unakidhi soko kwa asilimia 30 na asilimia 70 inaagizwa kutoka nje ya nchi.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani ya kuwawezesha wakulima na wafanyabiashara wa ndani ya nchi kutosheleza mahitaji ya mafuta kwa zaidi ya asilimia 80?

(b) Je, kwa nini waagizaji wa mafuta hususan *korie* wasishauriwe kujenga viwanda vyta mafuta ya kula hapa nchini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI) aliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biasara na Uwekezaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Morogoro Kusini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu sekta ya mafuta ya kula nchini, Serikali iliamua sekta hiyo kuwa ya kipaumbele na hivyo kuandaa mkakati wa kuendeleza mafuta ya alizeti uliozinduliliwa na kuanza kutekelezwa mwezi Mei, 2016. Tangu kuzinduliliwa kwa mkakati huo, Serikali imewezesha kukutanisha wadau wa sekta ya mafuta, kuanzishwa kwa jukwaa la wadau wa alizeti, kuanzishwa na kuimarisha mifumo ya kongano (*clusters*) za wazalishaji wa mafuta ya kula mfano Mtinko Singida na vituo vyta utafiti mfano *TEMDO* na *CAMARTEC*, kubuni na kuzalisha teknolojia sahihi za kusindika mbegu za kusindika mbegu za alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kama *FAO* na *UNIDO*, Serikali imeanza kuandaa mkakati wa kuendeleza zao la mchikichi ili kukidhi mahitaji ya ndani ya mafuta ya kula na mauzo nje ya nchi. Kutokana na juhudi hizo, uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula umeongezeka kutoka wastani wa tani 6301147 mwaka 2015/2016 hadi tani 6667893 mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji inaendelea kuhamasisha waagizaji wa mafuta ya kula wakiwemo *East Coast Oils & Fats, Mkoani Edible Oil & Detergents Ltd., Murzah Wilmar East African Industriesna BIDCO* kuanzisha viwanda vyta kusindika mafuta kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini ambapo baadhi yao wameonesha nia ya kuanzisha mashamba ya michikichi.

Aidha, Serikali imondoa kodi na tozo mbalimbali katika mazao ya kilimo likiwemo zao la alizeti pamoja na kuweka ushuru wa asilimia 25 kwa mafuta ghafi na asilimia 35 kwa mafuta yaliyosafishwa kutoka nje ya nchi ili kuhamasisha uwekezaji katika sekta hii. Tunashauri halmashauri na mamlaka nyingine zinazohusika kusaidia wawekezaji wanaohitaji ardhi kwa ajili ya kilimo cha michikichi ili kutatua changamoto ya malighafi ya mafuta ya kula nchini.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mbene.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyezekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado nataka kujua mkakati mahususi ambao unaweza kutuonesha jinsi ambavyo hawa waagizaji wa mafuta ya kula tayari wana mipango, maana yake yote aliyojibu hapa ni mazungumzo na mipango, lakini nataka kujua kama kuna hatua mahususi ambazo zinaonesha tayari kuna maeneo ambayo wawekezaji hawa wanaweza kuanza kulima?

Mheshimiwa Mwenyezekiti, itambuliwe kuwa mbegu za mafuta ndio kilimo kinachotegemewa sana na wanawake wengi wanaolima vijijini, vijana wengi na kinachoshindikana ni mbegu bora na utaalam mzuri zaidi wa kuzalisha na ule mnyororo wa thamani ambao unaeleweka. Tungependa sana kuona hili ili tupunguze uagizwaji, lakini vilevile tuboreshe mazingira ya wakulima wetu na hasa wanawake... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Uliza swali basi.

MHE. JANET Z. MBENE: Kwa hiyo, ni lini sasa tutauona huo mkakati na ni wawekezaji gani ambao wamekubali sasa hivi kuanzisha hayo mashamba makubwa? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI): Mheshimiwa Mwenyezekiti, kuhusu mkakati gani uliopo na mipango mahususi, kwenye jibu langu la msingi

nimezungumza kwamba Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji ambayo pia inafanya pamoja na wenzetu wa EPZA tumeshakutana na baadhi ya makampuni ambayo nilyataja katika majibu yangu ya msingi, ambayo yanazalisha mafuta kwa lengo la kuwashawishi kufanya uwekezaji katika nchi yetu. Hivi sasa kwa sababu tunayo ile *blueprint document* ambayo inasaidia ufanyaji biashara mrahisi katika nchi yetu, tunaamini kabisa kupitia majadiliano haya na mpango mkakati wa Serikali wa vishawishi vya watu kuja kuwekeza nchini, ndugu zetu hawa watatukubalia na watafanya uwekezaji katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatua ya kwanza ambayo tumeanza nayo ni hii ya kuwashawishi lakini vilevile tayari maelekezo yameshatoka kwa kila mikoa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kilimo. Hivi sasa katika Mikoa ya Dodoma na Singida uhamasishaji umekuwa ni mkubwa sana na ndio maana hivi sasa viwanda vingi vimeendelea kujengwa katika maeneo haya kwa lengo la kuwavutia wakulima wengi zaidi kulima alizeti ili kuondokana na changamoto hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimpongeze sana kwa kuwa mtetezi wa wakinamama lakini na sisi tunafahamu moja kati ya eneo kubwa ambalo linaweza likasaidia sana katika kuimarisha uchumi wa akina mama na hata kuwaongezea kipato ni pamoja na kilimo cha alizeti. Kupitia Serikali nataka nimuhidi Mheshimiwa Mbunge kwamba mkakati wetu ni kuwawezesha makundi ya wakinamama kushiriki moja kwa moja kupitia katika kilimo cha mkataba kwa viwanda ambavyo tayari tunavyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Dodoma hivi sasa tayari kuna kiwanda kipo chini ya Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambapo tayari tumeshakutana na makundi mbalimbali ya akina mama wa Mkoa wa Singida na Dodoma kuwahamasisha walime alizeti na kuzileta katika Kiwanda cha Dodoma ili kifanyiwe mchakato na baadae tuweze kupata mafuta. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nuru.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa eneo kati ya Dodoma na Gairo wananchi wanajitahidi sana kukamua mafuta ya alizeti lakini mafuta yale yanayokamuliwa hayapo katika ubora. Ni lini Serikali itawajengea wananchi hawa kiwanda ili waweze kukamua mafuta ambayo ni bora na yataweza kuliwa vizuri? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo kwa kifupi tu, ni lini mnaweza mkawasidia wananchi hawa. Mheshimiwa Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kuendelea kuwezesha wananchi wengi zaidi kwenda katika hatua ya kuchakata mbegu za alizeti na kuwa mafuta katika ubora. Hivi sasa viwanda vyetu vingi ambayo tumeamua kuvifanya katika kuboresha hali hiyo wataanza kuchukua mafuta yale mengi ambayo yanazalishwa na wafanyabiashara wadogo wadogo kwa ajili ya kuya-*refine* tena ili baadae kuyaongezea ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango mkakati wa kudumu kabisa ni kuwezesha wafanyabiashara wadogo wadogo kumiliki mashine zao na wenyewe waweze kuchakata katika hali ya ubora. Ni mpango wa Serikali na naamini kabisa tutawafikia wafanyabiashara hao wadogo pia.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Fatma Toufiq.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Dodoma unazalisha karanga kwa wingi na kwa kuwa mafuta ya karanga pia ni mafuta mazuri kwa matumizi ya

binadamu. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhamasisha wananchi kusindika mafuta ya karanga ili kupunguza uagizaji wa mafuta kutoka nje? (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, jibu kwa swali hilo Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli karanga nazo pia zinazalisha mafuta mazuri na katika Mkoa wa Dodoma mkakati uliopo ni kwanza, kuititia Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo (*S/DO*) katika eneo la Kizota imeanzishwa *industrial shade* ambayo itatoa mafunzo kwa wakulima wote wa karanga na alizeti katika Mkoa wa Dodoma ili baadae Serikali kuititia *industrial shade* hiyo ya Kizota ione namna ya kuweza kuwawezesha ili nao waweze kufikia malengo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mpango wa Serikali, nina amini tutawafikia katika hali hiyo ya kuzalisha mafuta kuititia karanga pia. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi na linaulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

Na. 63

Utekelezaji wa REA III – Lulindi

MHE. JEROME D. BWANAUSI aliuliza:-

Kwa kuwa utekelezaji wa umeme *REA III* unaendelea nchi nzima.

(a) Je, ni kwa nini mkandarasi aliye pangija kusambaza umeme katika Jimbo la Lulindi amesambaza umeme katika kijiji kimoja tu cha Kalipinde?

(b) Je, ni lini mkandarasi huyo ataanza kusambaza umeme katika vijiji vyote vya Jimbo la Lulindi?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Subira Mgusu, Naibu Waziri wa Nishati.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijiji (*REA*) inaendelea kutekeleza mradi wa kusambaza umeme vijiji awamu ya tatu mzunguko wa kwanza katika maeneo mbalimbali nchini. katika, Jimbo la Lulindi kazi za mradi zinatekelezwa na mkandarasi *JV Radi Service Ltd., Njarita Contractor Ltd. & Aguila Contractor Ltd.* ambapo hadi kufikia mwezi Oktoba, 2018 vijiji viwili vya Kalipende na Mpeta Mrashi vimewashwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kufunga miundombinu ya umeme zinaendelea katika vijiji vya Mpeta, naomba hapa isomeke badala ya Nangose, Nandete, ni Nakarara na Mkwaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za miradi zinahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometra 60.45, njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometra 81, ufungaji wa transforma 22 pamoja na kuwaunganishia wateja wa awali 795. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 4.99. kazi za ujenzi wa mradi huu zinatarajiwaa kukamilika mwezi Juni, 2019.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bwanausi.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze

Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu hayo kwamba pale Kalipinde na Mpeta wamekwishawasha na sasa wanaekelea Nakarara, Mkwaya na Namiomi. Swali langu ni kwamba pale Kalipinde wamefanya kazi katika vitongoji viwili na vitongoji viwili vya Mwiti na Joshoni hawajatekeleza. Je, nini kauli ya Serikali kwa kuwa mkandarasi ameshamaliza na kuondoka, kuhusu kumalizia katika eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa kuwa usambazaji wa umeme unakwenda kwa kasi ndogo sana katika Jimbo la Lulindi na ukizingatia kwamba Wilaya ya Masasi ina vijiji 64 na hadi sasa imefikia vijiji vinne tu. Je, nini kauli ya Serikali katika kumsaidia mkandarasi anayefanya kazi na hasa ikizingatiwa kwamba alichelewa kupewa *LC* na hadi sasa hana kibali cha kununua waya ili kuwafikia wananchi wa Jimbo la Lulindi ikiwemo Kata ya Mkolopora na Kata ya Mkundi ambayo Vijiji vya Nakalora, Namwanga na Kachindu havijapata umeme kabisa? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa kifupi tu kwa maswali hayo Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kwa Mheshimiwa Mbunge lakini pili nimpongeze Mheshimiwa Bwanausi jinsi anavyofuatilia miradi hii ya umeme katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika majibu yake mawili kuhusu maswali yake ya nyongeza la kwanza, katika Kijiji cha Kalipinde ni kweli katika Mkoa mzima wa Mtwara tulipowasha tulianza Kalipinde kwa Mheshimiwa Bwanausi, ndio maana tunampongeza sana na ndipo tulipofanya uzinduzi kimkoa. Ni kweli waliwashowi wananchi takribani 30 kati ya 52, nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba kuanzia jana wakandarasi wamerudi kwa ajili ya kuwasha

umeme katika vitongoji viwili vya Mwiti na Joshoni katika Kijiji cha Kalipinde ili wakamilishe wananchi 62. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kasi ya mkandarasi, ni kweli kabisa mkandarasi tumempa vijiji 64 na tulikuwa tunafanya maboresho ili kuongeza vijiji vingine 28 katika Mkoa mzima wa Mtwara na Masasi. Alichofanya mkandarasi sasa hivi ameshapata nyaya, ni matumaini yetu *speed* itaongezeka, lakini kwa vile vifaa vinapatikana ndani, tumeshakaa na mkandarasi na kuelekeza kuongeza *speed*. Nimpe taarifa na uwakilishi wa Mheshimiwa Mbunge kwamba mkandarasi atafanya kazi kwa *speed* na tutamsimamia kwa ushirikiano wako. Kwa hiyo, atakamilisha vijiji vyote Mheshimiwa Bwanausi. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Magige.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa kuna vijiji vingi vilivyopimwa kwa ajili ya umeme wa *REA* Wilayani Monduli, Mkoa wa Arusha, mfano kutoka Kijiji cha Engorika kupitia Lengitoriti hadi Mahao ambapo ni Makao Makuu ya Kata ya Naalaran na maeneo mengine Wilayani Monduli hayajapata umeme na wamekuwa wakiahidiwa mpaka sasa hivi na sehemu nyingine nguzo zimelazwa lakini hakuna kinachoendelea na wananchi wa Wilaya ya Monduli wamekuwa wakipata tabu sana...

MWENYEKITI: Swali sasa.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri upo tayari baada ya Bunge hili kufuatana na mimi hadi Wilaya ya Monduli ili ukaone wananchi wa Monduli wanavyopata taabu ya umeme ili uweze kutatua kero hii iliyodumu kwa muda mrefu? (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri hataki kufuatana na wewe. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Catherine kwa kazi nzuri anayofanya ya kufuatilia masuala ya Sekta ya Nishati na ushiriki wake katika kampeni katika Jimbo la Monduli. Na kwa kuwa Jimbo la Monduli Mheshimiwa Waziri wa Nishati alilitembelea na akawasha umeme vijiji vinne, kwa hiyo kazi inaendelea mkandarasi katika maeneo hayo.

Kwa kuwa amesema tutembelee tena, ameomba kwamba tufanye ziara pamoja, nimkubalie kwamba baada ya Bunge hili tutaambatana pamoja na Mbunge wa Jimbo, Mheshimiwa Julius Kalanga kuititia Chama cha Mapinduzi kuititia maeneo mbalimbali yale ambayo kazi inaendelea ili kuhakikisha kwamba Jimbo la Monduli kwa sasa linapata miundombinu ya umeme. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya ya usambazaji wa umeme vijiji. Kutokana na tatizo hili la wakandarasi wengi kutokontakteleza miradi kwa wakati ambapo Jimbo la Mbulu Mjini hadi sasa ni mitaa minne kwenye mji ndiyo imepewa nguzo kubwa, haina hata waya wala umeme na wakati Mheshimiwa Waziri wa Nishati alipokuwa Naibu Waziri aliahidi kupeleka umeme katika Kata za Murai, Silaloda, Nasei, Nambis na Gunyoda...

MWENYEKITI: Swali sasa.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Je, ni lini sasa ahadi hii ya Mheshimiwa Waziri wetu itatekelezwa katika Jimbo la Mbulu Mji?

MWENYEKITI: Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakupongeza kwa kunipa fursa, lakini nimpongeze Mheshimiwa Zacharia, ni kweli nilitembelea katika jimbo lake na tukawasha vitongoji vinne, nakupongeza sana kwa kufuatilia kazi hiyo kwa wananchi wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, mkandarasi yuko *site* huko Mbulu na bahati nzuri sana Jimbo la Mbulu lina vijiji vyote 29 tumevipatia umeme katika awamu hii ya kwanza. Kwa hiyo, nimpe taarifa kwa sababu mkandarasi yuko *site* na jana tumekaa na mkandarasi pamoja na Mheshimiwa Mbunge, ni matumaini yetu atakwenda *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kesho wanakwenda katika Kata ya Kunyoti na wataanza kazi katika kata hiyo katika vijiji viwili. Kwa hiyo ni matumaini yetu watafanya kazi kwa *peed* katika Jimbo la Mbulu, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge aendelee kutupa ushirikiano ili wakandarasi wakamilishe kazi hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwenye Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika sana kama ni uzembe wa meneja wa wilaya ama ni uzembe wa meneja wa mkoa au ni uzembe wa Wizara yenyewe, kwa mfano kuna vijiji...

MWENYEKITI: Uliza swali Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio. Vijiji vya Liputu, Ndolo, Chipite, Mlingura, Msikisi, Mbemba pamoja na Mumburu vinapitiwa na nguzo kubwa yenyе msongo wa KVA 33.

Sasa nataka kufahamu kauli ya Serikali, ni lini watafanya uamuzi wa kushusha waya kwenye hivi vijiji

nilivyovitaja ili wananchi waweze kupata umeme mara moja kwa sababu ni kazi tu ya kushusha waya kwenye maeneo haya? (*Makof*)

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nishati mwenyewe.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mwambe kuuliza swali la umeme katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa tunavyoongea hapa wakandarasi wapo katika Kijiji cha Liputo pamoja na Mbemba ambapo wanafanya kazi za kushusha umeme. Lakini hata hivyo kwa upande wa maeneo ya Masasi kuelekea Nanyumbu wakandarasi wanafanya kazi ya kusafirisha nguzo kubwa kwa ajili ya kuanza kazi hiyo. Kwa hiyo, nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge, wakandarasi wako site, cha msingi tutashirikiana na wewe Mheshimiwa Mbunge tuwasukume ili waongeze kasi, lakini kazi inaendelea.

MWENYEKITI: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene na linaelekezwa kwa Waziri wa Nishati.

Na. 64

Vijiji vya Mwamala, Lububu na Igusule Kupatiwa Umeme

MHE. SELEMANI J. ZEDI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali chini ya Mpango wa Kusambaza Umeme Vijijiini (*REA*) itavipatia umeme vijiji vya Mwamala, Lububu na Igusule?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Nishati Mheshimiwa Subira Mgali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji cha Mwamala ni katika ya viji 37 vya Wilaya ya Nzega vinavyopelekewa umeme katika Awamu ya Tatuy ya Mradi wa Kusambaza Umeme Vijiji (REA III) mzunguko wa kwanza unaoendelea kutekelezwa na mkandarasi, Kampuni ya *JV Pomy Engineering Co. Ltd.*, *Intercity Builders Ltd.* na *Octopus Engineering Ltd.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za mradi huo zinajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometra 163; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometra 73; ufungaji wa transforma 38 pamoja na kuwaunganisha wateja wa awali 2016 na gharama za mradi ni shilingi bilioni 9.37.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Lububu, Igusule pamoja na viji vingine 63 vilivybaki katika Wilaya ya Nzega vitapatiwa umeme kupitia Awamu ya Tatuy ya Mradi wa Usambazaji Umeme Vijiji (REA) Mzunguko wa Pili unaotarajiwa kuanza kutekelezwa mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Zedi.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kalemani na Naibu Waziri kwa kazi kubwa na wepesi kila mara ninapowafuata kuhusu utekelezaji wa miradi hii ya REA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu ni kwamba je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari mara tu baada ya Bunge hili afike Jimboni Bukene atembelee Vijiji vya Mwamala, Lububu, Kayombo na Igusule ili aone hali ya

utekelezaji na aweze kutoa maagizo mahususi akiwa *site* na kujiona hali halisi ilivyo?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nampongeza sana Mheshimiwa Zedi anavyofuatilia miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niko tayari kutembelea maeneo ya Mwamala Mheshimiwa Mbunge, na tutaongozana mara baada ya Bunge hili kuanzia tarehe 20 na 21 mwezi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya nyongeza katika maeneo haya, nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Bukene kwamba mkandarasi sasa hivi anaendelea kutandaza nguzo kutoka Mwamala kupitia Itobo umbali wa kilometra 12 lakini pia kutoka Kayombo kupitia Itanana umbali wa kilometra sita akielekea katika Sekondari ya Kili iliyopo katika Kijiji cha Isungwanghara. Kwa hiyo, kazi zinaendelea na nipo tayari kusirikiana naye.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwamoto. Muda hauko rafiki Waheshimiwa Wabunge.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi kubwa kabisa ambayo inafanywa na Wizara hii ya Nishati, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilolo Makao Makuu ni Kilolo lakini jirani tu ya Kilolo iko Kata ya Kising'a ambayo imesahaulika, mimi ningeomba tu ombi maalum uweze kunisaidia ili Kising'a wapate umeme haraka kwa sababu ni jirani na makao makuu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge Mwamoto. Ni kweli Kata ya Kising'a ni kata iliyobaki lakini tumeingiza katika mpango unaoanza kupelekewa umeme kuanzia mwezi Machi, mwaka unaokuja. Kwa hiyo, wananchi wa Kising'a watapata umeme.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona hivi sasa nguzo zinazosambazwa ni za miti, je, ni lini Serikali itasambaza nguzo za chuma ili kuerekana na ukataji hovyo wa miti? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa kunipa fursa hii nimjibu Mheshimiwa Mbunge. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu katika mwaka huu na mwaka unaokuja kwa kiasi kikubwa sana tunatumia nguzo za miti lakini za kutoka hapa ndani hasa baada ya kufanya zuio la kuingiza nguzo kutoka nje zilizotoka *South Africa* kwa muda mrefu. Lakini kwa maana hiyo tunaongeza viwanda vya ndani kuzalisha nguzo zaidi na uwezo wetu umeongezeka wa kuzalisha nguzo kutoka nguzo 840,000 mpaka 1,200,000 kwa mwaka.

Kuhusiana na nguzo za vyuma, ni kweli utaratibu tunaokwenda nao kwa sasa ni kuanza uzalishaji wa nguzo za zege ambazo ni imara sana, zinadumu kwa miaka zaidi ya 50 au 60, kwa hiyo utaratibu wa kujenga nguzo za vyuma bado tunajipanga kuangalia ustahimilifu wa viwanda hivyo, tutakapokuwa tayari napo tutaanza kufanya kazi.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, linaulizwa kwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Na. 65

Upungufu wa Mashine za *Oxygen* Katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi

MHE. TASKA R. MBOGO aliuliza:-

Mkoa wa Katavi una hospitali moja ambayo inatumika kama Hospitali ya Mkoa kwa wananchi wote wa Mkoa wa Katavi, lakini hospitali hiyo ina mashine moja tu ya *oxygen* ambayo huzunguka kwenye wodi zote.

Je, ni lini Serikali itawasaidia mashine nyingine mbili wananchi wa Katavi?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu ya swali hilo namuona Waziri wa Afya, Maendeelo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Ummy Mwalimu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji halisi ya mashine ya *oxygen* kwa Hospitali ya Mkoa wa Katavi kwa sasa ni mashine 18 ikiwa ni mbili kwa kila wodi, nne kwa wodi ya watoto na wazazi. Kwa sasa hospitali inazo mashine kumi zinazofanya kazi baada ya matengenezo ya mashine nane zilizokuwa mbovu na mashine mbili mpya ambazo zimenunuliwa kuanzia mwezi Mei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa idadi ya mahitaji halisi inafikiwa, hospitali imeweka katika mpango wake wa manunuzi wa mwaka 2018/2019 kiasi cha shilingi milioni 746 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba zikiwemo mashine hizi.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mbogo.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini nipende kumwambia kwamba mashine zinazofanya kazi katika Hospitali ya Mkoa, Mkoani Katavi ni mbili siyo 18, mbili tu ndio zinafanya kazi. Lakini pia Mkoa wa Katavi unazo kata 58, katika kata hizo 58 ina vituo vya afya 11 ambavyo ni Vituo vya Usevya, Mamba, Mtisi, Kanoge, Katumba, Lilego, Mwangaza, Inyonga...

MWENYEKITI: Uliza swali sasa.

MHE. TASKA R. MBOGO: ...Mishamo, Mwese na Karema.

Katika vituo hivi Vituo vitatu vya Mishamo, Kanoge na Usevya vimefanyiwa ukarabati wa vyumba vya upasuaji ili viweze kufanya upasuaji katika vituo hivyo lakini vituo hivyo havina vifaa tiba kama hizo mashine za *oxygen*, kama *warmers* kwa ajili ya watoto wachanga na kama vitaa vya upasuaji...

MWENYEKITI: Uliza swali Mheshimiwa Taska.

MHE. TASKA R. MBOGO: Je, ni lini Wizara ya Afya itapeleka vifaatiba kwenye vituo hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mkoa wa Katavi hauna Hostipali ya Mkoa, na hii hospitali inayojengwa kwa sasa hivi pesa zake zimekwisha. Sasa je, ni lini pesa za ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Katavi za *quarter* ya 2018/2019 zitapelekwa mkoani Katavi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa kifupi tu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Taska Mbogo kwa swali lake zuri, lakini pia kwa kufuatilia utoaji wa huduma za afya hasa afya ya mama na mtoto katika Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi na amenithibitishia hapa sina shaka, na timu yangu ilikwenda kule katika hospitali wiki iliyopita kufanya tathmini ya hali ya ubora wa huduma, mashine nane zilizotengenezwa zinafanya kazi. Lakini nalipokea na nitaenda kufuatilia kutuma timu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake kuhusu lini tutapeleka vifaatiba katika vituo vya afya vinavyobereshwa; kuititia Bohari Kuu ya Dawa tayari Serikali imeshatoa *order* ya vifaatiba kwa ajili ya kuweka katika vituo vya afya vyote 300 ambavyo vinabobereshwa ikiwemo meza za upasuaji, *oxygen machines*, mashine za usingizi na vifaa vyote ambavyo vinatakiwa kutoa huduma za upasuaji wa dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi; tumeanza ujenzi wa jengo la mama katika eneo la Rungwe ambapo shilingi bilioni 1.2 imeshatolewa.

Mheshimiwa Taska katika mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi, nafurahi kusema tayari fedha tumepokea na fedha hizo tutazipeleka Mkoani Katavi haraka iwezekanavyo ili ujenzi wa hospitali uweze kuendelea. Ahsante.

MWENYEKITI: Tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 66

Watoto Kuendelea Kufanyiwa Ukatili

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA aliuliza:-

Mbali ya kuwa na sheria nzuri inayolinda watoto, bado watoto wameendelea kufanyiwa ukatili kama vile kubakwa, kutumikishwa kazi ngumu na kukosa haki zao muhimu.

(a) Je, Serikali imefanya utafiti kubaini ukubwa wa tatizo hilo?

(b) Umaskini katika familia ni sababu mojawapo ya kuwatumikisha watoto kazi ngumu, je, Serikali inazisaidiaje familia hizo ili kuondokana na tatizo hilo?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Afya.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali na kukusanya taarifa za kiutawala ili kupata takwimu na sababu zinazochangia ongezeko la vitendo vya ukatili dhidi ya watoto nchini. Taarifa za vitendo vya ukatili kuititia Dawati la Jinsia na Watoto kutoka Jeshi la Polisi katika kipindi cha Januari – Desemba 2017 zinaonesha matukio 13,457 ya ukatili dhidi ya watoto yameripotiwa ukilinganisha na matukio 10,551 ya mwaka 2016. Aidha, kulikuwa na matukio ya ubakaji 2,984, ulawiti 501, kutelekeza familia 695, mimba za utotoni 1,323 na kuzorotesha wanafunzi masomo 381. Pia taarifa hii ya Jeshi la Polisi inaonesha kuwa Mikoa ya Kipolisi yenye matukio mengi ya ukatili ni Kinondoni, Dodoma, Tanga, Temeke na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imefanya Utafiti wa Kitaifa kuhusu Ajira za Watoto wa mwaka 2014 (*National Child Labour Survey, 2014*). Tafiti inaonesha kuwa asilimia 27 ya watoto wa miaka mitano hadi 17 wanashirikishwa kwenye ajira hatarishi zikiwemo kilimo, utumikishwaji nyumbani, migodini na uvuvi. Tafiti hizi zimeisaidia Serikali kupanga mikakati mipy ya kukabiliana na tatizo la ukatili nchini ikiwemo kuwa na Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/2018 – 2021/2022 ambao umelenga kutokomeza ukatili kwa asilimia 20 ifakapo mwaka 2022.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto kuititia eneo la kuinua uchumi wa kaya, Serikali kwa kushirikiana na wadau inatoa elimu ya ujasiriamali kwa kaya ili kuweza kuinua kipato cha familia. Kwa kipindi cha miaka mitatu kuititia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wanajsiriamali na wanawake walio katika kaya maskini imetolewa ili kuwezesha, kuanzisha na kukuza biahsara zao. Katika kipindi cha miaka mitatu, Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 28.5 kama mkopo wa wanawake wajasiriamali kwa vikundi vyta wanawake 14,976 vyenye wanawake 832,861.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuititia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaoratibiwa na *TASAF*, jumla ya kaya maskini 1,000,549 zimebainishwa ambapo jumla ya watu 5,186,660 wamenufaika na mpango huo nchini. Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini umesaidia kaya hizo kupambana na changamoto za umaskini na kuwawezesha kupata mitaji ya kuanzisha miradi na kuweza kuwapa watoto mahitaji muhimu ya shule.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Jecha.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na pia naipongeza Serikali kwa juhudhi kubwa inayochukua katika

kukabiliana na tatizo hili, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa amekiri kwamba watoto kuanzia miaka mitano mpaka 17 wanashiriki katika shughuli mbalimbali ambazo wanaoajiri ni watu wazima. Je, Serikali imechukua hatua gani pindi inapobaini watu wazima wanawaajiri watoto hawa? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kwa kuwa kuna wanawake, hasa maeneo ya mijini, wanazurura tu hawajui mahali ambapo wanakaa. Je, Serikali kundi hili wanalitazamaje, kwa sababu ndio wenyewe watoto wengi ambaao wanazurura sasa hivi watoto tayari wengine wamekuwa vigori na wengine wamebalehe; wanachukua hatua gani kulidhibiti kundi hili ili suala hili lisiendelee? Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Afya.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha kwa maswali yake mazuri mawili ya nyongeza na hasa katika kupambania kuhakikisha kwamba tunaondokana na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, hasa katika Zanzibar, kwa hiyo tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakata kuweka wazi sheria ya mtoto ya mwaka 2009 haikatazi ajira za watoto, lakini inakataza ajira zenyeye madhara kwa watoto, ambazo zinaweza zikawa na athari kwenye afya ya mtoto, athari katika maendeleo ya mtoto, kiakili na kimwili pamoja na elimu na eneo la tatu ni zile ambazo zinaweza kuharibu maadili ya mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sheria imeweka wazi mtu ye yeyote ambaye atakiuka misingi au katazo la kisheria la kuajiri watoto kwa kuwapa kazi ngumu amendeka

kosa la jinai na anatakiwa kupata adhabu. Kwa hiyo, nitumie jukwaa lako kuwaomba wadau wote kutoa taarifa kwa Maafisa kazi pale ambapo watabaini kuna watoto wameajiriwa katika migodi, wameajiriwa katika mashamba na wameajiriwa katika ajira ambazo zinahatarisha afya zao na maendeleo yao ya kielimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunategemea sana jamii itupe Maafisa Kazi wako katika kila Halmashauri. Hawa ndio wanajukumu la kusimamia uetekelezaji wa sheria ya mtoto hasa kuhusu ajira mbaya za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı lake la pili, ni kwamba kuna wanawake wanadhirura mitaani na hawa wanaterekeza au hawawajali watoto sasa wanachukuliwa hatua gani? Sitaki kusema kwamba ni ombaomba hawa, lakini zipo sheria ambazo zinasimamila sijui nitumie neno gani eti, zinasimamia watu ambao yaani wanatakiwa kufanya kazi wasiodhirura hovyohovyo au ombaomba hovyohovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, labda nitoe wito kwa wanawake hawa waende kwenye halmashauri zao kuchukua mikopo kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za kuzalisha mali na Waheshimiwa Wabunge ninyi ni mashahidi tumepitisha sheria ya bajeti hapa sasa hivi kutenga asilimia nne kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake siyo suala la kiutashi, ni suala la lazima fedha zipo kwa kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe wito kwa wanawake ambao wanadhirura na kukaa hovsky hovsky mitaani nisingetaka kuwaita ombaomba, lakini ni wanawake ambao hawana shughuli wajiongeze wafanye shughuli za kujiongezea kipato ili waweze kutimiza mahitaji ya watoto wao ikiwemo chakula, mahitaji ya shule pamoja na mahitaji ya kuiweka warembo ili waweze kuvutia zaidi.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea, Mheshimiwa muda wangu jamani hauko rafiki, tunaendelea Mheshimiwa

Yosepher Ferdinand Komba, Mbunge wa Viti Maalum swali lake analiuliza kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Na.67

**Skimu ya Umwagiliaji Iliyoko Kata ya Misozwe
Wilayani Muheza**

MHE. YOSEPHER F. KOMBA aliuliza:-

Serikali imekuwa na mpango wa kuboresha mabonde kwa lengo la kuanzisha skimu za umwagiliaji.

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya bwawa lenye skimu ya umwagiliaji liliopo Kata ya Misozwe ambapo wananchi wameanza shamba darasa zaidi ya miaka mitatu sasa?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kwa kunipa nafasi, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibuwa swali la Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Skimu ya Umwagiliaji ya Misozwe yenyewe uwezo wa kumwagilia hekta 100 iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ulitekelezwa kwa awamu tatu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya kwanza ilianza kutekelezwa kati ya mwaka 2009 na 2012 ambapo ujenzi wa bwawa lenye uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha lita za ujazo milioni 148 kwa ajili ya umwagiliaji ulifanyika kwa gharama ya shilingi bilioni 1.54. Awamu ya pili ilitekelezwa katika mwaka 2012/2013 na mwaka 2013/2014

kwa gharama ya shilingi milioni 199.4 ambapo kazi zifuatazo zilifanyika:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, uchimbaji na usakafiaji wa mfereji mkuu wenye mita 900; ukarabati wa utoro wa maji yaani *spillway* ili kuongeza kina cha maji kutoka lita za ujazo milioni 148 hadi lita za ujazo miioni 250; na ujenzi wa vigawa maji vinne na kalavati nne za kuvusha maji pamoja na kukarabati mita 60 za mfereji mkuu. Aidha, bwawa hilo liliikabidhiwa kwa Serikali ya kijiji cha Misozwe wakati taratibu za kusajiliwa na kujengewa uwezo wa kwa umoja wa umwagiliaji zikiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Tatu ya ujenzi wa skimu ya Misozwe ulifanyika mwaka 2014/2015 kwa gharama ya shilingi milioni 137.6 ambapo mita 675 za mfereji mkuu zilichimbwa na kusakafiwa pamoja na ujenzi wa vigawa maji vitatu na kalavati moja. Hadi sasa, jumla ya kilometa 1.6 kati ya kilometa 5.7 za mfereji mkuu zimechibwa na kujengwa. Utekelezaji huo umewevezeshwa kulimwa takribani hekta 50 zenyetija ya uzalishaji wa tani 4.5 kwa hekta katika zao la mpunga na tani 3.7 kwa hekta katika zao la mahindi. Uzalishaji huo unatokana na matumizi sahihi ya shamba darasa ambapo wakulima walijifunza matumizi bora ya mbolea madawa, utayarishaji wa shamba pamoja na matumizi sahihi ya rasilimali maji.

Aidha, katika kuhakikisha kuwa eneo lote la umwagiliaji linatumika kutoka takribani hekta 50 za sasa hadi hekta 100, mita 4.1 za mfereji mkuu zilizobaki zitakamilishwa na hivyo kuzinufaisha takribani kaya 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa skimu zote za umwagiliaji ambazo hazijakamilia zinakamilishwa. Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imefanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 na kuainisha maeneo ya kipaumbele yatakayotekerezwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza itatekelezwa kati ya mwaka 2018/2019 hadi mwaka 2023/2024 kulingana na upatikanaji wa fedha

ambapo Skimu ya Misozwe imeweka katika awamu ya kwanza ya utekelezaji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yosepher Ferdinand.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetembelea mradi huu wa Misozwe. Lakini hali ambayo iko sasa hivi mradi kina cha maji kinapungua kutokana na matope ambayo yanaingia kwenye mradi. Lakini mifereji illyojengwa imeanza kubomoka mradi huu umeanza tangu mwaka 2009 mpaka sasa hivi umetumia zaidi ya shilingi bilioni 1.3. Kwa hiyo, naomba nimuulize Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Ni għarama kiasi gani zinahitajika ili mradi huu ukamilike, maanayake bado hujakamilika, lakini inaonekana hela inazidi kutumika? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ukiangalia katika ujenzi kati ya kilometru 5.7 zimejengwa 1.6 katika kipindi cha miaka zaidi ya miaka kumi. Je, ni lini mradi huu utatengewa fedha ili ukamilike pamoja na kilipa fidia ya wakulima ambaω wanazunguka eneo lile? (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu kwa maswali hayo, kwa kifupi tu, muda wangu mnaona Waheshimiwa Wabunge.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anasema kiasi kikubwa cha fedha kimetumika shilingi bilioni 1.3 lakini mpaka sasa mifereji hiyo imeanza kuharibika, je, anataka kujua jitihada na kiasi gani ambacho tumekifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza cha kwanza kama Serikali jitihada kubwa tulizozifanya ni kuhamisha Tume hii ya Taifa ya Uwamgiliaji kutoka Wizara ya Maji kuna Wizara ya Kilimo. Lakini jitihada ya pili ni kuja na programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo *SDP II*; na katika jitihada hizi tumetenga zaidi ya trilioni 2.02 ambaω ni sawa na asilimia 15 ya pesa zote

zitakazoenda kugharamia programu ya *SDP II*. Lengo ni kuendeleza kuongeza tija na kuongeza uzalishaji kutika kugharamia miradi hii ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, katika jitihada hizi za Serikali kama Serikali miradi mingi ya umwagiliaji kitaifa nchi nzima inamapungufu makubwa sana kama sisi Serikali tunakusudia kuunda chombo ambacho kitafanya utafiti na tathimini ya kina nchi nzima ili kuangalia ufanisi, mafanikio na changamoto ili kuja na mikakati ya kuweza kumaliza changamoto hizo na kuboresha miradi yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu anasema kama eneo hili lilikuwa linatakiwa 5.7, lakini ambalo lililoendelezwa ni 1.6 yaani kama nilivyosema kwenye jibu langu la awali na katika jibu la kwanza, mikakati ya Serikali ya kwanza kwamba ni hiyo tulishaihamisha Tume, lakini tumetenga kiasi kikubwa cha fedha katika kutekeleza miradi ya umwagiliaji na hii miradi katika Jimbo ambao katika eneo la Mheshimiwa Mbunge imewekwa katika kipaumbele cha kwanza baada tukimaliza tathimini ambayo tutafanya kitaifa kugundua mapungufu yaliyokuwepo katika mradi huo.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba.

Na. 68

**Makampuni Yanayokusanya Madeni Kwenye
Vyama vyta Ushirika**

MHE. SUSAN L. KIWANGA aliuliza:-

Sheria ya Ushirika ya mwaka 2014 inavifuta vyama vyote vilivyokuwep kabla ya sheria hiyo.

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kuwepo kwa kampuni za udalali zinazokusanya madeni kwenye *SACCOS* za Wilaya kama vile Kilombero na kupeleka fedha

kusikojulikana zikidai kuagizwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika?

MWENYIKI: Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba.

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE OMARY T. MGUMBA)
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa SuSan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Jimbo la Mlimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Vyama vya Ushirika namba sita ya mwaka 2013 kifungu cha 18 kinaelekeza kuwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika itapaswa kuanzisha ama kudumisha mfumo wa ushauri wa ushirikiano na Taasisi nyingine kama itakavyoona ni muhimu kwa ufanisi na utekelezaji bora wa kazi.

Aidha, Tume katika kuimarisha taratibu za usimamizi wa Vyama vya Ushirika imekuwa ikiwatambua watoa huduma na kutoa vibari kwa watoa huduma wanaokidhi matakwa ya sheria baada ya kuingia mikataba na Vyama vya Ushirika ili kuimarisha huduma katika vyama husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa watoa huduma ya kukusanya madeni unafanyika kwa makubaliano kati ya mtoa huduma na uongozi wa vyama husika ambapo hao wakusanya madeni hao huwaendea wadaiwa sugu wa vyama vya ushirika ikiwa ni pamoja na vyama vya akiba na mikopo yaani *SACCOS* ambapo fedha inayokusanywa hurejeshwa kwenye akaunti ya chama na mwanachama anayedaiwa na si kwa mkusanya madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, madalali wanaokusanya madeni hulipwa kamisheni ya ukusanyaji wa madeni na chama husika kulingana na mkataba wa utekelezaji wa kazi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kuptitia Mrjis wa Vyama vya Ushirika ilipokea malalamiko kutoka vyama vya ushirika Wilaya ya Kilombero kuhusu kampuni ya kukusanya madeni ya *Chimbuko VICOBA* ambapo malalamiko hayo yameshughulikiwa na Mrajisi amesitisha kampuni hiyo kutoa huduma kwenye vyama hivyo. Aidha, nitoe rai kwa viongozi wa Vyama vya Ushirika kuzingatia sheria, kanuni na masharti ya *SACCOS* katika utoaji wa mikopo kwa wanachama wao ili kuepusha changamoto zinazojitokeza.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwenye *paragraph* ya mwisho kwa kuwa Mrajisi wa Vyama baada ya kumpelekea malalamiko amechukua hatua mara moja ya musimamisha hiyo kampuni isikusanye madeni na kwa kuwa hata kama walikuwa wanakusanya madeni viongozi wa vyama hao vya ushirika kwa mfano *Mwananchi SACCOS* pale Ifakara walishaua huo ushirika na mwenyewe nilikuwa mwanachama na hela walikopeka za wanachama hazijukani.

Je, Mrjis yuko tayari, sasa kwenda kwenye vyama vya Ushirika hususani *Mwananchi SACCOS* iliyoko Ifakara ambayo ilikuwa *SACCOS* kubwa kuitisha mkutano mkuu ili kujua kero na matatizo ya hiyo *SACCOS* ili wananchi wawe na imani tena na ushirika kwa sababu huo ushirika tena haupo? Kwa hiyo, hamuwezi tu mkafanya halafu mkaacha hivyo hivyo.

MWENYEKITI: Swali.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili je, sasa kwa kuwa ushirika Serikali bado inakazania ushirika uwepo nchini Tanzania na kwa kuwa ushirika umefanya vibaya sana katika Mikoa mbalimbali mfano wa Morogoro.

Je, Serikali iko tayari sasa kuupitia upya, na wanachama na watumishi mfano Mikoa wa Morogoro wa

ushirika ambao hawajapewa vitu vyao mali zao na kulipwa haki zao ili kurudisha imani kwa wananchi ili kuunda tena ushirika imara ndani ya nchi yetu ya Tanzania kuliko tu kupeleka watu kwenda kudai madeni? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa maswali hayo, kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE OMARY T. MGUMBA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la kwanza la kumtaka Mrajisi wa vyama kufika katika *Mwananchi SACCOS* ya Wilayani Kilombero kwanza hilo tuko tayari. Nichukue nafasi kumuelekeza Mrajisi aende haraka iwezekanavo katika *SACCOS* ya Mwananchi kwa ajili ya kwenda kutathimini na kuangalia hali halisi ya hapo baadae alete majibu Serikali kwa hatua zaidi tutachukua.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge hili mimi mwenyewe nitafika katika *SACCOS* hii kwenda kujiona hali halisi na kuchukua hatua stahiki kwa wale wote wanaofuja mali za wanyonge hawa wanachama wa ushirika...

MWENYEKITI: Ahsante.

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE OMARY T. MGUMBA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, je, Serikali iko tayari, kutoa elimu ya Vyama vya Ushirika ili wananchi wawewe kupata elimu pana kwa ajili hususani katika Mkoa wa Morogoro. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Serikali iko tayari na mimi mwenyewe binafsi nitaenda Mkoani Morogoro kutembelea *SACCOS* zote ambazo zenye matatizo makubwa na kwa taarifa yako nina tayari barua ya maombi zaidi ya *SACCOS* kumi katika Mkoa wa Morogoro na zingine zishawafikia. Nitoe rai katika wale wote ambao waliokopa katika *SACCOS* hizi Tanzania nzima Serikali iko macho iko na wanyonge hatutakubali fedha yoyote hata senti moja ya mnyonge ikapotea kuliwa na wajanja wachache, kila fedha itarudi kwa mwenyewe aliyepewa.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea swali letu linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula Mbunge wa Nyamagana anamuuliza Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo.

Na.69

Kujenga Majukwaa - Uwanja wa Michezo Nyamagana

MHE. STANSLAUS S. MABULA aliuliza:-

Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa kushirikiana na *TFF* wanaweza kutandaza nyasi bandia katika Uwanja wa Nyamagana ulioko Jijini Mwanza na kuufanya uwe wa kisasa zaidi.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kusaldia ujenzi wa majukwaa katika Uwanja wa Michezo Nyamagana kwa kupitia wadau mbalimbali ili kuongeza idadi ya viwanja vyenye ubora katika nchi?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo, namuona Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Juliana Shonza.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nitumie nafasi hii kuipongeza Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa kuboresha Uwanja wa Michezo wa Nyamagana kwa kushirikiana na *TFF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa majukwaa katika Uwanja wa Nyamagana utaongeza ubora wa kiwanja hicho.

Kwa kuwa kwa sasa Serikali inashughulikia uboreshaji wa viwanja vingi nchini vifike viwango kama kilivyo uwanja wa Nyamagana, naishauri Halmashauri ya Jiji la Mwanza itumile njia zingine kama vile kuhamasisha wadau wa michezo na kushirikiana nao kufanikisha lengo la kujenga majukwaa ya uwanja huo bila kuisubiri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya viwanja vingi vyatia michezo nchini ni mbaya hivyo nitume fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote washirikiane na Halmashauri zetu, vyama vyatia michezo na wadau mbalimbali wa michezo kuchangia katika kuboresha miundombinu ya michezo nchini na hivyo kuipungia Serikali mzigo mkubwa wa ujenzi wa miundombinu ya michezo.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru Mheshimiwa Naibu kwa majibu yake mazuri, na kimsingi mimi ninaafiki ushauri wake, lakini nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza. La kwanza moja kati ya Mikoa ambayo ina timu angalau mbili kwenye ligi kuu ukiondoa Dar es Salaam ni Mwanza pamoja na Mkoa wa Mbeya. Sasa unapotaja Mwanza ukiondoa timu ya Mbao na timu ya Alliance, sasa hivi tuna timu moja kweye ligi daraja la kwanza inafanya vizuri sana *Pamba Sports Club*, swali langu. (*Makofii*)

Pamoja na mawazo mazuri ya kuboresha viwanja na ushauri kwa Halmashauri, viwanja bora ni sehemu ya kukuza vipaji vingi sana kwa vijana wetu. Serikali haioni sasa ndio wakati wa kusaidia Halmashauri ya Jiji la Mwanza kupitia *TFF* ambao ndio wenye mpira wao. Lakini Wadau mbalimbali ili timu zinazofanya vizuri kama *Pamba FC* ziweze kupanda madaraja na kuendelea kuwa bora zaidi kwenye mikoa mingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa kuwa Serikali imehakikisha itaboresha viwanja vingi na nimesema moja ya

Mikoa yenyе timu mbili mbili ukiondoa Dar es Salaam ni Mwanza na Mbeya. Serikali inaonaje sasa ikijikita katika kuhakikisha kiwanja kilichoko Rungwe kule cha Tandale yaani maarufu kwa *Tulia Stadium* kinaboresha na kuwa kwenye ubora unaotakiwa? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mabula kwamba tunathamini sana jitihada zake katika kukuza maendeleo ya michezo nchini Tanzania, lakini vilevile nitumie pia fursa hii kuweza kuipongeza Halmashauri ya Nyamagana kwa jitihada zake kubwa ambazo imefanya. Lakini kama ambavyo amezungumza kwenye maswali yake ya msingi, ni wazi kwamba Mheshimiwa Mbunge anatambua Serikali imefanya jitihada kubwa sana katika kuboresha kiwanja hiki cha Nyamagana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni wazi kwamba Serikali ilitoa nyasi za bandia katika kuboresha kiwanja hicho, lakini vilevile pamoja na fedha. Kwa hiyo, ushauri ambao ameutoa mimi niseme kwamba tunathamini mchango wao lakini niwaombe yeye kama Mheshimiwa Mbunge pamoja na Halmashauri wana jukumu kubwa sana la kuendelea kushirikisha wadau ili kuweza kuboresha maendeleo ya hicho kiwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikija kwenye swalı lake la pili amezungumzia pia uwanja wa Rungwe, ni wazi kwamba sera yetu ya michezo ya Tanzania inasisitiza kwamba jukumu la michezo siyo jukumu la Serikali peke yake kwa maana hiyo basi jukumu la michezo ni jukumu ambalo ni jumuishi kwa maana ya Serikali, wadau pamoja na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo niombe kwamba kiwanja cha Rungwe ni kiwanja ambacho ni muhimu sana katika kukuza maendeleo hivyo niombe Halmashauri ya

Wilaya ya Rungwe kwa kushirikiana na Mbunge wa Rungwe akiwemo Mheshimiwa Naibu Spika washirikishane pamoja na wadau kuhakikisha kwamba kiwanja hiki kinakwenda kuboreshwa lakini sisi kama Serikali tutaendelea kuweka mazingira ambayo niwezeshi kwa sekta hii ya michezo nchini Tanzania. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsanteni sana Waheshimiwa. Nashauri, Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilizane. La kwanza; zile Wizara mbili zenyе majibu marefu mnajifahamu sitaki niwataje, naomba kabisa kwa siku za usoni majibu yetu yawe mafupi.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Zainab Mwamwindi amba ni viongozi wa CCM Wilaya ya Iringa Mjini pamoja na Madiwani wa CCM katika Manispaa ya Iringa wakiongozwa na Ndugu Said Rubeya, wako wapi? Karibuni sana lakini Waheshimiwa kabla hamjakaa karibuni sana kwenye ukumbi huu na kwenye *gallery* hizi za Bunge. Lakini kwa namna ya pekee tuwapongezeni sana sana kwa kazi nzuri mnayofanya katika eneo lenu la utawala, katika Manispaa ya Iringa na nafahamu hiyo Mheshimiwa Msigwa simuoni hapa. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Yupo mahakamani.

MWENYEKITI: Hiyo ndiyo *team eleven* ya CCM katika Manispaa, lakini kwa namna ya kipekee, kaeni sasa. Kwa namna ya pekee kwa sababu nafahamu mionganini mwa hawa Waheshimiwa Madiwani wetu yupo ndugu yetu na kwangu ni rafiki yangu na ni Meya Mstaafu wa Manispaa ya Iringa, Ndugu yetu Amani Mwamwindi. Karibu sana. (*Makofi*)

Lakini Waheshimiwa Wabunge mfahamu pia sasa huyu ndiyo mume wa Mheshimiwa Mwamwindi, shemeji yetu huyo. Ni Meya wetu mstaafu wa Iringa Mjini.

MBUNGE FULANI: (*Hapa hakutumia kipaza sauti*).

MWENYEKITI: Sasa hayo ni yako lakini muone timu hiyo, *first eleven* hiyo. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Tunaendelea. Angekuwepo Mheshimiwa Msigwa ningesema na mengine. (*Kicheko*)

Tunao wageni 17 wa Mheshimiwa Justin Monko ambao ni walimu na wanafunzi wa shule ya msingi ya Kinyamwenda kutoka Mkoani Singida wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya shule, Ndugu Hamisi Ngura. Waheshimiwa Wabunge Shule ya Kinyamwenda kati ya Itaja Wilaya ya Singida, imeshika nafasi ya kwanza Kiwilaya kati ya shule 93 na nafasi ya nne Kimkoo. Wanafunzi wote 26 walofanya mitihani walifaulu 14 kwa daraja la A na 12 kwa daraja la B. Hongereni sana ninyi, walimu lakini pia na wazazi na walezi. (*Makofi*)

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa Desderius Mipata ambao ni watoto na wajukuu zake kutoka Nkasi, Mkoani Rukwa wakiongozwa na mdogo wake ndugu Gallos Mipata. Karibuni sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 50 wa Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ambao ni wanamazoezi kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Said Suleiman Said. Karibuni sana wanamazoezi, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 51 wa Mheshimiwa Yahaya Massare ambao ni vijana kutoka Mkoa wa Singida wakiongozwa na Mwenyekiti wa Vijana CCM-Mkoa, Dkt. Denis Nyiraha. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Kundi la pili la wageni, hawa wamekuja kwa ajili ya mafunzo; tuna mgeni mmoja kutoka Jijini Dodoma ambaye amekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake ambaye ni Ndugu Edwin Barongo. Karibu sana. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Tuna mgeni kutoka *Shikana Law Group* ya Jijini Dar es Salaam ambaye ni Mkuu wa Shirika hili, ndugu Amness Swedi Kagaesheki na ye ye amekuja kwa mafundo, Kagasheki!! Karibu sana. (*Makofii*)

Tunae pia ndugu Naum Fungo ambae ni mjasiriamali wa *VICOBA* kutoka Mkoa wa Njombe. Karibu sana wageni wetu makundi yote mawili. (*Makofii*)

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa Mwamoto wakiongozwa na Mchungaji Kiyeyeu kutoka Iringa. Wageni kutoka Iringa karibuni sana wageni wetu na Mheshimiwa Mwamoto Balozi wetu wa mambo mengi, anafanyakazi nzuri, tunaendelea. (*Makofii*)

Tangazo, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa William Ngeleja anataka awatangazie kwamba matokeo ya mechi zilizochezwa siku ya Jumapili, tarehe 11 Novemba 2018 yaani jana kwenye uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma ni kama ifuatavyo; *Ndugai Boys* yaani *Bunge Sports Club* iliwafunga *VETA* ya Dodoma goli moja kwa sifuri na nyota wa mchezo huo alikuwa ni Mheshimiwa Abdallah Haji. Hongereni sana. (*Makofii*)

Kwa upande wa *netball*, *Bunge Sports Club* iliwabugiza bila huruma timu ya *VETA* jumla ya magoli 31 kwa 19 na nyota wa mchezo huo alikuwa Mheshimiwa Hawa Mwaifunga Bananga. Hongera sana Mheshimiwa Hawa. (*Makofii*)

Mgeni rasmi katika michezo hiyo alikuwa siyo mwingine bali ni Naibu Spika wa Bunge letu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. *Bunge Sports Club* inawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwa kujitokeza kwa wingi kushuhudia michezo hiyo na mazoezi yanaendelea kwa ajili ya kuijandaa na Mashindano ya Mabunge ya Afrika ya Mashariki. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo. Katibu!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. COSATO D. CHUMI: Mwongozo wa Spika, Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba mwongozo wako kutokana na Kanuni ya 68(7) jambo lilitotokea humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba mchezo wa mpira wa miguu mbali ya kuwa ni mchezo unaopendwa sana, lakini pia ni mchezo ambao kwanza ni chanzo cha ajira, lakini pia ni chanzo cha mapato. Hapa ninapozungumza hali ya ligi kuu ya nchi yetu ambayo kama nilivyosema ni chanzo cha ajira, chanzo cha mapato lakini ubora wake ndiyo ambao unakwenda kujenga timu bora ya Taifa. Timu zinazoshiriki ligi kuu hali ni mbaya kwa sababu ya kukosa udhamini kama ambavyo ilivyokuwa katika msimu uliopita na misimu mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba mwongozo wako, Serikali inasema nini juu ya hali hii ili iweze kuwasaidia TFF kushirikiana nao kutafuta mdhamini ila siyo kuokoa mpira wa Tanzania lakini pia kama nilivyosema mpira ni ajira, mpira ni mapato, mpira ni biashara, mpira ni uchumi. Tunakoelekeea kune uwerekano baadhi ya timu zikashindwa kuendelea kushiriki ligi kuu. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chumi kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) suala hilo halijatokea humu, huo ukata wa timu zetu zinazoshiriki kwenye ligi kuu halijatokea mapema humu Bungeni ili niseme kama linaruhusiwa au la. Lakini kwa vile Wizara yenye dhamana na masuala haya ipo na limetokana na swali la mwisho katika maswali yaliyopo kwenye *order paper* ya leo, nadhani walichukue waone

namna wanavyokwenda nayo kukabiliana na hali hiyo mbaya kifedha.

Mheshimiwa Mzee wa *NIPA*, Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuomba mwongozo wa kiti chako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kanuni ya 68(7) nasimama hapa nikiomba mwongozo wa kiti chako; kumekuwa na utaratibu sasa hivi kutoka kwenye upande wa Mawaziri hasa wanapokuwa wanajibu maswali ya msingi na kwamba mara nyangi wanaweza wakajibu majibu ya hovyo kabisa yasiyoendana na maswali yale ya msingi ambayo watu wanataka kuyasikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kiti chako kama siyo wewe basi wengine wamekuwa pia wakizua nafasi ya ule muda wa miongozo ambao uko Kikanuni kutoa taarifa, kuleta ule muda wa miongozo na mengine mengi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitokea hapa ndani Mheshimiwa Kabudi juzi wakati anajibu swalii la Mheshimiwa Zitto lakini akatumia maneno ambayo kwa kweli siyo ya Kibunge, kumueleza mtu kwamba umetumwa, umeelekezwa, unatumika, wewe siyo mzalendo ni kama namna fulani ya *ku-intimidate*.

Sasa nataka kiti chako kitueleze wazi ni wakati gani sisi kama Wabunge tunafanya kazi yetu ya Kibunge na ni wakati gani sisi kama Wabunge tunaweza kushutumiana wenyewe kwamba tunatumika, tunaelekezwa na sisi siyo wazalendo ili ielewewe kwamba ni nani anafanya sasa uzalendo, ni nani anaishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wa kiti chako.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwambe, Kanuni hiyo ya 68(7) lazima liwe jambo ambalo limetokea mapama leo. Umetoa mfano ambao haujatokea leo kwa hiyo, huo ndiyo muongozo wangu kwa hicho ulichokiomba. Mheshimiwa Godbless Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu linahusu *section 47* ya Kanuni za Bunge...

MWENYEKITI: *Section?*

MHE. GODBLESS J. LEMA: ...kifungu 47 ya Bunge kuahirisha shughuli zake kwa ajili ya jambo la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo liko katika vyombo vya habari kuhusiana na kauli ya Mkurugenzi wa TAKUKURU...

MWENYEKITI: Nisomee tu kwanza.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Kifungu cha 47(1)Baada ya muda wa maswali kuisha Mbunge yoyote anaweza kutoa hoja kwa shughuli za Bunge kama zilivyoonyeshwa kwenye orodha ya shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma.

(2)Hoja ya namna hiyo itakuwa ni maalum na inaweza kutolewa wakati wowote hata kama majadiliano yatakuwa yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge ndiyo chombo pekee ambacho kinatunga na kubadili sheria. Kuna *statement* ambayo imeleta tahaaruki kubwa sana katika umma, kauli iliyotolewa na Mkurugenzi wa TAKUKURU Kamanda Diwani ya kwamba makosa yote yanahusiana na masuala ya rushwa yote sasa yataingia kuwa ni masuala ya uhujumu uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Sheria ya makosa ya rushwa, *section 15* ya *Prevention and Combating of Corruption*, *section 15* inaelezea ni makosa gani ambayo hayawezi kuingia kwenye hiyo *Economic Crimes Act*, lakini kauli ya Mkurugenzi wa TAKUKURU inaonesha sasa *matter* yoyote ambayo inahusiana na mabo ya rushwa *automatically* itaingia katika masuala ya *economic crimes*. Na ni wazi kwamba masuala ya uhujumu uchumi na masuala ya *Money Laundering Act* yameanza kutumika katika Nchi hii kama kuumiza watu tofauti kabisa na mtazamo wa masuala yenye wewe yalivyo, hili jambo ni *serioussana*. Magereza wamejaa watu, watu wana...

MWENYEKITI: Enhee!!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba suala hili Waziri mwenye dhamana aseme hiyo kauli ya Mkurugenzi wa PCCB ni Bunge lipi lilibadilisha sheria wakati sisi tupo Bungeni hatujaona jambo kama hili limebadilishwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Godbless Lema umeomba kwenye dharura, kanuni ya 47 na hiki kifungu hiki Waheshimiwa Wabunge kina sura mbili, hatua ya kwanza ni ombi kwa kiti ili kiweze kupima, unasema kwa kifupi tu kiweze kupima kama kweli suala hilo ni la dharura kikisharidhika kwamba ni la dharura ndiyo unaruhusiwa sasa utoe na iungwe mkono na utaruhusiwa kuijadili.

Katika hatua hiyo ya kwanza ambayo ndiyo umejaribu kusema, uamuzi wangu ni kwamba sioni dharura yoyote kwa suala hilo. Kwa sababu kwamba ni masuala ya kwenye mtandao lakini sisi kama Wabunge ambao ndiyo tunaishauri na kuisimamia Serikali ungelipenda tu wewe ukalipata kwa uhakika na likaja kwa uhakika kwamba haya ndiyo maamuzi ya Serikali na sisi kama Wabunge hatukumbuki kama imekuja sheria au muswada wowote unaofanya marekebisho ya kuingiza makosa yote ya rushwa kwenye makosa ya uhujumu uchumi. Sasa tukienda kwa namna hiyo ndio itakuwa tunaenda vizuri kwa kazi yetu ya Kibunge.

Nilikuwa nasema, pamoja na hayo Serikali imesikia, lakini wewe kama unataka kuliendeleza suala hili, nakuomba uliletie vizuri, siyo kwa namna hii. Huo ndiyo mwongozo wangu kwa leo. (*Makofi*)

Tunaendelea, Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

KAMATI YA MIPANGO

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa
Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali Pamoja na
Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya
Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nina orodha ya wachangiaji wetu wa leo kutoka makundi yote yanayowakilishwa humu Bungeni, lakini ili kutenda haki, tuko kwenye Kamati lakini bado naweza nikawahoji tu ili twende vizuri, ni kuhusu muda wa kuchangia. Mnaonaje tukichangia kwa dakika saba ili wengi wapate?

WABUNGE FULANI: Ndiyooo.

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa tunaanza na Mheshimiwa Martha Mlata. (*Makofi*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naamini dakika saba zinatosha kwa sababu wachangiaji wengine wameshazungumza mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nimshukuru Mungu kwa kupata nafasi hii ili niweze kutoa maoni yangu

katika hoja hii iliyoko mbele yetu. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu pamoja na watendaji wote. Kwa kweli kazi imekuwa ni nzuri, tumeiona, tunaomba mwendelee hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Kiongozi wetu Mkuu, ambaye ameweza kwa kweli kuweka *discipline* katika Serikali hii kwenye makusanyo na sasa hivi tunayapata na tuona fedha zinakwenda kwa wakati. Nampongeza pia kwa namna ambavyo mipango imepangwa na inaendelea kuonekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza namna ya kukuza uchumi na kukamilisha mipango yetu ambayo iko mbele yetu, tumeona ni namna gani jithada zinafanyika kukuza uchumi upande wa ngazi za Kitaifa zaidi. Miundombinu mingi inayoendelea sasa hivi, hiyo yote inakuja kutusaidia namna ya kwenda kwenye uchumi wa kati na kutekeleza mipango ambayo tumejiwekea wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri kwenye upande wa kuziwesha Halmashauri zetu na kuzijengea uwezo kukuza uchumi kwa sababu wananchi wanyonge ambao tunawategemea ndiko waliko kule chini na vyanzo vingi vya mapato viko kwenye Halmashauri zetu. Nazungumza haya kwa sababu ninataka kuwe na uchumi shirikishi ina maana Wizara nydingi ziweze kushirikiana namna ya kuweza kukuza uchumi kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nikianza na upande wa ujenzi wa barabara za vijijini. Ujenzi wa barabara za vijijini utaweza ku-*support* mazao ya wananchi wetu waweze kujipatia masoko ili kukuza uchumi wao. Kwa hiyo, naomba sana *TARURA*, kwa sababu *TANROAD* wanapojenga barabara za Kitaifa ni lazima pia *TARURA* waongezewa fedha ili waweze kujenga barabara nzuri kule vijijini wananchi wetu

waweze kusafirisha mazao yao kwa urahisi zaidi kufikia kwenye soko. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema barabara ni lazima pia pembejeo zipelekwe kwa wakulima kwa wakati. Kwa mfano, mbegu na vifaa vyote ambavyo vinahitajika kwa wakulima ni lazima vipelekwe kwa wakati. Kwa hiyo, wakulima watalima vizuri, mazao watapata mengi, watapata barabara nzuri, wataenda kuuza mazao yao, tayari Halmashauri zetu zitawenza kukusanya mapato kutoka kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki mwengine ni kwenye upande wa maji. Haiwezekani ukamwacha mwanamke nyuma. Uki sema kwamba mwanamke ashiriki kwenye shughuli za kukuza uchumi, mwanamke hana maji, muda mwengine anashinda kutafuta maji, upande wa uzalishaji anatumia kidogo sana. Kwa hiyo, naomba sana, kwenye upande wa suala la maji fedha zipelekwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi imeshagundulika, maeneo yote mmejua, watu wanahitaji maji wapi, miradi inafanyiwa upembuzi lakini fedha haziendi. Tunaomba Hazina watoe fedha kwa wakati, ziende kwenye Mfuko wa Maji au Wakala wa Maji Vijijini, vyovyyote itakavyokuwa. Tunahitaji maji, tumtue mwanamke ndoo aweze kushiriki shughuli za maendeleo na kujijengea uchumi wake ye ye na familia yake lakini na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunapozungumzia zile fedha asilimia 10, Halmashauri haziwezi kukusanya fedha kutoka kwa watu wake kama hakuna miundombinu ya kuwfanya watu waweze kufanya biashara ili Halmashauri zikusanye fedha. Tunahitaji vikundi vipate fedha za kutosha. Kwa hiyo, Halmashauri zitakusanya fedha kwa sababu umeme utasambazwa wa kutosha, watu watafanya shughuli zao, watafanya biashara, Halmashauri watakusanya fedha; wanawake na vijana watapata fedha nyingi kwa sababu Halmashauri watakusanya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji akina mama wafanye biashara kubwa, wasiishie kuza vitumbua na vitu vidogo vidogo. Waanzishe na wao viwanda, wasafirishie bidhaa zao mbali, waanzishe mashamba na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, naomba sana kwenye upande wa uchumi shirikishi, Wizara zote zishirikiane kuhakikisha Halmashauri zetu zinapata vitega uchumi ambavyo wataweza kukusanya fedha za kutosha na kuwawezesha wananchi kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda nilizungumzie sana, wewe ni shahidi, ukienda vijijini kule wananchi wengi sana wana shida, wanataka waondoke kwenye umaskini walionanao. Mheshimiwa Rais ameshagundua, kwani anapopita anakutana na makundi mengi ndiyo maana ameamua kuacha suala la Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, nimirrie moyo, aachane na suala la Katiba. Wananchi hawahitaji Katiba, wananchi wanahitaji maendeleo, wanahitaji mpeleke miundombinu ambayo itawasaidia watokane na hali waliyonayo. Nataka niendeleee kumtia moyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukikuta kuna mtu anakupongeza na ni mpinzani wako, jiulize mara mbili. Wenzetu hawa wamekuwa wakizungumzia suala la Katiba, ni Katiba ipi? Mimi nilikuwepo humu ndani, walitoka na wala hawakuiunga mkono. Naomba shetani anayewanyemelea ili kuja kutaka kuvuruga mipango mizuri aliyonayo Mheshimiwa Rais wetu na ashindwe kabisa, tena mimi nasema alegee. Sisi tunataka tusonge mbele, Mheshimiwa Rais songa mbele, wananchi wanahitaji maendeleo wala hawahitaji Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine...

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. MARTHA M. MLATA: Nimesema ashindwe!

MWENYEKITI: Taarifa.

TAARIFA

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mwongeaji anaendelea sasa hivi kwamba kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi, mimi ninayo kopi kwa sababu huwa tunasoma, wakikosea namna hii tuwarekebishe, ukurasa wa 207 wanaongelea suala la Katiba Mpya. Kwa hiyo, naye aichukue hii akasome vizuri, inalekea haijui llani ya chama chake. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshmiwa endelea na mchango wako, unasemaje?

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, shetani alipotupwa duniani alikaa kwenye mioyo ya watu na ameleta mambo makubwa. Kwanza kupinga kila kitu....

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa hii fursa adimu. Pamoja na shukurani kwako, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wake kwa mapendekezo mazuri na nategemea akichukua mawazo na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, Mpango utakaotoka baadaye utakuwa mzuri kupita kiasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru vilevile Mpango huu kufunganishwa na maendeleo ya watu. Napenda kuendelea kuanzia pale kwamba unapofungamanisha Mpango na maendeleo ya watu, unajua kabisa dira

tuliyoweka itafikiwa. Nataka tuanze na kilimo ambayo ndiyo shughuli ya Watanzania wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Serikali imefanya kazi kubwa ya kupeleka umeme vijijini na hata maji kwa kuunda Mfuko wa Maji na vilevile barabara za vijijini kuundiwa Wakala kwa sababu ndiyo namna pekee ya kuwezesha kilimo kwani bila kuongeza kilimo, hatutakuwa na viwanda ambavyo vitaleta maendeleo ya watu. Kwa hiyo, naomba sana Mpango wetu ujielekeze kwenye kuweka viwanda ambavyo vitasindika mazao ya kilimo na wakati huo huo yatatupeleka kwenye sekta ya viwanda ambayo ndiyo azma yetu kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo, kulikuwa na miradi elekezi yaani miradi ya vipaumbele na bado ipo. Naomba niongelee Mradi wa Mchuchuma. Mchumchuma ni kiwanda mama kama tutatekeleza. Hakuna kiwanda kitajengwa bila kutumia vyuma na hata reli ya kati na reli nyingine zinatumia chuma, hata barabara kwenye madaraja chuma kinatumika. Naomba sana maandalizi na majadiliano yaishe, Liganga itekelezwe na hapo ndipo tutakuwa na uhakika wa sekta ya viwanda kuendelezwa na uchumi wetu kuwa wa viwanda na kutufikisha kwenye mapato ya kati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nalopenda kuongelea ambalo liilikuwa ni kipaumbele ni pamoja na *Kurasini Logistic Center*. Tulianzisha *Kurasini Logistic Center* ili Tanzania ili iwe *hub* ya Afrika kama Hong Kong ilivyokuwa kule Asia. Kama hatutekelezi *Kurasini*, Tanzania itakosa kuwa *hub* na *hub* hiyo itapelekwa mahali pengine. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Tanzania ni *centerya* Afrika na nchi ambayo ina bandari. Kwa hivyo, naomba tuanzishe Mradi wa *Kurasini Logistic Center* kwa sababu nchi nyingine zote zitakazozunguka Tanzania zitakuja *Kurasini* na kwa hiyo, mapato ya nchi yataongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, *Logistic Center* itatuonyesha ni viwanda gani ambavyo vina mahitaji au *demands*. Kwa hiyo, itaashiria wawekezaji watakapokuja waanzishe viwanda gani. Kwa hiyo, naomba *Logistic Center* ianze mapema kusudi tujue viwanda vitakavyoanzishwa ni vile ambavyo Afrika mahitaji yake yatatoka pale na hata kwenda duniani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana sekta binafsi iunganishwe, lakini pale ambapo sekta binafsi haiwezi kwenda, Serikali iende kama mahitaji yako pale. Kwa sababu tunaanzisha viwanda ili kuongeza thamani ya mazao na vitu kama madini lakini vilevile mahitaji ya watu yatakuwa yanapatikana Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tumuunge mkono Mheshimiwa Rais wetu ambaye hana mchezo, ambaye anaonekana kwamba anaitakia mema nchi hii kwa kuweza kutoa michango mizuri ili Mpango utakaokuja uwe ni ule ambao utatekeleza yale yote ambayo yeye ndiye anaongoza lakini na sisi Bunge tuko pale kusaidia kwa sababu hapa tunawawakilisha watu, tunayoyasema ni yale ambayo wananchi wetu wanataka. Wilaya ya Hanang ingetaka viwanda vya kilimo kwa sababu ni Wilaya ya kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nawahakikishieni kwamba Serikali inafanya kila njia zao la mbaazi sasa linapanda bei, kwa hiyo, Serikali imefanya kazi na wananchi wa Hanang wameshukuru. Tunaomba vilevile na mazao mengine kama mahindi ambayo bei yake iko chini, tuifanyie kazi na bei iongezeke ili iwafanye wakulima walime zaidi, kwani hawawezi kulima kama mazao hayanunuliwi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna ya kuhakikisha kwamba mazao ya kilimo yanaendelea kulimwa, ni kuhakikisha kunakuwa na viwanda vinavyosindika, vinavyoongeza muda wa mazao kukaa na mahitaji ya watu, lakini vilevile vinaongeza pato la watu. Naona nyumba za bati zimeongezeka. Kwa hiyo, anayesema kwamba uchumi unarudi chini, hasemi ukweli, kwa sababu katika Wilaya

yangu naona watu wanajenga nyumba za bati ambazo hazikuwepo na naona barabara zinakwenda vijijiini. Tuungane na Serikali Mpango utakaotoka uwe ni ule ambao utatupeleka mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Hasna Mwilima na Mheshimiwa Julius Kalanga ajandae.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mipango pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Nina hakika kabisa mwanzo tulikuwa hatujui nia yako, wengi tulikuwa tunakulaumu kwa kweli, lakini sasa hivi mambo yanakwenda vizuri, kwa hiyo, wewe endelea kufanya kile ambacho unafikiria. Kazi yetu sisi ni kukupa ushauri, nami leo nitajikita kwenye kutoa ushauri zaidi kwa sababu ndiyo kazi ya Mbunge badala ya kulaumu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la umeme, bwawa la *Stiegler's Gorge*. Mpango ni mzuri, nami nina hakika kwa kuwa tunakwenda kwenye nchi ya viwanda, tunaangalia wapi tutapata nafuu ya umeme kwa sababu viwanda bila umeme itakuwa ni ndoto. Napenda tu utakapokuwa unatoa majibu baadaye uweze kunipa ufanuzi kwenye baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunatumia mafuta kwa ajili ya umeme wetu Tanzania na gharama yake ilikuwa ni shilingi za Kitanzania 546. Baadaye tukafikiri labda twende kwenye gesi tukaainisha, tukaanza kuchimba gesi na gharama yake ilikuwa ni shilingi za Kitanzania 147. Tukaingia kwenye upopo pia, ikaonekana ni gharama kubwa, ni karibu shilingi 206. Baadaye tukagundua kwamba tukianza kutumia

lile bwawa la *Stiegler's Gorge* tutatumia shilingi za Kitanzania 36 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa tayari tumeshaona tunakwenda kwenye nchi ya viwanda na unafuu uko kwenye maji, naomba twende *speed* ili kuhakikisha tunaanza kutumia umeme wa maji, lakini tu tupate taarifa hatma ya gesi itakuwaje? Kwa sababu wenzetu wa Mikoa ya Kusini walishajiaminisha wakijua wameshapata ukombozi na gesi itatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nafikiri litasaidia kukuza uchumi wetu ni pamoja na kuangalia sasa, kwa mfano ukienda kwenye mifugo, mpaka leo hatuna mipango mahsus ya kuimarisha viwanda vyetu. Kwa mfano, Kiwanda cha Maziwa, Tanzania hii ukiuliza habari ya Kiwanda cha Maziwa, kiwanda kikubwa sasa hivi ni ASAS ambacho kiko kule Iringa. Nawapongeza sana watu wa Iringa kwa sababu kinafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kingine kiko kule Tanga. Hatujapata taarifa kama kuna viwanda vingine ambavyo vipo vinafanya kazi hiyo sasa uchumi utakuzwa pipi? Tuelezwe kwamba baada ya kwenda kwenye viwanda na tayari tuna Mawaziri, naipongeza sana Wizara ya Mifugo pamoja na ndugu yangu Mheshimiwa *Comrade Ulega* kwa kazi nzuri ambayo wanafanya, wanazunguka nchi nzima kuhamasisha lakini bado kuna matatizo kwenye suala la ufugaji. Kwa sababu gharama ya madawa iko juu, aina ya ufugaji bado watu wana ng'ombe wengi lakini siyo ufugaji wa kisasa. Kwa hiyo, nashauri tu elimu ya kutosha itolewe ili mifugo isaidie kukuza uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye suala la mifugo, naomba ndugu zangu, suala la uchomaji wa chapa ni la kizamani sana. Tujue kwamba tutakapoanzisha viwanda vyaa ngozi zile ngozi itabidi zitumike, lakini ukishaichoma vile ile ngozi haina thamani. Kwa hiyo, nafikiri kuna njia mbadala ambazo tukishirikishwa tunaweza tukatoa mawazo ili

tuachane na kuchoma chapa tuweke alama ambazo zinasaidia kusukuma mambo yakaenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni la kilimo cha mahindi. Watu wamelima sana mahindi lakini soko bado ni tatizo. Kwa hiyo, nafikiri Serikali isikate tamaa kwa sababu mahindi mengi ya mwaka juzi na mwaka jana bado wananchi hawajauza, hii imekatisha sana tamaa na ukiangalia bei ya mbolea, iko juu sana. Nafikiri Serikali kwa kuwa yenye we ina uwezo, ingeangalia jinsi gani iweze kuwasaidia wananchi ili kupunguza bei za mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni la michezo. Hatujaweka mipango mizuri kwenye michezo. Mwakani tuna mashindano tuna mashindano makubwa ya *AFCON* na tunategemea tutapata wageni wengi wa kidunia. Sasa nafikiri kwenye mipango yetu tungeainisha kwamba michezo iende na utalii, kwamba wale wageni watakaokuja wote tuhakikishe wanakwenda kufanya utalii ili fedha ile waiache hapa lakini sijaona kabisa kama kuna sehemu ambayo imezungumzwa jinsi gani unahusisha michezo na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nchi kama Cameroon, Nigeria, Burkina Faso uchumi wake unategemea michezo. Wanauza wachezaji nje, michezo inaingiza zaldi ya asilimia 45. Tanzania ukishiriki michezo inaonekana kama wewe ni mjanja mjanja, huna uelekeo, lakini sehemu nydingine michezo ni kazi. Mheshimiwa Waziri kuna watu ambao unaweza ukakaa nao kwenye hii nyanja ya michezo mkapeana ushauri wakakwambia jinsi ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda bado ninao, nizungumzie suala la *EFD machine*. *EFD machine* imetusaidia sana kukusanya fedha. Kwa hiyo, naomba itolewe elimu ya kutosha ikiwezekana hata hizo mashine gawa kwa sababu ile fedha inasaidia kwenye uchumi wa nchi. Wengi unapowaambia lipa halafu tutakata kwenye kodi, zako hawaelewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni la trafiki. Leo kaka yangu Waziri mahiri kabisa yupo, tuna shida huko na tunalalamikiwa. Uhampa fundi kwenda kutengeneza gari, anapigwa faini na trafiki, anakuja kukamatwa mwenye gari...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwilima.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Mpango huu wa Serikali. Nampongeza kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango pamoja na Naibu Waziri wake. Pia naipongeza Serikali kwa kuona namna ya kutuletea mipango mizuri ya utekelezaji kwa maana ya miradi ya vielelezo, mazao ya kimkakati na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia Mpango, natoa pole kwa wananchi wangu wa Kijiji cha Mpeta, Mwandubantu kwa maafa makubwa yaliyowakuta yaliyosababisha maaskarri kuchinjwa na kufariki dunia na yaliyosababisha baadhi ya wananchi kufariki. Nina imani na Serikali, kwa kuwa nimeshalileta mbele ya Mheshimiwa Spika, Serikali haitakuwa na kigugumizi katika kufanya maamuzi na kutenda haki kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kigoma Kusini, hususan Kijiji cha Mpeta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu nitazungumzia mpango wa barabara ya kutoka Uvinza mpaka Kijiji cha Mpeta. Wananchi wakinisikia naizungumzia barabara, sizungumzii mateso na manyanyaso wanayoyapata kwa uongozi wa utawala wa Uvinza, nitakuwa sikutenda haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, sote tumemsikia jana Mheshimiwa Kangi Lugola, amefanya maamuzi mazito ya kuwavua vyeo *OCDs* wa Uvinza, Afisa Upelelezi wa Polisi Uvinza na aliyekuwa Kaimu *RPC* wa Mkoa wa Kigoma. Swali langu, Mawaziri wote waliokwenda, wananchi wamesema hadharani, akina nani wanahusika katika mauaji yale. Leo unapowatao mapolisi wanaopewa *order* na watawala, ni uonevu, ni lazima Serikali ichukue hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama wananchi wa Kigoma, tunataka tuone Serikali inachukua hatua kwa wahusika wote. Wako wanaosema wao wana viongozi pale Ikulu wanaowatetea, tunataka tuone, ndani ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, nani yuko juu yake? Nani ambaye anaweza akachukua rushwa kwa wafugaji na ushahidi upo lakini mpaka leo hukumu haichukuliwi wala hatua hazichukuliwi? Naiamini Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, namwamini Mheshimiwa Waziri Mkuu na namwamini Spika, naomba haki itendeke. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee na Mpango. Huwezi kuuzungumzia Mpango hujatetea wananchi waliokupigia kura. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu *SGR, Central Line*. Tunaishukuru sana Serikali kwa kuanza kuijenga reli hii ya kiwango cha *Standard Gauge*. Mimi niko kwenye Kamati ya Bajeti, tulimwomba Mheshimiwa Waziri kwamba kwenye Mpango huu haioneshi kwamba hii reli ya *Central Line* au kwa maana ya ujumla wake hii *Standard Gauge* inapita wapi na wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 14 amejaribu kuielezea kwamba Tabora hadi Isaka kilometa ngapi; Isaka – Mwanza kilometa ngapi; Tabora – Uvinza – Kigoma kilometa ngapi. Namwomba Mheshimiwa Waziri, isiishie tu kwenye hii taarifa yake, tunaomba kwenye Mpango ionekane, hata kama itachukua miaka mitano ijayo, lakini tuoneshe kwenye

Mpango kwamba ya kutoka Tabora mpaka Kigoma nayo itakuwa kwenye utekelezaji na utekelezaji wake utafanyika lini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu huwezi kuzungumzia *Central Line* kwa maana ya ujenzi wa *Standard Gauge* usiiguse *line* inayokwenda Kagera ambayo inaunganika mpaka Rwanda, usiiguse na hii inayokwenda Kigoma inayokwenda kunufaisha Wazambia, Wakongo na Warundi. Tunapoweka hii mipango mikakati ya vielelezo, tuangalie mipango ambayo itaiingizia kipato Serikali. Hii *Standard Gauge* ikijengwa ina maana kutakuwa na uhakika wa mizigo yote inayokwenda Kongo, Burundi na Zambia kupitia katika hiyo *Central Line*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie Bandari ya Kigoma. Nimeona kwenye Mpango Bandari ya Bagamoyo imezungumziwa humu na imeingizwa katika Mpango wa *PPP*, Bandari ya Kigoma imekuwa inazungumzwa lakini utekelezaji wake haufanyiki na tunajua manufaa makubwa ambayo yatapatikana kwa ujenzi wa bandari yetu hiyo. Kwa hiyo, naomba Serikali iwe inaangalia ile mipango ya vielelezo au miradi ya vielelezo ambayo itakuwa na tija katika kuiingizia kipato Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kidogo hali ya miradi ndani ya Jimbo langu. Kwenye mazao ya mkakati, nimeona mazao yote yametajwa lakini kwenye Mpango zao la mchikichi haljazungumzwa. Tunaomba sana, tunajua Wizara ya Kilimo imeomba shilingi bilioni 5 kwa ajili ya kuzalisha miche milioni 20 ndani ya miaka minne. Naomba sana wapatiwe hiyo shilingi bilioni 5 ili mchikichi izalishwe. Ikalishwa haitakuwa tu na manufaa na watu wa Kigoma bali nchi nzima ili zao hili la mchikichi liweze kuipatia mapato mengi sana Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Malaysia zao la mchikichi ni chanzo cha tatu kinachowaingizia mapato...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hasna.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Godbless Lema, atafuatiwa na Mheshimiwa Julius Kalanga na Mheshimiwa Shally Raymond ajiandae.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naomba kuchangia juu ya jambo hili mahsusи kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahali popote duniani hofu (*fear*) huwa inaua *innovations*. Hatuwezi kuwa na mipango yenye *stability* kwa kiwango cha hofu ambacho Taifa hili linacho sasa. Wafanyabiashara wa ngazi zote, kuanzia wenyе viwanda na *traders* wana hofu kubwa sana katika Taifa hili kwa wakati huu. *TRA* siyo rafiki, *task forces* ambazo zinaundwa kwa ajili ya wafanyabiashara siyo rafiki na *attitude* ya TAKUKURU dhidi ya wafanyabiashara siyo rafiki. Mheshimiwa Dkt. Mpango angefahamu ni *capital* kiasi gani inahama katika Taifa hili sasa kwenda Mataifa ya jirani ange-realize kwamba mipango hii inaweza ikaja kuwa ni migumu sana kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haiwezi ku-*survive* bila wafanyabiashara kuwa na *peace*. Kwa sababu mbia namba moja anayeisadia Serikali ku-*survive* katika masuala ya kodi ni mfanyabiashara au mbia namba moja wa mfanyabiashara ni Serikali. Leo ukienda kwenye madini, korosho, mbaazi, samaki, Kariakoo na kila mahali wafanyabiashara wana hofu kiasi cha kwamba wanaanza ku-*allocate* biashara zao kwenye Mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu inaua *innovation*. Ukienda kwenye ofisi za Serikali, juzi tulikuwa na Mawaziri

asubuhi, jioni siyo Mawaziri. Leo *statement*nyingine imetolewa, hatujui hadi 2020 kama tutafika na hawa waliopo. Hizi *statements* zinaonekana ni za kawaida lakini zinaua *creativity*, zinaua *confidence*. Waziri hawezi kuwa na maana kama hawezi kuwa na *confidence*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Waziri aweze ku-*behave*, aweze kuwa na nguvu, anahitaji *confidence*. Leo katika Taifa hili Mkuu wa Mkoa anaweza akawa na sauti kuliko Waziri na *DC* anaweza akawa na sauti kuliko Waziri. Tumeshuhudia mambo haya, tumeona *statements* za Wakuu wa Mikoa, tumeona *statements* za ma-*DC* wakifanya *embarrassment* kwa wawekezaji. Inafika mahali *DC* anasema mweke ndani huyu mwekezaji saa zangu 48 ndani, watu wanaona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya utajiri ama mafanikio ni ku-*enjoy* lle *prestige*, ni ku-*enjoy* heshima, watu hawa wanaanza kukosa hiyo *prestige*, wanachokifanya sasa ni kuanza ku-*allocate*, kuondoa mali. Leo kesi zilizoko Mahakamani, wafanyabiashara walioko Magerezani, unakamatwa na dola 9,000 mfanyabiashara wa *hunting*, unapewa kesi ya *money laundering!* Dola 9,000 ni hela gani ya kwamba mtu anakamatwa nayo anapewa kesi ya *money laundering* ambayo haina *bail?* Halafu akishapewa kesi ya *money laundering* watu wanamuata Magereza wana-introduce kitu kinaitwa *pre-bargaining*, lipa kiasi hiki cha hela tukuachie. Sasa haya mambo watu wana-*communicate*, wafanyabiashara wana-*communicate* kwenye *circle* zao aidha ni Misikitini ama Makanisani, wanafanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa imetokea *kidnapping* ya Mheshimiwa MO. Jana nimeona sinema nyingine ya Mambosasa. Ile sinema nimeiangalia kwa makini, unashindwa kuelewa ni mtoto kiasi gani anadanganywa hivyo? Yule bwana anayesema kwamba yeye ndiyo aliywapangishia nyumba wale watekaji, huyo bwana kwenye picha anaonekana ni rafiki yake na Dkt. Shika. Kwa hiyo, mmeenda kutafuta Dkt. Shika mwingine, kutengeneza sinema nyingine ya ajabu ajabu, sasa wale watu wanaona. Huyu MO aliyetekwa anajua alipokuwa, anaweza asituambie

sisi akawaambia ndugu zake, ndugu zake wataongea kwenye *circle* zao, wanasubiri tu mambo fulani yakamilike wataanza kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpango msiporudisha *confidence* kwa wawekezaji na wafanyabiashara, mimi niko Arusha, Mererani imekufa kabisa, hali ni mbaya na kwenye korosho hali kadhalika hata huko mitaani hali imeanza kuwa mbaya na hakuna *political stability* katika Taifa hili. Mataifa ya nje kwenye *articles* kubwa kubwa yanatoa kila siku *articles* kuhusu Tanzania. Tanzania siyo sehemu salama ya kuwekeza; Tanzania siyo hivi na hivi na majibu yake yanavyojibwa ni kihuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha billionea kutekwa na Sirro kuja na picha za kamera ya kawaida, watu wanaona. Inaleta hofu kwa *Billionaires Club* ambao ndiyo *fundamental investors* katika mataifa mbalimbali. Leo hali ni mbaya. Hakuna mtu mwenye uhakika; CCM ama CHADEMA, ambaye ikiamuliwa kesho kupewa kesi ya utakatishaji fedha ama uhujumu uchumi atakuwa salama. Kwa maana hiyo sasa hali inazidi kuwa mbaya, huku chini *purchasing power* imepungua, biashara za watu zinakufa, watu wanashindwa kulipa ada na maisha yanakuwa magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mfanikiwe katika mipango hii, rudisheni *confidence* ya wawekezaji na wafanyabiashara, fanyeni watu kuwa na amani. Kuwa tajiri siyo dhambi. Achene yale mambo ya kusema kwamba matajiri wataishi kama mashetani. Tajiri akiishi kama shetani, maskini ataishi kama mtoto wa shetani. Kwa sababu maskini anakuwa *middle class* wakati *upper class* inaongezeka. Sasa watu wanateseka, wanaumia, kesi za ajabu ajabu zinafunguliwa, watu wanatishwa, kila mtu amekuwa ni mbabe, Mawaziri na Makatibu Wakuu hawana *confidence* maofisini, nchi itaendeshwaje? Nchi ili ifanikiwe, haihitaji *Ph.D* peke yake. Haihitaji *Doctor* peke yake kuwa Waziri, inahitaji *confidence* na *creativity* ambayo haipo katika Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Dkt. Mpango haya mambo ninayomwambia ni kweli. Rudisheni *confidence* kwa wafanyabishara. Nilikuwa kwenye msiba Kenya. Nimekaa kwenye msiba, watu hawakujua mimi ni Mbunge. Gavana wa Kenya anasema *capital inayo-shift* kutoka Tanzania kwenda Kenya kwa siku *it is amazing*. Msipozua haya mambo ya kukamata watu na Dola 9,000 mkawapa kesi za utakatishaji, mimi nikiwa nazo za kwangu nyingi nitazipeleka Namanga au Zambia. Kwa hiyo, haya mambo ya kuona matajiri ni adui wa nchi... (*Makofî*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Kalanga, Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Mgimwa.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nami naunga mkono hoja lakini la pili naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu na nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi pamoja na wananchi wa Monduli kwa kunihamini tena na kunipigania kurudi katika nafasi hii ya kuwatumikia. (*Makofî*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walwalizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo tumekuwa tukiyajadili katika Bunge hili kwa muda mrefu kuhusu mustakabali wa Taifa letu. Pia wapo wenzetu ambao tangu Bunge limeanza wao wanafikiri hakuna liliofanyika katika Taifa hili kwa miaka mitatu sasa na ndipo mahali ambapo panaanza kutokea utofauti katika jambo hili. Rais huyu ambaye watu wanasema hajafanya jambo lolote, sisi tumeamua kumuunga mkono, kumtia moyo na kumwambia songa mbele, Watanzania wanaona kazi tunayoifanya. (*Makofî*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, kupongeza siyo dhambi, *ku-appreciate* kazi anayofanya mwenzako siyo dhambi. Kama wenzetu wanaona wana haki ya kupinga tu, nasi tuna haki ya kupongeza na kukubali kazi inayofanywa na wengine. (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wenzangu wanapiga kelele kwa sababu makubaliano yao ni kupinga kila jambo jema linalofanywa na Serikali. Naamini kupanga ni kuchagua; ninyi mmeamua kupinga na wenzenu wameamua kuunga, ugomvi uko wapi?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MHE. JULIUS K. LAIZER: Kwa sababu makubaliano yenu ni kupinga, nataka nionyeshe machache tu ambayo sisi wengine yametugusa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma tulivyokuwa tunaangalia Bunge yapo mambo ambayo Serikali ilishindwa kuyafanya na sasa yamefanyika. Yapo masuala ya ujisadi ikiwepo *ESCROW* na masuala mengine ya wizi wa rasilimali za Taifa ikiwepo madini, Rais huyu ameyadhibiti. Kwa nini tusimpongeze? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, elimu ni haki ya msingi ya kila Mtanzania. Rais huyu amefuta ada watoto wetu wanasoma bure, hilo nalo hamlion? Vituo vya Afya vilivyojengwa kwenye nchi hii ndiyo hivyo hivyo na ninyi 2020 mtaenda kuwaambia wapiga kura kwamba mmejenga vituo vya afya, lakini mkija huku mnappinga.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. JULIUS K. LAIZER: Ndiyo maana tunasema mnahubiri msichokiamini na mnakiamini msichokihubiri. Kwa sababu hayo hayo ambayo yanafanyika katika Majimbo yenu, ndiyo hayo hayo ambayo mtaenda kuombea kura 2020. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Changia mpango.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala linazungumzwa hapa la Katiba. Ukitsemu nichangie Mpango, aliyetoka hapo naye alichangia Mpango, nami nina haki ya kuchangia Mpango huo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili la Katiba, kupanga ni kuchagua. Mheshimiwa Rais wetu hajasema Katiba siyo muhimu, amesema lazima tuwe na Taifa la vipaumbele. Tunalo tatizo la maji kwenye nchi yetu, tunalo tatizo la afya kwenye nchi yetu, sisi tumeamua kwenda na matatizo ya Watanzania wanyonge kwanza ikiwepo maji na matatizo mengine, mpaka wakati ambapo Watanzania wata-enjoymatunda ya nchi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu, naomba niseme machache katika maeneo ambayo nafikiri bado hatujafanya vizuri ili Serikali iongeze nguvu kubwa sana. Iko miradi mikubwa ambayo Serikali imefanya ikiwemo kufufua ndege, miradi...

MHE. KHATIB SAID HAJI: Taarifa, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa. Hebu subiri Mheshimiwa.

T A A R I F A

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji anasema kwamba Mheshimiwa Rais wetu hajakataa Katiba. Nataka nimpe taarifa kwamba Rais akiwa

Nkurumah Hall alisema hawesi kutoa pesa kwa ajili ya Katiba ili watu waje bure. Nampa taarifa hiyo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kalanga.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, mmoja wa wazee ambao ninaowaheshimu kwenye Bunge hili ni pamoja na Mheshimiwa Khatib, lakini nataka nimwambie kwamba Mheshimiwa Rais amesema ataweka vipaumbele katika miradi inayogusa maisha ya Watanzania wanyonge, ikiwepo maji, afya na elimu na ameanza kufanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tumefanya kazi katika maeneo ya afya, elimu na maeneo mengine ya kufufua shirika letu la ndege. Naomba Mheshimiwa Dkt. Mpango aje na utaratibu wa kuunganisha sasa sekta ya viwanda na sekta za uzalishaji ikiwepo ya kilimo na mifugo, ili wananchi wachache na wanyonge wa Taifa hili waweze ku-enjoy matunda ya Taifa na ya uchumi wa nchi hii. Tusipowekeza katika maeneo ya wafugaji na wakulima, hatutakuwa tunawasaidia wanyonge kupata mitaji na fedha ya kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ng'ombe. Wakati wote tunasema nchi yetu hii katika Afrika ni nchi ya pili kuwa na ng'ombe wengi lakini uchumi huu wa ng'ombe unasaidia vipi katika kuimarisha uchumi wa Taifa letu? Nafikiri kama nchi tungeweza kuweka mikakati katika kuanzisha viwanda vya ngozi, nchi yetu tutanufaika na ng'ombe milioni 21 ambao tunao ambapo mpaka sasa uchangiaji katika pato la Taifa haulingani na wingi wa ng'ombe tulionao. Tunataka Serikali ituletee mpango mkakati wa mahusiano kati ya rasilimali za mifugo, kilimo na viwanda katika nchi yetu. Haitoshi tu kujenga viwanda peke yake kama viwanda hivyo havisaidii kuchukua rasilimali zinazozalishwa na wafugaji na wakulima wetu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tumefanya vizuri katika afya na maeneo mengine, tunalo

tatizo kubwa katika eneo la maji. Hili ni tatizo kubwa kwenye nchi nzima. Tunaomba Serikali ije na mpango mkakati kama ilivyofanya kwenye afya na elimu bure ili tuondoe tatizo la maji, wananchi wetu wapate maji, kwa sababu hii ni kero kubwa kwenye nchi yetu, hasa kipindi hiki. Kwa hiyo, naomba tuone tuna mkakati gani wa kumaliza tatizo hili la maji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu la mwisho ambalo nilifikiri Serikali ifanye kazi ya kuwekeza zaidi ni katika eneo la ngozi. Hapa duniani 50% ya ngozi sasa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kalanga. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Mgimwa na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad wajiandae.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii. Namshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai kwetu sote ambao tunazungumzia mambo ya maendeleo ya nchi yetu. Nawashukuru sana wanawake wa Kilimanjaro walionipa nafasi na fursa ya kuwa hapa kupitia Chama changu cha CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ninaupokea Mpango ulioletwa hapa na Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wetu wa Fedha na Mipango. Niseme kwamba, sitakuwa na nafasi ya kuzungumzia mengi, nitajikita zaidi kwenye maji. Niende kwenye kitabu cha Mpango, ukurasa wa 31 ambao unaozungumzia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mafanikio, pamoja na ambalo lilionekana limefanywa vizuri ni huduma za maji, nayo iko kwenye ukurasa wa 31 na imeandikwa kwa mistari minne tu kwenye ile aya ya 12. Anasema, huduma za maji:

miradi 1,595 ya maji vijiji ni imekamilika ikiwa na jumla ya vituo vya kuchotea maji 126,610 na uwezo wa kuhudumia wananchi milioni 31,652,500. Wananchi wanaozungumziwa hapa ni zaidi ya nusu ya wananchi wote wa Tanzania. Napongeza hatua hiyo lakini nakuja na mwonekano tofauti. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba ni kweli mafanikio haya yamekuwepo lakini sasa naiomba Wizara au Mpango huu uweze kuainisha sasa ni wapi? Kwa sababu swali la maji likulizwa hapa ndani wote wanasimama mpaka aliye kwenye meza anasema, siwezi kuwaruhusu mjibu, hebu wewe mjibu swali uangalie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu, maji bado ni tatizo kubwa sana. Katika Biblia, kitabu cha Mwanzo 1:2, 6, 7, 9 na ule wa 20 ni maji tu yanazungumziwa na kwa siku tatu nzima; siku ya kwanza ya uumbaji, siku ya pili na ile siku ya tano Mungu alikuwa anahangaika jinsi gani agawe haya maji. Tanzania ni miaka 50 na kitu sasa ya Uhuru bado tunazungumzia maji ni shida. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetafakari sana nikaona shida iko kwenye vyanzo vya maji. Hatujaweka mpango thabiti katika kusimamia na kutunza vyanzo vyetu vya maji. Tumekuwa na Mamlaka za Maji Mijini na baadhi zinafanya vizuri sana zikiwepo Mamlaka za Maji Dar es Salaam (*DAWASCO*), Mamlaka ya Maji Dodoma (*DUWASA*) na Mamlaka ya Maji Moshi (*MUWSA*), hizi zimefanya kazi kwa ufanisi mkubwa na ni mamlaka za miji tu. Ni kwa nini sasa jukumu hilo lisipelekwe ikawa siyo Mamlaka ya Maji Mijini, iwe ni Mamlaka ya Maji Mkoani kwa sababu, tayari wameshaonesha *best practice*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia sasa inakuja Mamlaka za Maji Vijini. Tanzania ni maarufu sana kuanza vitu upya vile vilivyofanikiwa hatutaki kuviendeleza. Tunataka sasa Mamlaka za Maji Mijini kama tulivyoanzisha *TARURA* kwenye *TANROADS*. Hata hivyo, hizi Mamlaka za Maji Vijiji zikija, kama vyanzo vya maji havijasimamiwa vizuri, ni jinsi

gani wao wata-perform? Nashauri kwenye Mpango huu tuone vyanzo vya maji vinasimamiwa vipi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo hivi vya maji vinakuwa na sheria tofauti, kuna ambao wanasmamiwa na Wizara ya Maji ambayo inaitwa Mamlaka za Maji, lakini pia *NEMC*. Naiomba Serikali badala ya kutawanya usimamizi huu kwenye maeneo mawili, visimamiwe tu na Wizara moja ya Maji na ipewe kisheria, wasimamie vyanzo vya maji, upatikanaji wa maji yaani utengenezaji wa maji safi na salama na kusambaza maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu nimeona kabisa, kule *DAWASCO* wamefanikiwa sana chini ya yule *Engineer Luhemeja*. Sasa ni jinsi gani tunaendelea kupoteza hela kuanza vitu vipyta? Uanzishwaji ndiyo ni mzuri, lakini kwa nini tusiangalie *best practise* na tukajikita hapo hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, suala la maji hili limesumbua na kila mtu amelizungumza kadiri anavyoona. Anayeteseka na maji zaidi ni mwanamke na sio mwanamke tu aliye kijiji, hata wanawake wasomi bila maji nyumbani hakuna usafi na bila maji hakuna kinachoweza kufanyika. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mpango aweke kwenye Mpango mambo ya maji na wataalamu wake waone tuna bajeti gani sasa ya kuweza kusonga mbele kwa kuona kuwa Tanzania yote sasa inapata maji? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji mengi yanatoka vijijini. Maji yanatoka vijijini yanatiririka lakini kule yanakopita kwingine pia hawana maji, siyo jambo zuri. Tunaomba kote maji yanakopita watu wale wapatiwe maji safi na salama bila kujali ni mahali gani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niende kwenye suala lile la madai na jinsi ambavyo Serikali ...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako.
(Makofi)

Tunaendelea na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad na Mheshimiwa Selasini (Paroko) ajiandae.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyeekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jambo hili muhimu lililoko mbele yetu. Naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango pamoja watalaam wake na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara ya Fedha. Kwa namna ya kipekee nimpongeze sana Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango, kwenye kitabu chake amesema kwamba atasikiliza ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na ataufanya kazi. Mara nyingi tumekuwa tunamshauri lakini leo ametamka mwenyewe, naamini ushauri tutakaoutoa safari hii ataufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeekiti, ninaanza na suala la maji. Bunge hili lilitoa Azimio kutokana na ripoti ya Kamati, mwaka 2016 kwamba tuongeze shilingi 50 kwa ajili ya kusaidia sekta ya maji ilikuwa ni Azimio la Bunge lakini mpaka leo halijatekelezwa. Wakati Azimio lile linatoka, bei ya petroli na dizeli ilikuwa haizidi Sh.2,000 sasa hivi ni Sh.2,450 mpaka Sh.2,500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, tulikuwa tuna-control kuongeza shilingi 50 kwa ajili ya Mfuko wa Maji, tukiogopa kwamba kutakuwa kuna mfumuko wa bei lakini pamoja na kwamba hatujaongeza ile shilingi 50 mafuta yamepanda. Huoni kuna

jambo hapa tunashindwa kuwasaidia wananchi wetu kupata huduma? Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie sana suala hili watu wanapata shida. Ukiangalia kwenye sekta ya uchumi ile shilingi 50 inaonekana haina athari kwa sababu haya mafuta yameongezeka bei kutokana na *factors*nyingine ambazo zimesababisha mafuta yapande bei. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka kuchangia ni suala la umeme. Nchi yetu ina vyanzo vingi sana vya umeme. Tuna umeme wa maji, umeme wa makaa, umeme wa mafuta na tunategemea kuwa na umeme wa gesi, lakini miradi mingi ya umeme haifiki mwisho. Hapa ndipo Serikali inaweza ku-*control*/na ikafanya biashara, kwa sababu, *transmission line* ni mali ya Serikali, kwa hiyo, Serikali ina haki ya kuuza umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukulia Kihansi, tulitakiwa tuwe na mabwawa mawili, lakini tuna bwawa moja mpaka leo. Kwa nini hatumalizi ule mradi ambao ungeweza ku-*produce Megawatt* 180? Ukienda Ngaka ambako mpaka leo umeme haujaanza, tungeweza kuzalisha *Megawatt* 120. Ukienda Mchuchuma, tulikuwa tuna uwezo wa kupata *Megawatt* 50. Ukienda kwenye umeme wa Singida tulikuwa tuna uwezo wa kupata *Megawatt* 50. Hii yote ingekuwa biashara kwa Serikali kwa sababu wanaweza ku-*control transmission line*. Kwa hiyo, pamoja na mipango yetu mizuri ya umeme wa *Stiegler' Gorge*, lazima tuangalie na miradi ile ya umeme ya nyuma twende nayo *simultaneously*, siku zote tunaiacha. Tukiwa tunaanza mradi leo halafu tunauacha, Serikali ndiyo inayopata hasara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni suala la kilimo. Asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima. Hebu naomba Mheshimiwa Waziri aniambie, Serikali inapata kigugumizi gani kuisaidia Bodi ya Mazao Mchanganyiko wapate pesa kwa ajili ya kununua mazao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapozungumza ni mwezi Novemba lakini wale hawajaanza kununua mazao kwa wakulima, yale matatizo ambayo wakulima *always* wanayalamikia yataendelea kuwepo. Wale wametaka kukopa hela, Serikali itoe idhini tu wapate hela waweze kununua mazao kwa wakulima lakini mpaka leo kuna kigugumizi, hili jambo linatuathiri sana. Watu wa mahindi watakuja watasema, watu wa mbaazi watazungumza tena; tutarudi kwenye mabishano yale yale. Matokeo yake tutakuwa kila siku tunawasulubu Mawaziri wa Kilimo kwa sababu ambazo Serikali kwenye Wizara ya Fedha alitakiwa itoe maelezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo nataka kuishauri Serikali. Kwa mfano, *Kurasini Logistic Centre*, Serikali imeshawekeza shilingi bilioni 90 pale toka mwaka 2014, lakini mpaka leo huo mradi haujaanza. Shilingi bilioni 90 zimekaa hazifanyiwi chochote. Mradi huu wenzetu wa China wameupeleka Zambia, hatuoni kama tunapoteza? Mheshimiwa Waziri aje na majibu kwa nini mpaka leo *Kurasini Logistic Centre* haijaanza? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mheshimiwa Dkt. Nagu hapa, masuala ya Mchuchuma, *why?* Tumesaini mkataba wa Mchuhuma mwaka 2012 lakini mpaka leo huu mradi haujaanza, *why?* Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aje na majibu kwa nini Mchuchuma mpaka leo haijaanza kazi? Kwenye Mchuchuma tuna uhakika wa kupata *raw material* ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atusaide ni kwenye sekta ya utalii. Katika sekta ya utalii baada ya Kruger kwa ukubwa, mbuga inayofuata ni ya *Ruaha National Park*. Tulitegemea Serikali ingewekeza kwenye *Ruaha National Park*. Sasa hivi tulikuwa tunahitaji kujenga Kiwanja cha Ndege pale cha Nduli lakini Serikali imenyamaza kimya. (*Makof*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mgimwa.
(Makof)

Tunaendelea na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mheshimiwa Roman Selasini na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka wajiandae.

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nichangie maeneo machache. Nianze na suala la kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 23 kwenye kitabu cha Mpango amezungumzia suala hili kwamba uchumi unakua kutoka asilimia 7.0 mpaka asilimia 7.1. Kimsingi ameonesha namna uchumi unavyokua katika Tanzania yetu, lakini ukienda kwenye kitabu cha Kamati ukurasa wa 3, Kamati inashauri kwamba katika kukua kwa uchumi wa Tanzania unatakiwa kuakisi na kugusa maslahi ya wananchi mmoja mmoja. Pamoja na Mheshimiwa Waziri kuzungumzia kwamba uchumi unakua lakini bado maisha ya wananchi wa Tanzania ni magumu, maisha ya wafanyakazi wa Tanzania hayajaguswa na kukua kwa uchumi wa Tanzania. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge hili la Awamu hii ya Tano, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Kangi Lugola, aliyahi kusema kabla hajawahi Waziri na aliwashutumu Mawaziri kwamba wanamdaganya Rais kwa suala hili la kukua kwa uchumi kwamba wanatuaminisha kwamba uchumi unakua lakini fedha mifukoni mwa Watanzania hazionekani. Mheshimiwa Kangi alikwenda mbali zaidi akawaambia wanamdaganya Mheshimiwa Rais kwamba Watanzania wameficha fedha kumbe *BoT* ndio imezichukua fedha imezifungia ndani. Hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Kangi Lugola akiwa bado siyo Waziri. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mawaziri bado wanaendelea kumdaganya Mheshimiwa Rais kwamba uchumi Tanzania unakua lakini umaskini kwa Watanzania unaongezeka kila uchao. Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango,

lazima ajikite katika kukua kwa uchumi lakini unapokua uguse maisha ya wananchi wa Tanzania mmoja mmoja; lazima uguse maslahi ya wananchi mmoja mmoja. Kukua kwa uchumi na kukua kwa maendeleo ni lazima tuangalie maisha ya Watanzania yakoje na yameguswaje na mchakato huu wa kukua kwa uchumi wa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la ajira. Kimsingi na kiukweli kabisa kama kuna changamoto kubwa, miongoni mwa changamoto ambazo tunazo Tanzania ni pamoja na ajira. Mheshimiwa Dkt. Mpango katika kitabu chake hiki haujazungumzia hasa mkakati imara wa kuendeleza ajira kwa Watanzania hasa vijana wanaomaliza vyuo vikuu ambao kila siku wanahangaika kutafuta ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenyewe amekiri kwene kitabu chake kwamba changamoto moja ambayo imesababisha hata pato la nchi limepungua ni pamoja na kutokufikiwa malengo ya ajira. Tunamwomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango ahakikishe kwamba Watanzania wanapata ajira kama vile ambavyo Serikali hii inajinasibu kwamba ni Serikali ya viwanda, tuone sasa viwanda hivyo vinawafikiaje Watanzania katika kupata ajira. Kama vile ambavyo mnajinasibu mmetanua mawanda haya ya ajira katika sekta za elimu, sekta za afya, tuone kwa kiasi gani changamoto hii imeondoka? Tunaomba tu na hili uliangalie vizuri ili liweze kuwasaidia Watanzania kuowaondoa katika maisha hayo magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala lingine la uchumi. Namwomba tu Mheshimiwa Waziri kwamba wakati wanapoipanga kuandaa Mpango lazima usaidie kukua kwa uchumi wa upande wa pili wa Zanzibar. Ni dhahiri kwamba wakati mnapoipanga hamshirikishi wenzeni wa Zanzibar. Mpango unaelekeza kuimarisha uchumi wa Tanzania Bara, Kimsingi ukweli ni huo na kwa kiasi kikubwa unaathiri mipango ya uchumi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wetu unategemea sana kodi, lakini wakati mnapoandaa kodi, suala la kodi

kwenye Katiba yetu ni la Muungano kwa kiasi kikubwa. Sasa mnapojipanga mkaanza kupandisha kodi, mkaanza ku-create kodi mpya bila kuishirikisha Zanzibar, unakuta mnaathiri uchumi wa Zanzibar. Kwa mfano, leo Tanzania Bara wanaimarisha viwanda, Zanzibar vinafungwa. Bakhresa anafunga kiwanda cha maziwa kwa sababu ya utaratibu wa kodi ambao alikuwa hajajiandaa nao. Leo Bakhresa anafunga kiwanda cha uzalishaji maziwa kwa sababu maziwa yake yamezuiliwa kuingia Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la VAT. Mheshimiwa Dkt. Mpango tunakutafsiri vibaya Wazanzibar, kwa nini suala la VAT hadi leo halijaondolewa? Watu wa Sumbawanga wananaunua umeme kutoka Zambia hawalipishwi VAT, Tanzania wanaizua umeme Kenya hawaitozi VAT. Hivi kwa nini Zanzibar walipe VAT kwa umeme wanaotoa Tanzania Bara? Huo udugu uko wapi? Tunaomba kabla ya kumaliza Bunge hili Mheshimiwa Dkt. Mpango atupe jibu na jibu liwe ni kuondolewa kwa changamoto hii ya VAT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la kodi isiyo rafiki kwa wafanyabiashara. Suala la kodi linaathiri uchumi wa Tanzania. Hii ni ripoti ya Mamlaka ya Bandari ya Tanzania (*Tanzania Port Authority*) ya 2017, kodi inadhoofisha uchumi wa Watanzania kwa sababu wafanyabiashara wako huru kutumia bandari yoyote hasa katika nchi za Afrika Mashariki. Kwa mfano, kontena yenye urefu wa futi 20, Bandari ya Dar es Salaam wanalipa Dola 240 lakini ukienda Bandari ya Mombasa wanalipa Dola 70.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Prof. Tibaijuka na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama Taifa tufike mahali sasa tuwatie moyo wananchi wetu ambaa miongo yote tumekuwa tukiwatumia kuwachangisha kwa ajili ya madarasa, nyumba za walimu, maji, zahanati na kadhalika. Taifa hili bila kujikita kikamilifu kwenye elimu, hatutaweza kutoka hapa tulipo. Kama tutaendelea kuwaachia wananchi wetu suala la elimu wapambane nalo wenyewe kwa maana ya kuchangishana, hatutafika kokote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Dkt. Mpango, katika Mpango huu unaokuja, zitengwe fedha za kutosha kwa ajili ya kuunga mkono nguvu za wananchi, madarasa, maabara na nyumba za walimu zikamilike. Katika kushughulikia suala hilo kwa ujumla wake, tuisahau kwamba ili kuboresha elimu, lazima kuboresha na walimu wenyewe. Kwa sababu vyeo vya walimu hatuzungumzii, nyumba zao tumezisahau, posho zao tumezisahau na madaraja yao tumeyasahau. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni suala la afya. Tunazungumza sana kuhusu kujengwa vituo vya afya, zahanati na kadhalika, lakini Wabunge wote tunasema kuna kituo cha afya kimejengwa kwangu lakini vifaa tiba hakuna. Waziri wa Afya atatueleza, nchi hii tuna *MRI Machines* ngapi, *CT Scan* ngapi na vifaa vingine vyote ambavyo vinawasaadida Madaktari kuchunguza magonjwa? Sisi tunakimbilia kununua vifaa vya kujikinga na fujo ambazo hazipo; magari ya Polisi na vitu vingine lakini tungenunua vifaa tiba vya kutosha kwa ajili ya Hospitali za Rufaa katika Mikoa, tungeokoa maisha ya wananchi wengi sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wanaweza wakapata nafasi (*opportunity*) ya kwenda nje kutibiwa, ni kwa sababu moja tu; siyo kwamba Madaktari wetu hawana ujuzi, ila vifaa kwa ajili ya kugundua maradhi havipo vya kutosha. Naomba katika Mpango Wizara iongezewe fedha za kutosha kwa ajili ya vifaa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu maji. Hakuna Mbunge hata mmoja katika nyumba hii ambaye katika Jimbo lake kuna maji ya kutosha. Ukiangalia katika llani zote za Chama cha Mapinduzi kuanzia mwongozo wa TANU mpaka sasa hivi, ahadi ni kumaliza tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii tuna vyanzo vingi sana vya maji. Ukiniambia nichague kati ya *REA* na maji, ningesema twendeni kwenye maji. Kwa sababu wananchi wetu wakipata maji ya kutosha kuna uwezekano pia hata bajeti ya dawa ikapungua, kwa sababu magonjwa mengine yanababishwa na uchafu wa maji ambayo wananchi wetu wanatumia. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Dkt. Mpango katika suala hili la maji mkazo bajeti ya kutosha iwekwe ili angalau kupunguza tatizo la maji katika Majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, wananchi wamelima na wamelima kwa ufanisi kabisa, hakuna masoko. Ni kwa nini tusianzishe masoko mkakati katika nchi yetu? Kuna soko kwa mfano hili la Kibaigwa, Kamati yetu ya Utawala ilitembelea, wanakuja Waganda kununua mahindi Kibaigwa. Kwa mfano, kwa nini mahali kama pale Himo ambapo mahindi yanapita mengi sana kuelekea Kenya, Somalia, Sudan, Sudan ya Kusini pasiwe na soko la Kimataifa? Kwa nini mahali kama pale Holili lisijengwe soko kubwa la mazao nchi hizo nilizotaja zikaja zikanunua pale, badala ya kelele tunazopiga, wananchi wanalima halafu hakuna mnunuzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kazi kubwa sana ambayo Mheshimiwa Dkt. Mpango pamoja na wenzake walishafanya, walishabuni mambo mengi sana. Kwa mfano, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa amesema, yale maeneo ya kiuchumi; *Kurasini Logistic Centre* hajiaanza, Bagamoyo, Lindi na Mtwara na *Kigoma Economic Zones*, hazijaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naona reli yetu tunayojenga hii, ni jambo zuri, lakini tunaweza tusiitumie effectively kama wenzetu wa nchi jirani wa Kigali walivyoanza kujitayarisha kuitumia. Kwa sababu Kigali wanaanzisha

complex kubwa sana ya *economic zone*. Kwa hiyo, sisi tunaweza tukawa tunaishia kubeba mizigo ya kigeni, basi tukaridhika. Maana yake ni kwamba wakianzisha hiyo *special economic zone* wanakwenda kuua biashara zetu moja kwa moja. Kwa sababu wao wanataka kuhamishia Dubai Kigali; China wanahamishia Kigali; kwa hiyo, sisi wote tutakuwa tunatoka Dar es Salaam – Kigali; Nairobi – Kigali. Tufufue na kujenga zile *special economic zones* zetu ili ziweze kutusaidia sambamba na hii reli na vitu vingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ningependa kumalizia kukizungumzia, tuangalie yale maeneo ambayo yanawagusa moja kwa moja wananchi wetu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. (*Makofii*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami naomba niungane na waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa utilivu kabisa na kwa kweli tunapiga hatua. Sina budi kusema kwamba miaka mitatu ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Magufuli imeshazaar matunda yanayoonekana kwa wale wenye macho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, naomba niseme kwamba naunga mkono yale ambayo Mwenyekiti wetu ameshawasilisha, nami nataka kuboresha tu. Katika dhana nzima ya kuboresha, naomba kwanza ninukuu maneno ya Mwalimu Nyerere alipotufundisha kwamba Siasa ni Kilimo na niongezee kwamba kilimo ni masoko. Maana kama huna masoko, huna kilimo. Hapa napozungumzia kilimo ni kwa upana wake;

mimea, mazao, mifugo, uvuvi na misitu. Hayo yote ndiyo yanajulikana kama *agricultural sectors* au kilimo. Naamini kabisa kwamba Mheshimiwa Dkt. Mpango atakaporudi na anapoboresha bajeti yetu mpya ya 2019/2020, suala hili la namna ya kuhakikisha kwamba tunafufua kilimo chetu kwa ufanisi na kwa kasi inayokwenda na Kiongozi wa nchi litaonekane. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo hakiko kwenye hali nzuri sana na walio wengi hapa tunawawakilisha wakulima ambao wametutuma na bado hali yao haijaka vizuri. Siasa ni kilimo kwa sababu hayo ndiyo maisha halisi ya Mtanzania. Asilimia 70 na zaidi imeshasemwa na nitasema asilimia 90 kwa sababu hata na viwanda vinategemea kilimo, kama huna kilimo huwezi kuwa na viwanda. Kilimo ndiyo kitaza hivyo viwanda, *agricultural industrial linkages*, kwa hiyo, vitu hivi vinakwenda pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusudi twende vizuri, pendeleko langu ambalo Kamati ililiweka na naomba nili-*amplify* kidogo hapa, Mheshimiwa Dkt. Mpango anajua kabisa nchi yetu ni kubwa na inahitaji Kanda ambazo zina *balanced territorial development*. Kanda maalum kwa kila ukanda; ukanda wa nchi yetu kubwa. Kwa hiyo, haisaidii sana kwa mfano kusema unaweka soko la mahindi, limesemwa sasa hivi mahali fulani, kama hutaweza kuchukua mazao pale ambapo yanazalishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima hizi *special economic zones* ambazo amezizungumzia katika Ibara ya 4.3.7 ni pendeleko langu kabisa kwamba bajeti ikija tuone sasa Kanda mbalimbali zina *special economic zones*. Kwa sababu nchi yetu hatutaki watu wote wahamie Dar es Salaam au Dodoma Makao Makuu, hatutaki watu wote wakae sehemu moja, tunataka tuwe na nchi ambayo imeendelea huko watu walipo. Kwa hiyo, ni lazima huduma na miundombinu iwafuate. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kupongeza juhudzi za kujenga reli ya *Standard Gauge*, naona mipango ni mizuri

tunawapongeza. Hata hivyo, ni lazima pia tuseme kwamba michepuo ya reli hiyo lazima pia ilenge maeneo *strategic*. Kwa mfano, reli ile inatakiwa izunguke Mkoa wa Kagera, tupate michepuo kutoka pale Nyakanazi au Rusahunga iende Masaka iweze kupita Mtukula - Masaka inatafuta Congo ya Kaskazini. Katika miaka inayokuja, mzigo uko Kisangani Congo, niwaambieni, mzigo uko Kisangani Congo na njia ya kupita ni Masaka, Hoima unakwenda Congo. Kwa hiyo, jambo hili katika kuboresha huu mpango tuone *prospective plan* ya reli hii kwa miaka 25 kama siyo 50 inayokuja. Maana ukiwa na reli halafu huna mzigo, nayo kwa kweli ni biashara ambayo haitaza matunda. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunalindaje masoko? Tunashukuru kwamba tumepeiga hatua, sina budi kumshukuru Waziri Mkuu alipokuja kwa wakulima wa kahawa angalau kuna ahueni, lakini hapa napozungumza kahawa ipo kwenye maghala ya Vyama vya Ushirika kwa sababu ilichelewa. Soko la Dunia limeshajaa, sasa hivi kilichobaki ni *kui-damp in the international market*. Kwa hiyo, kama masoko yasipokwenda vizuri, kilimo hakiwezi kwenda vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda tunavikazania na tunapongeza juhudzi za viwanda. Hata hivyo, viwanda ni mchakato mkubwa. Niwaambieni sisi ambao tumekuwa *around* hapo *for some time*, unakumbuka kwamba Taifa hili lilipokea Kiwanda cha *Tanganyika Packers*, kilikufa siyo kwa sababu tulikuwa hatuna mifugo, hatuna *management*, lakini katika jitihada ya kukileta ndani ya Taifa, kilipobinafsishwa wale Wazungu wakaondoa Nembo yao (*TBS*), kwa hiyo, nyama ikakosa soko. Kwa hiyo, tunapozungumzia viwanda lazima tuwe na mkakati wa kuhakikisha hayo mazao tunayoyachakata yatakuwa na soko? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana wenzetu wale wamejipanga wanalinda masoko. Kwa hiyo, unakuta kama korosho, wengine wanasema tubangue, kubangua kweli tubangue, tuboreshe, lakini nytingine zitakwenda kama zilivyo. Kwa hiyo, ni lazima tutafute masoko twende nayo,

kahawa hivyo hivyo na mazao mengine ya biashara ni hayo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kama bado nina nafasi kidogo, *customer care*, kulea biashara, kulea *private sectors* ni muhimu sana. Hili jambo linatushinda kiutamaduni. Nilizungumzia mambo ya kukomoana, naomba nirudie tena. Watu wanapopewa kazi Serikalini siyo kuwakomoa wale wengine ambao wako nje. Sasa mwingine anakaa pale hata hajui anafanya nini, badala ya kuelea kitu, anadhibiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipendekeze, katika kutathmini utendaji wa hawa watu ambao wanawekewa Mpango, iangaliwe pia je, kama wewe ulikuwa Ofisa wa Biashara wa *TRA*, ni kampuni ngapi zimefunga blashara? Maana biashara zikifungwa, wewe umeshindwa. Biashara inapofungwa, umeshindwa wewe. Kama umepewa kusimamia jambo na watu wanafunga...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Profesa kwa mchango wako. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Nnauye na muda ukiruhusu Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie. Kwa sababu leo ni mara yangu ya kwanza tangu siku nimepindua meza, basi sina budi kuchukua nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa na Katibu wake na wanachama wote wa Chama cha Mapinduzi kwa kunipokea na kunipa nafasi hii niendelee kuaminika ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Liwale kwa kuendelea kuniamini ili niweze kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nami nawaahidi kwamba nitawatumikia kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyoniwezesha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utangulizi, naomba niseme kwamba napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mpango mzuri ambao wametuletea katika awamu hii. Kuna suala hapa limeibuka la Katiba, halikuja hapa kwa bahati mbaya, limekuja kwa sababu ya Mpango huu kusheheni mambo ya weledi na yanayokwenda na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kuna watu ambao kazi yao walijiandaa kupinga, sasa wanapokosa jambo la kupinga ndani ya mpango huu, lazima waje na ajenda nje ya mpango. (*Makofii*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu la kutukusanya wiki nzima hapa ni ili tuuboreshe huu Mpango kwa manufaa ya jamii yetu, lakini utakuta kwa sababu wenzetu walijipanga kupinga, badala yake wanatafuta sababu nyingine au hoja nyingine ambazo hazipo kwenye Mpango. Mimi siamini kama Katiba iliyopo leo inakataza watu kupata maji, vituo vya afya au kujenga barabara. Kwa hiyo, ingekuwa Katiba hii inakataza haya mambo, kulikuwa na sababu kubwa ya kuomba Katiba nyingine. Kwa kuwa Katiba iliyopo inakubali hayo mambo yote, hawana hoja. Kwa kuwa wamekosa hoja, wanakuja na hoja ya Katiba Mpya. (*Makofii*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye Mpango kujadili kuhusu mambo

ya kilimo. Kama ambavyo Taifa sasa linaelekeea kwenye viwanda na uchumi wa kati, jambo la kilimo kama ambavyo tunafahamu wote ni kwamba linachukua zaidi ya asilimia 60 au 70 ya Watanzania wote. Kwa hiyo, ni matumaini yangu ni kwamba kwenye mipango yetu, kipaumbele kikubwa kingekuwa uwekezaji kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, kilimo tunaweza kukiimarisha kwa mbinu mbalimbali. Mojawapo ni kuimarisha upatikanaji wa pembejeo na miundombinu ya umwagiliaji. Kubwa kuliko yote, ninaloliona hapa ni upande wa masoko. Wakulima watakapohakikishiwa masoko, lazima kilimo chetu kitapanda, ukizingatia kilimo chetu ni kilimo ambacho kinashirikisha sana wakulima wadogo wadogo. Tatizo kubwa la wakulima wadogo wadogo sio utafutaji wa pembejeo, wanao uwezo mkubwa wa kutafuta pembejeo, lakini uwezo wao wa kutafuta masoko ni mdogo sana. Kwa hiyo, ni lazima Serikali ijikite katika kuwatafutia masoko wakulima wetu hawa wadogo wadogo. (*Makofii*)

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Kwa mfano, zao la korosho. Zao la korosho miaka mitatu ya nyuma lilikuwa halina soko la kutosha...

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Hebu subiri kidogo, kuna taarifa.

T A A R I F A

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayeendelea hapa kwamba tunachangia Mpango, pamoja na yeye kuunga juhudhi kama anavyosema, lakini kwenye Mpango huu hatujaona sehemu yoyote inayotaja barabara ya

Nangurukuru - Liwale wakati ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Jimbo lake la Liwale. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kuchauka, endelea.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikasema hawa wenzetu kazi ya ni kupinga tu. Ilani ya Chama cha Mapinduzi nimekabidhiwa mwezi uliopita, inasema, barabara hiyo ya Nangurukuru - Liwale imeshatengewa shilingi milioni 800, tayari imeingizwa kwenye upembuzi yakinifu. Leo hii barabara ya Nangurukuru - Liwale, Nachingwea - Liwale imeingia kwenye upembuzi yakinifu. Hii ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Uuu, uuu, uuu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natolea mfano kwamba zao la korosho miaka ya nyuma watu wa Lindi na Mtwara walikuwa wameshaanza kulisahau, lakini pale Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alipolitafutia soko likapanda ndiyo maana mwaka jana tumepata mavuno makubwa sana, ni kwa sababu bei zilikuwa nzuri. Kwa hiyo, naona jambo kubwa la kuhimiza kilimo ni masoko. Wananchi wetu watakpopata bei nzuri ya mazao, hakuna sababu ya kuwahimiza kulima, watalima kwa bidii zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naomba niongelee suala la ajira. Watu wengi sana wameliongelea lakini naomba nimwambie Mheshimiwa Dkt. Mpango na Serikali kwa ujumla, hebu sasa tubadilishe utaratibu wa elimu yetu. Kwa mfano, hapa nazungumzia elimu ya juu kwa maana vyuo vikuu. Mimi sitarajji na sioni kuna sababu gani mtu anahitim *SUA*, anahangaika barabarani miaka miwili, mitatu anatafuta ajira badala ya kutafuta mtaji. Nilitarajia watu kama wale wawezeshwe kupatiwa mitaji wajiiingize kwenye kilimo, kama wamesomea kilimo, watakwendwa kulima;

kama ni wafugaji, watakwenda kwenye mifugo badala ya wao kuhangai na mafaili mabegani kutafuta ajira. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mpango ujielekeze kwenye kubadilisha miundo ya elimu yetu, kuwaandaa wahitimu wetu kujitegemea. Siyo jambo zuri mtu ametoka *VETA* au Chuo cha Ufundî, anahangaika barabarani kutafuta ajira. Yeye alitakiwa tu ahangaike kutafuta mtaji ili aweze kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee masuala...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka. (*Makofî*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Nnauye na Mheshimiwa Susan Kiwanga ajiandae.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie. Nimepitia haya mapendekezo, kuna kazi nzuri imefanyika, nami nitagusa maeneo matatu makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni hili la korosho. Nawashukuru wakulima wa korosho na kuwapongeza kwa utulivu waliounyesha katika kipindi hiki cha milima na mabonde tuliyopitia. Nami naamini wamekuwa wasikivu kwa Serikali wakati ikichukuwa hatua. Pia nitambue juhudî ambazo zimefanywa na Serikali na wadau katika kulishughulikia jambo hili. Ni dua zetu sisi wakulima wa korosho kwamba juhudî hizi zitazaa matunda ambayo tunayatengemea. Naamini kwamba mpito huu umetufundisha na tutatumia mafunzo tuliyoyapata katika hili na uzoefu wake ili tujipange vizuri zaidi kwa misimu

inayofuata kutuepusha kupita katika mawimbi haya tuliyoyapita. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya biashara katika nchi yetu yanategemea *factor* kubwa mbili. Zipo *factors* za ndani na za nje. Suala la korosho limetufundisha kwamba tukitumia maarifa na busara tunaweza kucheza na *factors* za ndani tukashindana vizuri katika soko la dunia. Inawezekana *factors* za nje zikawa nje ya uwezo wetu, lakini bila shaka za ndani zinaweza kutusaidia tukatumia maarifa na busara ili tuweze kushindana vizuri katika dunia, kwa sababu dunia ya leo ni ya ushindani. Kwa hiyo, naamini kabisa, mafunzo yaliyotokana na hapa tulipopita kwenye korosho bila shaka yatatumika vizuri yatusaidie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika hili, juhudzi zozote zinazofanyika, lazima tukumbuke kwamba tupo nyuma ya wakati. Kuna baadhi ya maeneo mvua zimeanza kunyesha, korosho zipo nje. Kwa hiyo, jitihada zozote ziende kwa kasi ilingane na kasi ya hali ya hewa ili wakulima wasiendelee kupata hasara zaidi na matatizo. (*Makof*)

Mheheshimiwa Mwenyekiti, zipo Halmashauri nyingi ambazo zilikuwa zinategemea sana mapato haya ya korosho kwa asilimia 60, 65 mpaka 70. Bila shaka sasa Serikali kwenye bajeti kama athari ni kubwa tuangalie namna ya kuzisaidia hizi Halmashauri ambazo zilikuwa zinategemea kwa kiasi kikubwa mapato yatakayotokana na mfumo wa korosho kama ungeenda katika mfumo wa kawaida. Vinginevyo zinaweza zikashindwa kufanya kazi na tukajikuta zime-paralyze kabisa. Ninaamini tumejifunza, tutaangalia namna ya kuboresha zaidi ili tusonge mbele. Nia ni njema, lakini tutumie maarifa na busara, tuone namna tunavyosonga mbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ukisoma hiki kitabu ukurasa wa 36, yapo maelezo yanayoonyesha kwamba Mpango wa Serikali ni kwenda kuweka mtambo wa kuchakata gesi asilia. Angalau imeonekana hapa, inatia matumaini. Swali langu, nilitaka ufanuzi, tunakumbuka

kwamba vyombo vya habari vilimnukuu Mheshimiwa Rais akisema hii gesi asilia imeshachukuliwa na mabeberu. Nami nikaamini hii *chapter* imefungwa, sasa mmeirudisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango bado hili jambo lipo? Kauli ipi ni ya Serikali? Ni ile iliyotolewa Mkoani Mara na Mheshimiwa Rais au haya yanayoelezwa kwenye huu Mpango? Lipi hasa tusimame nalo? Kwa sababu Mheshimiwa Rais alisema hili suala kama vile limeisha, mikataba mibovu, gesi asilia imeshachukuliwa yote na mabeberu lakini hapa mnaonyesha yapo mambo yatafanyika 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho katika hili, katika mstari wa mwisho inaonekana mtafanya majadiliano kati ya Serikali na mabenki kupata fedha za kuwekeza. Ambacho sisi tulikuwa tunakijua ni kwamba kuna wawekezaji wanakuja kuwekeza kwenye mtambo huu. Kwa maelezo haya ni kama vile Serikali tunafanya *negotiation* na mabenki tukope wenyewe tuweke hii fedha pale. Sina hakika kama ndiyo maana yake, nadhani tufafanuliwe hapa, tupate msimamo wa Serikali na ufanuzi wa namna tunavyoenda nalo. Hili litatusaidia kuokoa uchumi wa Kusini, hata kauli ya Serikali peke yake itasisimua ukuaji wa uchumi katika mikoa yetu ya kusini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la *tax base* katika nchi yetu. Ziko takwimu ambazo zimekuwepo kwa muda mrefu zinazoonyesha kwamba wanaopaswa kulipa kodi ni wengi kuliko wanaolipa kodi. Ni takwimu za muda mrefu. Kuna wakati walikuwa wana-*approximate* milioni 14, lakini wanaolipa labda ni milioni moja na nusu au milioni mbili na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, hizi takwimu bado ni hizo hizo? Kama bado ni hizo hizo na kwenye hutuba imezungumzwa kwamba tunalo tatizo la kushindwa kuwarasimisha walipakodi wengi zaidi ili tuu-*share* huu mzigo na hasa kwa wafanyakazi ambao hawa-*negotiate*. Tunakata juu kwa juu, lakini wapo wafanyakazi ambao wachache ambao

wamerasimishwa wanabeba mzigo wa watu walio wengi.
Nami nilidhani...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa
mchango wako.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti,
ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti,
ahsante kwa kunipa hii nafasi adimu. Naanza moja kwa moja
na ile hoja ya kwenye Mpango, Mheshimiwa Dkt. Mpango
anasema uchumi umepaa kwa asilimia saba *point
something*. Hoja hoja yangu bado iko pale pale kama
mwakilishi wa wananchi, mimi nasema uchumi haujapaa.
Labda umepaa kwenye vitabu lakini hali halisi ya wananchi
kule chini bado ni shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, watumishi wa
umma hawajapandishwa shilingi ya mshahara kuanzia
mwaka 2016 mpaka sasa hivi, lakini bei za bidhaa zinazidi
kuwa juu, mafuta juu, bati juu, *cement* juu, leo unasema
uchumi umepaa, umepaa kwa nani? Kwa hiyo, nakataa
kabisa kutudanganya Watanzania kwamba uchumi
umepaa. Kama nilivosema mwaka jana labda kwa wao,
lakini kwa Watanzania wa kawaida haujapaa, unazidi
kudidimia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ugatuaji wa
madaraka, hii hali inanitisha sana katika nchi hii. Serikali hii
ya Tanzania ilitumia hela nyingi katika suala zima la ugatuaji
wa madaraka. Tumeimba nyimbo, wataalamu
wamesomeshwa, wamekuja, tume pata hela kutoka nje,

watu wamepewa mafunzo kuhusu kupeleka madaraka ngazi za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata katika Sera ya CHADEMA tumesema siyo Mitaa tu, kwenye Serikali ya Mitaa sisi tutakwenda mpaka kwenye ngazi ya Majimbo. Kwa mfano, Kanda ya Kati ndiyo Jimbo moja la kiutawala. Hii sera hapa inazungumzia hivyo; kupeleka madaraka chini kwa wananchi ili wapate maendeleo yao na watambue rasilimali zilizopo kwenye maeneo yao ili wapate kujivekea uchumi endelevu. Kwa hiyo, huu mpango wa kuua Serikali za Mitaa unatishia maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe umeona kwenye Halmashauri mbalimbali, Serikali inatoa maelekezo kwamba watu wapewe asilimia 10 katika mapato ya ndani, Serikali Kuu kuchukua mapato kwenye Halmashauri, hiyo asilimia 10 itapatikana kama ilivyokuwa inapatikana kwa sababu mapato mmeshachukua. Je, kweli mnawajali vijana, akina mama na walemovu? Kwa sababu kama Halmashauri walikuwa wakusanye shilingi bilioni 5, kwa kuchukua vyanzo vyao vya mapato, sasa wanakusanya shilingi bilioni 2. Kwa hiyo, ile asilimia 10 na yenyeve itashuka. Hapo mmewajali viyi walemovu, vijana na akina mama? Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie upya namna ya kurudisha vyanzo kwenye Serikali za Mitaa ili akina mama, vijana na walemovu wapate asilimia kubwa katika Halmashauri ili wapate maendeleo yao. Huu Mpango ni mgumu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa vyuo vikuu, chekechea na masomo yote, sisi kama CHADEMA tunasema kwenye sera yetu, hakuna kijana atakayeambiwa amefeli, vijana wote kuanzia chekechea mfumo wa elimu utabadilishwa. Kila mtoto ataangaliwa pale alipo anapendelea kitu gani? Kwa hiyo, atakuzwa kielimu kutokana na uwezo wake. Siyo kumwambia mtu amefeli Darasa la Saba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa na vyuo vya ufundi mpaka vyuo vikuu ili hawa watoto waliomaliza vyuo vikuu waunganishwe na watengewe maeneo na wawezeshwe na mikopo ya benki, waende wakafanye maendeleo yao. Mpango wa nchi umekaa hovyo hovyo, ardhi haijapimwa, maeneo hayajatengwa, hivi hawa watu wanaenda kufanya nini? Mpango unazungumza nini kuhusu kutenga maeneo katika nchi yetu ili watu kama unapewa mkopo benki kama vijana na akina mama waende wakaambiwe ardhi hii hapa, wekeza hapa, lima, kiwanda hiki hapa. Leo tuko hovyo hovyo tu, hii nchi tutasonga mbele vipi? Mpango unasema nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji, tunataka Mpango utuambie, rasilimali tulizopewa na Mwenyezi Mungu; tuna mito mingi, Serikali ina mpango gani wa kutumia rasilimali za maji ya mito ili kutuletea maji safi na salama ya kunywa? Mfano Mlimba, kuna mito mingi lakini maji ya kunywa hakuna. Pale Mlimba Mjini watu wanapata maji mara moja kwa wiki, lakini Mpango hauzungumzii kutumia vyanzo vilivyopo katika kuboresha maisha ya wananchi ili wapate maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu pamoja na kusema unaunganisha barabara lakini hazijaainishwa. Naomba iainishwe, ni mikoa gani ambayo haijaunganishwa na mpango wa Serikali ni upi kuunganisha mikoa yote kwa barabara? Kwa mfano, Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Morogoro haujaunganishwa lakini Mpango hauzungumzii uthaunganisha vipi hiyo barabara? Tutakaa nyuma mpaka lini? Kweli kodi za Watanzania mpaka huko Morogoro na Njombe, zote mnaenda kuchukua mnajengea reli, mnanunua ndege, sisi hata barabara Mkoa wetu haujaunganishwa? Uje na mpango, mwisho wa kuunganisha mikoa nchi hii ni lini ili tuone sasa na sisi tunaenda kufaidika na hii nchi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya mapato imekuwa ni shida sana. Halmashauri kila ikibuni vyanzo, sasa

hivi unajua wamelemaa? Sasa hivi hatubuni tena vyanzo kwa sababu ukibuni vyanzo tu, Mheshimiwa Dkt. Mpango akiona anasema *TRA* kusanya. Nani atakuwa anaenda kubuni vyanzo katika Halmashauri? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watu hawabuni tena vyanzo. *Mme-paralyze* Halmashauri, Serikali za Mitaa, watumishi wamekuwa hawana raha, hakuna kuongeza mishahara, hakuna motisha, hakuna chochote. Hivi hii nchi itaendeleaje kama watu hawana raha katika maofisi yao? Mpaka vikatuni vinachorwa, leo ukiwa Katibu Mkuu au Waziri au nani, begi lako umeliweka kabisa *standby*, ukitoka jioni unaondoka nalo, kwa sababu hujui kama kesho utarudi ofisini, watu kama hawana amani...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Hilo begi unalibeba kwenda wapi? (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, ndiyo hivyo. Dakika tano hatutaweza kumtendea haki anayefuata. Kwa hiyo, jioni tutaanza na Mheshimiwa Janeth Masaburi, atafuatiwa Mheshimiwa Fredy Mwakibete na Mheshimiwa Raza na baadaye tutaendelea. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI: Bunge linarudia.

MWENYEKITI: Bunge linarudia.

(Bunge lilarudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa mpaka saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa
Kutekelezwa na Serikali pamoja na Muongozo wa
Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa
Mwaka wa Fedha 2019/2020**

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimewataja wachangiaji wetu wa kwanza watatu, tunaanza na Mheshimiwa Janeth Masaburi, tutafuatiwa na Mheshimiwa Fredy Mwakibete na Mheshimiwa Ibrahim Raza ajiandae.

MHE. JANETH M. MASABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika Bunge lako Tukufu. Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye yeye ndiyo amenipa zawadi ya uhai. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu aliowasilisha Waziri wa Fedha, nimeusoma mwanzo mpaka mwisho, nimerudia mara mbili mbili, kwa hakika ni mpango mzuri sana. Nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote katika Wizara hii, kwa kweli wamejitalidi sana lakini Mpango huwezi

kumaliza shida zote siku moja. Hata Roma haikujengwa kwa siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitu nachokiona hapa nchini ni majaabu makubwa yaliyoteka kwa kipindi kifupi cha miaka mitatu, chini utawala wa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Pombe Magufuli akisaidiana na Mheshimiwa Mama Samia, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri, Manaibu wote na Watendaji ambao ndiyo wanaomsaidia katika kuhakikisha Serikali hii inakwenda vizuri katika kutatua shida za wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala miradi kama reli ya *Standard Gauge*, mradi wa umeme wa Rufiji, mradi wa kufufua Shirika la Ndege, barabara ya Mfugale, *interchange* ya Ubungo, ujenzi wa meli katika Maziwa Makuu, kule Nyasa kuna meli inakaribia kuzinduliwa mwezi Desemba, ujenzi wa meli Ziwa Victoria, viwanja wa ndege, *Terminal* //inamalizika hivi karibuni, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete imefanya maajabu sana pamoja na Taasisi ya Mifupa. Taasisi hii imepunguza wagojwa wa kwenda kutibiwa nje ya nchi na ime-save kiasi cha fedha kingi kwa kutumia Madaktari Bingwa wazawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya mambo machache na mengine ambayo siwezi kuyataja yote, kwa kipindi cha miaka mitatu kimeushangaza ulimwengu, kimeitangaza Tanzania, kimewatisha wapinzani wetu, wamekosa la kusema, ndiyo maana wanadiriki hata kusaliti kusema kwamba Wazungu ndiyo wanaostahili kutetewa kuliko wale wananchi waliowaleta hapa Bungeni, wao wanatetea Mataifa ya nje, maana yake ni kukosa hoja. Yote hayo yametokana utendaji mzuri wa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli akisaidiana na viongozi wanzake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa Baba wa Taifa alipata taabu sana katika kujenga, kuiimarisha na kujenga umoja wa nchi yetu. Wakati ule pia walikuwepo Wakoloni wenye ngozi nyeusi waliomuwekea vikwazo Baba wa Taifa.

Kwa hiyo, hatushangai hata sasa hizi zama za Mheshimiwa Dkt. Magufuli kuwekewa vikwazo kwa sababu watu wengi ambao walikuwa wanainyonya nchi hii, sasa hivi mirija yao imefungwa. Sasa hawezি kukubali, ndio maana wanatumia vibaraka wao kwa kuwalipa pesa ili waweze kupotosha umma. Sisi tunasema, hatutakubali, tuko mbele katika kuhakikisha nchi hii inasonga mbele, tukimsaidia jemadari wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usifikirie ni Watanzania peke yake ambao wanatambua. Kuna Mkutano mmoja ulitokea kule Senegal, Watanzania walipotambulishwa kwamba wanatoka Tanzania, ule mkutano ulizizima ukishangilia Magufuli, Magufuli, Mafuguli. Ulikuwa umehudhuriwa na nchi kama thelathini na zaidi za Afrika na nchi za Ulaya na ulikuwa unafadhiliwa na taasisi moja ya Kikorea. Sasa kama Mataifa ya nchi nydingine wanatambua uwezo wa Mheshimiwa Dkt. Magufuli, kwa nini Watanzania sisi wenyewe tunakuwa wasaliti? Hiyo haitutishi. Sisi tunamwombea Mheshimiwa Dkt. Magufuli aendee kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kasoro au dosari ambazo zinasaidia au zinachangia kurudisha hii kasi. Katika suala la rasilimali watu, tunahitaji watu wenye sifa ambazo zitawenza kuwa kichocheo cha uchumi wa nchi hii. Kwa mfano, tuna upungufu wa watu wenye taaluma ya *marketing, customer care...*

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako.

MHE. JANETH M. MASABURI: Mhemimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Fredy Mwakibete.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia katika Mapendekezo ya Mpango ya Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuwakushuru na kuwapongeza viongozi wa Wizara hii ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mpango na pamoja na Naibu wake kwa namna kipekee sana ambavyo wameitendea haki Wizara hii. Nimesoma kwa umakini mkubwa katika hii hotuba lakini pamoja na hiki kitabu ambacho ni Mapendekezo ya Mpango wenye, nami nitakuwa na baadhi ya maeneo ambayo ningetamani yaje yazingatiwe hapo watakapokuja kuleta Mpango kamili mwakani tarehe 11 Machi, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni suala zima la umeme. Tunajua hakuna nchi duaniani inaweza kusimama au kuendelea kama hakuna umeme wa kutosheleza na tena wa uhakika. Kwa msingi huo, napenda kumpongeza Mheshimiwa Raís kwa maamuzi yake thabiti na imara kabisa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa *Stiegler's Gorge* katika Mto ule wa Rufiji ambao utakuwa na Megawatt 2,100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma katika *page* ya 35 ya hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mpango kuna vyanzo hivyo kutoka Mto Rufiji pia napendekeza kwamba kama ingefaa, kwa sababu ili uchumi wa nchi uweze kusonga mbele, ni lazima tuwe na *energy mix*. *Energy mix*ina maana ya kwamba hata kama umeme wa maji utapungua, kama ambavyo Watanzania wote tunajua kwamba kuna mabadiliko ya tabia nchi na wakati mwingine vyanzo vya maji vinakauka, lakini tukiwa na vyanzo mbalimbali vya nishati ya umeme itarahisisha sana kufikia uchumi wa kati kwa nchi yetu ifikapo 2025. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kama tutapendekeza katika Mpango wetu ujao kwamba umeme wa joto la ardhi na tumeshasema unapatikana kwa Megawatt 5,000 katika nchi hii, nilifurahi kusikia na kuona

kwamba tayari kampuni ya kushughulikia masuala ya uchorongaji wa visima kwa umeme wa joto ardhi kwa maana *geothermal* wameshapata kibali lakini kwenye Mpango huu sijauona. Kwa hiyo, nitafurahi sana ikiingizwa hiyo ili iwe sehemu mojawapo mbadala ya ku-supplement suala la umeme. Pia kuna umeme huu wa upepo, tumeona maeneo mengi ya katikati ya nchi yetu ya Tanzania ikiwepo hapo Dodoma, Singida na maeneo mengine mengi. Ni umeme ambao tunaamini hautakuwa na gharama kubwa katika uzalishaji kwa sababu ni upepo na utaenda kuzalisha *Megawatt* zaidi ya 600. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika Mpango huu napenda kupendekeza, ukisoma katika kitabu cha Mpango hasa ule ukurasa wa 50, amesema kuna miradi ambayo itaingiwa na Serikali pamoja na sekta binafsi, lakini hajazungumzia suala la upande wa barabara hasa upande wa *Public Private Partnership*. Suala la barabara limekuwa changamoto katika nchi yetu, tunaipongeza Serikali, imejitahidi kadri inavyoweza, lakini kama pia tutafanya kama nchi nyiningine, kwa mfano, hivi karibuni nilikuwa Kampala Uganda, tumeshuhudia wameshaanzisha Mpango kama nchi za Asia na China hasa kwa mfumo huu wa *toll road fee gate* kwa maana kwamba unazishirikisha kampuni binafsi zinategeneza barabara, halafu kwa yeote atakayetumia barabara hiyo analipa pale anapopita kwenye barabara hiyo. Miundombinu mingi katika nchi hizi imesonga mbele kwa njia hiyo. Sijaona katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, nafikiri pia angependekeza hilo, lingependeza zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado haitoshi, ukienda nchi kama China maeneo mengi ya *Province* au Majimbo ya China wametumia mfumo huu. Ukienda Nanxi, Shanxi, Shanghai, Beijing mpaka mji mmoja unaitwa Rieng kwa sababu tumeピta huko pia, kwa njia hii wameweza kutengeza miundombinu mizuri, tena ya uhakika, kwa sababu anayepita ndiye anayelipia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupendekeza jambo moja katika suala hili la ujenzi wa miundombinu ya

nchi yetu upande wa reli, barabara na maeneo mengine mengi. Wenzetu baadhi ya nchi wameanzisha benki maalum kwa ajili ya *facilitate* masuala ya ujenzi. Kwa mfano, ukienda China kuna benki inaitwa *Construction Bank*. Inawezekana nasi kwa kuwa tupo katika kujifunza, lakini siyo kujifunza tu, tunatenda sasa, nasi tukiwa na benki ya namna hiyo ili iweze ku-*facilitate* ama kuwezesha makampuni pamoja na Serikali yenyewe kwa ajili ya miundombinu hii, tunaamini tunaweza kufika sehemu nzuri zaidi kuliko hivi ambavyo tulivyo kwa sasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napendekeza ama kuongeza katika Mpango huu, ukisoma ukurasa wa 48 katika hotuba hii, amesema kuhusu kuanzishwa kwa Wakala wa Maji Vijijini. Hili ni jambo jema sana kwamba maisha ya Mtanzania katika suala la maji, Mheshimiwa Rais pamoja na kaulimbiu yake ya Kumtua Mama Ndoo Kichwani, naipongeza sana. Changamoto ninayoiona ni kwamba asilimia kubwa ya maji, hata miradi ambayo inaanzhisha, maji yanapotea yakiwa bado yapo njiani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukienda Dar es Salaam, *DAWASCO* tuliwaita kwenye Kamati, asilimia 48 ya maji yote yanapotea yakiwa bado yako njiani. Sasa basi, kwa sababu kama ni asilimia 48 ya maji yote, kwa maana ya kwamba vyanzo viro, mabomba yapo, lakini asilimia 48 hayawafikii wananchi wale nilikuwa na mapendekezo kwamba ni muhimu tutumie teknojia mpya na ya kisasa kwa ajili ya ku-*identify* ama kutambua ni maeneo gani ambayo maji hayo yanapotelea. Tulipowauliza wataalamu wa maji kutoka China walituambia kwamba ninyi kama mna mabomba ya mafuta, mnajua ni sehemu gani mafuta yale yametoboka ni sawa na gesi unaweza uka-*identify*kwamba wapi gesi bomba lile lina shida, kwa hiyo, vile vile hata katika teknolojia ya maji, lazima kuwe na teknojia ya kutambua ni mabomba sehemu gani ambapo yametoboka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwakibete kwa mchango wako. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Ibrahim Raza, akifuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Kishimba na Mheshimiwa Rehema Migilla ajiandae.

MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi hii. Kwanza namshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunipa pumzi yake kunifikisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa Mpango wao walitolutetea hapa wa 2018/2019. Kwa kweli kitabu hiki kinaleta matuamini kwa Watanzania. Nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali ya CCM ikiongozwa na Mheshimiwa Rais kwa utekelazaji wake mzuri ili kuwalettea wananchi wake maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia michango ya Waheshimiwa wakisema eti Tanzania siyo nchi salama kufanya biashara wala si nchi salama kwa wafanyabiashara. Nasema tena Tanzania ni nchi salama kwa wafanyabiashara na nchi salama kwa wananchi kwa ujumla. Nasema hivi kwa sababu mpaka leo sijaona ni mfanyakia gani aliyejimbia nchi ya Tanzania kwenda nchi za nje. Kwa sababu niko na wafanyabiashara, ningekuwa nimeshapata taarifa zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa liliokuwepo na linalopigwa kelele ni kwamba Mheshimiwa Rais sasa ametuweka sisi kwenye mstari, kwa sababu zile dili zote ambazo zilikuwa zinapigwa na watu mbalimbali kuanzia idara mpaka huko juu, ameshazifunga, ndiyo maana wanasesma kwamba hakuna pesa. Pesa zipo lakini pesa za

ulaji ndiyo hamna. Hiyo ndiyo tofauti kubwa iliyokuwepo sasa hivi Tanzania hii ya Awamu ya Tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasisitiza kwamba Mheshimiwa Dkt. Mpango usivunjike moyo, kwa sababu kuna watu wamezaliwa *gifted* kwa kutaka kuwavunja moyo wenzao. Kama Messi na Ronaldo katika mpira, basi kuna watu wamezaliwa na roho zao za choyo, wakiona jambo zuri linafanyika, kazi yao kupondaponda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie kwamba Mheshimiwa Rais yupo vizuri sana pamoja na Serikali yake ya CCM, tuko vizuri sana. Kibiriti cha Mheshimiwa Rais kimejaa, msijaribu kukitikisa. Namwombea Mheshimiwa Rais aendelee na kasi hiyo hiyo, sisi wapiganaji wake tupo tayari kumsaidia kwa jambo lolote lile na *Inshallah* huko tunakokwenda mbele ya safari 2020 - 2025 mabadiliko Tanzania yanakuja makubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya aliyofanya Mheshimiwa Rais katika kipindi cha miaka mitatu ni mafanikio makubwa sana, ni historia katika nchi yetu. Kuna mambo mengi Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yetu ya CCM . Kwa hiyo, naweza kusema kwamba hii peke yake inaleta picha tosha kwamba tuko *serious* na tuko karibu na wananchi katika kuwaletaa maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija katika kitabu cha Mheshimiwa Dkt. Mpango, changamoto zilikuwepo ni kwamba bado asilimia kubwa wafanyabiashara hawana mashine za *EFD*. Tunakosa mapato makubwa sana, naweza kusema asilimia 55 au mpaka 60, watu hawana mashine za *EFD*. Serikali inakosa mapato makubwa sana Mheshimiwa Dkt. Mpango. Nami kwa sababu ni mtu ambaye nazungukazunguka, naona mambo hayo kwa macho yangu, siyo kwamba nimeambiwa. Kwa hiyo, hiyo moja ni changamoto kubwa sana katika changamoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, natoa ushauri kwamba hizi ndege zetu ambazo nyingine ziko njiani zinakuja katika

kutuletea mapato, tuanzishe *Regional route* ya kwenda *Johannesburg* na nchi nydingine za Kiafrika, kwa sababu hapa mpaka Kenya sasa hivi *Kenya Airways* ni dola 400, kwenda *Johannesburg* ni dola 500, kwa hiyo, tukisafiri kwa usafiri wetu wa ndani, nina hakika kwamba Shirika letu la Ndege la *Air Tanzania* litatengeneza faida kubwa sana. Siyo vibaya tukapeleka ndege zetu *Bombay na Guangzhou* lakini tutazame hizi *Regional routes* ambazo zina masafa madogo, lakini pesa kwa wingi zinaingia. Kwa hiyo, hapa kidogo nilikuwa nataka naliweka sawa Shirika letu la Ndege la *Air Tanzania*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna *sabotage* inafanywa na wafanyakazi wa Shirika la Ndege la *Air Tanzania*. *Sabotage* yenye we inayofanywa ni kwamba unapokwenda kufanya *booking* ya ndege ya *Air Tanzania* kuja Dodoma, unaambiwa ndege imejaa, lakini ukifika uwanja wa ndege unakuta nafasi 10 mpaka 12 kwenye ndege zipo. Sasa najiuliza, hawa walioniambia kwamba ndege imejaa na unafika uwanja wa ndege nafasi 12 mpaka 15 ziko...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako.

MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Mpango wa Maendeleo wa 2018/2019. Shukrani, *Jazak Allah Khair*. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Jumanne Kishimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Rehema Migilla na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ajiandae.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuchangia Mpango huu wa mwaka 2019/2020. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu

yake na Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayopambana nayo hasa wakati huu wa bei ngumu ya mazao yetu ya biashara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna tatizo kubwa sana la bei ya mazao na hasa mahindi, mcèle na bidhaa nyéngine, lakini tatizo letu kubwa ni kwamba tumeelekeza nguvu kubwa sana kwenye mazao haya kwa ajili ya chakula. Nitatoa mfano, mwaka 1968, Serikali ilipitisha Sheria ya Kutengeneza Pombe za Kienyeji kama gongo ambazo ilikuwa inauziwa Kampuni ya Konyagi. Gongo hiyo, asilimia 80 ni mahindi na asilimia 20 ni muhogo au mtama. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, kama tunaweza kurudisha sheria hiyo leo, wananchi wakaruhusiwa kupika gongo wakaiuzia makampuni au viwanda vidogo vidogo vya pombe kali, mahindi yetu yakapata muafaka na mgogoro mkubwa kabisa unaotukabili unaweza kwisha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mzuri sana. Sasa hivi pombe hii ambayo inanyewa ambayo ni pombe kali inaagizwa kutoka nje. *Dram moja la spirit* ni Sh.1,200,000 na gunia moja la mahindi ukipika gongo linatoa lita 120 mpaka lita 150. Kwa hiyo, kama Serikali itakubali kama ilivyokuwa mwaka 1968, hawa wanaotengeza *spirit* wakanunua gongo wakai-refine, mgogoro wa mahindi utakuwa umemalizika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama kuna sababu ya msingi kwamba sisi tufe na *spirit* ya nje, kwa nini tusife na *spirit* ya Tanzania ambayo itakuwa imetumia mahindi yetu? Vilevile tutakuwa tumeokoa pesa za kigeni na *TRA* atapata pesa zake na wakulima tutakuwa tumewanusuru kwenye suala zima la masoko ya mazao yao. Kama Serikali itakubali, uzuri Sheria ya Halmashauri ya mwaka 2016 bado inaruhusu, Mkurugenzi wa Halmashauri anaweza kuruhusu kikundi cha watu wakapika pombe ya kienyeji au gongo waka-supply sehemu yoyote, tukiruhusu, kwa kuwa sasa hivi viwanda vya *spirit* ni vingi sana, Serikali ikazuia kama ilivyozuia kwenye *materia/mengine* kama chokaa, makaa ya mawe, maziwa,

ikizuia vilevile *spirit* ya kutoka nje, hao wenye viwanda wakanunua gongo ya Tanzania, kama Mheshimiwa Waziri atatangaza kesho kwamba ameruhusu, gunia la mahindi litakuwa shilingi 200,000/=.

(*Makof*)

MBUNGE FULANI: Kweli.

(*Makof*)

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Kutoka bei ya Sh.25,000 ambayo tutapata ongezeko la asilimia 1,000.

(*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri afikirie maana yake hatuna jinsi yoyote ambayo tunaweza kujinurusu. Kusema tu kwamba tutauza mahindi watu wakale, mvua tulipata Afrika Mashariki nzima, hakuna mtu ambaye hana chakula kwa sasa hivi.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MBUNGE FULANI: Wewe endelea bwana.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Selasini. Tulia tu kidogo, kaa Mheshimiwa Kishimba.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe mzungumzaji taarifa kwamba malighafi ya gongo ni zaidi ya anachokisema. Kutokana na malighafi hiyo kuwa mbaya, watu wengi sana wamekufa kwa kunywa gongo. Mfano mzuri kabisa ninao mimi, watu wameshindwa kufanya kazi, wako hoi. Kwa hiyo, hili analolisema ningemshauri alifanyie utafiti vizuri kabla hajalizungumza lisije likaharibu jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kishimba.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Selasini hajanielewa. Sina maana watu wanywe gongo *direct*, gongo iende kwenye viwanda vya *spirit*. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Iwe refined. (*Makofi*)

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, iwe refined ili iuzwe kama zinavyouza pombe zilizopo leo mitaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere alipoona tatizo kama hili miaka ya 1970, ndiyo alianzisha bia ya safari ambayo ilikuwa *hundred percent ni material* ya Tanzania. Pia alianzisha Konyagi na kununua gongo kutoka kwa wananchi. Hata hii *spirit* inayotoka nje, ana hakika gani siyo sumu? Ndiyo maana nimesema, ipi bora, tufe na sumu ya India au tufe na sumu ya Tanzania. (*Kicheko/Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kishimba.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Naam.

MBUNGE FULANI: Unga mkono hoja.

MWENYEKITI: Kutokana na uzoefu wako huo, acha nitumie madaraka yangu nikuongezee dakika nyingine mbili. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri ni kwamba gongo hii kama itaruhusiwa wataalam wa *TFDA* wapo na sidhani kama

spirit inayotoka nje kabla haijaenda kiwandani ina ubora zaidi ya gongo ya kwetu. Maana gongo yetu wananchi wanaendelea kunywa *direct*, lakini *spirit* ukiljaribu kunywa kabla haijaenda kwenye kiwanda unapofuka. Kwa hiyo, namwomba sana ndugu yangu Mheshimiwa Selasini ajaribu kulifikiria kwa mapana. Ni kweli, hili ndilo tatizo linalotusumbua, kama hatuwezi kwenda kwenye mawazo ya nyuma na kutafuta utaalamu na ufumbuzi, hatuwezi kwenda mbele. Kama tutaruhusu, itatusadia sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajapan wanayo pombe nzuri sana ya mchele. Ni vizuri vilevile wataalam wetu badala ya kila wakati kumwomba madawati Balozi wa Japan wamwombe basi na teknolojia ya kugeuza mchele kuwa pombe. Itatusaidia sana kulkoo sasa hivi tukiendelea tu kulla soko, soko, nani atakuja kutuokoa, hakuna! Isipokuwa lazima tuchukue *action* na maarifa yetu sisi wenyewe ili kuweza kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kishimba kwa mchango wako na ushauri wako mzuri. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Rehema Migilla, halafu Mheshimiwa Mwaifunga na Mheshimiwa Aisharose Matembe ajiandae.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami jioni hii nichagie kidogo kwenye Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2019/2020. Awali ya yote, napenda niwapongeze Mheshimiwa Dkt. Mpango na timu yake kwa kazi nzuri. Kuandaa Mpango siyo kazi rahisi, ina changamoto lakini nawapongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la maendeleo ni lazima tu-*focus* katika masuala ya vipaumbele.

Kipaumbele kimojawapo ni suala la elimu. Tunajua kabisa Serikali yetu imejitahidi kwa kiasi kikubwa kuwekeza katika elimu ndiyo maana sasa hivi tunaona kuna shilingi bilioni 20.9 zinapelekwa kwenye elimu msingi, lakini vilevile tunaona wanavyuo wengi sasa hivi wanapata mikopo kwa wakati na kwa idadi kubwa lakini kuna sintofahamu kubwa sana imejitokeza hapa kutokana na Tume ya Vyuo Vikuu kufanya maamuzi ambayo nitayaelezea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Tume ya Vyuo Vikuu ilifanya maamuzi magumu kwenye vyuo vyetu vinavyotoa elimu ya juu, kwa baadhi ya vyuo kuvifutia usajili, lakini baadhi ya vyuo vimefutiwa udahili, lakini kuna baadhi ya vyuo vimefutiwa kabisa kuendelea na baadhi ya kozi. Hili ni zuri sana, naipongeza Serikali kwa sababu ina nia njema kwa hawa wanafunzi na kwa Taifa kwa ujumla. Sintofahamu hili inakuja kutokea pindi ambapo unawahamisha wanafunzi, unawapeleka chuo kingine kwa kuwabadilishia kozi, hapo unawa-*disturb totally*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyikiti, mfano Chuo cha Stephano Moshi, kile chuo kina kozi ya *Bachelor of Arts in Public Administration and Management*, kozi ile imefutwa katika chuo kile, lakini wanafunzi wale wametakiwa wahamishwe kwenda chuo kingine. *TCU* imewahamisha imewapeleka Chuo cha Ushirika Moshi wakati hakina kozi hiyo. Baada ya kufika kule, wanaambiwa wasome *Bachelor of Arts in Human Resource Management*. Hivi kweli unamhamisha mwanafunzi mwaka wa pili kuingia wa tatu amesoma kozi nyingine halafu aende chuo kingine kusoma kozi nyingine, kweli tunataka hawa wanafunzi wetu wa-*develop carrierzao* au tunacheza na akili zao? Naomba Wizara ya Elimu kwa kuititia *TCU*, wahakikishe hili suala wanaliangalia kwa jicho la tatu. Haiwezekani mtu mwaka wa kwanza mpaka wa pili asome kozi nyingine halafu mwaka wa tatu asome kozi nyingine, tunawa-*disturb*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, watu wengi katika hivi vyuo, mfano Tabora kuna Chuo cha Teofilo Kisanji,

kilikuwepo pale. Kilikuwa kinatoa maendeleo kwa wananchi wetu, kulikuwa kuna ajira pale, kimefutiwa usajili. Kwa hiyo, tunaiomba *TCU*, kabla haijafanya haya maamuzi, ifanye *researchya* kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine napenda niongelee kuhusu masuala ya kodi. Huwezi kuwa na maendeleo pasipo kuwa na *financial resource*. *Financial resource* ya Tanzania kwa sasa tunategemea kodi tu. Kwa hiyo, kama tunategemea kodi, basi tuhakikishe kuna mazingira wezeshi ya kuhakikisha hii kodi inakusanywa inavyotakiwa na siyo ikusanywe tu, lakini pawepo na mazingira ambayo yatawezesha hii kodi itumike *effectively* na pawepo na mazingira ambayo yatawezesha hii kodi yetu iweze kufanyiwa *monitoring*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeona juhudzi za Mheshimiwa Dkt. Mpango, ameweza kusimamia kodi kule bandarini. Tuliona kuna sakata la makontena ya Makonda, lakini Watanzania tulikuwa tunakaa kwenye redio na kwenye *TV* kuangalia nini mwisho wa sakata la haya makontena ya Makonda ambayo ilisemekana kuna njia za ukwepaji wa kodi. Tunaomba atakapokuja ku-*wind up*, kama itampendeza Mheshimiwa Dkt. Mpango atuambie sakata la makontena ya Makonda yaliishia wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema hivi, tunataka tuone, je, huu ufuatiliaji wa ukwepaji wa kodi, unafanyika tu kwa watu wadogo wadogo au na kwa watu wakubwa? Tunataka *strong measures* zichukuliwe siyo tu kwa watu wadogo, hata kwa viongozi, Waheshimiwa Wabunge endapo kutakuwa kuna mazingira ya kukwepa kodi. Tunaamini kabisa Mheshimiwa Dkt. Mpango yuko *punctual*, tunataka sakata la makontena ya Makonda lifuatiliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie pia kuhusu kilimo. Tunajua kabisa, kilimo kinachukua *90 percent*

ya wakazi wa Tanzania lakini kilimo hiki kinachoongelewa humu katika Mpango ni cha mazao ya chakula tu, mkazo haujawekwa zaidi kwenye Kilimo cha mazao ya biashara. Kwa hiyo, napenda kumshauri Mheshimiwa Dkt. Mpango, hao wananchi wetu ili waweze kuendelea na ...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa mchango wako. (*Makofii*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mheshimiwa Matembe na Mheshimiwa Shamsia Azizi ajiandae.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ya kuweza kusimama hapa na kuchangia Mapendekezo ya Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu amenipa macho ya kuona, amenipa masikio ya kusikia na amenipa akili ya kupambanua ipi mchele na ipi ni chuya. Katika Mapendekezo haya, ningependa kuchangia kwenye eneo moja, nalo ni eneo la viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu sana kupidia hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mpango lakini nikawa naangalia na haya mapendekezo kuhusiana na suala zima la viwanda. Vitu ambavyo nimeviona hapa ni vilevile, ni yale yale ambayo pia kwa namna moja ama nyingine hayajatekelezeka. Nimeiona *SIDO* hapa, hakuna pesa ambayo imekwenda kwa ajili ya kusaidia haya, nimeiona *CAMARTEC*, juzi tulikuwa nao, nao pia wanalamika hawana fedha ya kufanya haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nishauri jambo moja. Tunavyo viwanda hapa nchini na vipo viwanda ambavyo vinalipa kodi kubwa na viwanda vingine vinalipa kodi za kawaida. Napenda kumshauri Mheshimiwa Mheshimiwa Waziri, vipo viwanda 65 ambavyo huwa vinakusanya kodi kila mwaka na kodi hii ni ile ambayo inafahamika. Katika viwanda hivi 65, viwanda 10 peke yake ndiyo viwanda ambavyo vinakusanya kodi kubwa hapa nchini, zaidi ya shilingi triliuni 4 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi vina changamoto za kutosha. Unapokwenda kuwasikiliza na unaona kwamba hizi changamoto zipo na kila siku zinasemwa lakini hazitatuliwi. Napenda kuishauri Wizara, hawaoni sasa kuna umuhimu wa kukaa na hawa walipakodi wakubwa wenye viwanda, wakazungumza nao, wakasikiliza changamoto zao, wakaona ni kwa namna gani wanawenza kuwasaidia kutatua hizi changamoto ili badala ya kulipa shilingi triliuni 4 kwa mwaka, iongezeke hata *double* ama *triple* kwa sababu inawezekana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo vipo viwanda vikubwa ambavyo vimepunguza uzalishaji kwa asilimia zaidi ya 50. Kiwanda ambacho kilikuwa kinazalisha kwa asilimia 75 mpaka 80, leo kinazalisha kwa asilimia 15, huu ndio ukweli; na hivi viwanda vikubwa ambavyo tunategemea vinalipa kodi ya kutosha. Vipo viwanda 55 ambavyo vinalipa *one trillion* kwa mwaka. Angalia viwanda hivi vilivyo vingi, lakini vinalipa kodi chache kuliko hivi vichache 10 vinavyolipa kodi nyingi. Kwa nini Serikali isijikite kwenye hivi vinavyolipa kodi nyingi na kushughulikia changamoto zao? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto walizonazo ni kubwa, masoko hawana, wanatengeneza bidhaa haziuziki, hata wale wanaotengeneza nondo hapa, bidhaa zao hazitoki wakiambiwa kwamba bidhaa hazina ubora. Viwanda tunavyo vingi na vya kutosha, lakini changamoto zilizopo nazo ni za kutosha kweli kweli. Kwa hiyo, naomba

sana wakati mnatuletea Mpango, tuleteeni Mpango ambao utatuonesha kwamba sasa tunasema habari ya viwanda, tukizungumza na hawa wenye viwanda, tunaona wananaufaika na moja, mbili, tatu, kuliko *story* iliyopo sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kaulimbiu ya nchi ya viwanda, sijui Watanzania wenzangu wanaichukuliaje? Nahisi mimi naichukulia tofauti, kwamba mtu anaposema Tanzania ya Viwanda, Mheshimiwa Rais, anapopita akitembea kifua mbele kutangaza kwamba Tanzania ya Viwanda lakini huku chini hivi viwanda havifanyi vile inavyotakiwa, havipo! Sijui haya mambo yakoje, sielewi sana. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Dkt. Mpango ajaribu kukaa na Wizara ya Viwanda, waone changamoto za hawa watu wenye viwanda ili waweze kuviendeleza viwanda vilivyopo wakati tunasubiri viwanda vipyta vije. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia suala zima la *SIDO*, *SIDO* ndiyo pekee itakayoweza kuwasaidia Watanzania wa hali ya chini katika nchi yetu. Leo ukienda *SIDO*, hawana mashine za kutosha na za kisasa na hata bajeti ambayo tunawatengea hapa haiendi jinsi inavyotakiwa. Kwa hiyo, hawa *SIDO* wanasuasua, hawawezi kufanya kile ambacho wamekikusudia na matokeo yake sasa tunaletewa taarifa kwenye maandishi ambayo wala siyo ukweli. Kwa sababu gani namwambia hili, mimi niko kwenye Kamati ya Viwanda, nayajua haya ambayo ninayazungumza. Kwa sababu ya muda kuwa mfupi, labda ningejitahidi kusema mengi, hata hawa *CAMARTEC* ambao tunaambiwa kwamba ...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. (*Makof*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Matembe.

MHE. AISHAROSE N. MATTEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mapendekezo yangu katika mchango wa maendeleo ya taifa. Kipekee ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kuweza kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. Nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali yangu ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwaletea Watanzania maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ya *Stiergler's Gorge*, ujenzi wa reli ya kisasa ya *standard gauge*, ujenzi wa barabara na madaraja na ufufuaji wa shirika letu la ndege ni kielelezo tosha kwamba Rais, Mheshimiwa John Pombe Magufuli ni kiongozi makini na mwenye maono na maamuzi thabitii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijiji pamoja na timu nzima kwa kutuletea mpango mzuri kwa mustakabali wa Tanzania tunayoitaka, hongereni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ningependa kujikita katika mambo mawili nayo ni kilimo pamoja na maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mambo yanayositisizwa na Serikali ya Awamu ya Tano ni uanzishwaji wa uchumi wa viwanda. Hata hivyo uwepo wa uchumi wa viwanda unategemea sana kuimariika kwa kilimo chetu. Sekta ya kilimo inayo mchango mkubwa katika uchumi wetu lakini imekuwa ikiachwa nyuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mapendekezo ya kwamba ni wakati muafaka sasa wa kuiangalia sekta ya kilimo ili iweze kuzalisha malighafi kwa wingi ambazo malighafi hizo zitatumika katika viwanda vyetu tunavyovianzisha au tunavyovifufua hivi sasa. Kwa

mfano katika Mkoa wangu wa Singida ambao ni mabingwa wa kulima alizeti, mahindi, vitunguu pamoja na mazao mengine, upatikanaji wa pembejeo umekuwa ni changamoto kubwa sana. Hivyo basi, ningependa kutoa mapendekezo katika mpango huu, kwamba wawaangalie zaidi wakulima wadogo wadogo kwa kuwawezesha zana za kilimo pamoja na mafunzo ili waweze kuzalisha mazao kwa wingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchumi tulionao ni rahisi kujikita katika sekta ya kilimo. Nasema hivyo kwa sababu tunayo ardi kubwa ambayo kama tutaitumia vizuri tutaweza kufikia vizuri malengo ya Tanzania ya viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kulichangia ni suala la maji. Kwa sasa tunajikita katika uchumi wa viwanda, je, tutawezaje kufika huko iwapo hatuna maji ya kutosha? Utafiti unaonesha asilimia 84 ya watu waishio mijini na asilimia 58 ya wakazi waishio vijijiini wanapata maji safi na salama. Takwimu hizi zinaonesha wazi kuwa watu wengi vijijiini hawana majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ningependekeza mpango uangalie zaidi au utoe kipaumbele kikubwa kwa maeneo ya vijijiini ili nao waweze kupata majisafi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waathirika wakubwa wa ukosefu wa maji ni wanawake, kwani hutumia muda mrefu kutafuta maji badala ya kujikita katika shughuli za kuzalisha mali na hii ni kwa sababu maeneo mengi ya vijijiini hayana majisafi na salama. Hivyo basi, ningependa mpango atoe kipaumbele kikubwa katika miradi ya maji haswa ile iliyopo vijijiini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilifanya ziara katika Mkoa wangu wa Singida na huko nilikutana na changamoto katika taasisi za elimu na taasisi za afya hazina vyanzo vyaa maji. Ningemba sana mpango pia utoe

kipaumbele kikubwa kuhakikisha maji yanapatikana katika taasisi hizi za afya na elimu kwani iwapo mlipuko wa maradhi unatokea waathirika wanakuwa ni wanafunzi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako.

MHE. AISHAROSE N. MATTEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Tunaendelea, Mheshimiwa Shamsia Aziz atafuatiwa na Mheshimiwa Zubeda Sakuru na Mheshimiwa Anastazia Wambura ajiandae.

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika mpango huu wa Serikali.

Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya nzuri na leo hii kuweza kusimama katika Bunge hili. Pia nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mwenyekiti wangu wa chama *full bright* Profesa Ibrahim Haruna Lipumba kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya ujenzi wa chama changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Naibu Katibu Mkuu Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya ujenzi wa chama changu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na sekta ya utalii. Bado hatujautangaza utalii wetu vizuri pamoja na kuwa na vivutio vingi na vizuri katika nchi yetu, bado hatujautangaza kimataifa. Kwa mfano, Mji wa Mikindani Mkoa wa Mtwara una historia nzuri ya soko la watumwa. Kama Serikali ingeweza kuboresha majengo yale na kupatangaza vizuri, Serikali na Halmashauri ingeweza kupata mapato ya kutosha kutokana na utalii ule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye sekta ya elimu. Elimu yetu Tanzania bado ipo chini sana kwa sababu hatuna walimu wa kutosha katika shule za msingi na sekondari na tuna uhaba wa walimu wa sayansi katika shule za sekondari na vyuo. Pia Bodi ya Mikopo bado hajjaweza kutosheleza mahitaji yake kwa wanafunzi wa vyuo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye sekta ya afya. Bado kwenye sekta ya afya tuna uhaba wa Madaktari Bingwa, madawa pamoja na vifaatiba. Kwa mfano, katika mkoa wetu wa Mtwara hatuna Hospitali ya Rufaa, hospitali kubwa ambazo tunazitegemea ni hospitali za Misheni iliyopo Ndanda na Masasi. Ninaionomba Serikali ijenge hospitali ya rufaa katika mkoa wetu ili wananchi wa mkoa ule waweze kupata huduma bora ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya kilimo, pembejeo bado zipo juu na kuna ucheleweshaji wa pembejeo hali iliyopelekea wakulima kuvuna mazao machache kinyume na matarajio yao. Ninaishauri Serikali ipeleke pembejeo kwa wakati na pia itafute masoko ya uhakika katika mazao yetu. Kwa mfano tumeona zao letu la korosho liliyosuasua, kama tungkuwa na masoko ya uhakika, tungeweza kuuza korosho zetu kwa wakati na kwa bei nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa uzalendo aliuonesha, kwa kununua korosho yetu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uzalendo huu ambaao ameuonesha, hongera sana Rais wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kuhusu sekta ya uvuvi. Serikali iwekeze kwenye sekta ya uvuvi na itoe elimu ya kutosha kwa wavuvi ili kuondoa mkanganyiko wa mara kwa mara na wavuvi, yakikamilika haya Serikali itapata mapato ya kutosha. Vilevile zitengewe bandari maalum kwa ajili ya uvuvi. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Zubeda Sakuru, Mheshimiwa Wambura na Mheshimiwa Jacquiline Msongozi ajlandae.

MHE. ZUBEDA H. SAKURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuweza kuchangia katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi wa Bajeti ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ningependa kuonesha masikitiko makubwa kwa jinsi ambavyo kwa muda mrefu suala zima la ukosefu wa ajira limekuwa likiachwa katika mipango ya Serikali. Ukiangalia katika hotuba ya Waziri Mpango, ukurasa wa 34 na 35 ameeleza mojawapo ya changamoto za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti na hatua za kukabiliana nazo kuwa ni pamoja na kutofikiwa kwa lengo la kodi zinazotokana na ajira (*payee*) kulikosababishwa na kutofikiwa kwa malengo ya ajira mpya, kutoongezeka kwa mishahara kwa wafanyakazi kama ilivyokuwa imetarajiwa na pia kupunguzwa kazi kwa wafanyakazi kwenye migodi ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu kubwa, nani atoe ajira mpya, ni nani aongeze mishahara, ni nani ahakikishe wafanyakazi wa Tanzania hawapunguzwi kazi? Leo hii tunapozungumza na kwa muda mrefu nimekuwa nikijaribu kujikita katika umuhimu wa Taifa letu kuwekeza katika mfumo wa elimu ili kuhakikisha kwamba tatizo la ukosefu wa ajira nchini linapunguzwa. Pamoja na kwamba kumekuwa na michango mingi ambayo imekuwa ikielekewa kwamba tatizo la ukosefu wa ajira ni *global challenge* lakini bado hii haitoshi katika kuacha Tanzania kulishughulikia ipasavyo tatizo la ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze masikitiko yangu ya wazi kuwa, wakati huu ambao Tanzania inashindana na nchi za Afrika Mashariki Serikali imeshindwa kuja na mkakati thabitii wa kuhakikisha inatatua tatizo la ukosefu wa ajira hasa kwa vijana. Kati ya mwaka 2013/2014 tunajua asilimia kubwa ya pato la Taifa ilikuwa inatokana na kodi itokanayo na pato

la *Pay As You Earn*,lakini leo hii tunavyozungumza, Serikali kuanzia imeingia madarakani imeshindwa kuongeza mishahara kwa wananchi. Serikali ya CCM ambayo inajinasibu kwamba imeongeza ama kumekuwa na uchumi mkubwa katika Taifa letu, imeshindwa kabisa kutoa ajira mpya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tutambue kwamba kadri siku zinavyoenda nchi za wenzetu zimewekeza katika elimu. Ukiangalia tu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, leo hii tunapozungumza Kenya wana mkakati kabisa wa kuhakikisha *youth unemployment* imewekewa *road map* ya kimataifa na wana *national dialogue* kuhusu kukabiliana na tatizo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo linasababisha kuwa na ukosefu mkubwa wa ajira nchini ni pamoja na kutokuwa na mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara. Ndani ya muda mfupi kodi zimekuwa zinaongezeka kila kukicha na kumekuwa na hali ya kutokuwa na usalama kwa wawekezaji. Leo hii Mawaziri wote wamekuwa wakija katika Bunge lakini wakiwa hawana *continuity* ya *government activities*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mipango mingi ambayo imewekwa na Wizara ya Kilimo katika kutatua tatizo la ajira halendani kabisa na mipango ambayo imewekwa na Wizara ya Viwanda kukabiliana na tatizo la ajira. Vilevile hakuna *integration* ya kuhakikisha kwamba Wizara ama sekta ambazo zinatoa ajira kwa mfano sekta ya maliasili, kilimo, ufugaji na uvuvi kwa kiwango kikubwa vina-set a *national roadmap* ya kuhakikisha tatizo la ukosefu wa ajira nchini linatatuliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ningependa kuzungumzia juu ya kutokuwa na soko la uhakika wa mazao ya chakula na kibiashara. Mkoa wa Ruvuma ni moja ya mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, lakini kwa mwaka jana ukiangalia kwa *trend* ya uzalishaji, umekuwa ukizalisha *surplus*, lakini kumekuwa

hakuna uhakika wa soko kutokana na ubovu wa miundombinu, kutokuwa na mipango mikakati endelevu ya kuhakikisha kwamba mkulima ananufaika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana mwaka huu wakati Naibu Waziri akiwa Mkoani Ruvuma alieleza kwamba *NFRA* imeshindwa kuwa na uwezo wa kununua tani za mahindi ambazo zilikuwa zimezalishwa. Sasa swali langu, katika mpango huu amba Serikali leo hii inatuletea ni kwa kiwango gani tumehakikisha kwamba wazalishaji wa mazao ya kibashara pamoja na mazao ya chakula wanaweza kupata soko la uhakika ili kuweza kufaidika na mchango wa sekta ya kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sekta ya kilimo tunajua kabisa... (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Anastazia Wambura atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi na Mheshimiwa *Engineer Christopher Chiza* ajiandae.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu mchana huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitangulie kwa kusema kwamba naunga mkono hoja Mapendekezo ya Mpango 2019/2020; kazi nzuri imefanyika na wote tunaona na ni mashuhuda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa utekelezaji mzuri wa llani ya Chama cha Mapinduzi, lakini kwa namna ya pekee kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ameweza

kukabiliana na tatizo la wakulima ambao walikuwa wananyonywa na wafanyabiashara. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipoteze muda mwingu, niende moja kwa moja kwenye kutoa mapendekezo yangu katika sekta chache na nianzie na sekta ya afya. Ukienda katika Ilani ya Uchaguzi ibara ya 50(p), ilani yetu inaelekeza Halmashauri ziwatambue wazee ili kusudi waweze kupata matibabu bure katika hospitali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba zoezi hili limesuasua kwa kiasi fulani kwa sababu ukienda katika baadhi ya mikoa utakuta utekelezaji wake ni chini ya asilimia tano. Hivyo, ningependa Serikali ilichukue hili na kuliweka katika mpango ili kusudi iweze kuweka mikakati jinsi gani tunaweza tukafanya utekelezaji na hii itachangia kuongeza *lifespan* ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende pia katika ibara hiyo hiyo ya 50(m) ambayo inaielekeza Serikali kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Mloganzila, Hospitali ya *UDOM* pamoja na Hospitali ya Mtwara. Haya mawili yamekamilika, Hospitali ya Mloganzila na Hospitali ya *UDOM* zimekamilika, nadhani tulishuhudia Mheshimiwa Rais wetu alizindua Hospitali ya Mloganzila. Vilevile tunashuhudia kabisa kwamba katika Hospitali ya *UDOM* upandikizaji wa figo unaendelea na hivyo nitoe pongezi kubwa sana kwa Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Hospitali ya Mtwara, hospitali hii haijakamilika. Katika bajeti ya mwaka huu ilitengewa shilingi bilioni moja, lakini mpaka kufikia mwezi wa tisa pesa ilikuwa bado hajatolewa; na tukiangalia katika vipaumbele utaona kwamba moja ya vipaumbele ni kipeleka vifaa tiba katika Hospitali za Kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mtwara ni moja ya Hospitali za Kanda hivyo napenda kushauri kwamba iwekwe katika mpango, ikamilike kusudi nayo iweze kupokea vifaatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa kilimo. Katika sekta ya kilimo kazi kubwa imefanyika na hasa ya kuinua uchumi na kama tunavyoona kwamba sasa hivi kilimo kimekua kwa *7.1 percent*. Pamoja na hayo kuna suala moja ambalo ni la *hidden hunger*, kuna tatizo kubwa la *hidden hunger* katika nchi yetu, na hili pia linachangia sana katika kupunguza *lifespan* ya Watanzania. Sasa taasisi zetu zimefanya jitihada ya kufanya *biofortification* katika baadhi ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa katika upande huu ni ukosefu wa mbegu za mazao lishe. Ninapendekeza liingie katika mpango ili hizi mbegu ziweze kufanyiwa *multiplication* na zisambazwe katika nchi nzima. Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi tumeomba mbegu hizi mwaka mzima sasa hivi, tumeshindwa kuzipata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika sekta ya uvuvi. Nimeona katika mpango, kuna mwelekeo kwamba bandari ya uvuvi itajengwa, lakini niongezee tu kwamba isiwe bandari ya uvuvi peke yake, iendane na ujenzi wa chelezo na vilevile tununue na meli za uvuvi. Nalisema hili ili tuweze kutumia fursa ya uvuvi wa bahari kuu katika nchi yetu ambayo tutaongeza pato la Taifa kutokana na *export* ya samaki pamoja na kutumia samaki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika nchi za Mauritius na Seychelles, wao kwa vipindi tofauti waliweza kupata mapato kutokana na *exports* kati ya dola milioni 270 hadi 480 ambazo ni sawa na shilingi za Kitanzania kati ya bilioni 600 hadi zaidi ya trilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi Tanzania tunaweza kufanya hivi, kwa sababu ukiangalia idadi kubwa ya samaki hawakutoka katika nchi hizo, wanakwambia ni kama robo au theluthi moja ndiyo iliyotoka katika hizo nchi lakini kati ya theluthi mbili na robo tatu ilitoka katika nchi ikiwemo Tanzania, nchi nyingine kama Kenya lakini Tanzania ilitoa samaki wengi zaidi ambao ni jodari. Tukijielekeza kwenye uvuvi tutasaidia kuboresha lishe ya wananchi wetu, kwa... (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Wambura kwa mchango wako, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi, lakini la pili, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenipa uzima siku hii ya leo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa kazi nzuri anazozifanya, lakini pia nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais siku ya leo nina furaha sana, baada ya kuondoa changamoto ambayo ilikuwa inawakabili watu wa mikoa ya Kusini, jambo ambalo ilikuwa linasababisha kuweka sintofahamu kwenye suala la korosho. Mheshimiwa Rais amefanya jambo zuri sana na nakupongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu ambao katika kipengele hiki walikuwa sasa wameanza kufurahia na kuona kwamba Serikali sasa inakwenda kuadhirika na kwamba hatutaweza kununua korosho, lakini mimi niseme kwamba wale wote waliokuwa na ajenda hii, waliokuwa wamejipanga...

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: ...kuona kwamba nchi yetu inaharibika na inadhalilika kwenye kipengele hiki, kimsingi wameaibika na... (*Makof*)

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: ...ninasema kwamba kama alivyosema Mheshimiwa...

MWENYEKITI: Hebu tusikie Taarifa.

T A A R I F A

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa Mjumbe aliyekuwa akiongea kwamba pamoja na kumpa sifa Mheshimiwa Rais, lakini pia akubali kwamba yapo mazao mengi sana ambayo sasa hivi yamekosa wateja, kwa mfano zao la mahindi, mtama, mbaazi na mazao mengine na kwa sababu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mjumbe, unachangia tena?

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwakajoka namheshimu sana, naomba nimpe onyo asirudie tena kunipotezea muda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye suala la mpango. Mheshimiwa Rais alisema yeye hajaribiwi na imejidhihirisha wazi kabisa kwamba yeye hajaribiwi na jambo hili leo limekwenda barabara, swadakta kabisa. (*Makofii*)

Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, hasa kwa umeme wa gridi ambao umepelekwa katika Mkoa wa Ruvuma. Ninaomba niseme kwamba nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa mpango wake mzuri aliyouleta na ninaamini kabisa kuititia mpango huu itakapofika 2020 Tanzania itakuwa imeshika kasi kwa maana ya kasi ya maendeleo katika nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pamoja na mipango ya Mheshimiwa Dkt. Mpango, nilidhani kwamba Serikali ingeongeza ruzuku kwenye pembejeo za kilimo ili mwisho wa siku mwananchi anunue pembejeo za kilimo kwa bei ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usalama barabarani. Kwenye suala hili ninaomba Mheshimiwa Dkt. Mpango aingize mpango huu hasa kwenye kipengele ambacho kinahusiana na suala la usalama barabarani hasa kwa watoto wetu ambao wamekuwa wakisafiri kwenye vyombo vyaya usafiri.

Tukiangalia hata hizi *school buses* hakuna mikanda maalum kwa ajili ya watoto ili kuwaweka katika hali ya usalama wanapokuwa safarini. Hata kwenye magari yetu sisi Waheshimiwa Wabunge hatuna mikanda ambayo itawafanya watoto wetu wawe katika hali ya usalama. Kwa hiyo, nalo hili naomba liingizwe kwenye mpango, hoja hii ipelekwe kwamba vyombo vyote vyaya usafiri viwekwe *belts* kwa ajili ya watoto ili watoto wasafiri katika hali ya usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usafiri wa Anga. Usafiri huu mimi ninavyojua ni kwamba ukiimashwa, kila mkoa ukawekewa kiwanja kizuri kwa ajili ya kutua ndege ninaamini kabisa kupitia usafiri wa anga tutaendelea kukuza uchumi. Kwa sababu ya muda naomba nisiguse maeneo mbalimbali ambayo yatasababisha uchumi huo kupatikana kupitia usafiri wa anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba katika usafiri wa anga kwenye mpango wake aweke mpango wa kuhakikisha kwamba ndege inafika katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ukiwemo Mkoa wa Mtwara, ambako mpaka sasa hivi hakuna ndege ya *Air Tanzania* inayokwenda huko. Sasa hivi kuna *Precision Air* ambayo inabeba abiria wengi na wanajaa. Kwa hiyo pia *Air Tanzania* iende pia katika Mkoa wa Ruvuma na mikoa mingine ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee suala la *NDC*, hili ni Shirika la Maendeleo Tanzania, naomba niseme hawa *NDC* chini yake wameyatamia miradi mingi mizuri ambayo ni rasilimali katika nchi yetu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako; tunaendelea.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer Christopher Chiza*.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote. Naomba pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge ambao wamezaliwa upya na kujiunga na CCM. Wale mliobaki nawaambia nyumbani kumenoga, rudini. Dkt. Magufuli anatosha, Mama Samia anatosha, Mheshimiwa Majaliwa anatosha na kwenye mpango Mheshimiwa Dkt. Mpango anatosha. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niunge mkono hoja, halafu...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: ...hebu kaeni kimya. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja halafu nichangie...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge! Waheshimiwa Wabunge, nawaona kutoka hapa! Tafadhali nawaomba sana!

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: ...hawana jipyा, wamefilisika kisera hao.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti,
Taarifa.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa
Mwenyekiti, naomba nichangie mambo makubwa mawili...

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti,
Taarifa.

MBUNGE FULANI: Nyamaza. *Shut up.*

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti,
Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haonga.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa
Mwenyekiti, nadhani dakika zangu zitalindwa.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti,
Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti,
naam.

MWENYEKITI: Hebu kaa chini.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti,
nataka nimpe taarifa mzungumzaji.

MWENYEKITI: Kaa chini.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti,
nampa taarifa kwamba kura zake hazikutosha huyu bwana.
(*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Hebu kaa chini; endelea Mheshimiwa
Engineer Chiza.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, amenipoteza muda, amefilisika kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nichangie mambo makubwa mawili. Nimeshachangia kwa maandishi, lakini ninayo mambo mawili ambayo ninapenda ikikupendeza Mheshimiwa Waziri uyaweke katika mpango wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najikita kwenye suala la kuiweka tayari kupambana na majanga yanapotokea (*disaster preparedness*). Yako majanga mengi ambayo yanatokea na yanapotokea yanachukua rasilimali zetu, rasilimali watu, mali zetu, ajali za barabarani, ajali za majani, matetemeko ya ardhi kama yale yaliyotokea Bukoba, radi zinaua na kujeruhi wanafunzi wetu madarasani na walimu, lakini pia zipo ajali za moto ambazo zinaunguza majengo yetu na mali zetu na baadhi ya watu wetu wanakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo yapo masuala ya ukame na mafuriko, yote haya yanapotokea yanaharibu mali zetu. Kwa mfano katika Mkoa wa Morogoro mara nyingi sana, karibu kila mwaka tunajikuta, nadhani kuna mto mmoja unaitwa Mto Mkondoa, mto huu unapofurika miaka yote barabara husombwa, reli na miundombinu mbalimbali zinasombwa. Yote haya yanarudi kwenye fedha zetu ambazo tulizi-*allocate*kwa ajili ya mpango wa maendeleo zinatumika kurejesha ile miundombinu ambayo tayari inakuwa imeshaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nataka nitoe ushauri, kwenye masuala kama la ukame na mafuriko si masuala mageni, ni masuala ambayo yanaweza yakafanyiwa *trend and periodicity*tukajua kabisa wataalam wanao uwezo wa kujua ukame na kwamba mafuriko hutokea mara ngapi kila baada ya miaka mingapi. Kwa hiyo tukiweka namna hii tunaweza tukajenga uwezo ndani ya Serikali wa kupambana na mambo kama haya ambayo yanapunguza na kudhoofisha uwezo wa Serikali kifedha wa kutekeleza mipango yetu hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ushauri wangu katika hili ni kwamba tujifunze na tuweke tayari mipango ya *disaster preparedness* ili tuweze kupambana na majanga yanayojitekeza katika nchi yetu hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende sasa kwenye suala la pili ambalo ninapenda nilichangie, ni suala la kilimo. Nimezungumzia suala la kupambana na mafuriko, unapopambana na ukame au unapopambana na mafuriko unaweza kujenga miundombinu ya umwagiliaji, miundombinu ya *drainage*, lakini pia na kujenga mabwawa makubwa kama hili Bwawa la Farkwa tunalopanga kujenga. Mabwawa kama haya tukiyatengeneza sasa yatatusaidia kwanza kuleta mafanikio katika kilimo, lakini pia yatatusaidia kupunguza mafuriko na mambo mengine kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu tulishatangaza tangu miaka ya nyuma; tunazo hekta milioni 2.3 ambazo zina *high irrigation development potential*, tunazo hekta milioni 4.8 zenye *medium irrigation development potential*, tunazo 21.3 million hectares ambazo zina *marginal irrigation development potential*. Sasa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer Chiza* kwa ushauri wako.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia Mpango wa Maendeleo wa 2019/2020, kama ifuatavyo:-

(i) Serikali kutojiingiza peke yake katika miradi mikubwa mikubwa inayohitaji pesa nyingi za walipa kodi.

Miradi hii kwa kiasi kikubwa inaathiri uwezo wake wa kutoa huduma mfano mradi unaendelea wa *SGR* kwa mwaka huu umetumia zaidi ya shilingi bilioni 41; ununuzi wa ndege kwa *cash*, miradi mikubwa ya umeme na mengineyo, badala yake fedha nyingi iwekwe katika huduma zinazowagusa wananchi mfano huduma za afya, miundombinu ya maji na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *SGR* ungefani kwa sana iwapo Serikali ingewekeza katika mradi wa Chuma cha Liganga na Mchuchuma ambapo kuna mwekezaji Sichuan Hongda kwa ubia na Serikali wangewezesha kupatikana kwa chuma badala ya vyuma hivyo vya reli kuagizwa nchini Japani. Kuwekeza katika chuma hiki kuna faida nyingi za kiuchumi, ikiwepo kutengeneza ajira na kupunguza gharama katika uwekezaji wa mradi wa *SGR*.

(ii) Kufungamanisha maeneo yanayogusa watu wengi na uchumi wa viwanda. Mfano kilimo kinaajiri wananchi wengi licha ya takwimu kuwa kilimo kinakua asilimia 7.2 bado wakulima wa kawaida hawajafikiwa, kuna changamoto za soko lenye uhakika, utunzaji na uhifadhi wa mazao, wadudu na upatikanaji wa mbolea ya kutosha kwa wakati. Msisitizo uwe kuwezesha wakulima kuzalisha bidhaa zinazohitajika katika viwanda na tushawishi wawekezaji kuanzisha viwanda vitakavyotumia malighafi za wakulima.

(iii) Deni la Taifa. Ukokotoaji wa deni la Taifa na umuhimu wake uende sambamba na madeni ya Serikali na fedha zilizokopwa katika mabenki ya ndani na kwenye mifuko ya hifadhi na yajulikane idadi/kiasi chake na mkakati wa kuyapunguza uelezwe wazi. Mfano kufikia Juni 2017 deni lilikuwa shilingi trillioni 46.08 la ndani likiwa shilingi trillioni 13.3 na nje shilingi trillioni 32.745, hili ni ongezeko la shilingi trillioni 5 sawa na asilimia 12 kutoka shilingi trillioni 41.03 mwaka 2016. Deni la ndani mwaka 2016 lilikuwa shilingi trillioni 11.193 na sasa ni shilingi trillioni 13.3 sawa na asilimia 19 ya ongezeko ukilinganisha na mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kujua *international bonds* na muda zitakao-mature ili kuepuka ku-

default. How much dept is sustainable, the answer is simple, we don't know, market signal don't work as well as they should. Abdul A8 Ostry J, IMF Economists on a paper Primary Surpluses and sustainable debt levels in Emerging market Countries.

(iv) Sekta ya afya kuwa moja ya vipaumbele vya Taifa kwa kuwa tukiwa na wananchi wagonjwa hatuwezi kufikia Tanzania ya viwanda. Mfano, pesa za wafadhili/pesa toka nje Sh.103,677,403 za kununua *MRDT* - kipimo, kampeni ya Siyo kila Homa ni Malaria, Nenda Kapime; matumizi ya Sh.104,304,328,000 fedha za mikopo kununua vyandarua vyenye dawa na Sh.31,916,336 kuanzia 2015-2018, pesa hizi zingeokolewa kama tungeimarisha na kutumia dawa zinazozalishwa katika kiwanda cha viuatilifu cha Kibaha ambacho Serikali kwa kushirikiana na nchi ya Cuba imeklanzisha. Dawa bado ziko *storena* wanalamikia kukosa wateja. Tujikite katika kuwekeza kuteketeza maralia ya mbu badala ya kupima maralia na kugawa chandarua.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wa watendaji wote walioandaa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa mwaka 2019/2020. Ukurasa wa 8 wa Mpango umezungumzia kuongezeka kwa mauzo kwa mazao ya korosho, karafuu, tumbaku, chai na mkonge vipi kuhusu zao la kahawa, zao ambalo miaka ya nyuma lilikuwa likileta fedha za kigeni? Je, nini kimetokea? Serikali ina mkakati gani kuhakikisha zao la kahawa linazalishwa kwa wingi na kuendelea kuleta fedha za kigeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na uzalishaji mkubwa wa mazao mbalimbali ya matunda, mfano, nanasi, nyanya, machungwa na kadhalika. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima na mazao haya kupata masoko ya uhakika nje ya nchi ili kupata fedha za kigeni? Je,

Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza mazao ya matunda na mbogamboga ambayo hayo yakiwekewa utaratibu mzuri yanaweza kuleta tija kwa Taifa? Mazao kama tangawizi, hiliki, mdalasini, vitunguu saumu na pilipili ni mazao yenye soko sana katika nchi za uarabuni. Je, Serikali haioni imefikia wakati kuwa na mkakati wa kuendeleza wakulima wa mazao hayo ili tuweze kuyauza nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuwa na ziada ya chakula. Kumekuwa na malalamiko mahindi yameshuka sana bei na bado soko lina tatizo, kuna baadhi ya nchi ikiwemo Sudani Kusini kuna uhitaji mkubwa wa mahindi, je, Serikali imesaидiaje wafanyabiashara kwa kuwaunganisha na masoko ya nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la ustawi wa jamii, ukurasa wa 25 – 26 wa kitabu cha Mapendekezo ya Mpango, naipongeza Serikali kwa kusimamia uanzishwaji wa vikundi vyta kiuchumi kwa wanawake kwa kutoa mikopo ya shilingi bilioni 7.3 kupitia Mfuko wa Wanawake. Nashauri kufanya tathmini kuona ni kiasi gani fedha hizi zimeleta tija kwa wanawake katika suala zima la kuondoa umaskini katika kufanikisha lengo Na.1 la Maendeleo Endelevu – Kuondoa Umasikini (*No Poverty*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la elimu, naipongeza Serikali kwa elimu bure na yote yanayofanywa na Serikali katika kuhakikisha watoto wa Watanzania wanyonge wanapata elimu. Serikali ione umuhimu wa lishe mashulenii kwani ukosefu wa lishe bado ni kikwazo katika elimu. Suala la ujenzi na mabweni katika shule nalo Serikali ione la kufanya ili kuwaweka watoto maeneo ya shule badala ya kupanga mitaani, hii ni kwa watoto wote wa kike na wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ya kipaumbele, ukurasa wa 36 wa Mapendekezo ya Mpango, kipengele 4.3.3, kuboresha Shirika la Ndege Tanzania, nashauri Serikali iimarishe Kitengo cha TEHAMA ili wananchi

wanapofanya *booking* na kulipa kwa njia ya mtandao iwe rahisi na mtandao uwe unapatikana muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 39, kipengele 4.4.2 kuhusu kilimo, naipongeza Serikali kwa kuhakikisha usalama wa chakula kupitia kilimo. Sambamba na hilo, nashauri Serikali iweke nguvu kubwa katika kuendeleza zao la zabibu kwa kuimarisha Kituo cha Utafiti Makutupora na pia zitolewa mbegu – miche mingi zaidi. Aidha, Serikali ione uwezekano wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao ya zabibu ikiwezekana wananchi au wajasiriamali wadogo wapewe elimu ya kutengeneza mchuzi wa zabibu ili wauze kwa viwanda vikubwa na si mvinyo tu hata *juice* inayotokana na zao la zabibu wapatikane watalaaam na kuelimisha utengenezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeanza mkakati wa kufufua zao la mchikichi na kuendeleza zao la alizeti ili kuweza kujitosheleza kwa mafuta, nashauri Serikali ione umuhimu wa kufufua zao la karanga katika Mkoa wa Dodoma ili kupata karanga kwa wingi ambazo pia zikisindikwa mafuta ya karanga hayo pia yatasaidia kupunguza kuagiza mafuta kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ya Ujenzi wa Taifa letu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Makatibu Wakuu wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mpango wa Bajeti nitajikita katika maeneo yafuatayo:-

(i) Serikali iongeze vyanzo vya ukusanyaji wa kodi. Serikali imefanya juhudni kubwa sana ya kuboresha vyanzo wa kodi hali ambavyo haikuwepo miaka ya nyuma lakini bado jitihada ziongezeke kupata vyanzo vipyta ikiwemo kwa wachimbaji wa madini wadogo wadogo.

(ii) Miradi ya kitaifa Reli ya *Standard Gauge* ni jambo muhimu na Serikali imefanya kitu kikubwa pamoja na ununuzi wa ndege nyingi lakini niombe Serikali uendeshaji wa miradi hiyo uendane na watendaji wenye ubunifu. Ni miradi mikubwa na inayochukua fedha nyingi lakini tufike sehemu miradi hiyo ikusanye fedha itoe huduma na ilete maendeleo kwa Taifa letu.

(iii) Napongeza Serikali kwa kujenga *flyoverya TAZARA*, ni jambo jema na imeondoa msongamano. Ni vyema sasa Serikali ikajenga baadhi ya barabara za pembezoni za kulipia kwa watu wenye haraka. Barabara hizo zitakuwa na tozo ambazo zitalipa gharama za ujenzi wa barabara hizo lakini pia zitaleta mapato makubwa kwa Taifa na pia zitaleta maendeleo katika Jiji la Dar es Salaam na vitongoji vyake.

(iv) Bado kuna baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam kama *Kilwa Road*, eneo la Bendera Tatu kukiwekwa kivuko cha pess tutaingiza fedha nyingi wakati wa asubuhi na jioni.

(v) Afya za jamii, niombe Mpango uonyeshe jinsi utakavyoboresha Hospitali ya Muhimbili kwa kuwa Kitengo cha *Emergency* ambacho kinaokoa maisha ya wengi lakini hakina vifaa vya kisasa na hata *AC* ni za mashaka, *Oxygen* nazo mitungi ni michache na wakati huo kitengo kile kinatibu kwa gharama kubwa tofauti na wodi ya kawaida.

(vi) Uwezeshwaji wa wanawake, vijana na wale mavu. Naipongeza Serikali kwa kutenga fedha za kuwezesha wanawake, vijana na wale mavu. Niombe Serikali wafanye utafiti kama hizi fedha zinaenda kwa walengwa? Katika Jiji la Dar es Salaam utakuta kila unayemuuliza anasema hajapata fedha za mkopo.

Wakati huo huo asilimia ya makusanyo katika Mkoa Dar es Salaam inaweza kufikia takriban shilingi bilioni 5, ni fedha nyingi lakini zinaenda kwa watu wasio walengwa na hatimaye haziweki alama kwa Taifa wakati tungejengewa maeneo kama *Community Center* au viwanda vidogo na makundi haya yakashirikiana kufanya shughuli za maendeleo

katika viwanda au center wangele ya maendeleo ya ujuzi na majengo yangesa vizazi na vizazi vinavyo kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja 100%.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuipongeza sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa sana iliyofanyika ya kujenga miundombinu katika sekta za elimu, afya, ujenzi, mawasiliano, utawala, utumishi, ajira na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi zangu hizi, nachukua nafasi hii kuishauri Serikali yetu katika maeneo yafuatayo:-

(i) Miradi ya maendeleo, naomba Serikali itenye fedha za kutekeleza miradi ambayo inaanizisha na wananchi ili kuwapa moyo waendelee kuibua na kuchangia miradi mingine mipya.

(ii) Kutokana na fedha za miradi ya maendeleo kutokupatikana kwa asilimia mia moja, tunaomba wakati wa kuibua miradi ya maendeleo Mamlaka ya Serikali za Mitaa ipitie upya miradi iliyokosa fedha katika mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, kila mwaka.

(iii) Bado kwa sasa kuna matumizi yasiyo na tija kuitia mpango wetu *force account* katika Halmashauri zetu.

(iv) Kamati ya Bunge ya kila sekta ifanye ziara ya kukagua miradi kwa mfano hivi sasa kuna mpango wa ujenzi wa hosteli za wanafunzi kwa shilingi milioni 75 kwa nchi nzima hivyo kuna maeneo majengo hayo yamekamilika na baadhi ya maeneo majengo yamekwama na kuhitaji fedha nyingi. Hivyo basi, kuna haja ya kuwachukulia hatua wale wote watakaobainika kuzembea katika suala hili.

(v) Katika miradi ya afya tulipeleka kiasi cha Sh.400,000 hadi Sh.500,000 lakini kwa wale wazalendo kiasi cha Sh.400,000 zimejenga majengo yote matano na wale wasio

wazalendo wameshindwa kujenga hata yale majengo matano. Hivyo basi tuna kila sababu ya kutuma timu ya watu wachache kwa ngazi ya Taifa ili kujenga msingi mzuri wa kusimamia rasilimali zetu kwa manufaa mapana.

(vi) Mkopo vyuo vikuu, tunaomba mikopo ya chuo kikuu iltolewe kwa wote kwa kuwa baadhi ya vigezo katika utoaji wa mikopo hiyo ni lazima wakopaji walipe na kwa kuwa Watanzania wote ni sawa.

(vii) Uchocheaji wa ajira, tunaomba Serikali iangalie utaratibu wa kuboresha maslahi ya wastaafu kwa kuwa umri wa Mtanzania unazidi kupungua na kwa kuwa watumishi wanaogopa sana kustaafu kabla ya umri wa miaka sitini kisheria. Hali hii ingeboreshwa katika maslahi ya pensheni ya kustaafu ili watumishi wa umma wastaafu kwa hiari miaka 50 na miaka 55 kwa lazima. Hapa nchi yetu itakuwa imeongeza nafasi za ajira kwa vijana wote ambao wamehitimu vyuo vikuu na kutoa mchango wao katika kulitumikia Taifa letu.

(viii) Mapato ya nchi, Tunaomba Serikali isimamie mkakati wa kuweka mazingira mazuri ya wawekezaji wa ndani na nje ili kukuza uchumi wa nchi. Kwa kuwa sekta binafsi ni nguzo muhimu sana katika uchumi wetu urasimu, ubabaishaji, uwazi, masharti mengi yasiyo na tija yaondolewe katika kuwakaribisha wawekezaji.

(ix) Tunaomba Serikali iangalie mfumo mzima wa ukusanyaji wa mapato. Bado kuna wafanyabiashara wengi sana ambao hawajasajiliwa kukusanya mapato ya nchi. Kodi hii ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) inaogopwa sana na wafanyabiashara wenyewe sifa ya kusaidia Serikali kukufanya mapao yake. Hata hivyo, kuna maafisa wachache wa ngazi ya mikoa wanaendelea kuwaogopesha wafanyabiashara kana kwamba ukisajiliwa *VAT* utafilisika, hali hii pia ipo kwa ngazi za Wilaya. Hivyo basi, kuwe na kamati ndogo ya kuangalia *TRA* kama jicho la mkoa na ngazi za Wilaya. Kwa sasa kuna idadi kubwa ya wafanyabiashara ambao bado

hawajasajiliwa kwenye ukusanyaji na usajili wa VAT kwa miji ya mikoa na wilaya.

(x) Kodi ya makadirio ya awali kwa wafanyabiashara wadogo na wale wa kati ipewe nafasi ya kupandishwa kwa asilimia 25% kwa mwaka. Kodi hii itakuwa inakusanywa kwa uhakika na kufikia lengo kamili kwa mwaka. Hivi sasa wanaolipa kodi hii wanagawana na baadhi ya maafisa wa TRA.

(xi) Serikali iendelee kuhamasisha ufungaji wa mashine za kielektroniki kwa wafanyabiashara wetu ili baadaye ione umuhimu wa kupunguza baadhi ya tozo za kodi za ndani. Hivi sasa wote waliofunga mashine hizi hawafundishwi manufaa ya zile mashine na athari zake. Kwa sasa kuna uwezekano mkubwa kwa nchi yetu kukusanya kodi kwa kufunga mashine nydingi na kusajili wafanyabiashara wengi kwa ajili ya VAT. Ninayo mifano ya wazi ambayo siyo rahisi kuelezea katika mchango huo. Kuwe na idadi inayosajiliwa VAT kila mikoa na wilaya kulingana uwezo wa mji huo ulivyo kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi bila kuwa na uwezo wa kukusanya kodi zake za ndani siyo rahisi iweze kutoa huduma bora kwa wananchi wake. Pia bila kujenga hali ya uzalendo kwa wafanyabiashara wetu katika kuisaidia Serikali kukusanya mapato siyo rahisi tukapiga hatua kwani hata mataifa yanayotuchangia wanapata moyo wanapoona tunafanikiwa kukusanya mapato yetu ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuwasilisha.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, katika kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/2020, ukurasa wa 42, aya 4.5.1.2, Vyuo vya Ufundi na Teknolojia, nashauri, kiongezwe kifungu kipyta (d) kitakachosomeka kutumia fursa zilizopo katika miradi yote ya kitaifa inayoendelea nchini ili kuhakikisha wahitimu wanapata ujuzi

ulio bora kupitia mafunzo kwa vitendo. Kifungu cha sasa (d) kisomeke (e).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, aya ya 4.5.1.3, nashauri, kiongezwe kifungu (e) kitakachosemeka kama ilivyopendezwa hapo juu. Kifungu cha cha sasa cha (e) kisomeke(f).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za mapendekezo/ ushauri ni:-

(i) Vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na kinga. Kwa miaka karibu yote mitatu 2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019 mojawapo ya vihatarishi katika utekelezaji mipango hiyo imetajwa kuwa ni kukosekana kwa rasilimali fedha na kutokuwepo kwa uwiano sawa na ubora wa rasilimali watu.

(ii) Mpango wa maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2016/2017 – 2020/2021, ukurasa wa 67, aya ya 4.3.2, *Skills Development, key targets by 2020: Proportion of working population with high level skills 12.1%, middle level skills 33.%*, ukurasa wa 179, Table B10: *Skill Dev. Interventions. Challenges - lack of opportunities for apprenticeship and Internship and lack of National Skills Dev. Strategy etc. Interventions required, provide internship training for graduates at working place and provide apprenticeship training for students at the working places.*

(iii) *Comprehensive Review Report for Tanzania Five Year Dev. Plan 2011/2012 – 2015/2016.* Ukurasa wa 91 na 92. *Skilled working population: Highly qualified (Professionals); Medium qualified (Technicians/associate professionals and medium skilled workers.* Changamoto kubwa ya ufikiaji malengo ni *capacity constraint in terms of quality and quantity of manpower and facilities.*

(iv) *The Tanzania Dev. Vision 2025* (Dira ya Taifa ya 2025). Sura ya 4.0 - *Driving Forces for the Realization of the Vision. 4.2 - Competence and Competitiveness Quality Education.* Hii ni lazima itazamwe katika sura ya nadharia na vitendo.

(v) Kutotumia miradi mikubwa inayoendelea kama fursa ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi vyuoni; wataalam wapya (wachanga) katika taaluma; elimu endelevu kwa wataalam waliomahiri na makampuni ya kitanzania ni hasara kwa Taifa. Kwa kutotumia fursa hii inasababisha kukosa utaalama na uwezo wa kuendesha na kuhudumia miradi hiyo siku za baadaye; kushindwa kujenga uwezo wa Taifa kwa ajili ya miradi kama hiyo siku zijazo na kushindwa kupunguza gharama za miradi kama hiyo siku zijazo.

MHE. COSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu soko la dhahabu kutokana na Tanzania kuwa na madini mengi ya dhahabu hasa Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Hivi sasa Mkao wa Geita umehamasisha ujenzi wa *Elusion Plants* na uzalishaji wa dhahabu umeongezeka mara dufu kutokana na taarifa za mapato ya ndani ya Halmashauri (*service levy*) inayotozwa kwenye makampuni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoza kodi kwa mzalishaji wa ndani na kumuacha mnunuzi wa dhahabu ambaye kwa sasa hajulikani. Ili kuifanya Serikali kupata mapato kwa mnunuzi wa dhahabu ya wachimbaji wadogo (*exporter*) ni muhimu sana kufungua soko maalum la dhahabu (*gold market*) ambapo wachimbaji wetu watauza kuliko ilivyo sasa wengi wanauza Kenya, Uganda na Dubai.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza ya mchango wa kuzungumza katika sekta ya afya na elimu. Bajeti tarajiwa ihahakikishe hospitali za wilaya zinazoenda kujengwa zinapata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Hospitali ya Mkao wa Rukwa ilianza kuzungumzwa miaka saba iliyopita na mpaka sasa hakuna jengo lolote liloanza kujengwa. Naiomba Serikali itoe fedha kwenye mpango huu wa bajeti ijayo Mkao wa Rukwa upate Hospitali ya Rufaa, itakuwa ukombozi kwa watu wengi sana wasiokuwa na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu, maboma mengi ya madarasa yamejengwa, Jimboni kwangu tu pekee zaidi ya madarasa 270 yanashubiri kuezekwa kwa kutegemea Serikali. Tumeshawishi wananchi nao wamehamasika tumejenga sasa maboma yamebaki. Maabara pia zimejengwa shule za sekondari zote lakini hazijapewa fedha ya kumalizia majengo haya yaweze kutumika.

Naiomba Serikali katika Mpango huu iangalie jinsi ya kukamilisha miradi ya wananchi iliyokwama ikisubiria mchango wake.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja kwa maandishi. Kwanza naipongeza Serikali ya CCM kwa utekelezaji mzuri wa llani ya CCM 2015 – 2020. Napenda kuongeza vipaumbele katika sekta za afya, kilimo, uvuvi na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya. Ibara ya (50)P ya llani ya CCM inazielekeza Halmashauri kufanya utambuzi wa wazee ili waweze kutibiwa bure katika hospitali za Serikali. Hali ilivyo ni kusuasua kwa utambuzi na utoaji wa vitambulisho vya NHIF; katika baadhi ya mikoa utekelezaji ni chini ya 5%. Napendekeza suala hili liwekwe katika mpango kama moja ya vipaumbele ili liweze kupangiwa mikakati ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya (5)M ya llani ya CCM inaelekeza Serikali kukamilisha ujenzi wa Hospitali za Mloganzila, Chuo Kikuu cha Dodoma na Mtwara. Hongera Serikali ya CCM kwa ukamilishaji Hospitali ya Mloganzila ambayo imekwishazinduliwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na pia Hospitali ya *UDOM* inaendelea na upandikizaji wa figo. Hospitali ya Mtwara bado hajakamilikia, kipaumbele kimojawapo katika sekta ya afya ni kupeleka vifaa tiba katika Hospitali za Kanda, Hospitali ya Mtwara ni moja ya hospitali za kanda. Nashauri ukamilishaji wa Hospitali ya Mtwara uwekwe katika mpango 2019/2020, ili na yenye we ipate mgawo wa vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo. Vipaumbele katika sekta ya kilimo vimejielekeza katika kuondoa umaskini na kuhakikisha usalama wa chakula kama *SDGs* Namba moja na mbili inavyoelekeza. Ni jambo jema na nipongeze jitihada hizi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu lipo tatizo la *hidden hunger* ambalo pia linaathiri *lifespan* ya Watanzania. Wataalam wa lishe katika taasisi za lishe wamejitahidi kufanya *biofortification* kwa baadhi ya mazao kama viazi na mahindi ili kuongeza vitamin A na kwa maharage kuongeza *zinc* katika kukabiliana na tatizo la *hidden hunger*. Changamoto kubwa katika eneo hili ni uhaba wa mbegu za mazao lishe haya ambayo ni lazima yasambazwe nchi nzima. Napendekeza katika skimu za umwagiliaji yatengwe maeneo kwa ajili ya kuzalisha mbegu za mazao lishe ili mbegu zisambazwe nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi. Naipongeza Serikali imeweka katika Mpango ujenzi wa bandari ya uvuvi kama moja ya vipaumbele. Napendekeza ujenzi wa bandari ya uvuvi uende sambamba na ujenzi wa chelezo (*dry dock*) na ununuzi wa meli za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina fursa nzuri ya uvuvi wa bahari kuu lakini haijawahi kuingiza pato la angalau shilingi billioni 10 ikilinganishwa na Visiwa vya Mauritius na Seychelles ambavyo kwa nyakati tofauti wameweza kupata kati ya dola za Kimarekani milioni 270 na 480 ambazo ni takribani kati ya shilingi za Kitanzania bilioni 600 na zaidi ya trilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushahidi uliopo wa meli zinazopewa leseni za uvuvi nchini, jodari wengi katika visiwa hivi wanatoka nchini Tanzania. Hata sisi tunaweza kuinua uchumi wetu kwa kutumia fursa ya uvuvi wa bahari kuu. Meli ya uvuvi pia itasaidia kuziba upungufu wa kitoweo cha samaki katika nchi yetu kwa ajili ya matumizi ya wananchi na kuweza kuboresha afya zao kwa kujikinga na maradhi kama uvimbe, shinikizo la damu, kiharusi, kupooza, saratani

na mengineyo, kazi inayofanywa na virutubisho aina ya *selenium na Omega 3*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji. Halmashauri ya Tandahimba iwekwe katika Mpango kwani upatikanaji wa maji ni asilimia 24% tu hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri suala la kilimo cha umwagiliaji lipewe mkazo kwa kutumia umwagiliaji wa maji ya ardhini badala ya kutegemea maji ya mvua, miradi ya maji ya maji ya mvua haina uhakika. Serikali iwekeze katika skimu za umwagiliaji wa maji ya visima virefu ambayo hayawezikukauka au kuleta mafuriko katika sehemu husika. Kilimo cha umwagiliaji kitaleta mazao mengi na kuzuia mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko skimu nyingi za umwagiliaji zilizokusudiwa kuzalisha chakula na sasa hazifanyi kazi pamoja na Serikali kuwekeza hela nyingi, skimu hizo zilishindwa kwa sababu ya kutegemea mvua. Nchi kama Israel, Misri, Sudan na nyinginezo wanafanya umwagiliaji kama kilimo kikuu na cha tija kubwa. Naishauri Serikali iwekeze katika kilimo cha umwagiliaji kama njia ya uhakika ya kupata chakula hasa mpunga na mahindi. Chakula kingi kitadhibiti mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa kiasi gani Mpango wa Maendeleo wa 2018/2019 umeweza kukamilika mpaka tupo kwenye miradi mipya? Viwanda vingi vilivyobinafsishwa havifanyi kazi mpaka leo, vingine vimefanywa *store* za kuhifadhi mizigo na kadhalika. Napenda kujua mpaka sasa hivi ni kwa kiasi gani viwanda vya kusindika nyama kama Tanganyika *Packers* kilichopo Dar es Salaam, *Machine Tools* kilichopo Kilimanjaro, *General Tyre*, kiwanda cha matairi kilichokuwa kikubwa Afrika Mashariki

mpaka leo havijafufufuliwa lakini Serikali inakuja na mipango mipyä. Je, viwanda hivi ndiyo vinasahaulika kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la Taifa. Serikali ina mpango gani wa kupunguza deni la Taifa? Deni hili limezidi kuongezeka kutoka 2016 deni lilikuwa Sh.43,906,702,000,000 hizi ni shilingi za KItanzania fedha za kigeni sawa na Dola milioni 840 za Kimarekani. Deni hili linazidi kuongezeka kwa sababu kila kukicha Serikali bado imezidi kukopa kwa kusingizia mikopo yenyé riba nafuu lakini tukumbuke deni bado linakua. Je, uchumi wetu utakua kwa kiasi gani kwa deni kubwa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kila siku deni hilo linazidi kuwa kubwa sababu ya riba na Serikali ikipunguza deni inajikuta inalipa riba na deni linabaki kuwa kubwa. Mfano, bajeti ya 2018/2019 Serikali imetenga Sh.10,400,840,000,000 ili kulipa deni la Taifa wakati huo huo Serikali imepanga kukopa Sh.8,904,727,000,000. Tukumbuke mkopo huu una riba ya kibiashara. Je, uchumi wetu unaweza kukua kwa mtindo huu? Je, deni letu la Taifa ni himilivu? Sababu deni hili ni zaidi ya nusu ya pato la Taifa. Ili uweze kukopa lazima deni liwe chini ya asilimia 50 ya pato la Taifa na deni letu kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* tayari tumevuka, deni lipo kwenye asilimia 63. Je, ni kwa kiasi gani Serikali imechukua ushauri wa *CAG* na kuufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upanuzi wa barabara zetu (*flyovers*) Jijini Dar es Salaam iliyopo *TAZARA*. Serikali inajivunia ujenzi huu umekamilika, je, hili ni daraja au ni *flyover*? Ingependeza Serikali kuja hapa na kuonyesha ina mpango gani wa kujenga *flyover* kutoka mfano, Dar es Salaam *International Airport* mpaka katikati ya Mji, *Samora Avenue*. Hii kwanza ingechangia kuokoa foleni iliyopo Dar es Salaam na kukuza uchumi kwa sababu muda ni pesa (*time is money*). Kupoteza muda mwingu sana barabarani inapoteza sana muda wa kufanya kazi. Ni vizuri Serikali ikatenga bajeti kwa ajili ya wataalam wetu, Maafisa wa mipango miji na kadhalika wakatembelea nchi kama *United Emirates* (Dubai)

wakijifunza jinsi *flyover* zinavyokuwa au zinavyojengwa siyo kujenga daraja na kuliita *flyover*.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa kuanzia 2018 hadi 2020. Kwa hali halisi ya sasa kwa upande wa wadau ni vyema Serikali ikaangalia upya namna ya kuwasaidia wawekezaji wetu waweze kufanya biashara yao bila kubughudhiwa badala ya kuwasumbua. Kwa nini nasema hivi? Kuna baadhi ya viongozi hasa Wakuu wa Wilaya wanawabughudhi wawekezaji wetu. Mfano mzuri ni Mkuu wa Wilaya ya Hai amekuwa akisumbua wafanyabiashara ni vizuri tuwe nao *friendly* badala ya kuwafanya *unfriendly*. Tunatambua ni wajibu wa kila mfanyabiashara kulipa kodi lakini wafanyabiashara hawa wanalipishwa kodi kubwa sana na kuleta bughudha kwa wafanyabiashara hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa viwanda. Tunasema Tanzania ya viwanda lakini hadi sasa hakuna kiwanda chochote kilicho jengwa. Ni vizuri Serikali ikajikita kwenye kufufua viwanda tulivyonavyo vya zamani ili kuinua uchumi wa viwanda ndipo tuangalie namna ya kujenga viwanda vingine. Viwanda vyetu vya zamani vilivyoachwa na Baba wa Taifa hili, Muasisi wa Taifa hili Mwalimu Julius Kambarage Nyerere viwanda kama *MUTEX*, *MWATEX*, Urafiki na viwanda vya ngozi na vya kusindika nyama vilisaidia kukuza ajira kwa wananchi wa Tanzania pamoja na kukuza uchumi na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni nguzo kuu ya kuinua uchumi wa Taifa letu kwani takribani asilimia 80 ya wananchi wa Tanzania ni wakulima. Pia Serikali imekuwa ikisisitiza wananchi walime sasa wakilima mazao yao wataya uza wapi? Ni vyema Serikali ingewasaidia wakulima hawa kutafuta masoko ya uhakika ili wanapolima wawe na uhakika wa masoko ya kuuzia mazao yao kuliko hivi sasa wakulima wanalima lakini hawana uhakika wa soko la kuuzia mazao yao kwani mazao mengi huharibika na kuozea kwenye maghala (*store*) na kuishia kuliwa na wadudu

(kubanguliwa) ukiangalia mazao mengi ni *genetic modified (GM)*.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia suala la Watanzania kupata maji safi na salama. Bila maji hakuna uhai wa Taifa katika maendeleo ya nchi. Natambua kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Rais na wasaidizi wake. Naomba Serikali ikubali kuongeza shilingi 50 katika kila lita ya mafuta ili fedha za kutosha zipatikane na miradi mingi ya maji itekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri wa Fedha aamue kutenga fedha za kusaidia uanzishwaji wa viwanda vyta kubangua korosho ili kuongeza thamani na Serikali itaongeza kipato na kuwafanya wananchi wake kupata ajira. Hatuna sababu za kuendelea kuuza nje korosho ghafi na hivyo hivyo mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la afya ni muhimu sana. Nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano inavyoshughulikia suala hili kwa ujenzi wa vituo vyta afya, hospitali na upanuzi wa hospitali za rufaa. Ombi langu ni kutenga fedha zaidi kwa ajili ya kuajiri watumishi wa afya na vitendea kazi. Kwa suala la usambazaji wa madawa Serikali ya Awamu ya Tano imefanya vizuri na liwe ni jambo endelevu. Huo ndiyo mchango wangu.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri iliyofanyika kipindi cha miaka mitatu chini ya uongozi wa Jemedari Mkuu, Mheshimiwa Dkt. John P. Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa 2019/2020, naunga mkono hotuba ya Waziri wa Fedha na maoni ya Kamati. Serikali imefanya kazi kubwa

katika kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa vituo vya afya na hospitali, ujenzi wa vyumba vya madarasa/ mabweni, matundu ya vyoo, miradi ya maji, elimu bila malipo – wazazi wameitikia wito wa kuwapeleka watoto shulenii na kadhalika, yote haya ni mafanikio ya mipango mizuri iliowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni kama ifuatavyo:-

(i) Shule zote za sekondari ungekuwepo mpango mzuri wa kupata fedha ili kuwezesha kujenga mabweni kwa lengo la kuwasaidia watoto kukaa shulenii ili waweze kujisomea vizuri zaidi na kuwa na ufaulu mzuri zaidi.

(ii) Kutengwe fedha kwa ajili ya kukamilisha maabara zilizojengwa kwa nguvu za wananchi ili ziweze kutumika kwa wanafunzi kupata elimu bora ya sayansi kwa vitendo.

(iii) Kuendelea kuzisimamia na kuzihimiza Halmashauri zote kuongeza vyanzo vya mapato lakini kukusanya mapato yote waliyojipangia kwa kutumia mashine za kukusanya mapato. Bado kuna tatizo kwa baadhi ya Halmashauri kutokuwa na mashine jambo ambalo linasababisha kupoteza mapato mengi na kuzisababishia Halmashauri hizo kutofikia lengo la ukusanyaji wa mapato. Nashauri kwa kuwa Halmashauri nyingi zinasema zinashindwa kununua mashine za kukusanya mapato (*POSS*), *TRA* wangechukua jukumu la kuwapatia mashine hizo na kuweka utaratibu namna ya kulipa ili ziwezeshe kukusanya mapato mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendelee kutenga fedha ya kutosha kwa ajili ya maji. Aidha, wakandarasi wamekuwa wakidai malipo yanachukua muda mrefu bila kulipwa hivyo kunachangia kuchelewesha uendelezaji wa miradi hiyo. Naomba kuwepo na utaratibu Wizarani wa kuwa na Mtendaji wa kuchambua madai yote na kuyapatia ufumbuzi wa malipo haraka ili wananchi waweze kupata huduma za maji kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya madai ya watumishi. Niombe Serikali pamoja na jitihada kubwa na nzuri iliyofanywa na Serikali ya uhakiki wa watumishi na madeni, ni vyema basi yale yanayokuwa yamehakikiwa walipwe mapema ili kupunguza manung'uniko ya watumishi, hususani wa kada za walimu, wauguzi, madaktari na wengine.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu sukari na mafuta ya kula. Mahitaji ya sukari yanatulazimisha kutumia zaidi ya shilingi bilioni 350 kuagiza sukari na tunaagiza mafuta ya kula tukitumia zaidi ya shilingi bilioni 470. Nashauri Serikali idhamirie kwa dhati kuwekeza kwenye sukari kwa mtindo wa viwanda vidogovidogo kama wanavyoshauri wenzetu wa *TASGA* (*Tanzania Sugarcane Growers Association*) na wenzao wa *Geoman Cane Estate Ltd, World Association of Beet and Cane Growers (WABC)* na *SAGCOT CATALYST TRUST FUND*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafuta ya kula nimeona jitihada za Mheshimiwa Waziri Mkuu kufufua zao la mchikichi. Nashauri tuongeze bidii katika zao hili ili tujitosheleze kwa mafuta ya kula, tupunguze *importation* ya mafuta ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira wezeshi ya biashara. Kama nilivyosema katika mchango wangu wa kuongea, tume-*drop* kutoka nafasi ya 137 hadi ya 144, tumezidiwa na Rwanda (29) na Kenya (61), Uganda (127) katika suala zima la mazingira bora ya kufanya biashara. Nashauri *blueprint* iwe *operational* na iwe chini ya *PM Office* na siyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Nashauri tupunguze milolongo hasa katika kuamua, siyo vyema mwekezaji azungushwe kwa jambo ambalo tukiamua kwa wakati, litaleta uwekezaji, ajira na *more revenue*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujitathmini kwa nini tuko nafasi ya 144? Je, kama Serikali tunaridhia? *It's not about tax exemptions, but it is about predictability.* Aliniambia Balozi wa Denmark kuwa *investors* wao hawataki misamaha ya

kodi lakini hali ya kutabirika na zaidi maamuzi kwa wakati ya hoja/mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano ya kuchelewa kufanya maamuzi na athari zake zipo nyingi lakini nitazitaja chache tu kama Kiwanda cha mbolea (*FEROSTAT*) kule Kusini; Mradi wa Bagamoyo; Mchuchuma na Ligang na *recently*, fursa ya kuuza muhogo China. Kuna mwekezaji kaomba ardhi eka kumi tu ili aweke *factory* hapa nchini walau ku-*process* lakini miezi sita anazungushwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya misitu (Mafinga). Zipo kanuni zinazuia kusafirisha mazao ya misitu kama mbao, milunda na nguzo usiku. Nashauri Waziri mwenye dhamana wa utalii na maliasili alitazame suala hili ili ku-speed up ukuaji wa uchumi.

MHE. MWANTUMU DAU HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri wa Fedha na Mipango kwa jitihada zake anazozichukuwa pamoja na Naibu wake. Nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa jitihada zake anazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie Mpango kuhusu Wizara ya Afya. Vituo vya Afya vingi vimejengwa, niipongeze Serikali lakini kuna vingine bado havijaguswa kama kufanyiwa ukarabati.

Naishauri Serikali ifanye jitihada ili na vilivyobakia navyo vipewe kipaumbele kwa kutengewe fedha. Pia naishauri Serikali yangu chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, nyumba za watumishi wa umma nchini zifanyiwe ukarabati bajeti ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upandikizaji figo. Naishukuru Serikali kwa jitihada, sasa badala ya kusafiri wagonjwa nje, matibabu tunayapata hapa nchini kwetu. Nashauri huduma za upandikizaji na vifaa vyake ziboreshwé vizuri ili Serikali isijekupata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu ununuzi wa dawa, chanjo na vifaa tiba. Nashauri dawa hasa za sukari na *pressure* ziongezwe zaidi ili akina mama na watoto walioathirika waweze kuzipata kwa muda waliopangiwa na daktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri kwa jinsi Mpango huu ulivyopangika. Nasema ahsante sana, naunga mkono hoja.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Waziri pamoja na timu yake yote kwa kuandaa Mapendekezo ya Mpango wa Taifa 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la afya. Niipongeze Serikali yangu Tukufu kwa kujenga vituo vya afya zaidi ya 300 nchi nzima. Pamoja na pongezi hizi, niiombe Serikali yangu sasa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuwaunga mkono wananchi wale ambao wanajenga wenyewe vituo vya afya pamoja na zahanati ili waweze kukamilisha vituo pamoja na zahanati hizo ili wananchi wetu waweze kupata huduma kwa wakati kama walivohamasihwa na Wabunge wao. Kama ilivyo ada mtu mwenye afya nzuri ndiye mtu ambaye atatumikia Taifa lake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu suala la elimu. Kuna maboma mengi sana yaliyojengwa na wananchi ambayo ni madarasa, maabara pamoja na nyumba za walimu. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu imalizie maboma haya ili watoto wetu waweze kusoma elimu kwa vitendo na ukizingatia tunaenda kujenga uchumi wa viwanda. Kwa hiyo, huu ni ukweli usiofichika kwamba tunahitaji wataalam watakaoendesha viwanda vyetu vinavyoendelea kufunguliwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili lakini ukiangalia wakulima wetu hawa hatuwawezeshi vya kutosha. Niishauri Serikali yangu iwezeshe

wakulima wetu kwa kuwajengea miundombinu wezeshi, kama vile mabwawa na mifereji kwa ajili ya kulima kilimo cha umwagiliaji. Ni imani yangu kubwa Serikali ikifanya yote haya ninayoyashauri moja, malighafi ya viwanda vyetu zitapatikana kwa wingi hapa hapa nchini, pili, ulipaji wa kodi utaongezeka na tatu, vijana wengi watakuwa wana ajira na hawatakimbia mijini tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishauri Serikali yangu Tukufu, kwa kuwa nchi yetu ina Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Jeshi hili liwe na mpango wa kuwakusanya vijana waliomaliza Darasa la Saba pamoja na wa Kidato cha Nne ambaao hawakuweza kuendelea na masomo. Vijana hawa wafunguliwe mashamba makubwa pamoja na kuwekewa miundomibunu wezeshi. Ikifanyika hivyo, Serikali itakuwa inazalisha chakula na biashara pia malighafi ya viwanda vyetu itakuwa inapatikana kwa wingi pamoja na ajira kwa vijana wetu ambaao kwa sasa wengi wapo mtaani. Suala hili na JKT iwe ni lazima kwa vijana hawa hata kama hawataki.

Mhesheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali iwawezeshe vijana hasa kwa wale ambaao wana uthubutu wa kufanya kazi, kwani vijana hawa wakiwezeshwa hata ukusanyaji wa kodi utakuwa ni mkubwa sana, tena ambaao hautatumia nguvu kubwa. Pamoja na hayo, kuna vijana wengi sana wamejiajiri hasa katika sekta ya bodaboda. Niishauri Serikali yangu vijana hawa wawe kwenye mfumo rasmi wa kutambuliwa ili nao waweze kuchangia Serikali yao. Vilevile Serikali ipunguze hii faini ya bodaboda ambayo ni Sh. 30,000 sawasawa na watu wa magari makubwa. Ningeshauri faini hii ipungue iwe Sh.10,000 kwani ikiwa faini hiyo vijana wengi hawatakuwa wakijificha na kupita njia za panya kama ilivyo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna haya makundi ambayo ni muhimu sana na makundi haya yakiwezeshwa kodi itapatikana na kukusanya kwa wingi. Makundi hayo ni wafanyakibashara wadogo wadogo; vikundi vya wajasiriamali na mama ntilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja kubwa sana kila Jimbo kujenga Chuo cha *VETA* ili kuwaandaa vijana wetu kwa kujajiri na siyo kutegemea ajira Serikalini. Likifanyika hili Serikali itakuwa imewakomboa vijana wengi hasa wale ambao wameshindwa kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za vijijini zinachangia wakulima wengi kupata hasara hasa unapofikia wakati wa mavuno, mazao hayatoki shambani na kupelekea mazao mengi kuharibika mashambani. Niishauri Serikali yangu hasa kitengo hiki cha *TARURA* wapewe fedha za kutosha ili wajenge hizi barabara za vijijini kwa wakati na kuepuka wakulima wetu kutopata hasara pamoja na kupoteza kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme vijiji ni muhimu sana, kwani unachangia ajira kubwa sana na pla kuna maeneo mengine maji ni ya kuchimba visima, kwa hiyo, bila umeme wananchi wanakosa huduma hiyo ya maji. Niishauri Serikali yangu itenge pesa za kutosha katika miradi hii ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara za kisekta zilizochangia na kuandaa Mapendekezo ya Mpango tunaoujadili Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, kwanza, ni kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Suala la elimu, tunaanzisha viwanda ambavyo ili viwe endelevu vitahitaji rasilimali watu wakiwemo Wahandisi, Mafundi Sanifu na Mafundi Mchundo. Kasi ya kuanzisha viwanda lazima iende sawia na kasi ya kuzalisha wataalam ambao watavihudumia viwanda vinavyoanzishwa. Elimu ya ufundi inayotolewa lazima ikidhi mahitaji ya wenye viwanda. Suala hili siyo tu kwamba litafanikisha uendeshaji

wa viwanda bali pia litachangia upatikanaji wa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, suala la kilimo. Viwanda vingi vinavyoanzishwa kwa ajili ya kuchakata na kusindika mazao ya kilimo vinahitaji uzalishaji wa malighafi bora kama pamba, mbegu za mafuta, miwa na kadhalika. Kuna haja basi ya kufungamanisha ukuaji wa kilimo na ukuaji wa viwanda katika sekta ya kilimo, napendekeza Serikali ifanye mambo yafuatayo:-

(i) Tuhimize mipango ya matumizi bora ya ardhi pamoja na upatikanaji wa Hakimiliki za Kimila na kuweka utaratibu wa hati zao kukubaliwa na taasisi za fedha ili wakulima wajipatie mikopo ya zana za kilimo, pembejeo na kadhalika. Mafanikio yaliyopatikana katika Wilaya ya Kilombero (Hakimiliki 8,303) na Ulanga (3,100) yapelekwe katika wilaya nyiningine.

(ii) Ili kupunguza changamoto ya masoko ya mazao, Serikali ianzishe *Price Stabilization Funds* za mazao. Tunaweza kuanza na mazao yenye changamoto kubwa kama korosho, pamba na tumbaku.

(iii) Kilimo cha umwagiliaji. Kuna mazao ambayo hata kama mvua zingenyesha kwa kiwango na mtawanyiko mzuri, kiutalamu, hatuwezi kufikia *break – even points* bila kuyamwagilia. Mazao hayo ni miwa – *growing season* ni zaidi ya *rainy season*; mpunga na mazao ya bustani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijwiwekee mpango unaoonesha mchango halisi wa kilimo cha umwagiliaji kwenye uzalishaji wa mazao. Kilimo cha umwagiliaji kichangie (*at least 20%*) ya utshelevu wa chakula wakati mnapokokotoa *self-sufficiency ratio* ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuboresha matumizi halisi ya Serikali. Ripoti za CAGzinaonesha kwamba kuna fedha "*D funds*" zinazopelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri za Wilaya. Serikali iweke utaratibu wa kutambua

fedha hizi ili zижумuishwe katika Bajeti za Serikali ili ziingizwe katika mfumo wa Serikali na kutuwezesha kupata bajeti halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati. Napenda kushauri Serikali iwe makini katika kuandaa utekelezaji wa mradi wa makaa ya mawe (Mchuchuma) na Chuma (Liganga) katika kuchenjua “*Iron Ore*” tuwe na hakika ya aina nyingine za madini kama *titanium* na *vanadium* yanayowezekana kuwamo ili Taifa linufaike zaidi kuepuka changamoto za Makinikia katika madini mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ili reli iwe na faida na ijisimamie, kwa kuchukulia mifano mingi basi inapaswa iwe na mizigo si chini ya asilimia 60 kwa sababu abiria hawawezi kupatikana zaidi ya asilimia 8 ya mapato yote ya reli. Tunaweza kupata mizigo ya majirani ila muhimu zaidi mizigo yetu ya ndani. Hilo litakuwa *mujarab* iwapo Serikali itajipanga kutengeneza barabara kutoka sehemu za ndani ili kukutana na reli kwa faida ya mazao ya kilimo ili kuwahi kufikia masoko. Suala la *advertisement* ni muhimu kubandikwa kwenye reli ili kukuza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuzungumzia Mpango wa Maendeleo bila ya suala la nishati na hasa ile ya gesi. Kuna kila dallili kuwa Serikali inatupa suala la gesi ambayo hadi sasa usambazaji wake ni mdogo. Tunajua gesi imezitoa nchi nyingi kinishati lakini hata kwa *LNG Pact*. Ushauri wangu basi *minimum* gesi itumike katika taasisi zote za umma. Naamini hilo likifanyika basi usambazaji utatoka kwenye asilimia ya sasa na itapanda na hivyo kumudu deni la malipo ya uendelezaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la gesi na mafuta ya Zanzibar, hasa baada ya mkataba wa *RAKGAS*na *SMZ* utata mkubwa zaidi utajitokeza na kuwa laana badala ya neema kwa Zanzibar. Mgawanyo wa vitalu, mapato na mkataba ni suala nyeti na kuwemo suala hilo bado kikatiba kunainyima

Zanzibar haki halisi ya umiliki hata kwa sheria ya Bunge ya 2015 na ile ya Zanzibar ya 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu ni vipi kunakuwa na mipango miwili tofauti katika nchi, matarajio mawili tofauti na malengo mawili tofauti lakini bado uwe na kipimo kimoja cha *GDP, Per Capital*/na vipimo vingine vya kiuchumi? Ni vipi unakuwa na mpango wa Taifa wa kiuchumi bila ya programu yoyote ya upande mwengine? *How can you have a federal program without any linkages to a member state or any connectivity?*

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kunipa afya njema na kuweza kuchangia machache katika hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ulioletwa kama utatekelezwa basi itakuwa ni chachu ya maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelekeza mchango wangu kwenye sekta ya mifugo na uvuvi. Uvuvi katika nchi yetu ni uchumi mkubwa na kama tutajipanga vizuri utaingiza pato kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu. Wako samaki wengi sana lakini sisi hatufaidiki na samaki hao kwani hatuna meli kubwa za uvuvi. Ziko meli nyingi za kigeni zinavua samaki wetu na Serikali inapoteza pato kubwa katika Taifa letu. Natoa ushauri wangu kwa Serikali kwamba sasa ijikite kununua meli kubwa ya uvuvi ili kuongeza uchumi wa nchi. Vilevile katika sehemu za fukwe, tujenge sehemu za kupumzikia baada ya kuogelea ili iwe kivutio cha watalii katika bahari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kuhusu mifugo. Nashauri uwekwe mpango maalum wa kuhakikisha kuwa migogoro ya wafugaji na wakulima imeisha ili waweze kuishi kwa upendo na waweze kufuga mifugo yao kwa

utulivu na kuacha kuhamahama na kuuana na kuua mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa sekta ya viwanda vidogo vidogo. Tunatambua Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuwezesha viwanda vidogo na vikubwa ili kuweza kufanya kazi na vile vilivyokufa kuvifufua. Huu ni mpango mzuri sana wa kuweza kuzalisha uchumi na vijana wetu kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba ikiwa hakuna umeme wa kutosha viwanda hivi havifanyi kazi, hivyo ni lazima tuwe na umeme wa kutosha ili viwanda hivi viweze kufanya kazi. Pili, ikiwa hatuna maji pia hatuwezi kuendesha viwanda hivyo na tatu, ikiwa hatuna malighafi pia ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri wangu kwa Serikali kwamba katika viwanda hivyo tuwe na viwanda vingi vyta kuzalisha malighafi ili Serikali iweze kupunguza gharama ya kuagiza malighafi kutoka nje. Pia tuboreshe miundombinu ya maji na umeme, hasa vijijini ili tuweze kupata mapato yatokanayo na viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo, naomba kuwasilisha.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mungu kwa kutupa uzima na kutuwezesha kuendelea na majukumu yetu. Nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kutokana na juhudini anazoendelea kuzichukua tangu aingie madarakani hadi sasa. Naipongeza Serikali na watendaji wote, kwa usimamizi wa miradi ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa katika kipindi kilichopita na inayoendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa mapato na kodi. Ni ukweli usiopingika kwamba kwa Mheshimiwa Rais kukemea na kutilia mkazo suala la makusanyo ya kodi ndiko kulikopelekea utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa

kiwango kilichofikiwa na kupunguza utegemezi uliokuwepo hapo nyuma. Tumeshuhudia katika bajeti ya Serikali mwaka hadi mwaka ikionyesha matumizi ya miradi ya maendeleo kupitia mapato ya ndani. Pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kusimamia mapato ya kodi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya mashine za *EFD*. Kumekuwa na mtindo kwa baadhi ya wafanyabiashara nchini kuendelea kukwepa kodi kwa kisingizio cha mashine kutokuwa na chaji au *network*. Naiomba sana Serikali iandae mkakati madhubuti wa kuwafuatilia wafanyabiashara hawa ili waweze kutumia mashine kama ilivyokusudiwa. Tunaendelea kuamini kwamba bila mapato ya kodi kwa sasa ni kuendelea kudhoofisha maendeleo ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wa wananchi. Katika Mpango huu sijaona asilimia 10 tulyoipitisha kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aone umuhimu wa kila Halmashauri kutenga asilimia 10 za kuwawezesha wananchi kwa kuliweka kwenye Mpango ili Halmashauri nazo ziweze kuliweka kwenye mkakati wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekuwa na malalamiko ya kukosa mitaji ya kuwaendeleza kiuchumi. Utaratibu huu wa asilimia 10 utapunguza malalamiko kwa wananchi hata kwa asilimia chache kwa Halmashauri zote nchini. Tukiangalia unapofika wakati wa kampeni za uchaguzi katika masuala tunayonadi kupitia llani ya Uchaguzi, suala la vijana na wanawake na wasiojiweza limekuwa likichukua sura ya aina yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa bahari kuu. Naomba niendelee kuomba na kuisisitiza Serikali kuwa suala la uvuvi wa bahari kuu ni sehemu mojawapo ya vipaumbele vitakavyotuungezea mapato makubwa nchini. Naomba sana Mheshimiwa Waziri aliorodhesha kwenye Mpango huu kuwa mionganoni mwa bajeti mkakati ili kuanza kulifanyia utafiti. Ndani ya mwaka mmoja tutaweza kuvua mara nne na kila *trip* moja kuna uhakika wa kuvuna jumla ya shilingi

bilioni 15. Mpango huu utasaidia sana kuongeza mapato ya Serikali kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kitakachotugharimu kama Serikali ni kutenga fedha kwa ajili ya kununua meli za uvuvi lakini kwa mwaka tutakuwa na uhakika wa kupata mapato ya shilingi bilioni 60. Tusiendelee kuacha rasilimali zetu za bahari kuendelea kuvuliwa na mataifa mengine siku hadi siku. Mipaka yetu ndiyo kwenye utajiri wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya VATinasamehe VATkwenye mitambo ya aina mbalimbali inayoagizwa kutoka nje ya nchi. Kanuni zilizoandaliwa kutekeleza sheria hii ziliweka kifungu chenye sharti kuwa msamaha utolewe kwenye mitambo ambayo VAT inayotakiwa kulipwa ni zaidi ya shilingi milioni 20. Kwa kanuni hii wajasiriamali wote wameondolewa kupata msamaha huo wa VATkwa sababu wajasiliamali walio wengi huagiza kutoka nje ya nchi mitambo yenyе thamani ya dola za kimarekani 5,000 hadi 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali irekebishe kanuni hii ili kuwezesha wajasiriamali kuagiza mitambo hiyo midogo midogo ambayo ni muhimu katika ujenzi wa Tanzania ya viwanda. Mitambo midogo midogo ndiyo itakayosaidia kujenga Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwa tuanzishe skimu ya hifadhi ya jamii kwa wakulima wa mazao ya biashara ili kuongeza akiba nchini na kutoa fao la bei (*price stabilization*) pale bei zinapoporomoka chini ya gharama za uzalishaji ili mkulima ahimili *shocks*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwa *export levy* ya korosho ifutwe au mapato yake yawekwe kama akiba

itakayotumika kama *price stabilization fund*. Tunaweza kuangalia suala hilo kama laweza kufanywa kwa mazao mengine.

MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma Kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango aliyoiwasilisha Bungeni kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2019/2020 hakuna hata mstari mmoja ulioongelea kuhusu wazee wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ulipaji wa madai kwa ujumla Serikali illlipa jumla ya shilingi 2.2839 za madai yaliyohakikiwa yakiwemo ya wakandarasi waliota huduma, wazabuni, watumishi wa umma na madai mengineyo. Kwa akili yangu nilitegemea madai mengine ni ya wastaafu wa Afrika Mashariki lakini mpaka mwisho hicho kitu sikukiona. Kwa masikitiko makubwa sana katika zoezi la kuhakiki wanaoidai Serikali wastaafu hawa hawaonekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ilivunjwa mwaka 1977 lakini hadi leo Serikali haijahakiki, hiyo ni miaka 41. Ni lini zoezi hili litafanyika hatimaye wanufaika waweze kupata haki zao? Wastaafu hawa walilitumikia Taifa lao kwa uaminifu na uadilifu lakini Serikali hili haillitambui. Naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa dhamana aliyonayo wastaafu wa Afrika Mashariki walipwe fedha zao ni haki yao.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wa Waziri kwa Mapendekezo mazuri ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi na Bajeti ya mwaka 2019/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie na kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye maeneo yafuatayo:-

(i) Ukusanyaji wa mapato. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 34 ameainisha moja ya changamoto ya utekelezaji wa Mpango kuwa ni ugumu wa kukusanya kodi kutoka kwa wafanyabiashara. Jambo hili ni kweli, nami naona kuna tatizo kubwa katika mfumo wa *TRA* kukusanya kodi, kwani siyo wafanyabiashara wote wanaotoa VAT. Mfano ni hapa hapa Dodoma, yapo maeneo wanalipa VAT, wengine hawalipi; kwenye mahoteli na maduka makubwa. Kwa mtindo huu, bado changamoto itaendelea. Naomba Mheshimiwa Waziri kuititia *TRA* ahakikishe kuwa ulipaji wa kodi hausichagui biashara. Kuna umuhimu wa kukitazama chombo hiki katika utendaji wake.

Vilevile Mheshimiwa Waziri ahakikishe kodi inayotokana na wafanyabiasha katika sekta isiyo rasmi inapatikana ili wafanyabiasha hawa wanufaike na mazingira mazuri ya biashara. Hili ni jukumu la Serikali, vinginevyo tusitarajie kupata kodi kutoka eneo hili.

(ii) Miundombinu na bombo la mafuta. Katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Miaka 2019/2020, moja ya eneo la mradi wa kimkakati ni wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga nchini Tanzania. Mradi huu ni mkubwa, utaleta tija kubwa sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika kuona kuwa moja ya shughuli zitakazofanywa katika mradi huu mwaka 2019/2020 (ukurasa wa 36) ni uuandaji wa kampuni ya mradi pamoja na majadiliano kati ya kampuni na benki. Mimi nilitarajia ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kuanzia Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kitoto – Nchemba inajengwa kwa kwango cha lami. Barabara hii ni muhimu sana, tena sana kwani bomba la mafuta litapita katika eneo hili. Naamini kabisa umuhimu wa barabara hii ni mkubwa ukiacha shughuli za kiuchumi za kilimo katika eneo hili ambapo inaunganisha mikoa minne (Tanga, Manyara, Dodoma na Singida).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali katika mipango yake ihakikishe kuwa barabara hii inajengwa kwa

kiwango cha lami na hata katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/2018 ilikuwa ni mionganini wa barabara za kimkakati na ambayo ilikuwa katika Mpango wa Maendeleo. Nashangaa kwa nini kwa mpango ujao haikujumuishwa.

(iii) Miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Naipongeza Serikali kwamba itaendelea na kuboresha mazingira ya uwekezaji kupitia utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*PPP*). Nimeona kama ipo baadhi ya miradi itatekelezwa kupitia *PPP* kama vile ujenzi wa *Hostel* ya *CBE* na ujenzi wa vituo vya *VETA*, hili ni jambo zuri sana litaipunguzia mzigo Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naona kama bado Serikali imechukua miradi michache sana, kwani bado tuna maeneo mengi sana ambayo utaratibu wa *PPP* ungeweza kutumika, lakini naona kama Serikalii imeamua kuchukua miradi michache. Aidha, sheria au mazingira ya utekelezaji wa utaratibu huu wana wasiwasi nao, nashauri, kama kuna upungufu katika sheria tuliyopitisha hapa Bungeni irudishwe tuifanyie marekebisho. Naamini sehemu nyingi duniani, nchi zimepiga hatua kupitia *PPP*. Hili linaweza kutatua changamoto tulizonazo katika ujenzi wa barabara, vituo vya afya na kadhalika. Naomba sana Serikari yangu ione fursa kubwa ipo katika *PPP*.

(iv) Changamoto ya masoko na bei ndogo za mazao kwa wakulima. Hili ni jambo kubwa na nyeti sana. Jambo hili kwa kiasi kikubwa linadumaza sekta ya kilimo nchini. Ili kutatua changamoto hii, nashauri Serikali itoe ruzuku kwa wakulima wetu japokuwa kiasi kidogo. Vilevile ihakikishe wakulima wetu wanapatiwa fursa ya kulima kilimo cha kisasa kwa maana ya kutumia teknologia ya kisasa ya kulima eneo dogo kupata mazao mengi. Hili litawezekana kama wakulima wetu watapata fursa ya mikopo yenye riba ndogo na kwa kuipa mtaji wa kutosha Benki yetu ya Kilimo. Kwa kupitia njia hizi, changamoto ya bei ndogo kwa mazao ya wakulima wetu itapungua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2012), ni kujenga uchumi wa viwanda kwa minajili ya kuchochaea maendeleo na mageuzi ya uchumi na maendeleo katika kaya zao mbalimbali nchini. Hata hivyo, uchumi wa awamu hii ni hali mbaya zaidi ukilinganisha na awamu zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ni muhimu katika ulimwengu wa sasa, ila hakuna viwanda kama uchumi wetu unayumba hadi kufikia kushuka kwa biashara za Kimataifa kulikosababishwa na uingizaji wa bidhaa kutoka nje, upungufu wa wafanyakazi na vitendea kazi ndani ya Mamlaka ya Mapato, kupungua kwa masoko na bei ndogo za mazao kwa wakulima na kupungua kwa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washiriki wa maendeleo wakati wa utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uchumi wetu wa viwanda na viwanda viendelee, nashauri mambo yafuatayo:-

(i) Ni lazima tufanye utafiti wa hali ya juu, je, ni viwanda gani tunahitaji na maeneo yapi viwanda hivyo viwepo, kwa kujali afya na maendeleo ya wananchi wanayozunguka maeneo yao. Pia kufanya utafiti wa mazao na kilimo kinachofaa.

(ii) Serikali itilie mkazo na kuipa fedha za kutosha Wizara ya Kilimo ili tulime kilimo chenye ubora na kupata vitendea kazi vya kutosha ili sekta ya viwanda ikue. Bila kuimarisha kilimo chetu ili kiwe chenye tija na kuangalia soko shirkishi, hatuna viwanda. Angalau bajeti ya kilimo iwe 95% na siyo 2% tu ya sasa.

(iii) Tuwe na nishati mbadala ili kuwa na nishati yenye uhakika, hapo ndiyo sekta ya viwanda itakua.

(iv) Serikali isidharau mdau muhimu ambaye ni sekta binafsi, kwani huyu ni mdau muhimu sana katika Tanzania ya Viwanda. Tutake tusitake, sekta binafsi ni mdau mkubwa

kwa Serikali. Serikali na sekta binafsi zikishirikiana, uchumi wetu utakua vizuri sana. Sekta binafsi inasaidia sana uchumi wetu nadhani takribani 55% ya mapato ya Serikali yanatoka kwenye sekta hii. Hivyo ni muhimu Serikali kuiona sekta binafsi ni jicho la pili au ni ubavu wake wa pili. Bila sekta binafsi hali itazidi kuwa ngumu sana.

(v) Elimu pia ni muhimu katika Tanzania ya viwanda. Sekta hii pia ipewe kipaumbele, itatusaidia kufanya tafiti zetu na kupata wataalam wa kuendesha viwanda vyetu.

(vi) Suala la utawala bora pia ni chachu ya maendeleo katika Taifa lolote duniani. Demokrasia, amani na utulivu, Katiba, siasa safi, yatakuza uchumi wetu wa viwanda kwa ujumla.

(vii) Suala la maji pia ni muhimu. Nashauri miundombinu ya maji iboreshwe. Maji ni uhai na pia yatasaidia sana katika viwanda vyetu. Kila kitu kinahitaji maji, hivyo Serikali iweke bajeti ya kutosha katika sekta ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba ushauri wangu huu uzingatiwe, bila sekta binafsi na masuala yote niliyoeleza hapo juu, tutaota suala la viwanda nchini Tanzania na tutaendelea kilalamika siku zote. Tuwe na soko shirikishi ndiyo tutafikia mafanikio yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile suala la elimu na walimu lishughulikiwe. Hawa ndiyo watetezi wa vizazi vyetu na ndiyo wanaokuza Taifa letu liwe na nuru. Tusingekuwa na Madaktari, Maprofesa, Marais, Mawaziri na wengine wengi bila walimu, hivyo, wasikilizwe madai yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizingatia haya, nategemea tutafika na kutakuwa tukilitendea haki Taifa hili na tutaacha taswira nzuri kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mchango wangu.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya viwanda inachangia pato la Taifa letu na pia huleta ajira kwa Watanzania. Kuna baadhi ya viwanda ambavyo vimebinafsishwa na havifanyi kazi vizuri na vingine vimefungwa. Naishauri Serikali ivichukue viwanda hivyo na kuwapa wawekezaji ili viweze kuzalisha na kuleta tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vitumiavyo malighafi za misitu, vingi vimefungwa kutokana na uharibifu wa mazingira kwa kukata miti. Hivyo kuliko kivifungia, Serikali ifanye mpango maalum wa kutenga maeneo ya kupanda miti kwa wingi ili viwanda hivyo viweze kufanya kazi kwa kutumia malighafi kutoka nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vinavyotengeneza vinywaji baridi, mfano Sayona, Coca Cola, Azam na vinginevyo, hutumia *industrial sugar* (sukari ya viwandani) na sukari hii huagizwa nchi za nje na mara ilingiapo nchini Serikali hutoza 15% ya sukari ilioingia ili kuweza kulinda sukari hiyo itumike kwa viwanda tu kisha baada ya matumizi, Serikali huwarudishia fedha hizo. Naomba Serikali irudishe fedha hizo kwa wakati ili kuweza kuwasaidia wafanyabiashara hao kuweza kuagiza tena na kuzalisha bidhaa kwa wingi, maana ni muda mrefu wamedai fedha zao. Mfano, kuna baadhi wanaidai Serikali shilingi bilioni 7, 10 na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashauri Serikali itengeneze mazingira rafiki kwa wafanyabiashara ili waweze kulipa kodi kwa wakati na bila manung'unico. Pia Serikali iwave muda maalum (*grace period*) angalau miezi mitatu kwa wale wafanyabiashara wanaoanza kufanya biashara, kisha ndipo wakadirije kiasi cha kulipa na ikadirie mapato kulingana na biashara aifanyayo na siyo eneo afanyalo biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wa sekta isiyo rasmi warasimishwe ili waweze kulipa kodi kwa Serikali. Pia watengewe maeneo maalum na siyo kufanya biashara mbele ya maduka ya wafanyabiashara wenzao na kupelekea

kuzorota kwa biashara kwa wenyewe maduka ambayo huchangia mapato ya Taifa hili kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali ipunguze utitiri wa kodi kwa wafanyabishara na kufanya wengi kushindwa kulipa na hatimaye kufunga maduka au viwanda vyao. Kodi zote huenda Serikalini, hivyo ni vizuri kuzijumuisha ili kumrahisishia mfanyabishara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vituo vya afya ambavyo havijamaliziwa na wananchi walionyesha nia ya kujenga. Naishauri Serikali imalizie na kuweka vifaatiba vya kutosha pamoja na dawa na Wauguzi. Kwa zile Hospitali za Rufaa zote, Serikali ijenge maeneo maalum kwa ajili ya watu ambaao husindikiza wagonjwa wao na pengine hawana ndugu au jamaa katika maeneo karibu na hospitali ili waweze kukaa karibu na hospitali na kuwasaldia kwa karibu kwa huduma ambazo huweza kufanya na mtu wa karibu, mfano, chakula na kadhalika na kujua mwenendo wa mgonjwa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukusanya mapato ya Serikali (ya nchi) huduma ya kuhifadhi maiti katika hospital zetu kususan za Serikali iwe bure. Serikali ijaribu kutafuta chanzo kingine na siyo kulipisha maiti pindi ihifadhiwapo hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali madaraja yote nchini yawe ni chachu kwa maendeleo ya wananchi wote kwa ujumla na yatoe au yapitike kiurahisi bila mwananchi kulipia gharama zozote wakati wa kutumia madaraja hayo. Dajara la Nyerere (Kigamboni) lilijengwa na NSSF na mara baada ya kumaliza deni, wananchi wapite na vyombo vyao vya moto bure, kama liliyyo daraja la Mkapa Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iondoe utaratibu huo wa kuwatoza tozo wananchi wavukapo. Hii itasaidia kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi wa Wilaya ya Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji utekelezaji mwema wa shughuli zao za kila siku.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naleta nyongeza ya mchango wangu kwa yale niliyochangia kwa mdomo, kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwenye mafanikio ya sekta ya afya, Mpango uwe na kipaumbele cha kumalizia miundombinu viporo hasa kuondoa *shortage* kubwa ya madarasa na matundu ya vyoo katika shule za msingi, maabara kwenye sekondari na hosteli za wasichana.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashauri Wizara iendelee kuongeza jithada za kukaa na wafanyablashara, *let us say, top 20 tax payer, then category* ya 21-40, 41-60 na kadhalika na kujikita kwenye kupunguza *cost of doing business* wanazokumbana nazo kwa lengo la kuongeza mapato ya kodi, ajira na mchango wa pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna *so called "Blueprint", but to me it is just a document, operationalization* yake ndiyo muhimu. Mfano, mwaka 2013 - 2018 *top ten tax payers* wa viwanda vilivyobinafsishwa walilipa kodi shilingi triliuni 4.5 (*approx.*) na wakati viwanda 55 vilivyobinafsishwa *same period* walilipa kodi ya shilingi bilioni 121 (*approx.*) peke yake. Hapa kuna meseji kubwa ya kisera.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hitaji la kufanya tathmini ya viwanda nilivyotaja hapojuu na kufungamanisha na mazao yenye uhitaji ikiwepo malighafi. Ajira viwandani zinapotea, zinaenda *automation (robots)*, inabidi Wizara iratibu zoezi na mkakati wa kutengeneza ajira zinazopotea kwenye kilimo, mifugo, uvuvi na usindikaji (*value addition*) wa mazao. Hilo suala la *linkages* mkiliacha Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji tutaendelea kukwama. Viwanda tajwa vipo tayari kuipa *Government* ushirikiano.

(iv) Mheshimiwa Mwenyekiti, *PPP* na *DFIs* bado ni *pipeline* muhimu ya kugharamia *flagship projects*. Jitihada na mikakati zaidi bado inahitajika, otherwise kuendelea kutumia *TRA collection* kugharamia *long term developments (flagship project)* kutaendelea kudhoofisha *household and private sector spending*. Pia kuna athari kwenye *currency stability* kwani *capital equipment* asilimia kubwa inanunuliwa nje ya nchi. Kuna athari kukopa kwa gharama ya juu kwani *development banks* nchini hazipo na *TIB* haina mtaji wa kufadili miradi hiyo.

(v) Mheshimiwa Mwenyekiti, msiache mihemko ya viongozi wachache tena wasio wa Kitaifa kuharibu sura ya nchi mbele ya sura Kimataifa. Kuna namna mambo ya mila na desturi yanaweza kushughulikiwa kimya kimya bila kuathiri diplomasia kati ya Tanzania na dunia. Yanayoendelea mfano *LGBT* tayari *World Bank* wamesusia kuja Tanzania (*missions*). Mambo haya yanazidi kufanya *PPP* na *DFIs* ziwe njia zenye changamoto kupata *financing*.

(vi) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha *flagship projects* haziwi *white elephants* siku za usoni, ipo haja ya kuhakikisha bandari zetu zinajengwa kisasa sambamba na *SGR* na *offtake agreements* kati ya Tanzania na nchi za jirani zinasainiwa mapema ili kupata uhakika wa mizigo na kuongeza *customs revenues*.

Vilevile nguvu ya kuzalisha umeme (*generation equally*) iende kwenye kuweka kipaumbele cha fedha za *transmission* na *distribution O & M (Operation & maintenance)*. Bila hiyo, tutazalisha umeme mwingu lakini kuwe na *power losses* kwenye *transmission* na lengo la umeme kuleta mageuzi lishindwe kutimia. *TANESCO* inahitaji mkakati kwenye *O & M* na *alignment* makini kati ya *generation* na *distribution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa, ni lazima tuzingatie suala la miradi ya kimkakati

kwa kuzingatia hali halisi ya Taifa letu ili miradi hiyo iweze kuwasaidia wananchi katika maendeleo ya Taifa letu. Suala la kilimo lipewe kipumbele kwa kuangalia umuhimu wa kilimo katika mapinduzi ya viwanda ili kuimarisha uchumi kwa kufanya utafiti wa kutosha.

Nashauri vituo vya utafiti viboreshwe ili kuinua kilimo chetu na kiwe chenye tija kwa kupata mbegu nzuri na zenyebora na zitakazoleta tija kwa kuinua uchumi wananchi wetu na kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango, suala la masoko halijapewa kipaumbele na kuwekewa mkakati wa kudumu, soko la ndani na la nje kwa ajili ya kusaidia wakulima wa mazao mbalimbali nchini. Kuongeza Maafisa Ugani, ni jambo muhimu sana ili kuinua kilimo. Endapo Maafisa Ugani watakuwa wa kutosha wataweza kuwafikia wakulima na kuwapa ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, tutafanikiwa tu endapo wakulima watapewa vifaa vya kisasa ili kuongeza uzalishaji katika kilimo na kukuza uchumi wetu. Vilevile Bodi ya Mazao Mchanganyiko ipewe fedha za kutosha ili waweze kununua mazao ya wakulima ambao hawajui hatima ya kilimo wanachokifanya, kwani changamoto ni soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi kubwa ya vijana wanahitimu na kukosa ajira na kusalia mitaani. Suala hili ni baya kwa nchi yetu. Ni vyema kama Taifa tukawa na mkakati maalum kwa ajili ya ajira kulingana na uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi zisizo rafiki kwa wafanyabiashara. Nashauri kuwe na mkakati maalum kwa kufuatilia tozo zenyeku kero ambazo siyo rafiki kwa wafanyabiashara wetu ili kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali itengeneze mazingira wezeshi kwa wavuvi, wakulima na wafugaji na kuondoa kero wanazokutana nazo ili kukuza uchumi.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukuwa fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango juu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi na Bajeti ya Mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wake wote kwa kuandaa Mpango huu kwa umakini na kwa utaalam mkubwa. Katika kuchangia hotuba hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu kilimo. Napenda kuipongeza Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Magufuli kwa kutambua mchango wa kilimo katika kupunguza umaskini. Bado inahitajika juhudhi za makusudi katika kuendeleza na kuinua sekta hii hasa katika upatikanaji wa pembejeo na vitendea kazi wezeshi kwa kilimo. Bado upatikanaji wa zana za kilimo hasa matrepta siyo rafiki kwa wakulima hasa wale wa ngazi za chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, mabenki kama *TPB Bank* inatoa mikopo ya matrepta kwa masharti ambayo ni magumu kidogo. Sharti la utangulizi wa asilimia 25 ya thamani ya *tractorni* gumu sana kwa wakulima wa kawaida na hawawezi kumudu. Ushauri wangu katika suala hili ni kuiomba Serikali iwarelekeze *TPB Bank* waangalie uwezekano wa kupunguza sharti hili la *advance payment* ya asilimia 25 ili liweze kuwa rafiki kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni miradi ya maendeleo. Naipongeza Serikali yetu kwa kuendeleza miradi mingi ya maendeleo ambayo ni kichocheo kikubwa cha uchumi wa nchi yetu. Tukumbuke kwamba hii ni miradi endelevu na ya kudumu. Hivyo, Serikali inapopanga kupeleka miundombinu katika eneo husika ni lazima kufikiria ubora na uwezo wa miundombinu hiyo kwa sasa na kwa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kufua umeme katika Mto Rufiji ni mionganoni mwa miradi mikubwa sana ambayo inahitaji kuzingatia ubora wa miundombinu inayopelekwa huko. Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa 33 KV unaopelekwa katika mradi huu wa kufua umeme wa Mto Rufiji ni mdogo kulinganisha na ukubwa na hadhi ya mradi huu. Naiomba Serikali ifikirie kwanza msongo huu wa umeme badala ya 33 KV iwe 220 KV.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa nafasi ya kuchangia katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kwenda na kasi ya uchumi wa kati, suala la ujenzi wa viwanja vya ndege ni muhimu sana kwa kusaidia ongezeko la wadau wa utalii nchini ambao ndiyo wanaojitahidi kuongeza pato la Taifa kuitia sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Serikali ina mkakati mkubwa wa kukuza utalii Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ni vema kuwa na mpango wa kuendeleza viwanja vya ndege kwenye mikoa yetu inayoongoza kwa vivutio vyetu. Hii itasaidia sana kupanua wigo wa sekta ya utalii na ajira nchini. Gharama za usafiri wa anga ni kubwa sana kwa ndege za kukodi. Hii ni kutohana na ndege zetu za Serikali kushindwa kutua maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imejaliwa ardhi kubwa na yenye rutuba. Tatizo kubwa ninaloliona ni mpango wa matumizi bora ya ardhi ambayo inachukuwa muda mrefu na kuchelewesha maendeleo ya uwekezaji kwenye kilimo, ufugaji na makazi bora. Changamoto hii ni kubwa na hasa inapokuja kwenye suala la utekelezaji wa upimaji wa ardhi nchini. Upimaji wa ardhi ukiachwa kwenye *level* ya Wilaya, utaendelea kuchukua muda mrefu kwa kuwa bajeti zao ni

ndogo na hii inapelekea kutumia wapima binafsi ambao wanakuwa na gharama kubwa ambazo wengi wanashindwa kuzimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na upimaji wa ardhi katika maeneo mengi nchini. Mfano, Dodoma kama Makao Makuu, wananchi wanalipa fedha za upimaji na kiwanja. Tatizo ni uendelezaji wa maeneo hayo kwenye eneo la miundombinu, jambo ambalo linachelewesha ukuaji wa mijji yetu kwa haraka. Kama wananchi wamelipia gharama zote za uwekezaji ni kwa nini kazi hii inachukua muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufunganisha sekta ya kilimo na ujenzi wa viwanda; yako mazao ambayo yakinengewa fedha yanaweza kusaidia sana katika ukuaji wa viwanda. Mfano, kilimo cha mahindi kwa ajili ya kutengeneza *corn oil*. Mafuta ya *corn* ni mazuri kiafya lakini tumekuwa tunapoteza mazao mengi ya mahindi kama zao la biashara kwa sababu tumejhindwa kuhamasisha wadau kufungua viwanda vidogo vidogo vya *SIDO*. Naomba Waziri anapokuja atuambie ni kiasi gani Serikali imewezesha wananchi kufungua viwanda vidogo ili kusaidia ukuaji wa soko la mazao kama mahindi na alizeti, kwa ajili ya ukamuaji wa mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iweke mkakati wa kulinda viwanda vya ndani ambavyo vinazalisha bidhaa zinazopatikana nchini.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Rais wetu kwa kazi nzuri anayoifanya kwa maendeleo ya wananchi wa Taifa letu kwa uzalendo wa dhahiri usiopindika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapa hongera Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu Waziri. Hongereni sana kwa kazi iliyotukuka bila kuwasahau watumishi wa Wizara kwa jinsi wanavyomuunga mkono Mheshimiwa Rais na kumwezesha kutimiza malengo ya maendeleo ya barabara, umeme, maji, afya, elimu na kadhalika, kwa kuonyesha njia

na ufunuo wa mwanga mbele ya jamii. Hakika Mpango wa Mwaka 2018/2019 ni mwanzo na msingi bora kwa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2019/2020, kuupelekeea kuboresha utekelezaji na ukamilishaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ushauri kwa utekelezaji utakaokuwa wenyе tija, tuwe na mpango wa kuweka vifaa wezeshi kwa rasilimali watu kuifanya kazi yao vema na kuwainua wanawake kiuchumi. Kwa mfano, wanawake katika nchi yetu ni sawa na asilimia 52 na wenyе kuwajibika katika kila nyanja, lakini pia ipo Idara ya Ustawi wa Jamii na Idara ya Maendeleo ya Jamii ambazo zinawajibika kuwawezesha wanawake kiuchumi, kwa kuwahamasisha kujiunga na kuanzisha vikundi vya wanawake vya kiuchumi na kuwapa elimu ya ujasiriamali, kwa hiyo tuweke kwenye mpango jinsi ya kuwawezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 25, kipengele 3.3.3.4, Ustawi wa Jamii, katika nchi yetu rasilimali watu wa Idara hizi wanahitajika. Hivyo, uwepo mpango mkakati wa kupatikana kwao na wapewe vitendea kazi kama magari, pikipiki kuliko ilivyo sasa wanategemea huruma ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya vikundi 4,365 vyenye wanawake 39,449 ndani ya Halmashauri 130 kati ya 185 ni takwimu dhaifu. Hii inatokana na rasilimali watu isiyotosheleza kwenye vijiji na mitaa ambako wanawake wapo na hawana usafiri wa kuwawezesha kuwafikia hao wanawake. Ni vema Mheshimiwa Waziri kutoa maamuzi magumu ya kuweka mpango wa kuibua vifaa na rasilimali watu hao wakati wa bajeti mwakani ifanyiwe kazi ili tupate vikundi vya kutosha na kuimarisha *SACCO* Sztetu na kuanzisha zilizo imara. Vilevile idadi ya mitaa na vijiji inafahamika, iwe ndiyo lengo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango umezingatia kuboresha huduma za afya, elimu, kilimo na nishati (umeme). Hakika Serikali ndani ya uongozi imara wa Mheshimiwa Rais, kazi inaonekana kwa mafanikio. Baada ya zoezi la vyeti,

kustaafu na kufariki kumepelekea rasilimali watu kupungua na bado vijiji na mitaa hakuna watendaji. Hivyo, kuwepo na mpango wa kutoa vibali vya ajira mbadala kwenye Halmashauri zetu, kuwepo mpango wa kukamilisha majengo na miradi iliyopo, tuzingatie maamuzi yetu na tuyafuatilie kwani idadi zinafahamika. Tuunge mkono nguvu za wananchi wetu, tuisiwakatishe tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurejea tena kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri waifanyayo. Naomba ushauri wangu uweze kuchukuliwa wa kuimarisha Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Jamii waweze kufanya kazi yenye tija kwa maendeleo ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na kuutakia mafanikio mema huu Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2019/2020.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu haujaonesha jinsi utakavyowakwamua vijana wasio na ajira. Nashauri Mpango uelekeze zaidi namna utakavyowezesha vijana kujajiri au kuajiriwa na kwa kuwa tunategemea kodi (*PAYE*), hivyo vijana wakipata ajira kwanza watajikwamua katika maisha na pia watalipa kodi. Tusipowekeza kwao kwa miaka kadhaa ijayo tutazidi kuwa na mkwamo wa kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la elimu hasa *VETA*, ni kwa nini hatuna *decentralized VETA Training?* Kwa mfano, katika sekta ya kilimo, wataalam hadi wakasomee *SUA* na kule wanapata kuanzia ngazi ya Diploma na kuendelea, sasa tukiwa na *VETA* za Kilimo kulingana na mikoa yetu na jinsi mazao yanayostawi katika kila eneo, vijana wengi wa kike na kiume wangepata mafunzo ya ngazi hata za cheti kuweza kujifunza utaalam wa kilimo katika maeneo yao. Hivyo Serikali ijikite kutenga fedha katika Mpango huu kwa ajili ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu pia hauonyeshi shabaha ya kuwa na wataalam au kuongeza wataalam wa fani mbalimbali ili kuweza kuwekeza katika ukuzaji wa sekta binafsi. Hakuna bajeti ya *ku-facilitate animal husbandry* na kadhalika, ambazo ndizo zinaweza kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu pia una mambo mengi lakini jambo muhimu ni kuangalia vihatarishi vya *investors ambavyo* kama hatutakuwa *consistency*, yaani kuwa na maamuzi yasiyotabirika na mambo kubadililikabadilika (*unpredictable political situation*) tutakosa wawekezaji. Hilo ni jambo la kuzingatia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri pia suala la mbegu bora katika sekta ya kilimo litiliwe mkazo kwani sasa tuna mbegu nyingi toka nje ambazo wakati mwiningine Tanzania tumekuwa ni soko. Kwa nini tusifufue au kuendeleza vituo vyetu vya mbegu? Mfano, kulikuwa na Uyole, Ukiliguru, Ilionga na kuwekeza mikoa kama ya Iringa, Morogoro ili kuwa na mbegu nzuri toka hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea, tunaanza na wachangiaji wa upande wa Serikali. Niwape ushauri tu, mnachangia kwa kutoa mapendekezo na ushauri, maoni na ushauri na ninawapa dakika tano kila mmoja.

Tunaanza na Mheshimiwa Elias Kwandikwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Angeline Mabula.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2019/2020 na nianze kwa kuunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu Waziri kwa namna ambavyo wanafanya uratibu mzuri kwenye shughuli za Wizara. Nishukuru kwa mapendekezo mazuri, ukianza kuangalia kwenye hotuba na mambo ambayo wameyaonesha kwenye mapendekezo ya mpango wenyewe ukurasa wa 13, 27, 34 hadi ukurasa wa 35, utaona kuhusu miradi ambayo ni ya kipaumbele katika Wizara, wameionesha vizuri kabisa, sihitaji kuzungumza sana kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wana nakala za vitabu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri pia kwa kutuwezesha kama Wizara. Tunaendelea kwa kasi kutekeleza miradi mbalimbali, tumeendelea kupata fedha kwa mtiririko mzuri na hata ukiangalia kwenye taarifa hii Mheshimiwa Waziri wa Fedha anazungumza kwamba katika sekta ya ujenzi, kuanzia Juni, 2016 mpaka Juni, 2018 kumekuwa na ongezeko la barabara za lami za mikoa na zile zinazounganisha mikoa na nchi jirani kilometra 941, si haba. Tunaendelea kwa kasi kutekeleza ujenzi wa barabara kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kutekeleza sera ya ujenzi, kwa sababu tunawezeshwa na Wizara, kuhakikisha kwamba maeneo ambayo ni korofi yanapitika na pia kuunganisha mikoa na mikoa na mikoa ya nchi za jirani. Niishukuru sana pia Wizara kwa kutuwezesha kulipa madeni ya wakandarasi kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye mpango utaona asilimia 71 ya madeni yote, kati ya shilingi triliuni 2.288, shilingi triliuni 1.611 zime-clear madeni ambayo yalikuwepo kwa wakandarasi mbalimbali, lakini sehemu kubwa ikiwa ni wakandarasi wa upande wa ujenzi wa barabara. Hii kwetu sisi kama Wizara ni fursa, kwa maana ya kwamba sasa tunaweza kuendelea kutangaza ujenzi wa barabara mbalimbali kwa sababu tumetoa mzigo mkubwa kwenye madeni ambayo yalikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wametoa mapendekezo. Kwa sababu haya ni mapendekezo ya mpango wa maendeleo niseme tu kwa ujumla wake kwamba tumeyachukua mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge. Kwamba tutakavyokwenda kwenye hatua nyingine, na tukienda sambamba na mpango wa utengenezaji wa bajeti ambao upo kwenye kabrasha tutazingatia michango ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu jambo moja kwenye upande wa uboreshaji wa madaraja, Mheshimiwa Obama alizungumza juu ya kutengeneza madaraja ambayo yanatuunganisha sisi na nchi za jirani. Niseme tu kwamba tumekuwa tukifanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo. Yapo maeneo ambayo kuna madaraja tutaendelea kufanya ujenzi, iko katika hatua nzuri, tunaunganisha upande wa Tanzania na Uganda kule Mulongo, Daraja la Mulongo. Vilevile kwa upande wa Ruvuma tunaendelea na harakati za ujenzi kule Mkenda, kwa barabara kutoka Likulufusi kwenda Mkenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande ule wa kuunganika na wenzetu wa Msumbiji tuna daraja zuri kubwa kabisa lenye mita 720, hili ni daraja la pili kwa ukubwa kwa Tanzania, sasa tumeshaungana na wenzetu wa Msumbiji. Kwa hiyo, niseme tu kwa upande wa Wizara tunaendelea kuhakikisha kwamba tukipata *ceiling* tutatenga ili tuweze kuendelea kufanya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengine tunaunganisha na nchi za jirani kwa kuimarisha maeneo ya vivuko, ukiangalia tunaendelea kuwa na... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kwandikwa. Tunaendelea, Mheshimiwa...

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Angeline Mabula, Mheshimiwa Mgumba na Mheshimiwa Aweso wajiandae.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa kupata fursa hii kwa ajili ya kuchangia hoja hii ya Mpango wa Maendeleo wa Bajeti. Pia nianze kwa kuunga mkono hoja nikiwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri. Nimpongeze sana Jemedari wetu, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna anavyoiongoza nchi hii, namna anavyotoa maelekezo na namna ambavyo sasa tunajikita katika kuhakikisha kwamba uchumi wa kati nchi yetu itaufikia kuititia Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ni Wizara wezeshi katika kuhakikisha kwamba mipango inayopangwa inatekelezeka kama ambavyo Mheshimiwa Dkt. Mpango ameweka katika ukurasa wa 46. Kwa hiyo, Wizara ya Ardhi ni Wizara wezeshi ya kuweza kuweka mazingira mazuri ili kuweza kuona mipango inakwenda namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika kuijandaa na hilo, nikijibu pia baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Lucy Mayenga alitaka kujua tu kwamba Serikali imejipangaje katika kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira wezeshi ambapo wawekezaji wanapokuja wakute tayari tuna akiba ya ardhi ambayo inaweza kutumika katika uwekezaji. Wizara ilishatoa maelekezo katika Halmashauri zetu zote kuhakikisha wanatenga maeneo ya uwekezaji na hasa pale ambapo Mheshimiwa Rais anakuwa amebatilisha umiliki wa baadhi ya maeneo na kuyawekea katika mipango mingine. Kila linalofutwa lazima liwe na eneo lililotengwa kwa ajili ya uvezeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi katika eneo la Kigamboni na Kibaha tunazo hekta 2,393, pia tuna

viwanja kwa ajili ya viwanda 240 viko vinasubiri. Kama hiyo haitoshi, kwenye Mpango wa mwaka 2019/2020 kuna maeneo zaidi ya 196 yametengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Mashamba 42 yaliyofutwa yenye hekta zaidi ya 183,000 nayo pia yana mwelekeo huo huo wa kuweka uwekezaji. Kwa hiyo katika hili kila kitu kinapangwa kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ushauri ninaoweza kuutoa, kama ulivyosema tushauri, kwa sababu mpango huu pia unakwenda sambamba na mipango iliyopo katika maeneo. Tunayo mipango kabambe ambayo imeandalishi na halmashauri zetu; na katika hiyo mipango yote kuna maeneo kumi ambapo wametenga kwa ajili ya uwekezaji, yenye ekari 127,442. Kwa hiyo, hayo yote ni maandalizi ya kutaka kuweka kitu kiweze kukaa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, kwa sababu pia kasi ya upimaji ni ndogo, Wizara imenunua vifaa vyatukosha kuweza kusaidia katika kuongeza kasi ya upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niwashauri Halmashauri zote ambao wana mwelekeo na wametenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji, kwa ajili ya viwanda na mambo mengine basi wavitumie vifaa hivyo kutoka katika Kanda na vinatolea bure hakuna gharama yoyote inayokuwa-charged, ni kiasi cha wewe kwenye kanda ukapata na kazi ikafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nizungumzie suala dogo ambalo sisi kama Watanzania hatulioni, na hasa upande wa pili ambao mara nyingi kila kitu wanakibeza. Wenzetu wa nje na hasa Mabalozi wanazungumza mambo ambayo yote ni chanya kwa Tanzania hii . Niomba nim-quote tu Balozi mmoja wa Palestina ambaye amezungumzia habari ya Tanzania na uzuri wake. Anasema; "*Tanzania lives true democracy transparence.*" Halafu anasema, "*It is too unique, never found in third world countries,*" lakini sisi hatulioni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lazima mtu anapoongea kitu hicho anaona ni nini ambacho kinaendelea. Ni kweli kuna uwazi na demokrasia iliyopo, kweli inaonekana. Haya yote yanapofanyika tunachotakiwa kama Watanzania, kwa sababu tayari tunao uongozi unaoangalia mwelekeo, na tukiangaa hata haya ambayo ameyachulia maamuzi Mheshimiwa Rais, suala la korosho, kwani watu hawakuwepo? Walikuwa hawaoni? Wanaona lakini bado wanabeza na huko huko wanalilia kwamba wakulima waweze kupata fursa za kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niseme tu kama Watanzania tunachohitajika kufanya sasa hivi ni kuunga mkono juhudhi zote za Mheshimiwa Rais, kuunga mkono mpango ambao umewekwa vizuri, tunachotakiwa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, haya, Mheshimiwa Omary Mgumba, Mheshimiwa Aweso na Mheshimiwa Dkt. Ndumbero wajiandae.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Kwanza na mimi nichukue nafasi hii kuunga mkono mapendekezo ya mpango ulioletwa mbele yetu na Dkt. Mpango. Pili niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu mzima ya wataalamu kwa kuleta mapendekezo ya mpango ambao unakidhi haja hasa kwenye sekta ya kilimo. Tatu, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kwenye sekta ndogo hii ya kilimo, namshukuru sana na nitaendelea kumuwalilisha vyema katika sekta hii. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wenzangu walivyotangulia, haya ni mapendekezo ya mpango, huu si mpango wala si bajeti. Kwa hiyo, kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia kwa maneno, lakini pia kwa maandishi

hasa katika mambo yanayogusa sekta ya kilimo. Niwaahidi hayo yatakuwa ni chachu na tumeyachukua yote tutaendelea kuyafanya kazi, ambapo tutayaboresha. Kwenye mpango wenyewe utaokuja nafikiri mawazo yao yatakuwa yako ndani ya mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, zimetokea hoja hapa kwamba kuna miradi ambayo ipo humu ndani ambayo ina faida kubwa katika taifa. Kwa mfano kuna mradi wa *Stiegler's Gorge* ambao uko kwenye mpango wa kuzalisha umeme, lakini pamoja na kuzalisha umeme utakuwa na faida kubwa sana kwenye sekta ya kilimo kwa sababu baada ya maji yale kutumika kuzalisha umeme, hatutayaacha yaende bure baharini, kuna hekta zaidi ya 150,000 kwenye Bonde la Rufiji ambazo tutaziedeleza kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo mradi huu utajibu hoja za Watanzania kwenye kuimarisha kilimo cha umwagiliaji na tutakuwa na hekta zaidi ya 150, 000 kwenye Bonde la Mto Rufiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia watu wanabeza miradi mikubwa iliyohumu kama *Standard Gauge*, hii ni miradi ambayo imechelewa sana ilikuwa kwamba tuitekeleze jana, kwa sababu miradi hii itarahisisha na kupunguza gharama za usafirishaji wa mazao ya kilimo. Kwa hiyo, leo gharama za uzalishaji wa mazao ya wakulima zikipungua maana yake kipato kikubwa cha wakulima kitaboreka, lakini tatu kuna miradi kama ya *Flyover*, watu wanaibeza, lakini sisi watu wa kilimo tuona ni suluhisho kubwa sana. Leo hii tukifika na mazao yetu pale Dar es Salaam tunachukua zaidi ya masaa matatu au manne, tena wakati mwininge tunawekwa Mbezi mpaka sasa tatu ndipo tuanze kuingia mjini wakati ndizi zinaoza. Kwa hiyo, kwa kutengua kile kitendawi cha *traffic jam* Dar es Salam maana yake wakulima watakuwa na uwezo wa kufikisha mazao yao kwa wakati na kufanya biashara zao, wataokoa muda na watarudi tena kwenda kuzalisha zaidi huko. (*Makofii*)

Kwa hiyo miradi hii si migeni, miradi hii ni muendelezo wa Serikali zilizopita za Chama cha Mapinduzi. Kuna watu walisema kwamba miradi hii ni migeni, Rais huyu amekuja

anaanza na vitu vyake, si kweli. Tumehamia Dodoma ni ahadi ya Serikali ya Awamu ya Kwanza, anajenga *Stigler's* ni ahadi ya Serikali ya Awamu ya Kwanza, lakini pia na miradi hiyo mingine kwa mfano hata ujenzi wa reli ilikuwa na katika SDP / ambayo ilikuwa inatekelezwa na Serikali ya Awamu ya Nne na ndiyo maana unaona kwamba Serikali ile ya Chama cha Mapinduzi Awamu ya Nne ndiyo Serikali ilijenga miundombinu ya mtandao mrefu wa lami kuliko Serikali zote. Kwa hiyo, tunapokuja kujenga sasa hivi *Standard Gauge* ni mwendelezo tu wa Serikali zilizopita na si kwamba ni jambo jipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye suala la sekta binafsi sisi kama Wizara ya Kilimo kwa niaba ya Serikali tumeshakaa nao vya kutosha na kuna kampuni zaidi ya sita zimekubali na zitaendelea kuwekeza hasa kwenye kilimo cha korosho, yaani kwenye ubanguaji wa korosho. Zaidi ya tani 60,000 zitapanguliwa kuanzia mwaka huu mpaka mwakani. Kampuni hizo ziko tayari na tutaziweka. Mjadala mkubwa ulikuwa kuhusu suala la korosho, suala la korosho mwongozo wa Serikali umeshatolewa na kweli tutanunua na kununua hii hatufanyi biashara kichaa, tunafanya biashara...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa kwa mchango wako na ushauri. Mheshimiwa Aweso, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro na Mheshimiwa Ulega ajiandae.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru, lakini nitumie nafasi hii kwanza kuunga mkono hoja asilimia mia moja kwa mpango huu uliopendekezwa, lakini kubwa nitumie nafsi sana sana kumpongeza Mheshimiwa Mpango pamoja na Naibu Waziri, nataka niseme tu itoshe kwamba huu mpango umekamilika na hakuna jambo lisilokwa na changamoto, kubwa nataka nikutie moyo, bahari kubwa ndiyo ivukwayo, chapa kazi sisi tupo nyuma yako tunakupa ushirikiano wa dhati kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuwashukuru sana Wahehimiwa Wabunge kwa michango yao. Nimeifuatilia kwa ukaribu sana Waheshimiwa Wabunge watano wakichangia zaidi ya watatu wamekuwa wakuzungumzia maji, maji. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo kwa Watanzania kupata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mpango, kwa maana Wizara kwa kutupatia fedha katika kuhakikisha tunawalipa wakandarasi ili wasikwame katika suala zima la utekelezaji. Nataka niwahakikishie wakandarasi ambao wanatekeleza miradi, watekeleze miradi kwa kiwango, wasitekeleze miradi kijuanja ujanja, kandarasi yejote ambaye atatekeleza mradi kwa kiwango bora sisi kama Wizara ya Maji tutamlipa fedha kwa wakati ili mradi wake usikwame na yeye apate fedha za kutekeleza wa miradi ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Mheshimiwa Rasi Dkt. John Pombe Magufuli ni kuhakikisha anamtua mwanamama ndoo kichwani. Ujisoma ilani ya Chama cha Mapinduzi inatutaka itakapofika mwaka 2020 tuwe na asilimia 85 ya upatikanaji wa maji vijijini, na mjini aslimia 95. Jithada kubwa sana zinafanywa na Serikali katika kuhakikisha inatekeleza miradi mikubwa sana ya maji. Ukienda Arusha zaidi ya bilioni 520 zinatumika katika utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Igunga, Nzega Tabora kuna mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka katika mji ule. Pia yapo maeneo mengine mbalimbali kama vile Orkasmet, Lindi pamoja na Kigoma, yote hayo tunahakikisha tunatekeleza miradi, zaidi ya wananchi 2000 watanufaika na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna mradi mkubwa sana wa Same Mwanga ambao utapeleka maji hadi Korogwe kwa mama yangu Chatanda. Nataka niwaambie

wananchi wa Korogwe pamoja na Same Mwanga mradi ule tutausimamia na tutahakikisha unakamilika kwa wakati na wananchi waendelee kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna miradi takribani 1,595 ambayo imekamilika vijijini. Pia tuna miradi 492 ambayo ipo katika hatua mbalimbali. Sisi kama Wizara ya Maji tutahakikisha miradi ile inakamilika kwa wakati ili azma ya Mheshimiwa Rais iweze kutimilika. Wizara ya Maji tunatambua kwamba nchi yetu sasa hivi ipo katika nchi ya viwanda, kwa maana katika suala zima la uchumi wa kati. Kwa hiyo, uhitaji wa maji ni mkubwa sana, lakini maji hayana mbadala na katika kuhakikisha tatizo la maji linakuwa historia Serikali kwa kusaini imeingia mkataba sasa na Serikali ya India dola zaidi ya milioni 500 ambazo zitatekeleza miradi katika zaidi ya miji 26 ili kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge ambao miradi hii katika miji 26 itatekelezwa ndani ya wiki hii tutakaa kuwaeleza namna gani tunavyokwenda na sasa hivi tuko katika hatua ya manunuzi. Mradi huu utakuwa katika awamu mbili, kwanza usanifu na pili ujenzi utaanza ndani ya mwaka 2019/2020. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tunaomba ushirikiano wenu wa dhati katika kuhakikisha tunatekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika kuhakikisha miradi vijijini inakuwa endelevu Serikali sasa hivi imeshasaini mkataba na Benki ya Dunia na zaidi ya dola milioni 350 tutakazozipata ni kwa ajili ya kuhakikisha miradi ya vijijini inakuwa endelevu. Sasa sisi kama Wizara ya Maji, kwa maana ya Serikali, *accountimeshafunguliwa* na sasa hivi tupo katika uandaaji wa mwongozo wa utekelezaji wa miradi hii. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, sisi ni Wizara ya Maji si wizara ya ukame, tutahakikisha tunafanya kazi usiku na mchana ili kuwesheza wananchi wa Tanzania wapate maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza, nakushukuru. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro atafuatiwa na Mheshimiwa Ulega.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO

WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa kuniamini na kunichagua kuweza kumsaidia Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Dkt. Mpango. Katika kutekeleza mpango huu, Tanzania ina mahusiano mazuri kabisa na nchi zote duniani. Mahusiano hayo ni muhimu sana kama sehemu ya utekelezaji wa mpango huu. Ukiangalia nchi mbalimbali, Jumuiya za Kimataifa, Jumuiya za Kikanda mahusiano yetu ni mazuri kiuchumi, kisasa, kijamii, kusalama na pia kidiplomasia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na ukweli kwamba Balozi zetu zilizoko nje zinafanya kazi nzuri kuhakikisha kwamba tunaimarisha uhusiano huo. Uhusiano mzuri pia katika Jumuiya za Kikanda, Jumuiya kama Afrika Mashariki, SADC pamoja na AU ambapo sisi Tanzania sio tu wananchama wa kawaida pia ni wanachama wa wawakilishi wanachama waanzilishi. Kwa hiyo, kutoptera na uhusiano huo mzuri ambao tunao, tunaujenga na tunaendelea kuujenga tutahakikisha kwamba unatumika vizuri ili kukuza uchumi na kuvutia wawekezaji na ili mpango huu ambao uko mezani uweze kutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi zetu huku nje zinafanya kazi nzuri sana, zinafanya kazi nzuri katika kukuza diplomasia ya kiuchumi, zinafanya kazi nzuri katika kuvutia wawekezaji, zinafanya kazi nzuri katika kutangaza vivutio vya utalii ambavyo viko hapa Tanzania. Kwa sababu hiyo utaona kumekuwa na ongezeko la idadi ya watalii ambao wanakuja hapa Tanzania. Kazi moja ya Wizara hii ni kuhakikisha kwamba tunakuwa chachu ya maendeleo na utekezaji unaofanywa na Wizara mbalimbali kama ambavyo

imeainishwa katika mpango huu, ndiyo maana tumeweza kupata misaada, tumeweza kupata mikopo yenyé masharti nafuu, lakini pia kuuza bidhaa za mazao mbalimbali Tanzania nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha hilo linafanikiwa bado kuna changamoto, ningependa kuchukua nafasi hii kuomba Watanzania tushirikiane katika kutatua hizi changamoto. Changamoto ya kwanza ni miundombinu hafifu. Ili uwekezaji uweze kukua tunahitaji tuwe na miundombinu mizuri kama vile ujenzi wa barabara na reli. Hivyo tunavyojenga reli ya *standard gauge* wote tuunge mkono ili tuweze kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuwe na uwekezaji wa viwanda tunahitaji umeme wa kutosha na wa bei nafuu, na katika hilo ujenzi *Stigler's Gorge* lazima upewe kipaumbele. Mpango huu umeelezea vizuri kabisa suala hilo, kwa hiyo, tuunge mkono tujenge *Stigler's Gorge*, tupate umeme wa bei nafuu tuweze kuwa na viwanda. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji inabidi wawe na mazingira rafiki. Mazingira rafiki kwa mwekezaji ni kuondoa urasimu, kuondoa rushwa na kuondoa ufisadi. Vita katika kuondoa urasimu, rushwa na ufisadi ni ya kwetu wote, vita hii ni ngumu tushirikiane tupambane ili tuondoe hivyo vitu na tuweze kuleta...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ulega atafuatiwa na Profesa Ndalichako na Mheshimiwa Ummy Mwalimu ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nichukue fursa hii kukushuru sana kwa fursa uliyonipa ya kuchangia, lakini pili, naomba niunge mkono hoja hii ya Mheshimiwa Dkt. Mpango ya

Mapendekozo ya Mpango wa Maendeleo na tatu, naomba nichukue fursa hii adhimu kabisa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa uamuzi wake wa kishujaa alioufanya kwa manufaa mapana ya wakulima wa korosho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa Mbunge ninayewakilisha wakulima wa korosho wa Wilaya ya Mkuranga ninatoa pongezi hizi za dhati kabisa; na hivi sasa ninavyozungumza sisi wakulima wa korosho tunayo matumaini makubwa na furaha kubwa sana. Tunamwombea kila la kheri Mhehsimiwa Rais wetu, tunamwombea afya njema na tunamuombea kwa ujasiri wa namna hii aendelee kuliongoza taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruksa yako uniruhusu ninukuu maneno matakatifu ya *Quran*. Katika *Quran* Mwenyezi Mungu katika *Surat Tawba* ya sura ya tisa aya ya 105 anatoa ahadi ya kuwataka wanadamu wafanye kazi, na wanapofanya kazi yeye Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wanadamu waumini wataona. Akaendelea kutoa ahadi ya kutomdhulumu mja yeyote atakayefanya jambo lililo jema katika *Surat An Nisa*, sura ya nne aya ya 40 pale aliposema kwamba tufanye yaliyo mema na hatamdhulumu yeyote atakayeyafanya hayo mema na baadaye atamlipa malipo yaliyo makubwa sana. Basi *In Shaa Allah* Mwenyezi Mungu amlipe malipo yalikuwa makubwa sana Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Dkt. Mpango, yeye na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii. Naomba pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge mbalimbali waliotoa hoja katika Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi. Tumepata hoja nyngi sana, na uzingatiaji katika hoja hizi ni kuwa Wizara yetu ni Wizara wezeshi, Wizara yenye uwezo wa kuinua kipato cha Mtanzania, Wizara yenye uwezo wakuinua pato la taifa letu, kuleta ajira na kuongeza tija katika afya za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue fursa hii kuipongeza Kamati yetu kwa sababu pia imetoa maelekezo mazuri sana ambayo sisi kama Wizara tumeanza kuendelea kuyafanya kazi. Yako mambo mengi yalizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na sekta ya mifugo yaliyozungumza ikiwemo kuhakikisha tunatatua migogoro kati ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Vilevile yako mambo yalizungumza katika sekta hii ya mifugo ya kuhakikisha tunachakata mifugo yetu. Naomba niwape taarifa njema Waheshimiwa Wabunge ya kwamba katika mkakati wetu wa kuhakikisha tunachakata nyama katika taifa letu tumeanza kurudisha viwanda vyetu. Tumerudisha kiwanda cha pale Shinyanga, tumerudisha kiwanda cha pale Mbeya. Vilevile tumejielekeza katika kuanzisha dawati la sekta binafsi, ambalo litawasaidia wawekezaji wazawa kutatua kitanzi kile cha kupata mitaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwape ahadi Waheshimiwa Wabunge ya kwamba kuititia dawati hilo, tunayohakikika kabisa ya kwamba sekta ya mifugo itafanya vizuri na itaongeza kutoka asilimia saba ya mchango wake katika pato la Taifa hata ifike asilimia kumi tutakapoingia mwaka 2020. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunao mkakati mzuri sana wa kuboresha kosafu zetu za ng'ombe na mifugo yetu mingine kwa kufanya utaratibu wa kuboresha mifugo hii kuititia teknolojia ya AI na *embryo transfer*. Tunao mkakati pia vilevile wa kudhibiti magonjwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Profesa Ndalichako, Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Mheshimiwa Angella Kairuki wajiandae.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii

ya kuchangia mpango huu, na ninaomba nianze kwa kusema ninaunga mkono hoja iliyoko mbele yetu ya mapendekezo ya mpango na mwongozo wa bajeti kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kazi nzuri ambayo ameifanya pamoja na watendaji wote na kutuletea mapendekezo haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyachangia. Niwashukuru wote ambao wameelekeza michango yao pia katika sekta ya elimu, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba nilikuwa nawasikiliza kwa makini na nilikuwa naandika yote ambayo walikuwa wanazungumza. Kwa hiyo, kama Wizara niwahakikishie kwamba michango yao yote tutaizingatia tunapokuwa tunapanga mpango wa bajeti wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wamezungumzia mpango huu upande wa sekta ya elimu wamejikita zaidi katika kutoa msisitizo wa kutoa mafunzo ya ufundu stadi na wameonyesha jinsi gani masuala ya ujuzi na masuala ya ufundu stadi ni muhimu katika kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie kwamba kama nilivyosema tutazingatia mapendekezo yao na Serikali inaendelea katika kuimarisha utoaji wa mafunzo ya ufundu stadi kwa kujenga vyuo vya mikoa. Sasa hivi tunajenga katika Mikoa ya Simiyu, Geita, Rukwa na Kagera na pia tunaendelea kujenga katika vyuo vingine vya Wilaya, kwa sababu ya muda sitaweza kuvitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shule za ufundu saba ambazo ziliikuwa zinatoa mafunzo ya ufundu. Tumezifanya ukarabati na wazo lile la kusema kwamba tuwe na vijana ambao wanapata mafunzo ya ufundu mchundo kupitia vyuo hivyo tutalizingatia katika mipango yetu ili tuone ni namna

gani na kwa muda mfupi tunaweza tukafanya kama walivyopendekeza Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa ni suala la ubora wa elimu. Kuna baadhi ya Wabunge ambao wamezungumzia kwamba wanafunzi ambao wanapelekwa katika shule za sekondari haizingatiwi idadi ya nafasi zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema tumepokea mapendeleko ya Wabunge, lakini katika hili naomba niseme kwamba sasa hivi maafisa elimu wanaendelea na uchaguzi wa wanafunzi kwenda kidato cha kwanza. Naomba niweke msisitizo, kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge, huo ndio utaratibu wa Serikali kwamba wanaochaguliwa kwenda kidato cha kwanza lazima tuzingatia nafasi zilizopo na si kuwapeleka wanafunzi wanakwenda kurundikwa bila kuzingatia nafasi zilizopo. Tufautishe ufaulu na kuchanguliwa kwenda katika kidato cha kwanza. Kwa hiyo, kunakuwa na *pass mark* lakini kunakuwa na *cut off point*, ilea lama ambayo unamchukua mtu wa mwisho kulingana na ufaulu na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, Wizara tutakuwa wakali na Maafisa Elimu wote ambao hawatazingatia hilo tutawawajibisha kwa sababu tumeshachoka kuwa tunawaambia wafuate maelekezo. Miongozo iko wazi na inapaswa kuzingatiwa na shule zote, ziwe ni shule za Serikali au shule binafsi lazima tufuate mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametuonesha katika ukurasa wa 33, Serikali inatoa shilingi bilioni 20.9 kila mwezi kwa ajili ya kugharamia elimu na sisi kazi yetu ni kuhakikisha kwamba tunatoa elimu bure lakini elimu yenye ubora. Kwa hiyo hatutaruhusu mtu yoyote kutuvurugia kwa kutofuata utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa ni suala la ushauri kwa Tume ya Vyuo Vikuu,

kwamba vyuo vinapofungwa wahakikishe kwamba wale wanafunzi wanaohamishwa kozi zao zinazingatiwa. Tumepokea ushauri lakini nitoe tu ufanuzi, *actually* kinachotakiwa chuo kinapositishiwa kuchukua wanafunzi au kinapoamriwa kuhamisha wanafunzi wake kinapokuwa kimefungwa kinapaswa chenyewe kuhakikisha kwamba kinafanya uhamishaji wa wanafunzi na kwa kuzingatia kozi zilizopo. Kwa hiyo, tunalipokea, na kama kuna vyuo ambavyo vinahamisha wanafunzi na kuwalazimisha wachukue *course* ambazo si matakwa ya wanafunzi huo siyo utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Profesa. Mheshimiwa Ummy Mwalimu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Dkt. Mpango na Naibu Waziri Dkt. Ashatu Kijaji kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanafanya katika kusimamia sekta hii ya fedha na mipango, lakini hasa kwa kutuletea Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa sababu moja kubwa, ukiangalia mapendekezo ya mpango ambayo ameyaleta Mheshimiwa Mpango na timu yake yanataka kufunganisha ukua ji wa kiuchumi pamoja na maendeleo ya watu. Kwa hiyo, kwa sisi ambao tunasimamia sekta ya afya tumeridhishwa sana na mapendekezo ambayo yameletwa katika kuboresha huduma za afya ya msingi kwa afya ya msingi kuanzia zahanati, vituo vya afya pamoja na hospitali za wilaya. Pia tunafurahi kuona kwamba mapendekezo ya mpango ambayo yameletwa yanataka pia kuhakikisha tunaboresha huduma za matibabu ya kibingwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Dkt. Mpango lakini hasa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe

Magufuli, alisema Tanzania itakuwa *donor country*. Tanzania sasa hivi tumekuwa *donor country* katika sekta ya afya. Tunafanya upandikizaji wa figo ndani ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, tunaokoa fedha kutoka shilingi milioni 100 kupandikiza mgonjwa figo India sasa hivi tunatumia shilingi milioni 30. Tunafanya upandikizaji wa vifaa vya kuwasaidia watoto kusikia, tunafanya India kwa milioni 80 sasa hivi inafanywa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Watanzania mapendekezo yaliyoletwa hapa yana nia njema na nzuri katika kuhakikisha kwamba ukuaji wa uchumi ambao tunataka kuujenga ikiwemo kuujenga viwanda yanakwenda sambamba na kuwa na rasillimali watu yenye afya njema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba sasa nichangie katika maeneo matatu ambayo yameletwa na Waheshimiwa Wabunge katika mjadala.

Eneo la kwanza ni kuhusu kuhakikisha kwamba kazi kubwa na nzuri ambayo Serikali inafanya lazima tuwe na watumishi wa kutosha. Tumepokea ushauri na mimi nataka kusema katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetoe ajira za watumishi wa sekta ya afya 8,000 na watumishi 1,500 wameajiriwa katika hospitali za Wizara ya Afya, watumishi 6,180 tumewapeleka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya vituo vya afya, zahanati na hospitali ya wilaya na nafasi 200 tumepeleka Hospitali ya Mloganzila na watumishi 120 tumewapeleka katika Hospitali ya Benjamin Mkapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumepokea ushauri, tutawasiliana na wenzenzu wa utumishi ili kuhakikisha tunaongeza watumishi wa afya katika vituo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe pia wamezungumzia suala la kuongeza bajeti ya vifaatiba, ndugu zangu, sasa hivi tunapata fedha za dawa, vifaa na vifaatiba shilingi bilioni 270 kutoka shilingi bilioni 30; na nataka

kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba katika zile shilingi bilioni 270, shilingi bilioni tisa zitatumika kwa ajili ya kununua vifaatiba tu. Tunanunua *x-ray machine* zaidi ya 100 na kuzisambaza katika hospitali za wilaya zote nchini, hospitali za rufaa za mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile lakini tunanunua *ultra sound machine* kwa ajili ya vituo vyya afya vyote vinavyoboresha, meza ya kufanyia upasuaji (*operating table*) pamoja na mashine ya usingizi. Nataka kukubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba majengo yamekamilika vifaa vimechelewa. Tumefanya maamuzi kama Serikali hatutaki kununua vifaa tiba kutoka kwa wafanyabiashara, watu wa kati, tunanunua kutoka kwa wazalishaji. Nataka kutoa mfanano mmoja Waheshimiwa Wabunge; mashine ya usingizi ndani ya watanzania kwa wafanyabiashara inauzwa shilingi milioni 75, tumeipoata kwa shilingi milioni 48 tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mambo ndiyo hayo. Waziri wa Madini, Mheshimiwa Angellah Kairuki.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi naomba kuchangia hoja hii ya mapendekezo ya mpango na kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wake na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa namna ambavyo wameandaa mapendekezo haya ambayo ni mazuri ambayo kwa sisi kwa upande wa sekta ya madini naamini yataweza kutuimarishia kwa kiasi kikubwa kukusanya mapato, lakini pia kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani wa madini pamoja na kuendelea na shughuli mbalimbali ikiwemo uwekezaji katika miradi ya kimkakati katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia kuwapongeza Wizara ya Fedha kwa namna ambavyo wamesimamia kuhakikisha kwamba uchumi wetu wa Taifa unaendelea

kuimarka mpaka tumefikia takribani asilimia 7.1 katika ukuaji wa uchumi na ninaamini kwa usimamizi wao thabiti tutaweza kufikia ukuaji wa uchumi wa Taifa wa asilimia 7.6. Niwahakikishie tu kwamba sisi wasimamizi katika sekta ya madini tutaendelea kusimamia kuhakikisha kwamba sekta ya madini inakuwa na mchango katika pato la Taifa. Lengo letu ni kwamba ikifika mwaka 2025 tuweze kuchangia kwa takribani asilimia kumi ambapo kwa sasa tumeshafikia asilimia 4.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya nikitambua kwamba ukiangalia katika mwaka 2017/2018 tumeendelea kuhakikisha kwamba tunakuwa na usimamizi thabiti ili kuhakikisha kwamba kweli sekta ya madini inachangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa na Watanzania wanaweza kujivunia kutokana na mapato yanayopatikana na rasilimali hi ya madini. Kwa mwaka 2017/2018 tulipoangiwa lengo la kukusanya takribani shilingi bilioni 194.4 na tuliweza kuvuka lengo na kukusanya shilingi bilioni 302 ambayo ni sawa na asilimia 155. Katika mwaka huu wa fedha tumeepangiwa kukusanya bilioni 310; na nioende tu kumtaarifu Mheshimiwa Mpango, mpaka sasa tumeshafikia lengo kwa takribani asilimia 108 na tumeweza kuvuka katika robo ya kwanza kama ambavyo mmetupangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu lingine au mkakati wetu mwingine ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kudhibiti utoroshwaji wa madini. Kwa kiasi kikubwa kwa sasa, kama Serikali hata matukio yenye ye utoroshaji kwa kiasi kikubwa yameweza kupungua. Ukiangalia tu kwa Mererani peke yake, tangu mwezi Julai ilikuwa takribani kila mwezi kuna tukio moja na kutokana na ulinzi imara na thabiti ambao tumeuweka wote waliojaribu kufanya hayo wameweza kukamatwa. Kutoka na hayo ukiangalia Mererani pia tuliweza kuweka ukuta wa mzingo wa takribani kilometa 24.5 ambao umeweza kwa kipindi kifupi kabisa kuongeza mapato na yameweza kukua kwa takribani asilimia kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumeendelea kufanya kaguzi mbalimbali ikiwemo kwa wale wote

wanaojihusisha na biashara ya madini ikiwemo masonara. Hapa nipende tu kusema kwamba mimi binafsi na wasimamizi wenzangu Naibu Mawazirini Katibu Mkuu katika Wizara hatutakuwa na msalie Mtume kabisa kwa sonara yoyote ambaye anajihusisha katika kufanya utoroshaji, kudhamini vitendo ambavyo haviendani na kanuni, sheria na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema kwamba katika kaguzi fupi tu tulizozifanya, katika maduka 21 ya Dar es Salaam tumeweza kufunga maduka sita na tumeweza kukamata na kesi nyingine zinaendelea mahakamani, mfano kwa Kampuni ya *Syno Africa Collection Company*, kampuni moja ya Wachina tulifanya ukaguzi, ukiangalia katika *stock* waliyokuwa nayo ilikuwa inaonesha wana takribani *karat* 121 lakini baada ya kwenda kuvamia kesho yake tuliweza kukamata *karat* 2,849, mzigo wenye thamani ya takribani shilingi bilioni 2.5. Bado tunaendelea, tumeunda timu maalum hivi sasa inakagua maduka yote ya Dar es Salaam na tutaendelea kukagua maduka yote na biashara zingine zinazoendelea za madini katika mikoa yote nchi nzima.

Mheshimiwa mwenyekiti, nipende tu kusema kwamba kwa wale wanaojihusisha vitendo hivi kwa kweli sitakuwa na msalie na wataweza kuona kile ambacho kinawastahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kuimarisha ulinzi lakini pia tutaendelea kuhakikisha kwamba tunasimamia uzalishaji katika maeneo yote ya machimbo ya madini. Hivi sasa tumeweka maafisa mahususi kabisa katika migodi ya kati pamoja na migodi mikubwa ili kuhakikisha kwamba taarifa zote za uzalishaji za kila siku pamoja...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mwisho tunaendelea pia kuhakikisha kwamba tunaendeleza wachimbaji wetu wadogo kwa kuhakikisha kwamba tunawatafutia mitaji na fursa zingine ikiwemo pia masoko

ya madini lakini mwisho, tumejenga vituo saba vya umahiri kuhakikisha kwamba wachimbaji wetu wadogo wanapata...na faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(Makof)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii ya mpango wa Serikali wa maendeleo wa mwaka 2019/2020 kwa asilimia 200. Asilimia 100 ni ya Wizara yangu ya Nishati na asilimia nyingine 100 kwa ajili ya Wizara ya Viwanda. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuleta mpango huu mahsus wa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, Wizara yetu ya Nishati kimsingi ndiyo injini ya kujenga uchumi wa viwanda. Nitangulie kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa michango yote waliyooita na sisi, mimi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango tumeichukua, tutaifanyia kazi, penye maboresho tutaboresha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Nishati yako mambo mengi yamezungumzwa lakini ningependa nizungumze mambo matatu makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kuhusiana na utekelezaji wa miradi mikubwa kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa Taifa letu. Ujenzi wa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme, megewati 2,100 ni mradi mahsus sana. Kwa sasa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwa kiasi fulani tunanunua umeme kutoka Uganda, Uganda ambao wanazalisha umeme mdogo kulikoa hata sisi. Kadhalika kwa upande mwingine tunanunua umeme kutoka Zambia ambao

kimsingi wanazalisha umeme mdogo kuliko sisi. Ili nasi tuzalishe umeme wa kutosha na kuweza kuwauzia wenzetu majirani hatuwezi kuepuka kujenga miradi mikubwa kama hii ya *Stiegler's Gauge*. Kwa hiyo, ningependa niwaombe Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania tuunge mkono juhudhi za Serikali za kuutekeleza mradi huu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpango nakupongeza sana kwa kuuleta mpango huu ili uweze kujadiliwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu unakwenda vizuri, ni matarajio yetu miezi mitatu ijayo tutaweza kuanza kujenga mradi huu ili utupunguzie adha kubwa ya nishati hapa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya umeme nchini kwa sasa kwa kiasi kikubwa inaridhisha ingawa tuna takribani megawati 148 za ziada lakini bado tunaona iko haja ya kujenga miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ningependa kutoa ufafanuzi kidogo. Waheshimiwa Wabunge wamesema katika kutekeleza mradi huu inaonekana kama Serikali tunajielekeza zaidi kwenye miradi ya maji kuliko miradi mingine. Ningependa kuwatoa wasiwasi wananchi na Waheshimiwa Wabunge, kwamba tunatekeleza miradi yote kwa kuzingatia vyanzo vyote vya nishati hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa taarifa tulionayo kwa sasa kwa upande wa matumizi ya gesi tunatarajia kuzalisha megawati 1,445 kutokana na rasilimali ya gesi ifikapo miaka minne/mitano ijayo. Mradi mahsusni katika upande huu, kwa sasa tunatekeleza mradi wa Somanga Fungu ambaao utaanza kujengwa rasmi mwezi Machi mwakani, utakaotuzalishia megawati 330.

Wakati huo huo tutaanza kutekeleza mradi wa takribani megawati 300 kutoka Mtwara ambaao pia utatuingizia katika Gridi ya Taifa ndani ya miaka miwili ijayo. Kadhalika, tunaendelea kukamilisha mradi wa *Kinyerezi One* wa megawati 185 ambaao utaingizwa kwenye Gridi ya Taifa

ifikapo Februari mwakani. Hii yote ni miradi mabsusi inayotokana na rasilimali ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuongeza tu, katika mradi wa *Kinyerezi Three* tunatarajia kuzalisha megawati 600 ndani ya miaka miwili/mitatu. Kwa hiyo ni matarajio yetu ndani ya miaka miwili/mitatu tutazalisha zaidi ya megawati 1,445 itokanayo na rasilimali ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nitoe ufanuzi huu kwa sababu inawezekana wananchi na Waheshimiwa Wabunge msijue kama bado tunaendelea kutekeleza miradi hii mikubwa inayokana na rasilimali ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo tunaendelea pia kutekeleza miradi mingine kutokana na vyanzo mbalimbali ikiwemo vyanzo vya upepo hasa katika maeneo ya Singida. Hivi sasa maeneo ya Kisasida wakandarasi wameshapa maeneo ya hekta zaidi ya 150 kwa ajili ya kujenga mradi wa upepo wa megawati 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna miradi mingine mingi midogo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa upande wa nishati niingie kwenye upande wa viwanda...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wetu ndio huo.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia 200 za viwanda na za kwangu, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Naelewa unayo mengi sana Dkt. Kalemani, anayefuata ni Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa na mimi fursa ya kuweza kuchangia kwenye mjadala unaoendelea kuhusu mpango, na nitajelekeza moja kwa moja kwenye ushauri uliotolewa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na baadhi ya wachangiaji ambao wamechangia mjadala katika mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kubwa lililoitokeza ni umuhimu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kujenga uwezo na kuongeza umakini kwenye masuala ya mikataba, lakini ikiwezekana kufanya rejea ya mikataba mbalimbali ambayo ilishaingiwa mikataba na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema kwamba ushauri huo tulishaupokea na kwa kweli tulishaanza kuufanyia kazi hata kabla maoni hayo hayajatolewa hapa Bungeni kwa sababu hatua zilishachukiliwa kuimarisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hasa katika eneo la uangalizi wa mikataba. Katika eneo hilo kuna mabadiliko tuliyofanya, ofisi imeimarishwa zaidi na sasa hata tumegawanya ile idara iliyokuwa inahusika na masuala ya mikataba kiasi kwamba sasa kutakuwa na *section* itakayokuwa inashughulika na mikataba ya rasilimali, kutakuwa na *section* itakayokuwa inashughulika na mikataba ya manunuvi, kutakuwa na *section* itakayokuwa inahusika na mikataba ya fedha na mwisho kutakuwa na *section* itakayokuwa inashughulika na mikataba ya Kimataifa na hii itakuwa na watu ambao wako *specialized*, watakuwa na ujuzi na utaalam wa kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la kurejea mikataba pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilishaanza kulifanyia kazi. Ninapozungumza hapa tayari ofisi inafanyia rejea ya mikataba kadhaa ikiwemo mikataba ya *Songas*, mikataba mbalimbali ya utafutaji na uendelezaji wa rasilimali ya petroli (*Production Sharing Agreements*), kuna *gas sales agreements*, kuna *power purchase agreements*, kuna *bilateral investment treaties* na mikataba mingine mingi ya aina mbalimbali. Hizi kazi ninavyozungumza sasa hivi zinaendelea.

Kwa hiyo ushauri kwa ujumla tumeuchukua na tutaendelea kuufanya kazi na maoni yote yalitolewa tunayapokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
(Makof)

MWENYEKITI: Ahsante, mwisho lakini sio mwisho kwa kutajwa, lakini siyo kwa muhimu Mheshimiwa Jestina Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Kwa dhati kabisa nimpongeze Dkt. Mpango kwa kazi nzuri anayoifanya ndani ya Serikali na Tanzania nzima, Naibu Waziri na wataalm wote katika ofisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na viongozi wote wa kitaifa, hawa wamekuwa wakitutengenezea miongozo na kujenga msingi wa namna gani Taifa letu linatakiwa kupiga hatua za maendeleo. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu pamoja na watendaji wengine wote ndani ya Serikali ambao wamekuwa wakipokea miongozo hiyo na kuifanya kazi. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge; hii ni Kanuni ya 94(6) ambayo imetuweka katika mjadala huu na tutakwenda kwenye Kanuni ya 97 mwezi wa tatu ili kuweza kuyatekeleza haya ambayo Serikali imeshauriwa katika kipindi hiki cha kujadili mpango. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge ninawapongeza na ninawashukuru mmetushauri vizuri Serikalini. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujikita kwenye mambo machache, la kwanza ni suala la ajira. Nataka kuungana na Dkt. Mpango na wale wote waliopanga mpango huu na kuuleta ndani ya Bunge. Dkt. Mpango anapozungumzia kuhusu miradi ya kimkakati ya taifa akisema

barabara anazungumzia ajira, akisema viwanda anazungumzia ajira, akisema bomba la mafuta anazungumza ajira kwa Watanzania, akisema kilimo anazungumza ajira kwa Watanzania, akisema viwanja vyatya ndege anazungumza ajira kwa Watanzania, akisema uvuvi ama mifugo anazungumza ajira kwa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wote waliokuwa wanataka kutushauri Serikali kuhusu ajira naomba niwahakikishie haya yaliyojitekeza kwenye hotuba ya mipango na hasa miradi ya kimkakati inayosimamiwa na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, miradi hiyo yote ni ajira kwa Watanzania, ni ufumbuzi wa ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya nini; baada ya kuona kwamba sasa tuna mageuzi makubwa ya klichumi ndani ya nchi na hasa miradi mikubwa hii ya kimkakati tumeamua sasa kutengeneza mwongozo kwanza wa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wetu wote wanao-graduate kwenye vyuo vyetu vikuu ndani ya nchi. Pili tumetengeneza mwongozo wa mafunzo ya uwanangezi kwa Watanzania wote vijana katika Taifa letu. Vilevile tumeshatengeneza mwongozo wa *local content* ambao utawashirikisha Watanzania kupata ajira kwenye miradi hii mikubwa ya kitaifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshatengeneza *dictionary* ya aina za kazi ambazo Watanzania watatakiwa wazifanye na wageni wazifanye kwenye miradi yote ya kimkakati ndani ya nchi yetu ambayo inaanishwa na Serikali yetu. Kwa hiyo, ukiangalia hayo yote unaona kabisa kwamba suala la ajira limetengenezewa mazingira wezeshi na vijana wa Tanzania na Watanzania watanufaika na maendeleo ya kuiuchumi na uwekezaji ndani ya Taifa letu na watafanikiwa kupata ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja, baada ya kutengeneza mwongozo wa *local content* nini ambacho tumeanza kuona matunda mazuri ya mwongozo huo.

Kwenye mradi ya Daraja la Mfugale ajira zilikuwa 616, Watanzania walipata ajira 589, wageni wa nje walipata ajira 27 na mradi ulikuwa na thamani kama shilingi bilioni kama 1.6, kwenye manunuzi ya huduma tulikuwa na kampuni 15 lakini kampuni 14 kwenye ule mradi zilikuwa za Watanzania, kampuni moja tu ndio ilitoka nje ya Tanzania. Kwa upande wa manunuzi ya bidhaa tulikuwa na kampuni 28, kampuni 24 za Kitanzania ndizo zilizopata manunuzi ya bidhaa kwenye mradi ule, kampuni tatu tu ndizo zilikuwa za nje na kampuni moja ilikuwa ya ubia tukafanya na mafunzo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye mradi huu wa *Ubungo interchange* na pale kwenye hatua hizi za awali ajira zipo 319, lakini ajira za ujuzi wa juu Watanzania wako 60, wageni wako 50, ujuzi wa kati ni Watanzania tu 129 na ujuzi wa chini ni Watanzania peke yao 80.

Kwa hiyo, ninaomba niseme kwamba ukiona Mheshimiwa Mpango anakuja na mipango ya miradi ya kimkakati anataka kutatua tatizo la ajira kwa wananchi wa Tanzania. Kwa hiyo ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tumuunge mkono Mheshimiwa Dkt. Mpango, tutoe ushauri wetu kama tulivyoutoa, yale maeneo ambayo Serikali tunakiwa kuyafanya kazi tutayafanya kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niseme neno lingine kidogo la mwisho; tunajitahidi kama Serikali kupokea mawazo ya Waheshimiwa Wabunge kuona namna gani tunatengeneza mazingira wezeshi ya uwezeshaji katika kuhakikisha tunaalika wawekezaji wengi kutoka nje kuja kufanya kazi. Kwa mfano baada ya kutoa *blue print* kitabu kile kimetuongoza kila Wizara, mimi ndani ya Wizara yangu tumeondoa ada ya usajili ambayo ilikuwa ni shilingi 50,000 mpaka shilingi 1,800,000 katika kuhakikisha masuala ya usalama kazini yanafanya, tumeiondoa ili kuwaalika wawekezaji wengi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeondoa ada ya fomu ya usajili ambayo ilikuwa ni shilingi 2,000,000, tumeondoa faini za Zimamoto ambazo tumewaachia sasa Wizara ya Mambo

ya Ndani wafanye zimeondoka kwenye Wizara ya Kazi, tumeondoa ada ya leseni ambayo ilikuwa ni shilingi 200,000, tumeondoa tozo ya utaaalam ilikuwa shilingi 450,000, kwenye tozo tu zilizoodolewa kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu chini ya OSHA zina thamani ya karibu shilingi 8,392,000. Hiyo yote ni mkakati wa Serikali kwa ushauri unaotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kuboresha mazingira kwa wawekezaji waje kuwekeza kwenye taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa tunaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba tunapokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ili kuboresha haya yote ambayo tunaona ni bora na hatimaye mwezi wa tatu tutakuja na Mpango ambao utasaidia kujibu maswali ya Watanzania wengi. Lakini kwa kweli tunampongeza sana Dkt. John Pombe Magufuli uongozi wake ni imara, anatuongoza vizuri, anatuonesha njia na sisi Mawaziri tunaomsaidia na viongozi wengine wote ndani ya Serikali, wote kwa pamoja tunatakiwa kujifunza kwenye *sprit* ya Mheshimiwa Rais wetu nini anataka na anataka kulipeleka taifa hili eneo gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la vijana nikizungumza hizo ajira zote ni vijana...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU...naomba kuunga mkono hoja na tunaendelea kumuombea Mheshimiwa Rais wetu aendelee kutuongoza vizuri na kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja ambayo imewekwa mezani na Mheshimiwa Waziri

wangu wa Fedha na Mipango kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/2020, na mwongozo wa maandalizi ya mwaka husika. Naomba pia nimshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetukutanisha tena katika Bunge lako tukufu kwa ajili ya kazi hii muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa utangulizi ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisoma kwenye kitabu chetu cha Mwongozo wa Mpango katika kiasi cha shilingi trilioni 6.5 zilizotumika katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/2018 asilimia 77.5 zilikuwa fedha zetu za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na utangulizi huu ili niweze sasa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu. Nampongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, haya hayajawahi kutokea kwenye hostoria ya Tanzania, lakini yamewezekana kwenye uongozo wake makini, kwenye uimara wake wa kusimamia mambo anayoamua kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa miongozo yao ambayo wamekuwa wanatupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi trilioni 6.5 nilizosema za utekelezaji wa mpango 2017/2018 zilielekezwa kwenye maeneo gani; shilingi trilioni 6.5 zilielekezwa kwenye maeneo yale ambayo yana matokeo chanya kwa Watanzania wa kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana *Chief Whip* Mheshimiwa Jenista ameeleza kwa uzuri sana kwamba wapi tunalekeza ni miradi ipi tunaisisitiza Serikali ya Chama cha Mapinduzi Awamu ya Tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasisitiza miradi ile ambayo ina athari moja kwa moja kwa Watanzania wa kawaida. Niseme tu mfano mmoja; wa kwanza ulikuwa ni ujenzi na ukarabati wa reli na ambapo tulitumia shilingi trillioni 1.22. Pia tulitumia shilingi trillioni 1.528 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara yote ya mijini na vijijini, tunakwenda kugusa maisha ya Mtanzania. Tumegusa maisha ya Mtanzania kwa sababu tunamthamini, tunamjali na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ni Rais wa wanyonge na ameonesha kwa vitendo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017/2018 umeme vijijini tumepeleka kwenye vijiji 3,153, hajjawahi kutokea kwenye historia ya Taifa hili, hajjawahi kutokea na ndiyo maana sasa tunasema tumpongeze Mheshimiwa Rais wetu, tumpongeze Makamu wa Rais, tumpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa usimamizi mzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nianze na utangulizi huu. Kwa nini nimeanza na utangulizi huu? Nimeanza na utangulizi huu kwa sababu napenda kuchangia hasa nikitembea kwenye ukurasa wa kwanza na wa pili wa kitabu cha hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Nimesema hivyo kwa sababu naomba niseme, katika *paragraph* ya pili, sitaki kuisoma kwa sababu ina ukakasi ndani yake; katika *paragraph* ya pili Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatuletea takwimu za kustaa jabisha dunia. Pamoja na haya yote yiliyo tekekelezwa na Serikali yetu ya Awamu ya Tano, naomba niwaulize Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wana dhamira gani na Taifa hili? Nini wanachokidhamiria kwa taifa hili? Kwa sababu haiwezekani hata kama wewe ni mpinzani basi pinga kwa hoja, pinga kwa hoja zenye mashiko. Miradi yote ambayo nimeieleza inaenda kugusa Watanzania wa kawaida halafu wanakuja watu wanaoijiita Watanzania kwamba asilimia 47 ya Watanzania ni maskini hawawezi kufanya chochote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliombe Bunge lako tukufu, hiki ni kitabu, hii ni *official document* na kuwa

official document na kuwa official document maana yake taarifa hii itaishi milele haitofutika, ndiyo maana nauliza Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wana dhamira gani kwa Taifa hili? Kwa sababu hii itatumika na Watanzania wanaweza kuitumia kama reference, lakini walichoki- quote kwamba wapi wametoa hizi taarifa hili ndio la kustaajabisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamem-quote, na naomba nitumie neno hili, mnisamehe kwa wale wakubwa, wamem-quote muhuni mmoja ambaye sijui ni aidha katumwa au kwa kuidhamiria kwa kwamba anataka kupotosha dunia, huyu namwita ni muhuni. Ni muhuni huyu kwa sababu ya alichokiandika na ndiyo maana naishangaa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Ningefurahi sana...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA FRDHA:...Mheshimiwa Mwenyekiti, waambie watulie! (*Makofi*)

MWENYEKITI: Dozi inaingia!

MBUNGE FULANI: Wahuni hao!

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Piga Naibu, Piga, piga!

MWENYEKITI: Naomba utulivu Waheshimiwa, Waheshimiwa Wabunge...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: (*Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti*).

MWENYEKITI: ...hapana hiyo ni dibaji tu ni dibaji, hebu endelea. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba watulie si wametuleta wenyewe kwenye taarifa rasmi? Na mimi siko hapa kujibu hoja kwa sababu tulichokuja kukitafuta na Mheshimiwa Waziri wangu ni maoni yenu hatuna sababu ya kujibu hoja tuna sababu ya kueleza jinsi ambavyo mna dhamira mbaya ya kupotosha jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza haya, nimewita muhuni huyu aliyeandika hii *document*, lakini pia naishangaa Kambi Rasmi ya Upinzani, na ningetamani sana Mheshimiwa Halima Mdee angekuwepo amekaa hapo, ningetamani sana kama angekuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya kwa sababu Mheshimiwa Halima Mdee ni mwanasheria. Tumefanya marekebisho na tumepitisha Sheria ya Takwimu hata miezi mitatu hajapita, leo mtu anakuja kuleta taarifa za ajabu za kuipoteza dunia. (*Makofi*)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ashitakiwe!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, inanipa wasiwasni na naomba niwaombe wachumi wote Tanzania waweze sasa kuanzisha Chama Rasmi cha Wachumi Tanzania ili angalau mtua anayekuwa na jukumu la kuongelea mambo ya uchumi awe ni mchumi aliyesoma na tunayemuelewa. *Credibilityya taarifa aliyo-cite* Mheshimiwa Halima Mdee na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwanza ina shaka kubwa. Sentensi ya kwanza ambayo inatia shaka kwenye *document* hii; kwa wale *researchers* mtaniambia; naomba kuisoma sentensi ya kwanza ya kutia mashaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sentensi ya kwanza inasema; *research for this article* naomba mnisikilize *researcha for this*

article was collected, research was collected, kosa la kwanza, research for this article was collected, naomba mtulie sawa!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Susan Kiwanga sikiliza Susan Kiwanga wewe!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *research was collected during William's recent visit to East Africa; research was collected during a recent visit. Do we collect research when we visit? Swali la kwanza. And usually tunachokifanya ndugu zangu we collect data and we conduct research kitu cha kwanza... (Makof)*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Haonga upo?

MBUNGE FULANI: Haonga jibu!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni kosa la kwanza kwa mchumi wa kawaida ambaye amesoma tu *micro economics* asingeendelea ku-cite document kama hii kuleta kwenye Bunge tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makof)

MBUNGE FULANI: Wape! Wape maneno!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Saada Mkuya alianza kueleza, lakini tulipoleta marekebisho ya Sheria ya Takwimu tulisema mtafiti yeoyote anayeta kufanya *generalization at the national level particular for economic data* lazima apate kibali katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, hilo halikufanyika. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ukisoma hii *document* ya muhuni huyu hata wapi alikusanya hizo taarifa zake haijulikani ni wapi. Wapi amekusanya haijulikani, wapi ameuliza Watanzania wangapi ili kufanya *generalization* kwamba Watanzania ni maskini asilimia 47 haijaoneshwa kokote kwenye *document* hii. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, najua Waheshimiwa Wabunge wanaweza kusema chochote ndani ya Bunge hili, lakini tuseme chochote chenye manufaa kwa Taifa letu. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Haonga upo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niliyosema na aliyoeleza Mheshimiwa *Chief Whip*, miradi yote tunayotekeleza, zaidi ya vituo vya afya 350 vilivyojengwa ndani ya Taifa letu kwa mwaka mmoja uliopita tunatumia *Force Account*. *Force Account* maana yake nini, Watanzania wanapata ajira za moja kwa moja, hawa maskini kawapata wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao masikini kawapata wapi? Katika miradi ya *REA* ambayo nimesema zaidi ya vijiji 3,000 vimepata umeme wanaochimba mashimo na kuweka nguzo ni watoto wetu wa Kitanzania, hao 50, 47 kati ya 100 kawapata wapi? (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Haonga upo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitendee haki Taifa letu. Tulitendee haki Taifa letu na ninaomba nirudie ambayo anayasema Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli siku zote, zile kazi za magumashi Serikali ya Awamu ya Tano imezifuta zote, lakini tumetengeneza kazi halali nydingi za kutosha na Watanzania wameuelewa muziki wa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda wangu umekwisha, naomba niseme moja la mwisho, nalo pia ni kutoka kwenye kitabu chake hiki katika miradi ya *PPP*. Naomba pia, najua muda umekwisha, naomba wafahamu kwamba, kwenye vitabu vyetu vya mpango miaka yote mitatu na mwaka huu cha nne, tumeandika miradi ambayo sekta binafsi inatakiwa kufanya.

MBUNGE FULANI: Muongezee.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:Mheshimiwa

Mwenyekiti, na Mheshimiwa Rais wetu kwa dhamira njema ya kutaka sekta binafsi itekeleze miradi hiyo, ameshakutana na sekta binafsi mara tatu. Mara ya mwisho akawaita wenyewe viwanda wanaotaka kuwekeza kwenye viwanda vya binadamu ili milioni 270 alizosema Mheshimiwa Ummy zibaki ndani ya Taifa letu. Je, tuendelee kusubiri hata kama hawapo? Haiwezekani, lazima tutende kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwaka jana wakati nachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri kipindi kama hiki niliwha kuwaambia kwamba ni lazima tuelewe *the economics of structural development*, miradi ambayo ni miundombinu, nani anatakiwa kuwekeza, tuelewe *economics*yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *economics* yake iko hivi, kwanza uwekezaji wake ni mkubwa, uwekezaji ukishakuwa mkubwa mfanyakishara ambaye anatafuta *commercial/financial viability*hana, hawezi kuja kuwekeza kwenye miradi hiyo. Tumesubiri vya kutosha kuhusu reli yetu ya kati *SGR* na sasa tunatekeleza kwa fedha zetu za ndani na ninaomba niliseme hili kwa nguvu zote, tunatekeleza kwa fedha zetu za ndani. Hata hivyo hatujafunga milango, yejote ambaye yuko tayari kuja kuwekeza nasi bado kuna vipande, ndiyo maana tunatengeneza kwa *lots*. Aje tutampa *lot* ili aweze kuwekeza, lakini mfahamu hilo ambalo ninawaambia, lakini mfahamu hilo ambalo ninawaambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kusema, tumeshasubiri kiasi cha kutosha, naomba nizishukuru Serikali za Chama cha Mapinduzi Awamu ya Kwanza, Serikali ya Chama cha Mapinduzi Awamu ya Pili, Serikali ya Chama cha Mapinduzi Awamu ya Tatu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi Awamu ya Nne, ambazo zote zimewezesha haya yote anayoyafanya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuyafanya na kuyatenda kwa nguvu zake zote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namaliza kwa kumpongeza tena Mheshimiwa Rais wangu. Naomba niseme Chama cha Mapinduzi tuliahidi na tunatekekeleza, Watanzania ni mashahidi. Ahsante sana. (*Makofii/vigelegele*)

MWENYEKITI: Ahsante! Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maeleo yako mazuri ya kina na yamesaidia sana kusafisha njia kwa wasilisho la Waziri wako; na ndio maana rafiki zangu naona, nimeelewa kwa nini, haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 6 Novemba, 2018 niliwasilisha katika Bunge hili Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/2020. Napenda kukushukuru sana wewe binafsi, lakini pia Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendesha mjadala wa Mapendekezo ya Mpango wa Taifa vizuri tena kwa umahiri mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kuwa Serikali imepata maoni mengi na ushauri mzuri sana kuhusu vipaumbele na mambo mengine ya msingi ya kuzingatiwa wakati wa kuandaa Rasimu ya Mpango na Bajeti ya Mwaka ujao wa Fedha. Rasimu ya Mpango itaswalishwa mbele ya Bunge hili mwezi Machi, 2019. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika mjadala huu. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni 185, kati yao 151 wamechangia kwa kuzungumza na 34 kwa maandishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niishukuru tena Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge

wa Kibakwe, kwa maoni na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kuboresha mwongozo na mapendekezo ya mpango. Aidha, natambua Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe. Vilevile napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote ambao wametoa ufanuzi wa hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa namna ya pekee kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliota michango inayotambua na kuthamini juhudu kubwa zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM - Taifa ambazo zimewezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa na yanayoonewa husuda katika kipindi kifupi cha miaka mitatu katika kuwalettea wananchi maendeleo. Kusema kweli pongezi zenu za dhati zimetutia moyo sana ili tuweze kuendelea kufanya vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo nami nitumie fursa hii kumpongeza sana Rais wetu ambaye ni sehemu ya Bunge hili kwa uongozi wake thabiti na dhamira yake ya dhati ya kushughulikia matatizo ya Watanzania na hasa wanyonge na kulipeleka Taifa letu mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uhodari wao katika kazi zao za kumsaidia Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kubwa la mkutano huu wa Bunge lilikuwa ni kupata maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ambao utatumika kuboresha mwongozo na kuandaa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha. Napenda nirudie tena kwamba mmetupatia maoni mengi ya kuzingatia na kuyafanya kazi

tunapokwenda kuandaa Mpango wa Taifa na Bajeti ya Serikali 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivutiwa sana na michango mahiri ya baadhi ya Wabunge. Kwa kweli zamu hii tofauti na miaka miwili iliyopita kwa kweli, michango ilikuwa mizuri na wengi walichangia vizuri. Nitaje tu wachache, lakini sio kwa kubagua, Mheshimiwa Seneta Ndassa alitoa mfano mzuri, Mheshimiwa Balozi Kamala, Mheshimiwa Munde, Mheshimiwa Kingu, Mheshimiwa Ridhiwani, Mheshimiwa Genzabuke, Mheshimiwa Amon, Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Zungu, Mheshimiwa Maghembe, Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Bashungwa, Mheshimiwa Mwilima, Mheshimiwa Kiula, Mheshimiwa Kiruswa, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa Shabiby, Mheshimiwa Masele, Mheshimiwa Christine Ishengoma, Mheshimiwa Rehani, Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Raza, Mheshimiwa Musukuma na niseme Mheshimiwa Dkt. Sware alijitahidi kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ni vyema niseme wazi na mimi ni mkweli, ndivyo mnavyoniandika kwenye magazeti na ni kweli. Naomba niseme wazi kwamba baadhi ya yaliyosemwa na hasa kutoka upande wa pili, yale ya kubeza mafanikio yaliyopatikana katika awamu hii na mengine kupelekwa kwenye Magazeti ya Tanzania Daima, Mwananchi na mitandao ya kijamii, niseme kwamba yalikuwa nje ya mstari na yalikosa *objectivity*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo anayetilia mashaka uzalendo wangu na kunituhumu kwamba, ninaogelea kwenye utajiri ni Mkristo aende akatubu kwa sababu amenishuhudia uongo. Yupo mwingine anayedai kwamba *Tanzania is not strategic* na kuwa nchi moja jirani ina *vision* na *commitment* kuliko nchi yetu, mimi sijui, sijui anangoja nini? Si akaombe uraia huko, mbona madhaifu ya hiyo nchi hayasemi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu nilieleza juu ya mwenendo mzuri sana wa viashiria vyा

kiuchumi kuanzia ukurasa wa nne mpaka wa 10 na mafanikio makubwa yaliyopatikana niliyaeleza kuanzia ukurasa wa 23 mpaka ukurasa wa 34, lakini Tanzania Daima wakaenda kuandika eti Dkt. Mpango akiri uchumi kuperomoka, kwa sababu tu katika hotuba yangu niliwaambia Watanzania baadhi ya changamoto tunazokabiliana nazo katika jitihada za kukusanya mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, hiyo ni kukosa maadili ya weledi (*unprofessionalism of the highest order*), ni ukhanjanja uliokubuhu. Kama hawakusikia au kuelewa nilichozungumza ni bora wakae kimya kuliko kuandika kwenye vyombo vya habari maneno ya kutengeneza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba sasa kutoa ufanuzi kuhusu mambo machache ambayo yalijitokeza katika mjadala wetu. La kwanza ni ushauri ambao mimi ninauona ni muhimu sana. Waheshimiwa Wabunge wengi walisisitiza umuhimu wa kutoa kipaumbele cha juu katika mpango ujao kukuza sekta ya kilimo cha mazao, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo makubwa tulivoambiwa tuzingatie ni pamoja na mikakati ya kuongeza tija, upatikanaji wa pembejeo, mbegu bora, huduma za ugani, matumizi ya teknolojia na zana za kisasa, kilimo cha umwagiliaji, ufügaji wa kisasa, dawa za mimea na mifugo, miundombinu kwa ajili ya ufügaji, zana bora za uvuvi, ujenzi wa bandari ya uvuvi, meli za uvuvi bahari kuu, upatikanaji wa mitaji na mikopo kwa wakulima, kuboresha vyuo vya utafiti wa kilimo, mifugo na uvuvi na kuongeza bajeti ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema ushauri huu ni wa msingi sana kwa kuwa kilimo ndiyo sekta mama na tegemeo la wananchi wetu wengi maskini. Aidha, sekta hii isipofanya vizuri inakuwa na athari kubwa kwenye mwenendo wa uchumi jumla, kama vile kuongezeka kwa mfumuko wa bei na gharama za maisha, kuongezeka kwa

umaskini, kupungua kwa upatikanaji wa fedha za kigeni na hata kupungua kwa thamani ya shilingi ya Tanzania na urari wa malipo (*balance in payments*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongeza bajeti ya kilimo, na hapa ningependa nitoe angalizo. Ni kweli, Azimio la Maputo na Malabo linataka kila nchi kutenga angalao asilimia kumi ya bajeti yake kwa ajili ya kilimo, lakini ni muhimu kukumbuka kuwa, sekta ya kilimo ina mwingiliano mkubwa na sekta nyine kisi kwamba mwenendo bora wa kilimo unategemea sana uwekezaji wa sekta saidizi, hasa miundombinu ya umwagiliaji, barabara vijiji, umeme kwa ajili ya kuendesha viwanda vya kuongeza thamani ya mazao, uzalishaji wa zana za kilimo na dawa, elimu, huduma za afya kwa wakulima na kadhalika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kuwa uongezaji wa bajeti ya kilimo ni muhimu. Narudia tena, uongezaji wa bajeti ya kilimo ni muhimu, lakini lazima ufanyike kwa ulinganifu na mahitaji ya kibajeti ya sekta nyine muhimu kama nilivyo zitaja. Hivyo, pamoja na umuhimu wa kuongeza bajeti ya kilimo katika mazingira ya nchi yetu ambapo wigo wa mapato ya Serikali ni mdogo ni muhimu tuhakikishe kwamba fedha inayopatikana inaelekezwa kwenye maeneo machache yenye tija kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ni muhimu tukaongeza jitihada za kuvutia sekta binafsi kuwekeza kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi, kuimarisha upatikanaji wa mitaji na mikopo kwa wakulima, wafugaji na wavuvi pamoja na kutafuta masoko ya mazao kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe zipo sekta nyine ambazo nazo kuna makubaliano ya kimataifa kuhusu kiwango cha chini cha bajeti. Kwa mfano elimu asilimia 20, afya asilimia 15, maendeleo ya takwimu asilimia 0.5 na kwa upande wa utafiti ni asilimia moja ya pato la Taifa. Kusema kweli kama sekta hizo tungezipa viwango hivyo ambavyo vinashauriwa kimataifa, sekta zilizobaki ambazo pia ni muhimu mimi nadhani zingepata makombo tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge walisisitiza Mpango wa Taifa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, subiri kidogo. Napenda nitumie mamlaka niliyonayo kuongeza muda usiozidi nusu saa, ili Mheshimiwa Waziri aendeleee na wasilisho lake, karibu Waziri.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge walisisitiza kwamba mpango ujao uje na mkakati wa kutatua changamoto kubwa ya masoko na bei ndogo za mazao kwa wakulima, ikiwa ni pamoja na pendelezo la kuanzisha mfuko wa kutegemeza bei za mazao (*price stabilisation fund*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nilihakikishie Bunge lako kwamba tutafanya kazi masuala yote haya, kwa maana ya kubaini masoko ya kikanda na kimataifa, kuongeza ushiriki wa Tanzania katika maonesho mbalimbali ili tuweze kutangaza bidhaa zetu na kuweka msukumo kwenye uongezaji wa thamani, lakini pia kuimarisha bei za mazao. Hata hivyo, ni vizuri kutambua jitihada mbalimbali ambazo zimeshachukuliwa na Serikali katika kushughulikia changamoto hizo. Niseme chache tu kuwa ni pamoja na uanzishwaji wa soko la bidhaa ambalo limehuishwa na mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani, lakini pia Serikali imeendelea na juhudi za kuimarisha vyama vya ushirika ambavyo idadi yake imeongezeka kutoka 7,888 mwaka 2015 mpaka 10,990 mwaka 2017. Vilevile lakini tutaendelea kutekeleza *ASDP II* ambayo inalenga kufanya mapinduzi katika sekta ya kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu ushauri wa kuanzisha mfuko wa kutegemeza mazao Serikali italiangalia pendelezo hili kwa kina na hususan kupitia soko la bidhaa na Bodii ya Nafaka au Mazao Mchanganyiko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauriwa kuhusu hatua za ziada za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Niseme tu kwa kifupi kwamba ushauri huu tutauzingatia ni

jambo muhimu; na niwajulisse tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, ndani ya Serikali Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshakuelekeza kila Wizara kuandaa mkakati na mpango kazi wa kutekeleza ile *Blue Print on Policy and Regulatory Reforms*. Kwa hiyo, hili ni jambo tunalitilia mkazo sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tulilisikia ni kwamba, miradi mikubwa ya kielelezo ambayo imekwama ikwamuliwe na ianze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili ninapenda wafahamu kwamba kwa kweli wote tunayo kiu kubwa ya kuona nchi yetu ya Tanzania inaendelea haraka kwa kutumia vizuri rasilimali za Taifa tulizonazo. Hata hivyo, Serikali inayo dhamana ya kuhakikisha kwamba rasilimali zetu hizi zinatumika vizuri na kwa kulinda maslahi mapana ya Taifa. Kwa kifupi Waheshimiwa Wabunge miradi mingi ya kielelezo ambayo inaonekana kukwama imetokana na masharti hasi wanayokujanayo wawekezaji ambayo Serikali inaona kwamba hayana maslahi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu nitoe mifano mitatu tu. Yupo mwekezaji ambae anadai apewe hati ya kumiliki ardhi wa miaka 99 kwa eneo atakalolipia fidia na aruhusiwe kuhaulisha ardhi itakayokuwa imeendelezwa kwa wawekezaji wengine. Hii ni tofauti na utaratibu wa wageni kupewa *derivative land rights* kulingana na Sheria ya Ardhi ya Taifa letu. Mwekezaji huyu pia ameomba wawekezaji wengine kutoka nje ya nchi waruhusiwe kununua ardhi kutoka kwa mwekezaji na kuiuza kwa wawekezaji wengine kwenye eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili, yuko mwekezaji mwengine ye ye anataka aruhusiwe kutoza kodi kwa miaka kumi na kutumia hayo mapato na kisha arudishe fedha hizo kwa kipindi cha miaka kumi mingine bila riba, jambo ambalo halikubaliki na ni kinyume na matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa tatu, yupo mwekezaji ambaye anataka Serikali ilete Muswada wa Sheria Bungeni tubadilishe sheria za nchi zilizopo ili kulinde maslahi yake, jambo ambalo linaingilia mamlaka ya Bunge hili kutunga sheria kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania na hii ni mifano michache tu, yako masharti ni hovyo kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Tanzania naomba mtambue hivyo na muendelee kuiamini Serikali ya CCM kwamba pale utekelezaji wa miradi hii mikubwa unapochelewa ni kwa sababu bado tunahaingaika kuhakikisha kwamba tunalinda maslahi ya mama Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakwenda kwenye mradi mmoja mmoja kwa kuwa tutawasilisha ufanuzi wa hoja hizi kwa maandishi, basi Waheshimiwa Wabunge watapata nafasi ya kuzisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kidogo kuhusu ufanuzi juu ya upimaji wa uhimilivu wa deni la Taifa na hususani kwa sababu Kamati ya Bajeti ilitutahadharisha kuwa ingawa deni letu ni himilivu limeendelea kukua kwa kasi na hivyo waliishauri Serikali ijpime na kuweka ukomo kwenye uwiano wa ulipaji wa deni na mapato ya ndani ili kuona athari zake kiuchumi na kibajeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine hili ni eneo ambalo linahitaji semina maana kila Bunge swali kuhusu deni la Taifa linaulizwa, lakini ngoja nijitahidi kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura ya 134, Serikali ina wajibu wa kufanya tathmini ya uhimilivu wa deni kila mwaka ili kupima hali ya deni na uhimilivu wake kwa kipindi cha muda mfupi, wa kati na muda mrefu. Uhimilivu na kasi ya ukuaji wa deni la Taifa unapimwa kwa kutumia viashiria vyatupima uwezo wa nchi kukopa na viashiria vyatupima uwezo wa nchi kulipa deni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze na viashiria vyatupi uwezo wa nchi kukopa. Kwa kawaida tunatumia vigezo vitatu, cha kwanza ni uwiano wa thamani ya sasa ya deni lote kwa Pato la Taifa na pili, ni uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo cha kwanza kinapima gharama ya leo ya kulipa deni ikilinganishwa na pato la Taifa kwa sasa na kigezo cha pili kinapima gharama ya leo ya kulipa deni la nje ikilinganishwa na pato la Taifa; kigezo cha tatu cha kupima uwezo wa nchi kukopa ni uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje ikilingalishwa na mapato yatokanayo na mauzo nje ya nchi, na kiashiria hiki kinapima uwezo wa kiasi cha mapato yanayotokana na mauzo ya bidhaa nje ya nchi na kulipa madeni ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo viashiria hususani viwili, ambavyo vinapima uwezo wa nchi kulipa deni. Cha kwanza ni uwiano wa jumla ya malipo ya madeni ya nje ikilingalishwa na mapato ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi, na cha pili, ni uwiano wa malipo ya madeni ya nje na mapato ya ndani. Hiki kinapima uwezo wa Serikali kulipa deni la nje kutoka kwenye makusanyo ya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vigezo vyote hivi, nimekuwa ninasema tena na tena kwa vigezo vyote hivi tuko vizuri, deni letu ni himilivu na naomba niliarifu Bunge lako tukufu kwamba mwezi huu wa Novemba, Serikali kwa kushirikiana na *IMF* itafanya tena zoezi la kuangalia uhimilivu wa deni letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilidaiwa pia kwamba uwezo wa wananchi kununua bidhaa (*purchasing power*) na ukwasi katika uchumi vimepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili naomba niseme tu kwamba, haya madai yanahusishwa na kupungua kwa fedha mifukoni mwa wananchi na pia kupungua kwa ukwasi katika benki za biashara na kwamba benki za biashara zimeshindwa kutoa mikopo kwa sekta binafsi. Kitaalam

uwezo wa sarafu kununua bidhaa unategemea, kwanza mwenendo wa mfumuko wa bei, unategemea thamani ya sarafu husika dhidi ya sarafu nyingine duniani na hali ya uhitaji na upatikanaji wa bidhaa na huduma (*demand and supply*). Ukweli ambao upo Mheshimiwa Mbunge mmoja ameusema muda mfupi uliopita, baadhi ya watu hawataki tu kukubali; ni kuwa mianya ya upatikanaji wa fedha kwa njia zisizohalali umedhibitiwa chini ya Serikali ya Awamu ya Tano. Ukwepajji kodi, madai hewa, posho zisizostahili, rushwa, ujisadi, wizi, ubadhilifu wa mali ya umma na hivyo kilichopungua mifukoni ni fedha zisizo halali. Katika misingi ya uchumi ni lazima upatikanaji wa fedha uendane na uzalishaji wa bidhaa na huduma. Vinginevyo kinyume chake ni kushamiri kwa uchumi bandia na uwepo wa tofauti kubwa za kipato mionganii mwa jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ili fedha zija mifukoni lazima sisi wananchi tujishirikishe zaidi na zaidi katika shughuli halali za uzalishaji mali na utoaji wa huduma, na malipo ya kila mmoja yawiane na kazi au biashara halisi anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitazama mwenendo wa shilingi, tukiangalia mfumuko wa bei bado viashiria vyote vinaonesha kwamba *purchasing power* ya wananchi wetu bado iko sawasawa na hakuna shida kwenye thamani ya shilingi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kidogo juu ya masuala ambayo yanagusa Zanzibar. Kwanza kuhusu kutoza kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) kwenye kiwango cha asilimia sifuri kwa umeme unaouzwa na *TANESCO* kwa *ZECO*, naomba niliarifu tena Bunge lako Tukufu kwamba Serikali tayari imekamilisha utafiti uliokuwa unapitia gharama za kujenga miundombinu, kuzalisha na kutoa huduma ya umeme katika mazingira ya sasa hususani kwa ununuzi wa jumla ili kukokotoa kiwango cha gharama kwa *Unit (KVA charge na kWh per unit)*. Serikali imeandaa waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kutoza kodi hiyo kwa kiwango cha asilimia sifuri kwa umeme unaouzwa na *TANESCO* kwenda *ZECO*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka huo naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba unatarajiwa kujadiliwa katika ngazi ya *IMTC* kesho na baadae hatua nyingine zitafuata. (*Makofii*)

Kuhusu kukosekana kwa miradi ya maendeleo ya Zanzibar katika mapendekezo ya mpango ujao hili linatokana na ukweli kuwa miaka yote Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaandaa mpango wake wa maendeleo ili kutekeleza dira yao ya maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020. Aidha, miradi ya maendeleo ya Zanzibar inagharamiwa kutoka fedha zake za ndani, gawio kutokana na Mashirika ya Muungano na hususani Benki Kuu, mikopo, lakini pia asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti na misaada ya kisekta. Mengi haya yataonekana katika sehemu ya ugharamiaji ya mpango wa maendeleo wa Zanzibar. Hata hivyo baadhi ya miradi ya Zanzibar inaonekana katika miradi ya maendeleo ya Wizara za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifafanue kidogo kuhusu namna ya ugharamiaji wa *Standard Gauge Railway*. Serikali imedhamiria kukamilisha mtandao wa reli kwa kiwango cha kimataifa kwa kuanza na sehemu ya Dar es Salaam kwenda Morogoro na baadae kutoka Morogoro kuja Makutupora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza (*Lot 1 - Dar es Salaam/Morogoro*) inafanyika kwa kutumia mapato ya ndani kwa asilimia mia moja. Kipande cha Morogoro mpaka Makutupora hiki kitagharamiwa kwa fedha za mikopo. Kwa hiyo, hadi sasa Serikali inaendelea na mazungumzo na Taasisi mbalimbali ambazo zimeonesha nia ya kugharamia hicho kipande cha kutoka Morogoro kuja Makutupora. Sehemu kubwa ya mkopo itakuwa kwa utaratibu wa *Export Credit Agency* ambayo kimsingi masharti yake yana unafuu ikilinganishwa na mikopo mingine ya kibiashara na tunaendelea na jitihada za kutafuta taasisi za fedha za kimataifa na benki kama *Standard Chartered Bank*, *Afreximbank* na *Credit Swiss* ili tuweze kupata mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa reli hiyo. Lengo hatimaye

ni kukamilisha mtandao wote wa Reli ya Kati kama ambavyo tumeueleza katika kitabu changu cha hotuba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja moja, naomba niseme hii ya mwisho halafu nihitimishe; kwamba Serikali ihakikishe kasi ya ukuaji wa ongezeko la watu inaanishi kasi ya ukuaji wa uchumi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Tanzania ilikuwa ina ongezeko la watu la asilimia 2.7 kwa mwaka. Kwa ongezeko hili inakadiriwa kwamba mwaka jana tulikuwa tumefikia milioni 52.5 na kufikia mwaka huu 2018 tutakuwa milioni 54.19. Ongezeko hili litafanya nchi yetu kuwa ya tano kwa idadi kubwa ya watu Barani Afrika baada ya Nigeria, Ethiopia, Misri na *DRC*. Hali hii inatoa changamoto kwa nchi na jamii kuchukua hatua za makusudi kukabiliana na hili ongezeko la watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nchi nyingine kama China waliweza kuendeleza uchumi na kupunguza umaskini kwa kuweka ukomo wa idadi ya watoto kwa wanandoa, lakini pia kwa kutumia vizuri idadi ya watu walionao. Sasa kwa Tanzania sera yetu haiweki ukomo wa idadi ya watu kwa wanandoa kwa sababu mbalimbali ikiwemo mila na desturi zetu, dini, lakini pia kiwango kikubwa bado cha vifo vya watoto. Nyenzo muhimu tunayoona ni elimu ambayo inaweza kutupatia mafanikio makubwa na ya hararaka na inakubalika katika jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa vijana na hasa wa kike wanapata fursa ya elimu, na wao wenyewe baadaye wakishasoma watapima idadi ya watoto ambao wanamudu kuwalea vizuri na kuwapatia mahitaji ya msingi. Kwa hiyo, kwa kifupi jitihada za Serikali kuhakikisha ongezeko la idadi ya watu lina akisi ukuaji wa uchumi, zimejielekeza zaidi katika kuwekeza katika elimu hasa ya mtoto wa kike, lakini pia huduma muhimu za jamii, afya, maji, umeme lakini na kujenga uchumi imara ambao ni jumuishi na endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na watu waliokuwa wanahoji takwimu zetu na hususani kuhusu fedha za kigeni. Napenda niwahakikishie kwa niaba ya Serikali kuwa takwimu za akiba ya fedha za kigeni zilizotolewa katika kitabu cha mapendeleko ya mpango ni sahihi. Mpaka kufikia juni mwaka huu, akiba ya fedha ya kigeni ilikuwa dola bilioni 5.48 ambayo ilikuwa na uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 5.6. Ingawa kumekuwa na uwiano hasi wa kibashara ya kimataifa mauzo ya bidhaa na huduma yamekuwa yakiongezeka; mwaka 2017/2018 mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, yalikuwa dola za Marekani bilioni 8.9 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 8.7 mwaka 2016/2017. Ongezeko hilo linatokana na kuiongezeka kwa thamani ya mauzo ya mazao ya korosho, karafuu, tumbaku, chai, mkonge na kuimarika kwa bei ya dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda noamba nihitimishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha kwanza kwa kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa kujibu baadhi ya hoja ambazo zimesemwa humu ndani, lakini vilevile kwa kuwa msaidizi mahiri sana katika Wizara hii ya Fedha na Mipango. (*Makofii*)

Naomba pia nimshukuru Katibu Mkuu Bwana Dotto James na timu yote ya wataalam na watumishi wote wa Wizara ya Fedha, ambao kwa wiki nzima hii wamekuwa wakifanya kazi ya ziada kupokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge lakini pia kuweza kuandaa baadhi ya hoja za ufanuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia mjadala huu. Bunge lako tukufu limetimiza jukumu lake la kuishauri Serikali juu mpango utakaoteklezwa katika Taifa letu. Serikali itazingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wote katika maandalizi ya mpango na bajeti kwa

mwaka 2019/2020. Hata lile la kutengeneza gongo kwa ajili ya kuuzia viwanda vya kutengeneza pombe kali totalitafakari, ingawa nilikuwa nawaza afadhalii tungetumia zaidi mahindi yetu kwa ajili ya kutengeneza chakula cha mifugo ambako nako tuna shida kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila sina hakika sana na lile lililosemwa na ndugu yangu, Mheshimiwa Musukuma juu ya kilimo cha bangi. Yapo mengi ambayo ningependa kuyatolea ufanuzi na mwisho kabla sijahitimisha, yale makontena yanayoitwa ya Mheshimiwa Makonda naomba tu niseme kwamba tulifuata taratibu na makontena yale yamekuwa yanagawanywa kwa Halmashauri maskini nchini kote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuunga mkono juhudii ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi madhubuti wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuwaletaa wananchi maendeleo. Nawaomba pia Watanzania wenzangu, tufanye kazi kwa bidii, weledi na ufanisi mkubwa ili kujenga Taifa letu. Azma yetu ya ujenzi wa uchumi wa viwanda ni thabitii, lakini itafanikishwa na Watanzania tunaofanya kazi kwa kuwajibika, tukijua kwamba hayupo mtu mwagine wa kutuletea maendeleo bali ni juhudii zetu wenywewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa wasilisho lako zuri, umehitimisha vizuri, tutaenda hatua inayofuata. Katibu! (*Makof*)

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI: Bunge linarudia.

(Bunge Lilarudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, hapa ndipo tumefika mwisho wa shughuli hii ya Kikatiba, lakini nilazimike kutoa maelezo mafupi, nadhani mmegundua mliokuwa mnafuatilia na ninaamini mlikuwa mnafuatilia vizuri, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kahitimisha maelezo yake tukiwa kwenye Kamati ya Mipango. Tulikuwa tumezoea anahitimisha kwenye Bunge na hoja inatolewa na tuna wahoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninyi kama Wabunge mnafahamu, Bunge likiamua kitu kwa hoja iliyombele yake limeamua. Kama unataka kubadilisha uamuzi wake lazima urejee Bungeni humu kwa utaratibu uliopo kwenye Kanuni za Bunge.

Sasa kwa kuwa katika hatua hii kwa mujibu wa kanuni zetu, lakini nianze na hilli la Katiba kwa sababu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalipatia Bunge hili jukumu la kuandaa mpango wa maendeleo wa muda mfupi na mrefu kupitia kifungu cha 63(3) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndiyo haya ambayo mmekuwa mnafanya.

Sasa shughuli hiyo imewekewa utaratibu na Kanuni za Bunge kupitia Kanuni ya 94. Kwa hiyo, Serikali inacholeta hapa ni Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa, unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka unaokuja. Ni hatua muhimu hii sasa, ya kwetu ni ya Kibunge kwa sababu iko ndani ya Katiba, lakini kuna wadau wengine nao wanaisaidia Serikali kutoa mawazo yao, ndiyo, lakini hii ni ya kikatiba na ndiyo maana mmeifanya kazi hii vizuri sana katika kipindi cha siku tano.

Sasa kwa kuwa ni mapendekezo huwezi ukatoa hoja muiamue maana mtakuwa mmeifunga mme-lock in, sasa nyinyi mmetoa maoni na ushari kwa Serikali kuanzia Kamati ya Bajeti, ikaleta iliyofanya uchambuzi kwa niaba yenu wa ndani, lakini na nyinyi mmeutumia taarifa hiyo ya Kamati na mapendekezo yake lakini na nyinyi mmejiongeza katika hayo ambayo Serikali imeyasikia.

Ninaamini kwa sababu ni hatua hiyo, tunaenda nayo haya waliyoyachukua wanaenda wakayafanyie kazi, lakini hata tarehe 11 Machi, *In Shaa Allah* mwaka kesho, watakachokuja nacho bado ni rasimu ya mpango, itasomwa tu lakini pia Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mpango hata katika hatua hiyo hata kuwa na mpango. Atatumia pia nafasi hiyo kuelezea mapendekezo ya Serikali kuhusu ukomo wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wenyewe sasa ndio utakuja kusomwa rasmi na hoja itatolewa siku ambapo bajeti ya Serikali itakapowasilishwa kabla ya tarehe 20 Juni mwaka kesho, sasa hiyo ndiyo itakuwa hoja. Tunaamini sasa itakuwa imesheheni, imebeba ushauri mlioutoa ninyi kama Wabunge na wadau wengine wa maendeleo ya Tanzania mpaka Waziri na Serikali kwa ujumla, Rais wa Jamhuri ya Muungano naye anasema huu ndio mpango kwa mwaka ujao wa fedha 2019/2020. (*Makofii*)

Kwa hiyo, ndiyo maana nimeona tuliseme hili ili mfahamu kwa nini hoja yetu tulikuwa tunaunga mkono mbona hatujahojiwa, kwa hiyo ni hilo tu ili tukae vizuri na hakuna mwenye *monopoly* ya *knowledge* huwa nawakumbusheni kila siku tunakwenda vizuri. (*Makofii*)

Sasa nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu wako, napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wewe na timu yakoya wataalam wizarani hapo kwa mapendekezo haya, kwa usikivu wenu, lakini kubwa zaidi kwa jinsi mlivyoweza kuyachukua haya yaliyosemwa na Waheshimiwa Wabunge.

Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, mmeefanya kazi yenu ya Kikatiba vizuri, hongereni sana. Sasa tunaiachia Serikali katika hatua hii, waendelee kuyachambua haya mliyoyatoa kwa faida ya maendeleo ya nchi yetu. Naamini kwenye wengi haliharibiki jambo, tutaenda vizuri. Mimi niungane na ninyi wengi tusibeze haya tunayoyafanya Waheshimiwa ya maendeleo ya nchi hii. Tumetoka mbali na ndiyo maana namshukuru sana

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Dkt. Kijaji, umeyasema vizuri misingi imejengwa tangu awamu ya kwanza, awamu ya pili, awamu ya tatu, awamu ya nne na sasa awamu ya tano inaendeleza misingi hiyo kwa faida ya umoja wa taifa hili kwa faida ya maendeleo ya Taifa hili. (*Makofii*)

Bunge limetekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali. Tutafanya kila lililo ndani ya uwezo wetu, kuiunga mkono Serikali kwa faida ya maendeleo yetu kupitia mpango utakaoletwaa baadaye mwaka kesho.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho tarehe 13 Novemba, 2018 saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.06 Usiku Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 13 Novemba, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*